

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 6 Julai, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

### **MHE. JOB Y. NDUGAI-MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

### **MHE. HEMED MOHAMMED HEMED-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

### **WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 176

#### **Usimamizi wa Sheria ya Uchaguzi**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kama inavyoonekana, Tume ya Uchaguzi inasimamia Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 wakati inapotangaza ratiba ya Uchaguzi Mkuu hadi kukamilisha utekelezaji.

- (a) Je, Sheria hiyo inasimamiwa na nani katika kipindi cha kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu au Mdogo hadi kingine cha Uchaguzi?
- (b) Je, Wakuu wa Wilaya wanahusika vipi katika kuhakikisha kuwa sheria za nchi ikiwemo sheria ya uchaguzi kwa ujumla hazivunjwi?
- (c) Je, ni malalamiko mangapi ya ukiukwaji wa Sheria ya Uchaguzi yameshawasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kutoka kwa Wabunge na Vyama vya Siasa kwa ujumla?

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kusimamia Sheria ya uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979 pamoja na marekebisho yaliyofanywa. Tume inatekeleza jukumu hilo wakati wote katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi Mdogo hadi kipindi kingine cha uchaguzi.
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Wilaya ni Viongozi na wana jukumu la kuhakikisha kuwa Sheria zote za nchi hazivunjwi. Ifahamike kuwa Sheria ya Uchaguzi

inasimamiwa moja kwa moja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na pale inapovunjwa mhusika anachukuliwa hatua za kisheria.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi haitakiwi kuingiliwa inapotekeleza majukumu yake.

Aidha, yapo maeneo katika Sheria ya Uchaguzi yanayohusika na makosa ya jinai. Kwa maeneo hayo, Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya Serikali mfano TAKUKURU vinaweza kuhusika na kuchukua hatua.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko yoyote ya ukiukwaji wa Sheria za Uchaguzi hupelekwa moja kwa moja Tume ya Taifa ya Uchaguzi au Mahakamani na siyo Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Uchaguzi kwa kipindi cha miaka takribani 20 kuanzia 1992 hadi sasa imepokea malalamiko mbalimbali ambapo baadhi yake yamepatiwa ufumbuzi na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi hata hivyo kwa siku za Karibuni malalamiko yanayohusu vitendo vya utoaji na upokeaji wa rushwa yamekuwa yakipelekwa TAKUKURU ambao wamekuwa wakiyashughulikia kikamilifu. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya kisheria ya Waziri, napenda kujua kwa sababu ratiba ya uchaguzi bado haijatolewa, sasa wale watu wanaofanya kampeni sasa hivi ni nani anawachukulia hatua? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwa sasa hivi kuna watu wanaofanya kampeni kwa kujiandaa na Uchaguzi Mkuu, iwapo wanavunja sheria kwa maana ya makosa ya jinai kwa mujibu wa sheria za Uchaguzi na Sheria zinginezo, basi itabidi sheria hiyo hiyo ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge na Wananchi wanafahamu kwamba sheria huwa zinavunjwa na zikivunjwa kama Polisi hajataarifiwa au kama hakuna raia mwema aliyetoa taarifa kama ilivyo kwenye makosa mengine ye yeyote yale, basi hali inabaki kama ilivyo. Na iwapo hakuna sheria iliyovunjwa basi ni kwamba hao wanatekeleza majukumu yao ya kujitafutia uongozi kwa njia halali. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Namshukuru sana Waziri wa Nchi alipojibu kwamba sheria hizi za uchaguzi zinasimamiwa na Tume ya Uchaguzi na Mamlaka ya Jinai ni Polisi.

Kwa kuwa, katika chaguzi zilizopita hasa chaguzi ndogo za Busanda na Biharamulo, tuliyaona matukio ambayo yaliwahusisha Wakuu wa Wilaya na Polisi walipopelekewa matukio yaliyohusu uvunjifu wa sheria hawakuchukua hatua.

Je, Waziri anatoa tamko gani kwa watu hao ili sheria za nchi ziweze kulindwa na haki iweze kulindwa na Demokrasia ya kweli iweze kustawi katika nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**Mheshimiwa Naibu Spika, Uchaguzi wa Busanda na Biharamulo, tumetoa maelezo mengi katika Bunge hili, ikiwa ni pamoja na wakati tulipokuwa tunajibu hoja za Bunge wakati wa Bajeti ya Waziri Mkuu.

Lalamiko kubwa ambalo lilikuwa limepelekwa Polisi la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ni pamoja na baadhi ya Wanachama wa chama fulani kukusanya kadi za wanachama wake na baadaye lalamiko hili lilipelekwa Polisi na Mkuu wa Wilaya ilionekana hakuna kosa lolote lilitotendeka kwa mujibu wa sheria zetu, Mkereketwa au Kiongozi wa chama anaweza akachunguza kadi ya wanachama wake, akaziorodhesha.

Lakini pia anaweza akaandika namba za shahada za uchaguzi kuhakikisha kwamba wanachama wake idadi yake ni kiasi gani na kuhamasisha wapige kura. Hii imethibitishwa kule Busanda na Polisi wameona hakuna kosa lilitokea. Kwa hiyo basi hizo ni tuhuma ambayo kimsingi haikuwa na msingi wowote.

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH:**Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtumishi wa Umma anapotaka kugombea nafasi ya kisiasa kuna masharti ya utumishi ambayo yanambana kabla hajagombea au kutangaza nia. Wapo watu ambao sasa hivi wanafanya hivyo.

Je, Serikali inasemaje katika hili, kwa maana hatuoni hatua ye yeyote ikichukuliwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo kuna watumishi wanafanya hivyo, toa taarifa kwa Mamlaka inayohusika. Nimesema pale awali, Duniani kote tunatunga sheria na sheria huwa inavunjwa pale ambapo taarifa haitolewi kwa vyombo husika mara nyingi kosa hilo linaishia hivi hivi bila hatua ya kisheria kuchukuliwa.

Kwa hiyo, tunasihi sana, makosa ya jinai na makosa ya utaratibu wa Utumishi wa Umma unapovunjwa basi taarifa ipelekwe kwa vyombo vinavyohusika ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa mara moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri. Mnaona swali moja tumewapa nafasi maswali ya nyongeza matatu, dakika tuko zile zile tano. Sasa huu ndiyo utaratibu unavyokwenda. Tunaendelea.

**Matumizi Mabaya ya Fedha za Serikali Katika Halmashauri**

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE (K.n.y.    MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM)** aliuliza:-

Mara kadhaa kumekuwepo na matumizi mabaya ya Fedha za Serikali katika Halmashauri mbalimbali na kusababisha kusuasua kwa Maendeleo yaliyokusudiwa kwenye Halmashauri:-

Je, ni Halmashauri ngapi zimebainika na kero hiyo na waliohusika ni wangapi wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2010?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu kuwa Serikali kupitia Bunge lako Tukufu imetunga sheria, Kanuni na Taratibu zinazotawala na kuongoza masuala ya Watumishi na yale yanayohusu mapato na matumizi ya fedha za Serikali ikiwa ni pamoja na za mamlaka za Serikali za Mitaa.

Sheria, Kanuni na Taratibu husika huelekeza namna bora ya kusimamia fedha za Umma na kutoa adhabu kwa watumishi wanaobainika kutumia fedha za Umma kinyume na Kanuni na taratibu ziliwekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007 hadi 2009/2010 jumla ya Halmashauri 30 zilibainika kuwa na matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Watumishi wa Halmashauri hizo waliobainika kuhusika na matumizi mabaya ya fedha za Umma, hatua za nidhamu zilichukuliwa dhidi yao.

Jumla ya watumishi wa Umma 921 walifkishwa mahakamani kutohana na kutuhumiwa kwa ubadhirifu wa fedha/mali ya Umma kama ifuatavyo:-

- (i) Mwaka 2006/2007, Jumla ya Watumishi 215 walifkishwa mahakamani kwa makosa ya Matumizi mabaya ya fedha za Umma;
- (ii) Mwaka 2007/2008 Mashauri ya Watumishi 297 yalifkishwa Mahakamani;
- (iii) Mwaka 2008/2009 Watumishi 307 walifkishwa Mahakamani kwa makosa mbalimbali yakiwemo ubadhirifu wa mali ya Umma;
- (iv) Mwaka 2009/2010 kufikia Desemba 2009, mashauri ya Watumishi 102 yamefikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010 jumla ya Wakurugenzi 31 wa Halmashauri walichukuliwa hatua za nidhamu na wengine kufikishwa Mahakamani kutohana na kupatikana na tuhuma za kutumia vibaya madaraka na mali za Umma (idadi hii haiko ndani ya wale 921 niliowataja hapo awali) Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

- (i) Wakurugenzi 14 walivuliwa madaraka ya Ukurugenzi;
- (ii) Wakurugenzi 2 kesi zao bado zinaendelea;
- (iii) Wakurugenzi 8 mchakato wa nidhamu bado unaendelea;
- (iv) Wakurugenzi 2 walishinda kesi na kurudishwa kazini kwa uwadhifa wao wa Ukurugenzi;
- (v) Mkurugenzi mmoja (1) alishushwa mshahara;
- (vi) Mkurugenzi mmoja (1) alipewa onyo; na
- (vii) Mkuurugenzi mmoja (1) alikabidhiwa Mashtaka ya nidhamu na sasa ameshafikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali sasa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeandaa Kanuni yenyewe adhabu na faini kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa ambayo itaanza kutumika mwaka huu wa fedha wa 2010/2011. (*Makofi*)

Kanuni hiyo inaamuru Serikali kumchukulia hatua Mtumishi pale anapobainika kusimamia au kutumia vibaya fedha za Umma ikiwa ni pamoja tozo, kufidia hasara au kuvuliwa madaraka kwa Afisa aliyeziuka Kanuni husika. (*Makofi*)

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumeona Wakurugenzi wanafanya mambo mengi ya ubadhirusi pamoja na viongozi wa Serikali za mitaa na kwa kuwa wanapelekwa mahakamani na wakitoka Mahakamani wanaachishwa kazi bila ya kafilisiwa mali zao.

Je, hawaoni kwamba wanaendelea tena kuwafundisha hao wengine wanaobaki kazini, kuwa wabadhirusi wakisema kuwa tukifukuzwa tutaendelea na mali zetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimeeleza na nilitumia zile takwimu kwa sababu nilifikiri nitakuwa nimeondoa maswali mengi sana ya nyongeza.

Suala linalokwenda Mahakamani likifiki mahakamani hukumu ile inapotolewa itasema nini kifanyike. Kama ni kufungwa itasema afungwe, kama ni kumyang'anya mali zake itaeleza kila kitu.

Sina mahali popote ambapo nafahamu na kama Mheshimiwa Mwijage ana mahali anajua kwamba kuna mtu amekwenda mahakamani amehukumiwa kwamba anyang'anywe mali zake zichukuliwe na sisi tukaendelea kumwacha na mali zake zile. Tutahitaji kulifanya kazi hilo. Lakini utaratibu ni kama huu niliusema. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa jibu fupi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza;

Kwa kuwa Watumishi wa Halmashauri wanapotumia fedha vibaya wanahamishwa kupelekwa katika maeneo yenye mazingira magumu.

Je, Serikali inaona kwamba adhabu kama hiyo itawasaidia wananchi wale walioibowi au anapelekwa kwenda kuanza wizi mwingine kule anapohamishiwa tena, Serikali inaona kwamba adhabu hiyo ni sahihi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niliambie Bunge hili kwamba *Controller and Auditor General* anapotuletea taarifa kutuambia kwamba hela zimetumika vibaya, nataka niwathibitishie Wabunge kwamba hatukai tukasema kwamba kule Kilwa hela zimechukuliwa kwa hiyo tunanyamaza kimya. Tunatuma timu kwenda Kilwa, hao wanaoonekana kwamba wametumia hela za Serikali bila kufuata taratibu zilizowekwa.

Kwa hiyo, kama yupo Mtumishi, tumefika mahali tumeridhika kwamba kuna makosa yamefanyika hapa si suala ya kwamba unamhamisha unampeleka mahala pengine ni suala la kumchukulia hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hapa kwamba zipo Kanuni, sasa hivi tunayo *Proposal za Local Government Finances za Charge and Penalties Regulations* ya mwaka 2009 ambayo inatakiwa ifanyiwe kazi kwa maana ya kwamba kutoka sasa itatamka kwamba ni nini kifanyike.

Wale wanaohamishwa ambao wanatolewa kituo kimoja mpaka kituo kingine mara nyingi ni pale tunapoona mtu amezoeleka sana mahali. Kwa hiyo, kutokana na hilo inaweza ikasababisha haya yote yanayozungumzwa hapa, ndipo tunapofanya hivyo. Lakini hakuna mahali ambapo tumemchukua mtu amethibitika amefanya makosa tunamtoa hapa halafu tunampeleka Longido kule aende akaharibu zaidi. Hilo hapana.

Na. 178  
**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege – Dodoma**

**MHE. COL. FETEH S. MGENI (K.n.y. MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo ya Msalato Mjini Dodoma ndipo kitakapojengwa kiwanja kikubwa cha Ndege badala ya kiwanja kidogo kilichopo Dodoma Mjini kwa sasa:-

- (a) Je, upembuzi yakinifu unaofanywa sasa utamalizika lini?
- (b) Je, ujenzi wa kiwanja hicho utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu wa kiwanja kipywa cha ndege kitakachoengwa eneo la Msalato ilikamilika tangu Desemba 2008. Kazi hiyo, ilianza Novemba 2007 na iligharimu Dola za Marekani 440,000 ambazo zilitolewa na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (*BADEA*) kama mkopo kwa Serikali.

Aidha, zoezi la kulipa fidia kwa wananchi wa Msalato ilianza mwezi Novemba 2008 na kukamilika mwezi Februari 2009 ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.283 zilitumika kuwalipa wananchi 1,438. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 50.386 zilitumika kuhamisha makaburi na shilingi bilioni 1.233 zilizobakia zilitumika kulipa fidia ya nyumba na mali nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wakina pamoja, na kulipa fidia Wizara yangu inafanya juhudzi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho kwa kufanya mazungumzo na taasisi za fedha na wadau wa maendeleo. Gharama za kutekeleza mradi huo zinakadirwa kufikia Dola za Marekani milioni milioni 62. Moja ya taasisi za fedha ambayo Serikali inafanya maongezi nayo ni Benki ya Maendeleo ya Kiarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzuia uvamizi wa eneo la kiwanja katika mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.56 ambazo zinatumika kuweka mipaka ya kiwanja kusafisha eneo linalokusudiwa kujenga miundombinu ya kiwanja pamoja na kujenga barabara ya kuingia kiwanjani (*access road*).

Mheshimiwa Naibu Spika, muda rasmi wa kuanza kwa ujenzi wa kiwanja kipywa cha Ndege cha Msalato utajulikana baada ya kukamilika kwa mazungumzo na taasisi za fedha na wadau wengine wa maendeleo.

**MHE. COL. FTEH S. MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotupa ya matumaini. Lakini katika juhudzi hizi ambazo sasa hivi zinaendelea imakeonekana kwamba zitachukua muda kidogo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri asingeona vyema hivi sasa basi tukakishughulikia kiwanja chetu kilichopo hapa Dodoma ili angalau pakapendeza? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba ni vizuri tukakishughulikia kiwanja cha ndege cha Dodoma kilichopo hivi sasa. Hapo awali kulikuwa na wazo la kukiongezea uwezo urefu lakini ikabidi barabara ambayo sisi tumezoea kuitumia ilikuwa lazima ifungwe. Kukaonekana kwamba hakuna safety ya kutosha kwa sababu mbele kabisa kama mtakubaliana nami kuna nyumba.

Kwa hiyo, hatuwezi kukiongeza kilichobaki ni kuboresha kitu ambacho kinafanya kila baada ya muda wakati fedha zinapopatikana. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba viwanja vyote tunafanya hivyo kwa kuviwekea hela ili ndege ziweze kufanya kazi ya kuruka na kutua muda wote.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeandaa mpango wa kupanua kiwanja kidogo kilichoko Dodoma na sasa hivi nyumba zote zilizoko upande wa kulia zimepigwa X na tathimini imeshafanyika wakati huo tuna mpango wa kujenga kiwanja kipyga cha kisasa. Je, Serikali haioni kupanua kiwanja kilichopo ni kupoteza fedha kwa sababu lazima walipe fidia badala ya kuendelea na mpango mahususi wa kujenga kiwanja kipyga kwa haraka? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Sakaya hata kama tutafikia *stage* ya kujenga kiwanja cha ndege cha Msalato, kiwanja tulichonacho kitatumika kwa ndege ndogo ndiyo maamuzi ambayo tumekubaliana.

Kwa hiyo, kuweka X ni kuhakikisha kwamba tunakidhibiti kile kiwanja kukiwekea mipaka vizuri na kukidhibiti ili kiwe kinatumika vizuri zaidi. Kujenga kiwanja cha ndege kunachukua muda sana kitakachojengwa kitachukua muda wakati huo huo hiki kilichopo itabidi kiboreshw na kiweze kuendelea kutumika. (*Makofi*)

Na. 179

### **Ujenzi wa Barabara Mkoani Tabora**

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu sasa kumekuwa na taarifa kuwa Serikali inafanya matayarisho mbalimbali kuhusu ujenzi wa barabara za Nzega – Tabora na Itigi – Tabora-Kigoma na kwa kuwa matayarisho hayo ni pamoja na utafutaji wa fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hizo:-

Je, Serikali inaweza kuliarifu Bunge hili kuwa ni hatua gani imefikiwa mpaka sasa katika utafutaji wa fedha zinazohitajika na ni lini ujenzi wa barabara hizo mbili muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Tabora unatarajiwa kuanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Tabora – Nzega yenye urefu wa kilomita 116 ulikamilika tarehe 8 Machi, 2010. Uchambuzi wa zabuni za kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami uko katika hatua za mwisho. Ujenzi wa barabara hii utagharamiwa na Serikali kwa kutumia fedha za ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Kidahwe – Uvinza hadi Ilunde yenye urefu wa km. 104 itajengwa kwa fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Abu Dhabi. Mchakato wa kumpata mkandarasi atakayejenga barabara hii upo katika hatua za

mwisho na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusainiwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa kina wa sehemu ya Ilunde – Malagarasi – Kaliua (km 156) ulikamilika mwezi Februari 2009. Serikali ya Korea ya Kusini imekubali kugharamia ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi na barabara za maingilio (*approach roads*) zenyе urefu wa kilomita 24 kila upande wa daraja.

Uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya ujenzi umekamilika na mkataba wa ujenzi utasainiwa baada ya kupata *no objection* kutoka Serikali ya Korea. Serikali yetu inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za kugharamia ujenzi wa kilometra 108 zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara ya Itigi – Tabora wakati Serikali ikiendelea na mazungumzo na Serikali za Iran na Kuwait kupata fedha za kugharimia ujenzi wa sehemu hii, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara kwa awamu. Zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Manyoni – Itigi – chanya (km 85), Tabora – Nyahua (km 80) na Tabora – Urambo (km 90) zilitangazwa tarehe 31 Machi, 2010 na kwa sasa uchambuzi wa zabuni hizi uko katika hatua za mwisho.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba majibu haya yanatia moyo. Lakini katika taaluma ya usimamizi wa miradi (*project management*) huwa kuna ratiba inayoonyesha jinsi mradi toka unapoanza kuufikiria unapita hatua zake mpaka utakapokamilika. Sasa naomba nipewe majibu kwa mujibu ya ratiba ya miradi hususan ya barabara kutoka Itigi – Tabora na Nzega – Tabora:-

- (a) Ni lini hasa uchambuzi huu utamalizika na ujenzi kuanza?
- (b) Kwa kuwa hali ya barabara ya Itigi – Tabora na Nzega – Tabora ni mbaya sana. Serikali itafanya nini katika kipindi hiki cha mpito ambapo bado wanachambua wanachakata wako mbioni ili maisha yaendelee kwa gharama nafuu kwa maana ya magari yasiendelee kuharibika kwa ajili ya ubovu wa barabara hizi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kujibu swali hili mtu anatakiwa kuwa mwangalifu kwa maana kila siku mimi nasikiliza mazungumzo yanatoka hapa kutoka Tabora na kutoka Kigoma ninajua wananchi wa Kigoma na Tabora sasa hivi wanasiliza majibu ya Serikali.

Nataka niseme hapa mimi ndani ya Serikali naiona ile *political will*. Mheshimiwa Rais kila siku anaondoka hapa anakwenda Tabora anakwenda Kigoma sisi wote tunamsikia na matamshi yake tunayasikia.

Mheshimiwa Kawambwa anauliza maswali hapa kuhusu barabara hizi zinazozungumzwa hapa na sisi wote majibu yao tumekuwa tunayasikia wakionyesha *commitment* ya Serikali kuhusu barabara hizi. Na Wabunge wanaotoka Tabora na Kigoma ninataka niseme msiposema hivyo mnayosema *then mtabaki hivyo hivyo*.

Kwa hiyo, ni haki yenu kusema hivyo mnavyosema ni sahihi kabisa kusema hivyo kwa sababu mtaondoka hapa muda siyo mrefu kabisa.

Pamoja na Kaimu Waziri Mkuu ni haki yenu mseme hayo maneno. Wasiposema maneno haya wanayosema hapa watabaki hivyo kwa sababu kila mtu anaangalia upande wake. Sasa naulizwa kuhusu ratiba tuliamiwi hapa Bungeni kwamba Waziri atakutana na Wabunge hawa na nina habari kwamba walikutana wakakutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu akaelekeza kwamba wakae wazungumze na wapeane ratiba hiyo na kuonyesha mpango mzima utakavyokuwa kwa maana ya *details* ambazo Mheshimiwa Kaboyonga atazungumza.

Nimecheki na Waziri Kawambwa asubuhi hii akaniambia alipokuwa ameondoka hapa kwa sababu ya jambo lingine la dharura ambalo limesababisha sasa sisi ndiyo tujibu swalii hili hakuwa amewatelea hiyo orodha na kuwaonyesha ratiba na kila kitu kitakachokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nithibitishe mbele yako kwamba nina hakika kwamba ananisikiliza kwamba bwana ehee ratiba ya kazi hii inatakiwa. (*Makofi*)

La pili, amesema sasa tunapoendelea na mchakato na hiyo mipango mingine yote. Je, mnasema nini kuhusu hizi barabara ambazo zinaendelea kuharibika?

Kuna bodi ya barabara ya Mkoa wa Tabora, kuna bodi ya barabara ya Mkoa wa Kigoma. Mle ndani *TANROADS* wanakwenda wanaonyesha mipango inayofanyika pale.

Kwa kawaida wakati tunasubiri hii mipango mikubwa ije, kinachofanya kazi pale ni *TANROADS* pamoja na Halmashauri zinazohusika katika eneo lile.

Nataka nimthibishie Mheshimiwa Kaboyonga kwamba zimetengwa hela kwa kazi hiyo ili uharibifu unapotokea mahali popote kazi ile iweze kufanyika. Sina *details* zake

lakini najua kwamba yeye ni Mjumbe wa Bodi ya Barabara atakuwa anajua kwamba *TANROADS* wamepanga nini hayo ni majibu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, angekuwa Mheshimiwa Spika, ingekuwa hivyo hivyo.

Na. 180

**Ruzuku kwa Ajili ya Zana za Kilimo**

**MHE. JOB Y. NDUGAI (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kuboresha kilimo ni pamoja na kuondoa jembe la mkono na kuleta kilimo chenye tija:-

(a)Je, ni lini Serikali itaamua kwa makusudi kutoka ruzuku maalum katika matrekta ya mkono na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi na matrekta makubwa ili wakulima wayapate kwa bei nafuu na kwa urahisi?

(b)Kwa kuwa bado Mfuko wa Taifa wa Pembejeo hautoshelezi mahitaji ya maendeleo ya kilimo na hasa katika kusambaza zana bora za kilimo kwa wananchi.

Je, Serikali inalitambua hilo na kama inalitambua inalitatuaje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutoa ruzuku kwa zana za kilimo kwa wakulima kupitia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo *ASDP* kwa kila

Halmashauri. Wakulima walioibua miradi ya kuendeleza matumizi ya zana za kilimo kupitia mipango ya Wilaya ya kuendelea kilimo *DADPs* wanachangia asilimia 20 tu ya gharama ya zana hizo na asilimia 80 inatolewa na ruzuku hiyo.

Katika mwaka wa 2009/2010 hadi tarehe 31.04.2010 kupitia programu hii wakulima wamewezeshwa kununua matrekta madogo ya mkono 1,524 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.5 na matrekta makubwa 14 yenye thamani ya shilingi milioni 453.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mfuko wa Taifa wa Pembejeo hautoshelezi mahitaji ya usambazaji wa zana bora za kilimo kwa wakulima.

Hata hivyo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2007/2008 – 2009/2010) Mfuko wa Taifa wa Pembejeo umetoa mikopo ya matrekta makubwa 379 yenye thamani ya shilingi bilioni 11.9 na matrekta madogo ya mkono 131 yenye thamani ya shilingi milioni 827 na hivyo kuwa mchango mkubwa katika kuendeleza matumizi ya zana bora nchini.

Aidha, Serikali katika mwaka huu wa fedha wa 2000/2010 imeiwezesha Benki ya Rasilimali *Tanzania Investment Bank (TIB)* kufungua dirisha kwa ajili ya kutoa mikopo kwenye sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na zana bora.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na swali hili muhimu sana wakati huu wa kilimo kwanza. Tutakubaliana kwamba kiwango cha matrekta makubwa plau na matrekta madogo kwa maana ya *power tiller* ambacho kimetolewa ni matrekta machache sana. (*Makofi*)

(a) Sasa Serikali inasemaje kuhusu kuongeza idadi ya hizo plau, *power tiller* na matrekta makubwa kwa mfano ameeleza matrekta makubwa 14 tu katika utaratibu ule wa mwanzo.

(b) Tunafahamu kabisa kwamba kilimo chetu kinakwama kwa sababu ya matumizi ya jembe la mkono. Kwa hiyo, iko kila sababu ya kuongeza kilimo chetu kwa kutumia zana

bora zaidi kwa maana ya plau ya kukokotoa ng'ombe *power tiller* na matrekta makubwa na benki ya rasilimali ambayo ameitaja sasa iko Dar es Salaam.

Sasa kuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba benki ya rasilimali inakuwa na tawi kila Mkoa lakini vile vile mfuko wa pembejeo unakuwa na tawi kila Mkoa ili wakulima wa kila Mkoa waweze kufikia vyombo hivi na kupata mikopo kwa ajili ya kuboresha kilimo chao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu kuongeza matrekta, matrekta haya yaliyonunuliwa na Halmashauri yanatokana na miradi ilioibuliwa na wananchi. Fedha hizi sisi kama Serikali Kuu tunapeleka Halmashauri kwa ajili ya wao Halmashauri kupanga mipango yao ya kilimo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ndugai kwa kushirikiana na Halmashauri yake basi wakae na kuona kuna umuhimu wa kuongeza matrekta makubwa katika Halmashauri yake kwa sababu fedha hizo tunazitenga mwaka hadi mwaka na huwa tunaziongeza kutoka na upatikanaji wa fedha hizo.

Kuhusu swali lake la pili, nakubaliana na yeze kwamba kunapotokea huduma za benki kusema kweli kama hii ya *TIB* inatakiwa isogezwe karibu na wananchi. Lakini nikiri kwamba hii ni mara ya pili huu ni mwaka wa pili wa Bajeti ambapo Serikali imetenga fedha kwenye dirisha la *TIB* kwa ajili ya kuhudumia kilimo.

Kwa hiyo, wazo lake ni zuri tutaangalia uwezekano wa kupeleka matawi yale angalau basi kwa kanda siyo kwa kila Mkoa kwa sababu ya gharama za uendeshaji lakini angalau basi kwa kanda za kilimo kusudi wakulima waweze kupata mikopo kwa bei rahisi. Lakini kuhusu Mfuko wa Pembejeo kupeleka matawi yake kule nikiri kwamba hilo ni suala ambalo tunaweza tukalizungumza tukaangalia ni maeneo gani tunaweza tukaweka kutokana na upatikanaji wa fedha zile kusudi wakulima waweze kupata mikopo maeneo yaliyo karibu badala ya kufuata Dar es Salaam.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la viwanda vya kutengeneza zana za kilimo hapa nchini linabaki kuwa muhimu sana. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tunafufua viwanda vya kutengeneza zana za kilimo hasa majembe ya kukokotwa na ng'ombe. Lakini pia na viwanda kwa ajili ya kuunganisha zana kama *power tiller* pamoja na matrekta makubwa ili kukwepa gharama kubwa za waagizaji wa zana hizi kutoka nje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na yeze kwamba kuna haja ya kufufua viwanda vyetu vya zana za kilimo kama kile kilichokuwa Mbeya.

Lakini nipende kusositiza kwamba Serikali haijengi viwanda na wala haifanyi biashara, lakini kazi yetu sisi kubwa kama Wizara ni kuhamasisha wafanyabiashara wakubwa kusudi waweze kujenga viwanda kama hivi vya kutengeneza zana za kilimo, lakini pia viwanda vya kuunganisha matrektka.

Sisi kazi yetu ni kuhamasisha hata nchi za nje tumeshaongea na watu wa India, tumeshaongea na watu wa Ulaya, Italy pamoja na Korea kwa ajili ya kuweka viwanda vya kuunganisha zana za kilimo hapa nchini.

Kwa hiyo, kazi yetu kubwa kusema ukweli ni kuhamasisha na yeze tunaweza tukashirikiana na yeze tukahamasisha wafanyabiashara hao waweze kuweka viwanda vya zana za kilimo.

Na. 181

### **Kuwapatia Usafiri Watendaji wa BMU - RORYA**

**MHE. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Serikali imeonesha dhamira ya kuendeleza wavuvi kwa kujenga Milao na kuendeleza Milao mingine na kuanzisha BMU; katika Wilaya ya Rarya kuna Milao 32 inayoendeshwa na wavuvi wanaoishi maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje watendaji wa BMU kupata usafiri kama vile pikipiki?

(b) Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa Milao mingine 31 baada ya kukamilisha ujenzi wa SOTA?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Sarungi, Mbunge wa Rarya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia miradi mbalimbali inayotekelawa katika Halmashauri zake imeanzisha na imeimarisha vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi (*Beach Management Units- BMUs*), ambapo hadi sasa zipo jumla ya BMU 642 nchini.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Rarya, Serikali imenuna boti 1 ya doria na injini moja yenye ukubwa wa nguvu za farasi (*Horse Power*) 45 na injini

nyingine yenyewe ukubwa wa *HP 18* kupitia mradi wa utekelezaji wa mpango wa menejimenti ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Victoria na mradi wa *Lake Victoria Environmental Management Project (LVEMP 1)* ili kuimarisha usafiri wa kwenye maji hususan doria inayofanywa na Serikali kwa kushirikiana na *BMUs*. Serikali hajaweweza kutoa usafiri wa pikipiki kwa *BMUs* kutokana na ufinyu wa Bajeti.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuboresha mialo ya Nyang'ombe na Kibuyi na kukamilisha ujenzi wa mwalo wa Sota, Serikali kupitia Halmashauri ya Rarya imepanga kuboresha Mialo ya Rwang'enyi na Ruhu katika mwaka 2010/2011. Aidha, Serikali kupitia Halmashauri zake itaendelea na utaratibu wa kuboresha Mialo mingine nchini ikiwemo Mialo 31 iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wake kwa jinsi wanavyofuutilia na kutatua matatizo ya wavuvi katika nchi yetu hususani Wilaya ya Rarya, nawaombea mafanikio mema katika uchaguzi ujao. Ninalo swali moja la nyongeza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza azma yake ya kuwashawishi sekta binafsi kuanzisha kiwanda cha kusindika samaki na kutengeneza zana za uvuvi katika Wilaya ya Rarya tukizingatia nchi jirani tunayopakana nayo inayo ivanda kumi vyta kusindika samaki?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sarungi napenda sana kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wakati ya Bajeti yetu walitupongeza na katuombea na leo tena Mheshimiwa Sarungi ametuombea mimi na Waziri wangu tunashukuru na naamini kwamba Mwenyezi Mungu atasikia maombi hayo ili tuweze kurejea tena Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali yetu kwa sasa hivi ni kuhamasisha sekata binafsi kuwekeza na kwa sasa hivi tunajenga Mwalo mkubwa kabisa pale Rarya, Mwalo wa Sota na mingine tunaifanya ukarabati na kuna samaki wengi sana pale. Kwa hiyo, sisi kwa sasa tunaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza ivanda vyta samaki kule Rarya pamoja na vile vyta nyavu, ahsnate sana. (*Makofî*)

Na. 182

**Ukosefu wa Walimu na Kuzifanya Shule za Sekondari za Lulumba na Iguguno  
kuwa High Schools**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. JUMA H. KILLIMBAH)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna mpango wa kuzifanya shule za Sekondari za Lulumba na Iguguno Wilayani Iramba kuwa *High Schools* na kwamba, mpango huo ulishakubaliwa na maandalizi yake yapo tayari pale Wilayani na Mkoani:-

- (a) Je, Serikali inatambua mpango huo na ina mkakati gani kukamilisha hatua zilizobakia ikiwa ni pamoja na kuzitambua shule hizo?
- (b) Je, kama mpango huo umepitishwa kwenye ngazi ya Wilaya na Mko, ni kwa nini utekelezaji wake haujaanza?
- (c) Kwa kuwa, wananchi wa Iramba Magharibi wamejitolea na kuweza kujenga shule ishirini na tano (25) kwa nguvu zao. Je Serikali itapeleka lini walimu hasa wa taaluma ya Sayansi ili kuunga mkono juhudhi hizo za wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassani Killimbah, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b),(c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaunga mkono jitihada za wananchi katika kujenga shule za sekondari katika kila Kata. Aidha inatoa pongezi kwa Wilaya ya Iramba kwa kuweza kujenga shule za sekondari 25. Pia, Serikali inatambua mpango wa Wilaya ya Iramba kuzifanya shule za sekondari za Lulumba na Iguguno kuwa *High School*. Mpango huu wa Wilaya unaungana na nia ya Serikali kuhimiza Mikoa na Wilaya kujenga shule za Kidato cha 5 na 6 katika kila Tarafa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji mpango wa kuzifanya shule za sekondari za Lulumba na Iguguno kuwa *High School* umeanza. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kupitia Idara ya Ukaguzi wa shule imefanya ukaguzi wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuongeza juhudhi kukamilisha mapungufu kama yalivyobainishwa na wakaguzi wa shule ili shule hizi Shule zisajiliwe na kuweza kuchukua wanafunzi wa kidato cha 5 katika mwaka 2011/2012.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na juhudhi za kutoa mafunzo ya ualimu ili kupata walimu watakaokidhi uhaba uliopo. Walimu hao pamoja na wa Sayansi, hupangwa katika Halmashauri zote mara wanapomaliza mafunzo yao. Hivyo ni jukumu la Halmashauri kuwapanga walimu kwenye shule zake kulingana na mahitaji. Wilaya ya Iramba walipangiwa walimu 114 katika mwaka wa fedha 2009/2010. (*Makofii*)

Katika mwaka 2010/2011 walimu wengi zaidi watahitimu na kupangiwa kazi katika shule za sekondari Wilayani Iramba. Ni matarajio yetu kuwa kila shule ya

Sekondari ya Serikali yenyе upungufu itapelekewa angalau walimu 5 ili kupunguza uhaba wa walimu uliopo hivi sasa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a)Kwa kuwa, mapungufu yaliyohainishwa na wakaguzi yanatokana tu na upungufu wa pesa. Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia fedha ili kuunga mkono nguvu za wananchi ambao wamejenga shule 25 kwa Jimbo la Iramba Magharibi tu ili kukamilisha mapungufu hayo haraka iwezekanavyo, ili shule hizo ziweze kufunguliwa?

(b)Kwa kuwa, Naibu Waziri amekiri kwamba shule hizo za elimu ya juu zitaanza mara moja mwaka kesho 2011/2012. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuanza maandalizi kwa maana ya kupeleka vitabu, maabara na mambo mengine yanayohusu elimu ya juu, ili muda ukifika shule hizo zisiwe na mgogoro tena wa kushindwa kuanza kufundisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** : Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza yeye kama Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake kwa Mkoa wa Singida ka namna ya kipekee anavyofuatalia maendeleo ya elimu kwa Mkoa wake. Serikali kwa kuzingatia juhudzi za wananchi kwa Wialya ya Iramba imeipelekea shule hizo mbili jumla ya shilingi milioni 76 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu muhimu kama vile mabweni, mabafu, vyoo na upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali na Wizara ya Elimu hususani kuhakikisha kwamba shule zote za kidato cha tano na sita hazifunguliwi bila kuwa na maabara. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hivi sasa pamoja na juhudzi za wananchi wa Iramba kwa pamoja tunashirikiana kuhakikisha kwamba vifaa, maabara na walimu vinapatikana kabla ya kupeleka wanafunzi itakapofika mwaka 2011. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitufikisha na kama tutakuwa tumerudi tutajulishana.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ujenzi wa shule za Kata umeitikiwa sana hapa Tanzania katika kujenga. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapatia usafiri shule za Kata hususan kwa Kilwa Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** : Mheshimiwa Naibu Waziri, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu rahisi kwa kadri tutakavyoweza, vyombo vya usafiri ni muhimu sana kwa karibu kila shule. Kutohana na ufinyu wa bajeti kwa hivi sasa nitashindwa kumwahidi rasmi kwamba tutampatia. (*Makofii*)

Hata hivyo, namuomba awe na subira na utaagiza kuweza kuona mazingira halisi yaliyopo na endapo tutajaliwa katika bajeti itakayokuja ya 2011/2012 tunaweza tukaliweka kwenye mkakati.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa nafsi hii ya kuuliza swali la nyongeza na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini pia niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuinua sana sekta ya elimu. Sasa je, kutokana na kiwango cha elimu hapa nchini na kuwa shule za sekondari zimeenea kila mahali.

Je, Serikali haioni sasa kiwango cha chini cha elimu hapa nchini kiwe ni form four badala ya kuwa darasa la saba?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) :** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Wizara ipo katika mchakato wa kuhakikisha kwamba inapata maoni na maboresho ya sera yanafanyika. Katika maboresho hayo, suala la kiwango cha chini cha elimu limezingatiwa.

Naomba tu kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu wale tutakao jaliwa kurudi sote hapa tukirudi tutakutana maana hiyo tumeiweka *pending* ndio hoja ya kwanza, tutakayoijadili, Sera ya Elimu kwa ubora wake kutegemea na muda tulionao. (*Makofi*)

Na. 183

#### **Shirika la Bima la Taifa (N.I.C.)**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi wanachama wa Shirika Bima la Taifa (*NIC*) hudaiwa kupeleka *Salary Slip* zao tangu walipoingia Shirika la Bima ya Taifa (*NIC*), punde Mkataba wa Bima unapoiva, hali inayoonekana kuwa ni usumbufu:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa, ni kutowatendea haki wananchama hao?
- (b) Je, kwa nini Serikali isiboreshe Kumbukumbu zake ili kuzuia kumsumbuu mwanachama wakati muda unapofika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanueli Luhahula, Mbunge wa Jimbo la Bukombe, lenye sehemu (a), (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi anapoamua kukata Bima ya maisha kupitia Shirika la Bima la Taifa (*NIC*) anatakiwa kujaza hati maalum ya makubaliano kati yake na shirika. Makubaliano hayo yanatoa pia idhini ya makato kutoka kwenye mshahara

kama ni mfanyakazi kupitia mwajiri wake au kuwasilisha ada ya Bima kwa utaratibu utakaokubalika.

Aidha, sehemu ya makubaliano hayo, ni kwa mteja kukubali kuwasilisha Hati itakayoonyesha kuwa alikuwa anachangia malipo ya ada ya Bima wakati wa kudai mafao yake. Hata hivyo, baadhi ya waajiri wamekuwa wakichelewesha au kutopeleka kabisa makato kwenye Shirika la Bima.

Kutokana na baadhi ya waajiri kutowasilisha makato ya watumishi wake, Shirika limekuwa likilazimika kuomba Hati ya Mshahara (*Salary Slip*) ili kujiridhisha kama ada hiyo imekuwa ikikatwa na kuwasilishwa katika Shirika la Bima kwa mujibu wa makubaliano. Utaratibu tunaoutumia wa kuomba Hati ya Mshahara (*Salary Slip*) haina maana kwamba hatuwatendei haki wateja wetu, bali ndio njia pekee kwa sasa ya kujiridhisha pamoja na kupekana na upotevu wa fedha za Umma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Bima katika mkakati wake wa biashara (*Business Plan*) imejumuisha pia uimarishaji wa mtandao wa mawasiliano (*ICT*).

Mtandao huo unalenga katika kukusanya na kutunza Kumbukumbu za wateja pamoja na kukokotoa madai kwa urahisi zaidi kulingana na aina ya Bima iliyochukuliwa na mteja. Inategemewa kwamba uboreshaji wa mawasiliano utakapokamilika utaimarisha zaidi uwekaji wa Kumbukumbu na hatimae wateja hawatalazimika tena kupeleka *Salary Slip* zao wakati wakiwasilisha madai yao ya Bima. (*Makofit*)

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa lakini katika jibu lake (a) amesema kwamba tatizo ni ucheleweshaji wa Serikali wa mwajiri kupeleka malipo yale na ndio maana mwajiriwa, mteja analazimika kuombwa *Salary Slip*.

(a) Kwa kuwa, wanaoleta usumbufu huo niwaajiri, Serikali inawachukulia hatua gani waajiri hao badala ya kuwasumbua hao wateja?

(b) Wateja wa Shirika Bima ya Taifa (*NIC*) ambao Bima zao zimeiva, mimi nimeona mwenyewe katika Wilaya ya Bukombe walipokuja Wilayani Bukombe wakawakuta walimu, wakawakusanya walimu kwenye *guest house* na wanapofanya malipo wanalipa zile hela ndogo tu. Anayedai hela nyingi halipwi.

Je, hawa wanaodai hela nyingi tuwapeleke wapi wakapate fedha zao?  
(*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu anaechelewesha kuwasilisha makato ya Bima ya mteja hulazimika kulipa faini. Sasa hivi kwa mujibu wa sheria yetu ambayo tumeirekebisha kuna kipengele ambacho hata kufikishwa katika Mahakama atafikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbuge kwamba hakuna atakae kosa kulipwa mafao yake. Hao wanalipa Bima ndogo ndogo kwa sababu hali ya fedha kwa sasa siyo nzuri, hawana, isipokuwa tayari tumeshafanya utaratibu na Shirika la Bima (NIC)litapewa fedha zake na Serikali ili liweze kulipa malipo yote wanayodaiwa. (*Makofi*)

Na. 184

### **Kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Mashirika na Taasisi nyingi za Umma zimekumbwa na matatizo mengi likiwemo la ukosefu wa mitaji ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya mashirika hayo:-

Je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kukabiliiana na tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Jimbo la Wete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma zinakabiliwa na ukosefu wa mitaji kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge katika swalii lake la msingi. Aidha, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kuwa, kutokana na tatizo hilo, Serikali imefanya marekebisho ya mfumo wa uendeshaji wa uchumi ikijumuisha kumiliki na kuendesha Mashirika ya Umma, chini ya Sheria ya

marekebisho ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 (*Public Corporations Amendment Act 1992*). Kulingana na maekebisho hayo, Mashirika na Taasisi za Umma zinapaswa kujiendesha kwa faida. Hatua hii inalenga katika kupunguza mzigo wa utegemezi kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuyawezesha Makampuni au Taasisi za Umma na za Kitanzania ambazo zina miradi mizuri lakini zimekosa mitaji, Serikali kupitia kituo cha uwekezaji imefanya juhudni za kutafuta mbia kutoka ndani na nje kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa mitaji, teknolojia na utaalam wa kuendesha miradi kulingana na mahitaji. Kadhalika Serikali pia imeanzisha Benki ya Rasilimali (*TIB*) kwa lengo la kutoa mikopo kwa Kampuni na Taasisi za hapa nchini. (*Makofi*)

Hivyo ni muhimu kwa Mashirika na Taasisi za Umma kuwa na mipango mizuri ya kibahsara ambayo itawezesha kupata mikopo kutoka Benki ya Rasilimali au benki nyingine za biashara pamoja kuvutia mitaji kutoka ndani na nje ya nchi. Hii ndiyo hatua muafaka ya kuyawezesha mashirika kuondokana na ukosefu wa mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inafuata mfumo wa soko huria, Serikali haioni kama kuna sababu ya msingi ya kuanzisha mfuko wa uwekezaji kwa ajili ya Mashirika ya Umma. Hii inatokana na ukweli kwamba katika mfuko wa soko huria Serikali hajijuhishi na kufanya biashara bali inalenga katika kuweka mazingira bora ya uwekezaji na ushindani pamoja na kusimamia sera ambazo zitawezesha mashirika, taasisi za umma na sekta binafsi kuhimili ushindani. Jambo la msingi ambalo Serikali tutalazimika kuliangalia kwa undani zaidi ni suala la kuiongezea mtaji Benki yetu ya Rasilimali ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, na hili tunalitekeleza.

**MHE. MWADINI ABAB JESHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mashirika ya umma yanatengeneza faida hupaswa kutoa gawio kwa wana hisa ambao wamechangia katika mtaji wa mashirika hayo. Kwa kuwa mengi ya mashirika hayo bado yanahitaji kupata mtaji kwa ajili ya kujiendeleza kiufanisi zaidi. Sasa yako yale mashirika ya umma ambayo ina hisa asilimia 100 iko tayari kusamehe gawio kwa muda fulani ili watumie faida ile ku-*recapitalize* mashirika hayo ili yajiendeshe kwa ufanisi?

Lakini swali la pili, kwa yale Mashirika ya Umma ambayo Serikali ina sehemu ya hisa pamoja na wanahisa wengine, iko tayari kushirikiana na wanahisa wenzake ili kuruhusu kipindi fulani kutumia faida ya mashirika hayo ku-*recapitalize* mashirika hayo ili yajiendeshe kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kusamehe gawio kuliruhusu shirika liweze kufanya vizuri baada ya kuona kwamba kama gawio hilo likisamehewa

itakuwa ndiyo *solution* kuweza kufanya vizuri, Serikali iko tayari kusamehe gawio.  
(*Makofii*)

Na. 185

### **Wananchi Kilwa Kulipwa Fidia Kwenye Maeneo ya Utafiti**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI (K.n.y. HASNAIN G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa utafiti wa mafuta na gesi uliofanyika katika Wilaya ya Kilwa, Tarafa ya Pande, eneo la Kisongo umesababisha kutengwa maeneo makubwa ambayo ni mali ya wananchi wa kijiji:-

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia zao?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, naomba kutoa maelezo kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Kampuni ya *Gas Rak* ya *Ras Al Khaimah* ilianza utafiti wa awali wa mafuta na gesi asili katika maeneo ya Pande Mashariki mwaka 2007 kwa kukusanya takwimu za mitetemo kwenye eneo hilo. Kazi hiyo ilifanyika kwa kutayarisha mikuza ambayo baadhi yake ilipita kwenye mashamba ya wananchi. Takribani kilomita 162 za takwimu za mitetemo zilikusanya. Aidha, hakuna maeneo ya kudumu yaliyotengwa kwani utafiti bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Gas Rak* imelipa jumla ya shilingi milioni 15 kama fidia kwa wananchi 317 wa vijiji mbalimbali likiwemo eneo la Kisongo kwa mazao na mali zilizoharibiwa kutohana na utafiti huo.

Kabla ya malipo kufanyika, lilifanyika zoezi la uhakiki na kukadiria mazao na mali itakayoharibiwa ili kupisha mikuza ya utafiti kutayarishwa. Zoezi hilo lilifanyika kwa kushirikisha Afisa Ardhi wa Wilaya na Uongozi wa Serikali ya Kijiji husika.

Baada ya kuhakiki na kukadiria uharibifu uliofanyika malipo yaliandaliwa kwa kutumia viwango vya fidia vya Serikali. Malipo yote yalifanyika mbele ya Mtendaji wa Kata, Afisa Ardhi na Viongozi wa Serikali ya Kijiji husika mara baada ya taratibu zilizotajwa hapo juu kukamilika. Nakala za malipo yote zipo Wilayani Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tulizokuwa nazo, hakuna mwananchi aliyeharibiwa mazao yake ambaye hajalipwa. Iwapo kuna mwananchi ambaye alisajiliwa na hajalipwa, tunamwomba kuitia Mheshimiwa Mbunge atupatie vielelezo vyake ili Wizara yangu ivifanyie kazi.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa jambo hili limeleta utata pale Pande pamoja na kijiji cha Kisongo na pia sisi viongozi. Je, Serikali haioni kuna haja ya kukaa na wananchi hawa na kuwaambia kwamba ninyi wote mmelipwa, kelele iishe. Au ninyi wote mmelipwa, makaratasi ni haya, aliyelipwa ni huyu. Unajua tatizo kama hili ambalo linawagusa wananchi ni tatizo gumu inabidi kuwaelewesha kwa makini sana? Naomba tafadhali nijibiwe. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwamba kuna ulazima, kama malipo yamefanywa lakini bado yanaleta utata, kuna ulazima wa Serikali kukaa na wananchi wa Pande na kuzungumza nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maelezo ya msingi nilisema kwamba viongozi wa kijiji hapo hapo walipo na viongozi wa Kata na viongozi wa Wilaya walihusika moja kwa moja katika usimamizi wa malipo haya ya fidia yaliyofanywa ya mazao. Kwa hiyo mimi namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba atawasiliana na viongozi wa Wilaya, nitawaagiza watupe taarifa kamili ya tatizo husika ni nini. Kama ikilazimu mkono wa Serikali Kuu kuingilia kati suala hili basi naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Maeneo ambayo kuna mikataba ya kutafuta mafuta au gesi kama ilivyo kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Kigoma kule kuna vitalu vitatu na maeneo mbalimbali ya kusini. Mikataba ile haina vipengele vyta ni jinsi gani ambavyo Halmashauri za Wilaya ambazo ndani yake zitakutwa kuna mafuta au gesi zitafaidika na ile rasilimali, kama ilivyo kwa upande wa watu wa Madini ambao wanapata dola 200,000 kwa mwaka.

Serikali haioni kuna haja kuingiza vipengele hivi katika mikataba ya mafuta na gesi ili wananchi wa Wilaya ambazo gesi au mafuta yanapatikana waweze nao kufaidika na rasilimali zao kama ilivyo wananchi wa maeneo ya dhahabu?

**NAIBU SPIKA:** Ni swali lingine kabisa. Hili lilikuwa la fidia, lakini naomba tu kwa sababu ya umakini basi umjibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri hili suala limezungumziwa mara kadhaa humu humu Bungeni na nadhani Bunge lako Tukufu, Wizara ilipokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tunataka kulifanyia kazi. Lakini hili Mheshimiwa Zitto anatambua kwamba ni lazima lije kwenye mikataba hii mipyä ambayo itakuja katika *exploration*. Lakini pia itakopatikana gesi na mafuta kwa maeneo haya kama ya Mkuranga, kwa Adam Malima na hata hiyo Kilwa yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niseme kwamba kwenye utaratibu ambao haukuweka malipo haya kwa Halmashauri kwenye mikataba ya gesi lakini imo kwenye mikataba ya madini. Mimi nadhani kwamba utaratibu huu kama ukitumika kwenye gesi mimi naamini kwamba itakuwa imeenda sambamba tu kwa sababu ni

*activity ambazo zinafanyika kwenye Wilaya hiyo na Halmashauri hiyo na ingekuwa vyema pia kwamba wananchi husika wafaidike kwa gesi kama wanavyofaidika wananchi wa madini. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda tulioongeza unatokana na uwasilishaji wa Hati mbalimbali. Kwa hiyo, tumefidia muda ule pale. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha. Sasa tunao wageni. Wageni asilimia kubwa sana ni wa Mheshimiwa John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, amba ni viongozi waandamizi toka Wizara hiyo amba ni pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, alipo. Ahsante sana. (Makofi)

Kuna Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ndugu Alfayo Kidata. Tuna Kaimu Kamishna, Ndugu Mdenyi Ulomu. Tuna Msajili wa Hati, Ndugu Subira Sinda, Kaimu Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, Dr. Selasie Mayunga, Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), Ndugu Nehemia Msechu, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), Ndugu Kesogukewe Msita. Nafikiri tulikuona siku ile kwenye Semina. Tuna Kaimu Mkurugenzi Mipango Miji, Ndugu Martin Mhagama, Mkurugenzi wa Mifumo ya Habari, Ndugu Elias Nyabusani. Ahsante sana na karibuni sana. (Makofi)

Wengine ni Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, Ndugu Alois Mogofi, Mkurugenzi Msaidizi, Urasimishaji Makazi, Ndugu Sarah Kesi. Ndugu Sarah yuko upande huu huku. Mkurugenzi wa Nyumba, Profesa Tumsifu Nkya, Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, Ndugu Gerald Mango na Mkurugenzi Mkuu, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi, Dr. Godlakson Kawishe. Wote tunawakaribisheni sana, leo ni shughuli zenu hapa Bungeni basi mtasaidia Waziri ipasavyo. (Makofi)

Halafu tuna Makamishna na viongozi wengine 20 Waandamizi wa Wizara hiyo. Aidha, Mheshimiwa Waziri anao wageni wake amba siyo watumishi wa Serikali. Hao ni mke wake Bibi Gilena Chiligati. Ahsante sana kwa kumsaidia huyu Ndugu Chiligati kufanya kazi vizuri. (Makofi)

Tuna mdogo wake Mwalimu Chideni Chiligati. Tuna mjomba wake Gideon Palingo, tunaye shangazi yake Bibi Palingo. Tunaye mdogo wake Mwalimu Raphael Chiligati. Tunae Mjomba wake Mwalimu Dorika Uledi. Sasa wote wamekamilika, maana yake unapoomba kura za maoni basi hawa ndiyo nguvu. Ahsante. (Makofi)

Jumla tunao wanafunzi 22 pamoja na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Mwanzi, Manyoni amba wameongozana na Katibu wa Mbunge, Jimbo la Manyoni Mashariki. Katibu wa Mbunge yupo wapi? Sasa na wanafunzi wale 22 pamoja na walimu naomba wasimame walipo. Ahsanteni sana. Haya karibuni sana. Haya karibuni sana. (Makofi)

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja, ambao ni wanafunzi 20 na pia ni Wabunge kutoka Bunge la Shule ya Kibamba, wameambatana na walimu wafuataa:- Mwalimu Mkuu, Asia Mpate, yuko wapi? Ahsante Mwalimu Mkuu. Kuna Elizabeth Kimbe, Ndugu Ashura Waziri na Ndugu Margereth Mganga ni wanafunzi wa shule ya Kibamba, wasimame ambao ni Bunge hili lazima kutakuwa na Spika, kutakuwa na Naibu Spika hapa. Basi karibuni sana, tumefurahi kuwaoneni. Ahsante sana. (*Makofi*)

Halafu nina mtu mmoja ameletwa bila kuwa *Official* hapa. Mheshimiwa Waziri, Dr. John Pombe Magufuli, ana wageni wake wawili ambao wanatoka Mwanza. Hawa anasema pamoja na mambo mengine, wamekuja kuona shughuli za Bunge. (*Makofi*)

Lakini anasema wote hawa wanashughulika na masuala ya operesheni ya uvuvi haramu, Kanda ya Ziwa, Mwanza. Nao ni Bwana John Makongoro, wako wapi hawa. Wana harakati hawa na Bwana Mashauri Bayai. Anasema hawa wanashughulikia na masuala ya operesheni ya uvuvi haramu. Nadhani ni wanaharakati wa kuzuia huo uvuvi haramu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri aliyevaleni hapa ni mwanaharakati kabisa katika kupambana na hayo matatizo ya uvuvi haramu. Ahsanteni sana. Wageni wengine wote tunawakaribisha hapa Bungeni muwe huru kabisa, hili ni Bunge lenu na hawa Wabunge ni wawakilishi wenu. Siyo lazima utambulishwe hapa lakini basi wote mnakaribishwa sana. (*Makofi*)

Tunayo matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa leo tarehe 6 Julai, 2010 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika kuanzia saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 227. Hiyo ni Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo tarehe 6 Julai, 2010 kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao kitafanyika katika Ukumbi wa *Basement* hapa kwenye Ukumbi wa Bunge kuanzia saa 7.00 mchana. Wajumbe wote mnaombwa kukaribishwa na mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Masoud, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati leo tarehe 6 Julai, saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 231 jengo la Utawala. Hiyo ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Halafu Katibu wa Bunge anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote, kwenye Maonyesho ya 34 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yatakayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere. (*Makofi*)

Sasa nashangaa kwa sababu tarehe naziona zimeisha. Maonyesho haya yatafunguliwa rasmi na Mheshimiwa Luis Inasiyo Lula Da-Silva, Rais wa Brazil tarehe 7 Julai, 2010. Maana yake muondoke leo hii. Sasa nafikiri utaratibu umefanywa. (*Makofi*)

Sasa haya matangazo niliyotangaza haya wote wanafanya Semina yao saa 7.00. Lakini jana nimewatangazieni kwamba kutakuwa naSemina ya kuwasikiliza wenzetu ambao wasiosikia saa 7.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Sasa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wenyeiti kutangaza hivi mimi ningependa sana mkahudhurie ile semina. Kwa sababu mtawapa moyo mzuri sana wenzetu kuona kwamba tunajali, kuliko nyie wote mtawanyike kwenye Semina zenu halafu hawa wamekuja toka lini wanatusubiri sisi tuongee nao halafu tusionekane au tukahudhuria wachache siyo vizuri kufanya hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ningetamani sana kipindi cha kwanza baada ya saa 7.00 mchana tuwasikilize hawa wenzetu. Halafu baadaye muende kwenye semina zenu. Kwa hiyo, semina zote tulizotangaza zitaanza saa 8.00 mchana hivi na kuendelea kusudi tuwasikilize wale wenzetu katika Ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningefurahi sana kama Wenyeiti mkafanya maandalizi hayo, wakishakusanyika wajumbe wenu waende kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa kwenda kuwasikiliza wale watu. Ni nafasi yao ya pekee hawajawahi kupata nafasi nyingine kama hii. Kwa Waheshimiwa Wabunge nadhani tujali hilo.

Lakini kesho tarehe 7 Julai, 2010 saa 4.00 asubuhi kutakuwa na semina ya Sheria ya Ubua baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010. Ni ile sheria ya *The Public Private Partnership Act, 2010* na hivyo hivyo saa ngapi, mchana kuna wale wanaopiga shabaha, Chama cha Walenga Shabaha, watatakiwa kwenda Msalato huko. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtajipanga kufuatana na hali halisi. Katibu, tunaendelea na shughuli za leo.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka**

**wa Fedha 2010/2011 - Wizara ya Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza Rais Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi zake za kusimamia uchumi wa nchi yetu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais, na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kumsaidia vizuri Mheshimiwa Rais katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kunipatia ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya awamu ya nne ambapo kwa kushirikiana tumefanikisha miradi mingi ya maendeleo. Vilevile, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge katika Bunge lako Tukufu. Waheshimiwa hao ni Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, kutoka Chama cha Mapinduzi (*CCM*) na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kutoka Chama cha Wananchi (*CUF*). Vilevile, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Wabunge wenzetu na Watanzania wote waliopoteza maisha yao kutohana na sababu mbalimbali, Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Milenia (*MDGs*), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (**MKUKUTA**) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Lengo la msingi la miongozo hiyo ni kuboresha maisha ya wananchi; kudumisha amani, utulivu na umoja; kuimarisha utawala bora; kujenga uchumi madhubuti na endelevu; kuboresha afya; kutunza mazingira na kuboresha makazi. Wizara yangu imetekeliza miongozo hiyo kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, kutoa hatimiliki za kimila kwa wananchi wa vijiji na kutoa leseni za makazi kwa wananchi waishio kwenye maeneo yasiyopimwa ili kuwawezesha kukopesheka na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile Wizara yangu imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa Kitaifa pamoja na Bunge. Maagizo hayo yanayotokana na hotuba za bajeti, maswali na hoja za Waheshimiwa Wabunge na ahadi mbalimbali za viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 kwa kipindi cha Miaka Mitano (2005 – 2010). Wizara yangu imetekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, hususan ibara ya 42 vifungu (a-d) kuhusu ardhi; ibara ya 68 vifungu (a-h) kuhusu maendeleo ya makazi na ibara ya 108 kifungu (f) kuhusu sheria ya mabaraza ya ardhi na nyumba. Utekelezaji wa maelekezo ya ibara hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 42, kifungu (a); Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya benki na mifuko mingine ya fedha inayokopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kurasimisha ardhi na nyumba nchini iliendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Majiji, Miji, Wilaya, MKURABITA na wadau wengine. Kuanzia Januari 2006 hadi Mei 2010, milki za nyumba 301,961 zilitambuliwa kwenye maeneo yaliyojengwa bila kupimwa mijini. Milki hizo zilitambuliwa katika miji ya Mwanza (nyumba 25,929); Dar es Salaam (265,417), Tanga (3,945), Moshi (1,019) na Dodoma (5,651). Kati ya nyumba zilitambuliwa, jumla ya leseni za makazi 92,565 zilitolewa. Leseni hizo za makazi zinaweza kutumika kama dhamana kuombea mikopo kwenye taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliongeza kasi ya kupima mashamba na kutoa hatimiliki za kimila (*certificates of customary right of occupancy*). Kati ya mwaka 2005 na Juni 2010, jumla ya Masjala za Ardhi za Wilaya 25 na Masjala za Ardhi za Vijiji 182 zilikarabatiwa au kujengwa. Hatimiliki za kimila 111,905 zilitayarishwa, kusajiliwa na kutolewa kwa wananchi katika Wilaya mbalimbali nchini. Katika kipindi hicho, vyeti vyaa ardhi ya vijiji 4,227 katika Wilaya 60 za mfano vilisajiliwa na kutolewa, sawa na asilimia 46 ya vijiji vipatavyo 11,000 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 42, kifungu (b); Kuendeleza kwa nguvu mpya kazi inayofanywa na Halmashauri za Wilaya katika kutambua mipaka ya vijiji na kuvipatia vyeti vyaa kumiliki ardhi ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilikamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji 5,890 nchini vilivyokuwa havijapimwa. Idadi hiyo imekamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vyote nchini vipatavyo 11,000. Vilevile, katika kipindi hicho mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 705 katika Wilaya 48 iliandaliwa kuitia mipango shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 42, kifungu (c); Kuendelea kurahisisha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imefupisha muda wa upatikanaji wa hatimiliki, zilikuwa zinachukua zaidi ya mwaka mmoja kutolewa na imefikia lengo la kusajili ndani ya wastani wa siku 180 kama ilivyotamkwa kwenye sheria za ardhi. Hatua zilizochukuliwa kufupisha mchakato huo ni pamoja na kurekebisha taratibu na kuanzisha Ofisi za Ardhi za Kanda sita ambazo ni Mwanza, Dar es salaam, Moshi, Mbeya, Dodoma na hivi karibuni Mtwara. Katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Mei 2010, jumla ya hatimiliki 56,130 zilisajiliwa na kutolewa kwa wananchi. Kasi ya utayarishaji na usajili wa hati imeongezeka kutoka hatimiliki 5,464 ilivyokuwa mwaka 2005/06 na kufikia hatimiliki 17,390 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 42, kifungu: d (i); Kupima na kutayarisha ramani za msingi za nchi yetu kwa ajili ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utayarishaji wa ramani za msingi za nchi yetu uliendelea kwa lengo la kuwezesha mipango mbalimbali ya maendeleo kuandaliwa na kutekelezwa. Mipango hiyo ni pamoja na mipango kabambe ya miji, umwagiliaji, utalii, matumizi bora ya ardhi na mazingira. Katika kipindi kilichoanzia Desemba 2005 hadi Mei 2010, ramani za msingi za miji katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Kigoma, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya na Iringa zilitayarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 42, kifungu: d(ii); Kujenga uwezo wa kupata wataalam na vitendea kazi kwa ajili ya kupima na kutayarisha ramani za maeneo ya maji, maziwa na bahari kuititia Tangazo la Serikali Na. 467 la Desemba 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na taasisi za Kimataifa za haidrografia ambazo ni *International Hydrographic Organization (IHO)* na *United Kingdom Hydrographic Office (UKHO)* kwa kupatiwa ramani za majini (*hydrographic charts*) na taarifa zinazohusu usalama majini. Vilevile, ujenzi wa kituo cha kuratibu mawimbi Baharini (*tide gauge*) kando kando ya Bahari ya Hindi eneo la Mtwara ulikamilika. Kujengwa kwa kituo hiki kutusaidia kuratibu na kutoa taarifa mbalimbali muhimu zinazohusu hali ya bahari, kuongeza ukanda wa kiuchumi baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ibara ya 68, kifungu (c)*; Kuendelea kuimarisha utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuititia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*) iliboresha maabara yake kwa kufunga vifaa vipya vya kupima ubora ili kuwezesha upatikanaji wa matokeo bora ya utafiti. Wakala ulizalisha vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na vya gharama nafuu, na ilieneza matokeo ya tafiti zake katika Wilaya 40. Vilevile ultengeneza mashine 450 za kufyatulia matofali ya udongo na saruji yanayofungamana, mashine 110 za kutengenezea vigae vya kuezekea na kalibu (*moulds*) 120 za vigae hivyo. Kazi ya kuhamasisha, kutoa mafunzo, ukandarasi na ushauri wa kitaalam zilifanyika katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ibara ya 68, kifungu (d)*; Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuptitia *NHBRA* ilitoa mafunzo kwa vitendo na kufanya uhamasishaji kuhusu ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kujenga nyumba za mfano katika Mikoa 19 na Halmashauri za Miji na Wilaya 49. Kazi hizo zimewawezesha wananchi wengi kuanza kutumia teknolojia bora ya ujenzi inayotumia matofali ya udongo na saruji yanayofungamana. Pia, ushauri wa kitaalam na ukandarasi juu ya utumiaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora vilivyo fanyiwa utafiti, ulitolewa katika Wilaya mbalimbali. Wizara iliendelea kushirikiana na makampuni kutoka sekta binafsi kuwezeshe wa kuingizwa nchini teknolojia mpya ya vifaa vya ujenzi wa nyumba vya gharama nafuu. Kwa mfano, kampuni ya *Prairies Wind International* kutoka Marekani, *African Eco Housing* ya Uingereza na *P&P Developers Limited* ya Dubai walionyesha aina mbalimbali za vifaa vya ujenzi vyenye gharama nafuu.

Aidha, kampuni ya *INOVIDA* kutoka Ujerumani imejenga Dar es Salaam kiwanda cha kutengeneza vifaa vya ujenzi usiotumia saruji, nondo wala mbao kwa lengo la kujenga nyumba za bei nafuu, vifaa hivyo ndivyo vilivyo tumiwa kujenga jengo la Wizara la maonyesho ya Nane Nane hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ibara ya 68, kifungu (f)*; Kusimamia uanzishwaji wa taasisi za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kilichoanzia Disemba 2005 hadi Mei 2010 Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo (*Unit Titles Act*) ya mwaka 2008 na Sheria ya Mikopo ya Nyumba ya Mwaka 2008, zilitungwa. Kanuni kwa ajili ya kutekeleza sheria hizo zilikamilika na kuanza kutumika mwezi Mei, 2009. Kazi ya kutoa Elimu kwa umma kuhusu sheria hizo imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari. Pia, Serikali imeongeza rasilimali kwenye mfuko wa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba kwa watumishi wa serikali (*revolving housing loan fund*) ili uweze kuwanufaisha watumishi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ibara ya 68, kifungu (g)*; Shirika la Nyumba la Taifa kuendelea kujenga nyumba za makazi na za biashara kwa ajili ya kuza na kupangisha na kuzifanyia matengenezo zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010 Shirika la Taifa la Nyumba (*NHC*) liliweka msukumo zaidi katika ujenzi wa nyumba za kuza kuliko za kupangisha. Uamuzi huu unalenga kuwawezesha wananchi kumiliki nyumba zao wenye na hivyo kuzitumia kwa kupata mikopo ya kuendeshea maisha yao. Katika Kipindi husika, jumla ya nyumba na majengo 447 kwa ajili ya kupangisha na kuza yalijengwa katika miji mbalimbali nchini. Kati ya nyumba na majengo hayo, nyumba 236

ni kwa ajili ya kuuza na majengo makubwa ya vitega uchumi 211 yaliyengwa kwa ajili ya kupangisha (Angalia Jedwali Na. 3a & b).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010, jumla ya miradi 18 ilitekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Shirika na waendelezaji binafsi. Ujenzi huo unahusisha kuendeleza upya majengo machakavu yaliyopo katikati ya miji mikubwa ili kupendezesha miji kulingana na matumizi bora ya ardhi katika miji yetu. Kutokana na majengo hayo Shirika limejenga nyumba 280 za makazi. Pia, kwenye majengo haya zimejengwa sehemu za ofisi, maduka, vyumba vya hoteli, maghala na viwanda. Kutokana na kutekelezwa kwa miradi ya ujenzi wa majengo hayo, wananchi 1,052 walijiriwa kwenye nafasi mbalimbali zikiwemo za uhandisi, uchoraji, usimamizi na wafanyakazi katika maduka na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika liliendelea kukusanya kodi ya pango na malimbikizo yake pamoja na kuzifanyia matengenezo nyumba zilizo chini yake. Katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010, Shirika lilikusanya jumla ya shilingi bilioni 131.7 kutokana na kodi ya pango la nyumba na malimbikizo yake. Kwa kipindi hiki makusanyo ya kodi na malimbikizo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, mathalan mwaka 2005/06 zilikusanywa jumla ya shilingi bilioni 19.2 na mwaka 2009/10 zimekusanywa jumla ya shilingi bilioni 33. Kwa upande wa matengenezo, Shirika limekuwa likiyafanyia matengenezo majengo yake 2,332 nchini kote kulingana na mahitaji, umuhimu na uwezo wa Shirika kifedha. Kila mwaka shirika hutenga asilimia 25 ya mapato yake yanayotokana na kodi za pango kwa ajili ya kugharamia matengenezo. Katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010 jumla ya majengo 2,146 na nyumba (*apartments*) 14,679 zilifanyiwa matengenezo yaliyogharimu shilingi bilioni 34.8 katika miji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ibara ya 68, kifungu (h)*; Kuendeleza miradi ya kupima viwanja katika miji hasa kwenye Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Halmashauri za miji na wilaya katika kutekeleza miradi ya upimaji wa viwanja mijini. Katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Mei, 2010, Halmashauri za Miji 48 zilikopeshwa jumla ya shilingi bilioni 6.9 kupitia mfuko wa mzunguko wa kupima viwanja (*Plot Development Revolving Fund (PDRF)*) ambapo hadi Juni, 2010 jumla ya viwanja 25,094 vilipimwa. Hadi Juni 2010 Halmashauri 21 kati ya 42 zimerejesha jumla ya Shilingi 306,428,932.80 ikiwa ni pamoja na riba ya asilimia ishirini. Aidha, kupitia mradi wa Kupima Viwanja 20,000, jumla ya shilingi bilioni 3.3 zilikopeshwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kupima viwanja na kuwagawia wananchi. Katika kipindi kilichoanzia Julai 2006 hadi Mei 2010, Jumla ya viwanja 59,614 vimepimwa katika miji ifuatayo: Jiji la Dar es Salaam (41,000); Mwanza (10,000), Morogoro (2,764), Mbeya (2,350), Kibaha (500) na Bagamoyo (3,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ibara ya 108, kifungu (h)*; Kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hususan Ujenzi wa Majengo ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Ngazi za Wilaya na kuajiri Mahakimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kilichoanzia Julai, 2006 hadi Aprili 2010, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 16 yaliundwa na Wenyeviti 29 walijiriwa. Katika kipindi hicho jumla ya mashauri 40,287 yalifunguliwa na mashauri 26,865 yalisikilizwa na kuamuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2009/10 na Malengo ya Mwaka 2010/11, Ukusanyaji wa Mapato, Wizara yangu ina jukumu la kukusanya ada mbalimbali zinazotozwa kupitia umiliki wa ardhi. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi 15,550,006,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2010, jumla ya shilingi 11,642,119,118.98 ambazo ni sawa na asilimia 75 ya lengo zimekusanywa. Kati ya makusanyo hayo, shilingi 10,430,902,549 ambazo ni sawa na asilimia 90 ya makusanyo ni kodi ya pango la ardhi itokanayo na viwanja na mashamba. Upungufu wa makusanyo ya maduhuli umetokana na udhaifu uliopo katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/11, Wizara ina lengo la kukusanya kiasi cha shilingi 20,641,200,000. Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo:- kukijengea uwezo kitengo cha ukusanyaji wa maduhuli; kuhakikisha kila mmiliki wa kiwanja analipa kodi stahili kulingana na matumizi yake; kuboresha kumbukumbu za ardhi; kuongeza wigo wa walipa kodi ya ardhi kwa kupima viwanja na kukamilisha upimaji katika maeneo mbalimbali, kuelimisha wananchi juu ya wajibu wao wa kulipa kodi ya ardhi kila mwaka; kurahisisha utaratibu wa malipo; kujenga kituo cha huduma kwa wateja; kuhakikisha huduma zinapatikana pale zinapohitajika ikiwa ni pamoja na ramani kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kufuutilia kwa karibu vituo vya makusanyo ili kudhibiti mapato kwa mujibu wa sheria za fedha. Natoa wito kwa wamiliki wa ardhi nchini kulipa kodi za pango la ardhi na ada zingine kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 33,483,299,000. Kati ya fedha hizo shilingi 5,962,158,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 15,507,598,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 12,013,543,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Juni 2010 jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 26,261,423,816. Kati ya fedha hizo, shilingi 11,952,752,127 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 5,950,436,058 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 8,358,235,631 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Juni 2010, kiasi kilichotumika ni shilingi 25,963,529,778.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya ardhi. Ardhi ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi wa nchi na ni muhimili wa shughuli mbalimbali mijini na vijiji. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Wizara yangu inaendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi kwa lengo la kuimarisha uhakika na usalama wa milki. Huduma hizo ni pamoja na kutoa hatimiliki za ardhi, kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma na kutatua migogoro ya ardhi kiutawala.

Aidha, Wizara inashughulikia uhamasishaji wa uanzishaji wa masjala za ardhi za Wilaya na Vijiji kwa lengo la kusajili na kuhifadhi vyeti vya ardhi ya kijiji, hatimiliki za kimila, pamoja na kutoa elimu ya sheria za ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji milki, mchakato wa kuandaa hatimiliki za ardhi unaanzia kwenye ngazi za Halmashauri za Jiji, Miji na Wilaya na kwa sasa unaishia katika ofisi za Kanda. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ililenga kutoa hatimiliki 20,000 ambapo lengo hili lilivukwa kwa kutoa hatimiliki 22,491. Ningependa kuzipongeza Halmashauri ambazo zimeonyesha juhudini kubwa za kuandaa hatimiliki katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri hizo ni:- Jiji la Mwanza, Manispaa za Kinondoni, Ilala, Arusha na Arumeru. Pongezi hizi pia ziwaendee, Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa Mikoa na Wilaya kwa kuhimiza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu iliahidi kufungua ofisi ya ardhi, Kanda ya Kusini Mashariki, Mjini Mtwara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ofisi ya ardhi ya Kanda ya Kusini Mashariki Mjini Mtwara tayari imefunguliwa na imepatiwa watumishi na vitendea kazi, na imeanza kutoa huduma, hivyo kufikisha kanda sita. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu itafungua ofisi ya ardhi ya Kanda ya Magharibi Mjini Tabora itakayohudumia Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Kigoma. Natoa wito kwa wananchi, viongozi na watendaji wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri waendelee kutoa ushirikiano na kuhakikisha kuwa ofisi hizo zinatoa huduma kwa wananchi bila usumbufu na ucheleweshaji kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi na Uhakiki wa Milki, katika kipindi hiki Wizara yangu iliendelea na utatuzi wa migogoro ya ardhi na kushughulikia kero mbalimbali za wananchi kuhusu ardhi. Migogoro ya aina hiyo ilitatuliwa kwa njia za kiutawala na iliposhindikana wahusika walishauriwa kwenda kutafuta haki zao mahakamani. Migogoro hiyo inatokana na wananchi kughushi nyaraka za umiliki, ugawaji wa kiwanja kwa zaidi ya mtu mmoja, wamiliki wa asili kutokulipwa fidia, na wananchi wenye milki halali kuacha kuendeleza viwanja walivyomilikishwa kwa wakati. Wizara imeimarisha matumizi ya tecknolojia ya kompyuta katika uandaaji wa hati na utunzaji wa kumbukumbu za miliki ya viwanja ili kupunguza migogoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, jumla ya milki 4,500 zilihakikiwa na kukaguliwa katika maeneo ya Mbezi, Jangwani Beach, Tegeta, Ununio na Boko Jijini Dar es Salaam. Kutokana na uhakiki huo nyaraka mpya za umiliki kwa viwanja 4,098 kati ya 5,000 vilivyokusudiwa zilitolewa. Zoezi la uhakiki katika maeneo haya limehusisha kuweka miundombinu ya barabara zenye urefu wa kilometra 50.8. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu itakamilisha uhakiki na ukaguzi wa milki za viwanja 4,018 zilizobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa tahadhari kwa wananchi wanaonunua ardhi katika maeneo hayo wahakikishe kuwa milki hizo zimehakikiwa na Wizara kabla ya kufanya maamuzi ya malipo ili kuepuka hasara inayoweza kupatikana kutokana na udanganyifu. Aidha, nawaarifu wamiliki wote wa viwanja katika maeneo hayo ambao hawajawasilisha nyaraka za umiliki wa ardhi, wawasilishe Wizarani nyaraka hizo kwa

ajili ya uhakiki na kupatiwa nyaraka mpya kwa vile zoezi hili litakamilika mwaka wa fedha 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utwaaji na ubatilishaji Milki. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi na sheria za ardhi kila mwananchi anayemilikishwa ardhi anawajibu wa kulinda mipaka ya ardhi yake, kuiendeleza na kulipa kodi ya pango la ardhi. Mwananchi anayeshindwa kutekeleza masharti hayo serikali ina haki ya kubatilisha umiliki wake kwa mujibu wa sheria za nchi. Aidha, ardhi inapohitajika kwa manufaa ya umma hutwaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji wa Ardhi Na. 7, 1967 (Sura Na. 118). Katika mwaka wa fedha 2009/10 milki za wananchi 52 zilitwaliwa na kubatilishwa. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kushughulikia utwaaji na ubatilisho wa milki za wananchi wanaoshindwa kutekeleza masharti ya uendelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ilitoa vibali vya uhamisho wa milki 351 na rehani 98 kati ya lengo la kutoa vibali vya kuweka rehani na uhamisho kwa miliki 400 katika jiji la Dar es Salaam. Vilevile kazi hizo ziliendelea kutekelezwa kwenye Halmashauri nchini. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inakusudia kushughulikia na kutoa vibali vya kuweka rehani na uhamisho kwa milki 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5, 1999 (Sura 114), katika Wilaya zilizochaguliwa kutekeleza miradi ya mfano, Wilaya hizo ni Babati, Bariadi, Namtumbo na Manyoni. Utekelezaji wa miradi hiyo una lengo la kuhakikisha mipaka ya vijiji imepimwa na kupatiwa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji (*Certificates of Village Land*), kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi, kupima na kumilikisha mashamba ya wananchi kwa kuwapatia Hati za Hakimiliki ya Kimila (*Certificates of Customary Right of Occupancy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara iliahidi kujenga masjala za ardhi za vijiji 92 na masjala za ardhi za Wilaya 15 na kusajili hatimiliki za kimila 100,000. Nafurahi kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Juni, 2010 jumla ya masjala za wilaya 15 na za vijiji 61 zilijengwa au kukarabatiwa kwa kushirikiana na Halmashauri, Ofisi ya Rais (MKURABITA) na wadau mbalimbali wa ardhi. Jumla ya vyeti vya ardhi ya vijiji 3,296 na hatimiliki 93,400 zilisajiliwa na kutolewa kwa wananchi katika Wilaya za Babati, Bariadi, Namtumbo na Manyoni (Angalia Jedwali Na. 4). Kwa mwaka wa fedha 2010/11 Wizara itasimamia uandaaji na usajili wa vyeti vya ardhi ya vijiji 5,000; hatimiliki za kimila zipatazo 138,000 katika vijiji 138 vilivyosalia kwenye Wilaya za mfano za Babati na Bariadi na vijiji vingine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa umma. Katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau mbalimbali iliendelea kutoa elimu ya sera na sheria zinazohusu majukumu ya sekta ya ardhi. Elimu hiyo ilitolewa kuititia vyombo vya habari ambavyo ni redio, televisheni, pia kuititia ushiriki katika maonesho ya wiki ya utumishi wa umma na nane nane.

Aidha, Wizara ilikamilisha utayarishaji wa mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kuchapisha nakala 5,000. Mwongozo huo utatumika kutoa elimu kwa umma katika ngazi za vijiji wakati wa maandalizi ya kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itachapisha nakala za mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kutoa elimu kwa umma kuhusu sera na sheria zinazosimamia sekta ya ardhi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilijiwekea lengo la kusajili hati za kumiliki ardhi pamoja na nyaraka za kisheria zipatazo 42,000. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa lengo hilo limevukwa kwa kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria 45,559. Kati ya hizo hatimiliki 17,390 pamoja na nyaraka 18,974 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334 (Angalia Jedwali Na. 5a); Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria Sura Na. 117 ni 8,275, Sura Na. 210 ni 920 (Angalia Jedwali Na. 5b). Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara ina lengo la kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria 50,000. Kati ya hizo 20,000 ni hatimiliki na 30,000 ni nyaraka za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilikuwa na lengo la kufanya marekebisho ya Sheria za Usajili wa Hati (Sura ya 334) na Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) ili kuboresha shughuli za usajili. Mtaalam Mwelekezi aliyeteuliwa kufanya utafiti na kutoa mapendekezo ya namna ya kuimarisha mchakato wa usajili wa hati na utunzaji wa kumbukumbu pamoja na marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334) amekwishawasilisha mapendekezo yake. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara yangu itaanzisha mfumo wa usajili wa elektroniki (*Land Registration System*) utakaoboresha uwekaji kumbukumbu na kufanya marekebisho sheria ya usajili wa ardhi (Sura 334) ili iendane na wakati. Vilevile, Wizara itaanzisha Ofisi ya Msajili wa Hati Kanda ya Tabora ili kupeleka huduma karibu na wananchi ambao hivi sasa wanapata huduma katika ofisi iliyopo Mwanza. Kanda hiyo mpya itahudumia Mikoa ya Tabora, Kigoma na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uthamini wa mali. Wizara yangu iliendelea na kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuthamini nyumba na mali nyinginezo kwa ajili ya kulipa fidia, kutoza kodi ya ardhi, mauzo (*transfer*), mizania (*balance sheet*) kuomba mikopo, mirathi na bima. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ililenga kufanya uthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa nyumba na mali nyinginezo 10,000. Hadi Juni 2010 jumla ya nyumba na mali nyingine 7,386 zilithaminiwa na kuidhinishwa.

Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inakusudia kufanya uthamini na kuidhinisha taarifa zipatazo 12,000. Vilevile, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010 niliahidi kutayarisha rasimu ya sheria ya kusimamia kazi za uthamini (*Valuation Bill*) na Sheria ya Wakala wa Milki (*Real Estate Agency*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Miswada hiyo imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa katika Mkutano ujao wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya fidia, hupatikana kwa kuzingatia mahali ardhi ilipo, maendelezo na gharama zingine na uthamini wake hufanyika kulingana na matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Hata hivyo, Wizara imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wanaolazimika kuachia maeneo yao kwa ajili ya kuruhusu uendelezaji wa maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali za kiserikali na hata uwekezaji binafsi. Malalamiko hayo ni kuhusu kiwango duni cha fidia kinachotolewa. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara imefanya utafiti wa gharama za fidia za mazao na ardhi katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kufanya tafiti katika mikoa iliyobaki ili kuwa na mwongozo wa viwango vya fidia unaozingatia gharama halisi za soko kwa lengo la kuboresha viwango vya fidia na kumaliza malalamiko ya wananchi kuhusu suala la fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Hazina ya Ardhi (*Land Bank*). Wizara yangu iliendelea kuratibu uanzishwaji wa Hazina ya Ardhi (*Land Bank*) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kuwepo kwa Hazina ya Ardhi ni sehemu muhimu ya kuwezesha uwekaji wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii, maendeleo ya Miji na utekelezaji wa kaulimbiu ya Kitaifa ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 uhakiki na ukaguzi wa mashamba 72 yaliyotelekezwa na wawekezaji ulifanyika katika Mkoa wa Morogoro wa mashamba matano. Taratibu za kufuta milki za mashamba hayo zinaendelea ili yaweze kugawiwa kwa wawekezaji wa ndani na nje ili yatumike kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya itafanya uhakiki wa mashamba yote nchini yaliyotelekezwa na kuyaandalia mipango mipy ya uendelezaji. Kwa upande wa viwanja mijini, Wizara itashirikiana na Halmashauri zenye mahitaji makubwa ya uwekezaji kupima viwanja kwa ajili hiyo. Naendelea kusisitiza kuwa ardhi itakayoingizwa kwenye Hazina ya Ardhi itakuwa imeandalisha mipango ya matumizi ya ardhi yenye kuzingatia maslahi ya wanavijiji na sharti ipimwe. Hivyo, ardhi hiyo haitahusisha mashamba ya wanavijiji na haitaathiri mahitaji ya baadaye ya ardhi kwa wanavijiji. Natoa wito kwa Halmashauri za Miji na Wilaya nchini kuendelea na uhakiki wa mashamba yaliyotelekezwa kwa kutuma ilani kwa wamiliki wake na kuwasilisha mapendekezo ya ufutaji wa milki. Kwa upande wa mijini, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji itaendelea kupima viwanja kwa ajili ya matumizi mbalimbali kulingana na mahitaji ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kumbukumbu za Ardhi na Mawasiliano. Katika kipindi hiki Wizara iliendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha kumbukumbu za ardhi kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi, mifumo ya habari na mawasiliano. Wizara iliendelea kuhifadhi kumbukumbu za viwanja na mashamba kwa kutumia mfumo wa kompyuta wa *Management of Land Information System (MOLIS)* na kukadiria kodi za ardhi kwa kutumia mfumo wa *Land Rent Management System (LRMS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, ofisi za ardhi katika Halmashauri nane za Kilombero, Bunda, Arusha, Mufindi, Geita, Moshi, Nzega na Bagamoyo zilipatiwa mafunzo ya kutumia mfumo wa kukadiria kodi na kuimarisha kumbukumbu kwa kutumia kompyuta. Kutokana na juhudhi hizo, hadi kufikia Mei 2010, jumla ya kumbukumbu za wamiliki 32,301 zilihifadhiwa katika kompyuta. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara yangu ina mkakati wa kuziwezesha Halmashauri zingine nane kuweka mfumo wa kompyuta wa kukadiria kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, tafiti mbili zenyenye lengo la kuboresha huduma kwenye sekta ya Ardhi zilifanyika, tafiti hizo zilihusu utoaji wa huduma katika ofisi ya Msajili wa Hati (*needs assessment for the registry of titles*) iliyofanywa na kampuni ya SwedSurvey ya Sweden kwa kushirikiana na *International Land System (ILS)* ya Marekani; huduma katika ofisi ya Kamishna wa Ardhi (*systems reform in the office of the Commissioner for Lands*) iliyofanywa na kampuni ya kizalendo ya *InfoBridge Consultants Limited*. Madhumuni ya tafiti hizo ni kuwa na mfumo mmoja wa kumbukumbu za ardhi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2010/2011 mapendekezo ya tafiti hizo mbili yatafanyiwa kazi kwa lengo la kuwa na mfumo mmoja utakaorahisisha utoaji wa huduma katika sekta ya Ardhi (*integrated database system*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara iliendelea kuboresha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 39 yaliyoanzishwa kwa kuyapatia watumishi na magari Mabaraza 21 yaliyopo katika Makao Makuu ya Mikoa. Katika kipindi hicho, watumishi 38 wa kada mbali mbali walijiriwa. Aidha, ofisi za Mabaraza tisa za Wilaya ya Temeke, Ilala, Kinondoni, Songea, Morogoro, Kigoma, Musoma, Mtwara na Mwanza zilifanyiwa ukarabati. Vilevile katika kipindi hicho, jumla ya mashauri 9,219 yalifunguliwa, kati ya hayo mashauri 7,756 yalamuliwa na 12,735 yanaendelea kushughulikiwa (Angalia Jedwali Na. 6). Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaanzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya za Nzega, Kilosa, Manyoni na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa mabaraza haya unakwenda kwa kasi ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti. Mabaraza yenye mashauri mengi yataongezewa idadi ya vikao kutoka viwili hadi vitatu kwa wiki kwa lengo la kupunguza mlundikano wa kesi. Aidha, posho ya Wazee wa Baraza itaongezwa kutoka shilingi 20,000 kwa siku za kikao za sasa hadi shilingi 30,000 kwa kikao kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilipitia upya mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba, na kuchunguza chanzo cha migogoro kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi katika Mabaraza katika ngazi ya Wilaya. Wizara pia iliendelea kutoa Elimu kwa umma juu ya Sheria Namba 2 ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ya Mwaka 2002 (*The Land Disputes Courts Act, 2002*) kuitia vyombo vyaa habari, katika maonesho ya wakulima na wiki ya Utumishi wa umma. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya itaendelea kutoa elimu juu ya Sheria Namba 2 ya mwaka 2002 katika ngazi za Wilaya, Kata hadi Vijijini. Elimu

itakayotolewa itawajengea uwezo wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili waweze kutoa haki kwa wananchi katika migogoro wanayoshughulikia. Uelewa wa sheria hii utawapunguzia wananchi usumbufu katika kutafuta haki zao na hivyo kuelekeza nguvu zao katika shuguli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za upimaji na ramani. Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa majukumu ya kusimamia upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi nchini. Upimaji ardhi huwezesha kupata vipimo, ukubwa na mipaka ya vipande vya ardhi, taarifa na takwimu ambazo ni msingi wa usimamizi wa ardhi katika sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utayarishaji wa Ramani, katika mwaka 2009/10 wizara iliahidi kukamilisha uhakiki na utayarishaji wa ramani za vitalu vya Kagera, Kigoma, Musoma na Mbeya na Miji 10 ya Kanda ya Magaharibi. Kazi hiyo ilikamilika katika vitalu vya Kigoma, Musoma, Songea na Mbeya. Kazi ya utayarishaji wa ramani katika kitalu cha Kagera inaendelea. Kazi zingine zilizotekelizwa ni upimaji picha (*ground photo control*) na uhakiki ardhini kwa ajili ya utayarishaji wa ramani za msingi katika Miji 15 ya Kanda ya Kaskazini Mashariki inayohusisha Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uhakiki ardhini katika vitalu vya Kigoma na Ruvuma ulikamilika na utayarishaji wa ramani ya Wilaya ya Nzega katika uwiano wa 1:350,000 unaendelea. Kwa mwaka 2010/11, Wizara itatumia picha za anga (*satellite imagery*) kwa ajili ya kuhuisha ramani za msingi za uwiano wa 1:2,500 katika miji kumi (10) ya Kanda ya Magharibi inayohusisha Mikoa ya Mbeya, Tabora, Rukwa na Kigoma. Pia, uchapaji wa ramani utaboreshwaa kwa kufunga mtambo mpya wa kisasa wenyekutoa ramani zenye ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaanza kujenga kituo cha kupokelea picha za Satilaiti (*Direct Satellite Receiving Station*) Mjini Dodoma. Kujengwa kwa kituo hiki kutarahisisha upatikanaji wa takwimu za ardhi na ramani mbalimbali ambazo zitatumika kutayarisha mipango ya maendeleo ikiwemo ya upimaji wa mashamba ya wananchi. Picha za *satellite* zitatumika pia na vyombo vya ulinzi na usalama, utabiri wa hali ya hewa na utengaji wa maeneo katika zoezi lijalo la sensa ya watu. Aidha, Serikali itaongeza mapato yatokanayo na kuuzwa kwa picha za *satellite* katika nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea na mchakato wa kujenga alama za mtandao mpya wa alama za msingi za upimaji ardhi (*National Geodetic Control Network*). Mtandao huu utapunguza gharama za upimaji wa ardhi na kuwawezesha wananchi wengi kupimiwa mashamba yao. Katika mwaka 2009/10, Wizara iliahidi kusimika alama 300 za msingi za upimaji ardhi ambapo hadi kufikia Juni, 2010 jumla ya alama za msingi 387 zimesimikwa nchini. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itasimika na kupima alama nyingine 300 katika Wilaya mbalimbali nchini hususan Kanda ya Kusini na Kusini Magharibi mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sera ya Upimaji na Ramani. Katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2008/2009 nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ilikuwa imeanza kuandaa Sera ya Taifa ya Upimaji na Ramani na ilitarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2009/2010. Hadi Juni, 2010 rasimu ya sera hiyo iliwasilishwa kwa wadau na hivi sasa inaendelea kufanyiwa maboresho kwa kuzingatia michango iliyotolewa na wadau. Matarajio ya Wizara ni kuhakikisha kuwa sera hiyo inakamilishwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipaka ya ndani ya nchi. Wizara yangu inalo jukumu la kutafsiri mipaka ya Vijiji, Wilaya na Mikoa kwa mujibu wa matangazo husika ya Serikali (*Government Notices*). Uzoefu unaonyesha kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya mipaka hiyo ni wananchi katika baadhi na vijiji na wilaya kutotambua mipaka iliyowekwa rasmi na kutafsiriwa kwenye matangazo ya serikali (*GN*).

Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri, Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliveza kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala kati ya Halmashauri ya Geita na Hifadhi ya Msitu wa Geita; Kijiji cha Shume Magamba na Hifadhi ya Msitu wa Shume Magamba; kati ya vijiji na Hifadhi za Taifa za Mikumi, Selous na Serengeti, pia, kati ya wilaya ya Sikonge na Manyoni kwa kutafsiri *GN* za mipaka hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kushirikiana na TAMISEMI na Maliasili na Utalii kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa mipaka ya Kimataifa unafanywa kwa ushirikiano kati ya nchi zinazopakana. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilipanga kuhakiki na kuongeza alama za mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imeanza kutekelezwa katika eneo la nchi kavu katika Ziwa Nyasa kwenye makutano ya Mito Misinje na Ruvuma kwa kukagua alama za mipaka zilizoharibika na kuzijenga upya na kuongeza alama zingine za mpaka mahali ambapo alama hizo ziko mbali. Vilevile, mikutano ya kujadili mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani za Msumbiji, Shelia, Comoro na Kenya ilifanyika. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, kazi ya kuhakiki, kukarabati na kuongeza alama zingine za mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji; na Tanzania na Kenya itatekelezwa. Aidha, mazungumzo ya mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa yatafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upimaji wa Mipaka ya Vijiji, Maendeleo nchini yataletwa baada ya kila kipande cha ardhi kutambuliwa, kupimwa mipaka yake na kumilikishwa kwa mmiliki mmoja mmoja au vikundi. Umilikishaji huo unategemea kutambuliwa kwa mipaka kati ya kijiji na kijiji. Katika mwaka 2009/10, Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya vijiji 1,500 vilivyokuwa havijapimwa nchini. Hadi Juni, 2010 vijiji vyote 1,604 vilikuwa vimepimwa katika Mikoa ya Kilimanjaro (93), Singida (316), Mara (351), Mwanza (33), Kagera (284), Kigoma (21), Tabora (127), Shinyanga (243), Dodoma (54), Manyara (5) na Morogoro (87) (Angalia Jedwali Na. 7). Kwa mwaka wa

fedha 2010/11, Wizara itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji vipyta 300 vilivyoongezeka mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji wa Ardhi chini ya Maji, moja ya jukumu la Wizara ni upimaji wa ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani zinazoonyesha umbile la ardhi iliyo chini ya maji hususan milima, mabonde, miinuko na kina cha maji. Ramani hizi hutumika kuongozea vyombo vya majini na matumizi mengine. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilijenga kituo cha kuratibu mawimbi Baharini (*tide gauge*) kando kando ya Bahari ya Hindi eneo la Mtwara. Kujengwa kwa kituo hiki kutasaidia kuratibu na kutoa taarifa mbalimbali muhimu zinazohusu hali ya Bahari (*early warning system*).

Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa ya Hydrografia itaendelea kujenga uwezo wa kupima ndani ya maji kwa kuwasomesha wataalam na kuimarisha kituo cha kuratibu mawimbi Baharini cha Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilikamilisha andiko la awali la kuongeza ukanda wa kiuchumi Baharini (*Exclusive Economic Zone*) na kuliwasilisha Umoja wa Mataifa tarehe 13 Mei, 2009. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itakamilisha andiko la kuongeza ukanda wa kiuchumi Baharini na kuliwasilisha rasmi kwenye Umoja wa Mataifa. Tanzania ilipewa tarehe ya mwisho kuwasilisha andiko kamili kuwa 13 Mei, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upimaji wa Viwanja na Mashamba, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliidhinisha upimaji wa viwanja 37,820 na mashamba 609 kati ya lengo la viwanja vипатавы 35,000 na mashamba 1,000 kwa mwaka (Angalia Jedwali Na. 8). Aidha, katika juhudzi za kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, jumla ya ramani za viwanja 15,116 zimepigwa picha (*scanned*) na kuhifadhiwa kwenye mfumo wa elektroniki. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara inatarajia kuidhinisha upimaji wa viwanja 50,000 na mashamba 100 kutoka Halmashauri mbalimbali nchini na kuendeleza kazi ya kupiga picha (*scanning*) ramani za viwanja na mashamba.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu kuwa mwaka 2009/2010, Wizara ingekasimu madaraka ya kusimamia na kuidhinisha upimaji viwanja na mashamba katika ngazi za kanda. Wizara imekamilisha tathmini ya mahitaji na maandalizi ya kukasimu mamlaka ya kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba katika ngazi za kanda. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itakasimu mamlaka ya kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba katika kanda sita (6) za sekta ya ardhi ambazo ni Kanda ya Kati (Dodoma), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kaskazini (Moshi), Ziwa (Mwanza), Kusini Mashariki (Mtwara) na Magharibi (Tabora). Ili kufanikisha azma hiyo, wataalam wa upimaji na ramani wenye sifa zinazotambulika na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi (*National Council of Professional Surveyors*) watahitajika sana kwa ajili

ya kukagua kazi zote za upimaji ardhi kabla ya kuziwasilisha kwenye ofisi za kanda kwa ajili ya kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itatoa kipaumbele katika kuboresha kumbukumbu za ardhi zikiwemo za upimaji wa ardhi ambazo zinaongezeka kila siku kutokana na uzalishaji wa viwanja vipyta. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Wizara imepanga kuanzisha mfumo mpya wa kielekitroniki wa utunzaji kumbukumbu za upimaji ardhi (*Cadastral Survey Information System*) utakaowezesha upatikanaji wa taarifa za ardhi kwa urahisi na kuboresha utoaji wa huduma za upimaji ardhi nchini. Mfumo huu utaunganisha shughuli zote za utoaji huduma za ardhi makao makuu, ofisi za Kanda, Mikoa na Halmashauri za Miji na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango ya Miji na Vijiji, upangaji na usimamiaji wa uendelezaji wa miji na vijiji hapa nchini hufanyika kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na Sheria zinazohusika na uendelezaji wa miji. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007, Sheria ya kusimamia taaluma za maafisa mipango miji Na. 7 ya mwaka 2007 na Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 pamoja na miongozo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji Miji, idadi ya watu wanaoishi mijini nchini imeongezeka kutoka 786,567 (sawa na asilimia sita) mwaka 1967, hadi 7,943,561 (sawa na asilimia 23.1) mwaka 2002 na inakadiriwa kufikia watu 12,000,000 (sawa na asilimia 30) mwaka 2010. Idadi hiyo inatarajiwaa kufikia zaidi ya watu 30, 000,000 (sawa na asilimia 50) ifikapo mwaka 2025. Kasi hiyo, kubwa ya ongezeko la watu mijini ni changamoto kwa mamlaka za upangaji miji kukidhi mahitaji ya msingi kwa watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upangaji wa Miji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na miji huandaa mipango ya jumla (*General Planning Schemes*) ya aina mbili ya kuongoza uendelezaji wake. Mipango hiyo ni ile ya muda mrefu (*master plans*) ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji kwa miaka ishirini na mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi ambayo ni ya miaka kumi. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Mbarali, Manyoni, Kahama na Isaka ilikamilisha mipango ya muda mfupi. Aidha, mipango kabambe ya Jiji la Tanga na Mji wa Bagamoyo inaendelea kuandaliwa. Kwa mwaka 2010/11, wizara itaandaa mipango ya muda mfupi ya miji ya Misenyi, Geita na kuhuisha mpango wa Makambako. Vilevile, uhuishaji wa mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali pia huandaa mipango ya uendelezaji upya maeneo mbalimbali ya miji (*Redevelopment Schemes*). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Mpango wa uendelezaji upya eneo la kati la Manispaa ya Temeke ulikamilika. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Songea itakamilisha mpango

wa uendelezaji upya eneo la kati na kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni itaandaa mpango wa uendelezaji upya eneo la Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kupanua ukubwa wa eneo la Bandari ya Dar es Salaam, ili liweze kuhudumia mizigo mingi zaidi, eneo la Kurasini lilipangwa na kutengwa ili liweze kutoa huduma zinazoendana na shughuli za bandari. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilithamini na kuhakiki mali 191 na kulipa fidia ya kiasi cha shilingi bilioni sita kwa wananchi wa Mtaa wa Mivinjeni ili kupisha upanuzi wa bandari, wananchi hawa walipewa viwanja mbadala eneo la Kibada. Kutokana na ulipaji wa fidia hiyo eneo huru lenye ukubwa wa ekari 8.7 lilipatikana na kupimwa viwanja vikubwa kwa ajili ya matumizi yanayoendana na shughuli za bandari. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kazi ya ulipaji wa fidia, upimaji wa viwanja na umilikishaji wa eneo lenye jumla ya ekari 21 utatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Urasimishaji, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura Na. 113 na Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya 2007 zinaelekeza kurasimisha maeneo yaliyojengwa bila kupimwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilishirikiana na Jiji la Mwanza kutambua miliki 19,876 katika maeneo yaliyojengwa bila kupimwa na kuandaliwa mipango ya urasimishaji. Kupitia mradi wa urasimishaji unaotekelawa Jijini Mwanza jumla ya viwanja takribani 7,000 vimepimwa na hati 518 kuandaliwa na wananchi 135 walimilikishwa kwa kupatiwa hatimiliki.

Vilevile, mpango wa urasimishaji wa maeneo katika Jiji la Dar es Salaam uliandaliwa ambapo viwanja 1,057 vilipimwa. Katika mwaka wa fedha 2010/11, Wizara, itakamilisha Programu ya Taifa ya Kuzuia Ujenzi Holela na Kurasimisha Makazi. Programu hii ni dira ya kuzuia ujenzi holela na kuboresha makazi holela nchini. Vilevile, kwa kushirikiana na MKURABITA itaendelea na kazi ya kurasimisha milki katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango ya Uendelezaji Vituo vya huduma na Miji mipyä, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam iliendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa watu na magari katikati ya Jiji kwa kuanzisha vituo vya huduma za jamii katika maeneo ya pembezoni (*satellite centres*). Katika mwaka wa fedha 2009/10, jumla ya wakazi 259 walilipwa fidia katika eneo la Luguruni na kutengewa viwanja mbadala 1,110 huko Kwembe Kati watakapohamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaendelea kuendeleza Kituo cha Huduma cha Luguruni kwa kushirikiana na Mwendelezaji Mkuu Mshiriki (*Co-master Developer*) na kuandaa mipango ya maeneo ya Vyuo Vikuu ambavyo vina uhitaji mkubwa wa ardhi kama Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*Institute of Finance Management*) huko Bunju, pamoja na Chuo cha Tiba ya Afya Muhibili huko Mloganzila - Kwembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, mchakato wa kuanzisha mji mpya wa Kigamboni uliendelea ambapo Mpango Kabambe wa mji huo sasa ulikamilika. Mpango huo unaohusisha eneo la hekta 6,400 umeainisha matumizi mbalimbali yakiwemo ardhi ya makazi, biashara, viwanda, utalii na burudani. Matumizi mengine ni shughuli za taasisi za Serikali, miundombinu, michezo, maeneo ya wazi (*open spaces*) na huduma za jamii. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaratibu kuundwa kwa mamlaka maalum itakayosimamia utekelezaji wa ujenzi wa mji mpya. Vilevile wananchi wa Kigoma wataelimishwa na kushirikisha katika kila hatua ya utekelezaji wa hiyo *master plan* katika eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uandaaji Mipango ya Uendelezaji Vijiji. Wizara yangu iliendelea kuratibu kazi za uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji mbalimbali nchini. Lengo ni kuziwezesha mamlaka (Halmashauri za Wilaya) kupanga, kuidhinisha, kutekeleza, kufuatilia na kuhuisha mipango ya kina ya makazi katika maeneo yao ya utawala. Kwa mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilikamilisha mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya makazi vijijini. Vilevile, mipango ya kina ya makazi imeandalisha katika maeneo ya kati ya vijiji 20 katika Wilaya za Namtumbo, Manyoni, Bariadi na Babati. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itatafsiri mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya makazi vijijini kwa lugha nyepesi ya kiswahili na kuusambaza kwa wadau mbalimbali zikiwemo halmashauri za wilaya na vijiji. Aidha, Wizara itashirikiana na Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Babati na Bariadi kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya makazi ya vijiji ilioandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa Miji. Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI huweka kanuni na miongozo inayosaidia katika usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji nchini. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilitayarisha kanuni za sheria ya usajili wa Maafisa Mipangomiji ya mwaka 2007 na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matakwa ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 kwa lengo la kukasimu mamlaka ya kuidhinisha mipango ya uendelezaji miji kutoka kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji kwenda katika ofisi za ardhi za kanda. Aidha, Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 itatafsiriwa kwa lugha nyepesi ya Kiswahili na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mipango ya matumizi bora ya ardhi, iliendelea kuandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi za wilaya na vijiji. Mipango hiyo inasaidia kwa kiwango kikubwa katika uendelezaji wa ardhi na rasilimali zake, kuondoa migogoro baina ya watumiaji ardhi, huwezesha upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya wawekezaji, uhifadhi wa mazingira na huongeza ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na jamii ya wananchi walio wengi hasa wanaoishi vijijini. Katika mwaka 2009/10, Wizara kuitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ilitoa elimu kwa umma juu ya Programu za Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi. Wadau muhimu walishirikishwa ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri Wilaya na Asasi za Kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji katika mwaka wa fedha 2009/2010. Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Asasi zisizo za Kiserikali na wadau mbalimbali kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi ya Wilaya na Vijiji. Katika kipindi hicho Tume ilikamilisha kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya wilaya nane za Longido, Bariadi, Mtwara, Pangani, Mkinga, Muheza Ngorongoro na Babati.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara itatayarisha mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 100 nchini. katika kipindi hicho, tayari vijiji 128 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya za Kilosa, Mpanda, Nkasi, Kongwa, Kiteto, Kisarawe, Misenyi, Kigoma Vijijini, Kilosa, Uyui, Kilombero, Babati, Longido, Bariadi, Namtumbo, Ulanga, Singida, Bagamoyo, Monduli na Morogoro Vijijini. (Angalia Jedwali Na. 9). Katika vijiji hivyo, maeneo ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yametengwa kwa kushirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itatayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa njia shirikishi katika vijiji 150 katika Wilaya zilizopo katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Arusha, Morogoro, Bukoba, Mtwara, Lindi, Tanga, Manyara, Mara, Singida na Ruvuma. Pia, mafunzo kuhusu sheria za ardhi na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi yatatolewa kwa watendaji katika ngazi ya Wilaya zitakazoandaliwa mipango. Vilevile, Wizara yangu itaanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kutekeleza programu tatu ambazo ni programu ya Kilimo, Maji na Mifugo kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo, Mifugo na Maji. Tume kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itasaidia kupatikana kwa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume itafanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro, uhamiaji mijini kutoka vijijini, ushirikishwaji wananchi katika kuendeleza ardhi mijini na viwango vya matumizi ya ardhi mijini na vijijini. Napenda kutoa wito kwa Wizara na Halmashauri za Wilaya zote kutenga bajeti ya utekelezaji wa programu zilizoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya nyumba. Wizara yangu inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta ya nyumba katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya nyumba nchini kutachangia katika kuongezeka kwa nafasi za ajira, kuinua vipato vya watu, kuchangia afya njema, kuboresha mazingira ya kuishi na hivyo wananchi kuweza kupata maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Pamoja na juhudzi za Serikali za kuanzisha Idara ya Nyumba na kuanza kuweka mazingira stahiki ya uendelezaji nyumba hapa nchini, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ya kutokuwa na mfumo wa kiutawala katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara katika mwaka 2010/2011 itawasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuanzisha mfumo wa kiutawala kwa mfano Idara au Kitengo kitakachoshughulikia masuala ya uendelezaji wa nyumba katika kila Halmashauri ya Wilaya na Majiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Mikopo ya Nyumba ya mwaka 2008 [*Mortgage Financing (special provisions) Act No. 17*] iliyoanza kutumika Mei, 2009 tayari benki tano (5) zimeanza kutoa mikopo ya kujenga na kununua nyumba. Benki hizo ni *Azania Bank Limited*, *Commercial Bank of Africa Ltd*, *International Commercial Bank*, *Stanbic Bank Limited* na *United Bank of Africa*. Ni matarajio kwamba benki zingine nazo zitaanza kutoa mikopo ya aina hiyo baada ya Serikali kuunda kampuni inayojulikana kama *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)*. Kampuni hii binafsi inamiliikiwa na mabenki ya hapa nchini itakuwa inatoa mikopo ya muda mrefu kwa mabenki, ili nayo mabenki yaweze kuwakopesha wateja wao mikopo ya nyumba ya muda mrefu (miaka 20 – 25 au zaidi) na yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilikamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Nyumba na rasimu ya mwongozo wa kuanzisha na kuendeleza Vyama vya Ushirika wa Nyumba hapa nchini. Kwa mwaka 2010/2011, Sera ya nyumba itazinduliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Rasimu ya mwongozo wa kuanzisha na kuendeleza vyama vya ushirika wa nyumba itawasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yao kabla ya kuanza kutumika na utafiti wa hali ya nyumba nchini utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kuratibu Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali (*Revolving Housing Loan Fund*) unaotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ununuzi wa nyumba. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, mfuko ulitoa mikopo ya shilingi 2,363,502,144 kwa watumishi 218. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Mei, 2010 jumla ya shilingi 353,291,365.82 zilikusanywa kutoka kwa wanufaika wa mfuko huo. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaandaa utaratibu wa kuubadili mfuko huu uwe wa dhamana ili uweze kuwahudumia watumishi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*), Wizara yangu kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*National Housing and Building Research Agency - NHBRA*) ni kufanya tafiti, kuelimisha, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utsalam wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu. Lengo la Wakala ni kuinua na kuboresha viwango vya nyumba kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa na vinavyopatikana hapa hapa nchini, jambo ambalo litaongeza ubora wa maisha ya wananchi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, maabara ya wakala imeboreshwa ili kuwezesha kupata matokeo bora ya utafiti. Uhamasishaji na mafunzo kwa vitendo yalifanyika katika wilaya za Dodoma mjini, Singida mjini, Manyoni, Morogoro mjini, Mvomero, Moshi vijijini, Bariadi, Kasulu, Tabora Vijijini, Ilala, Temeke na Kinondoni; na kutengeneza mashine za kufyatulia matofali yanayofungamana na kuzisambaza kwa wadau. Pia, uhamasishaji kwa wananchi juu ya kuanzisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ulifanyika katika mikoa ya Tanga, Mara na Ruvuma. Ushauri wa kitaalam na ukandarasi juu ya utumiaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu zilizotafitiwa ulifanyika katika wilaya za Mvomero, Ilala, Temeke, Korogwe na Same (Angalia Jedwali Na. 10a &10b).

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu zilizotafitiwa katika wilaya mbalimbali nchini; kujitangaza kupitia vyombo vya habari na kushiriki katika Maonyesho ya Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kusambaza teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba nchini; kushiriki katika uhamasishaji kwa njia ya semina na vitendo katika Halmashauri za Miji na Wilaya zilizowasilisha maombi kwa wakala. Vilevile, Wakala utaendelea kutoa huduma za ushauri kwa kutumia vifaa na teknolojia iliyofanyiwa utafiti na Wakala na kupatikana hapa hapa nchini. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuzihamasisha halmashauri za wilaya kutumia huduma za Wakala kwa kazi za ujenzi wa majengo mbalimbali hasa majengo ya umma (madarasa, nyumba za walimu na zahanati) ili kunufaika na huduma za Wakala na pia kusambaza teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Shirika lilitumia Shilingi bilioni 4.03 kugharamia miradi ya ujenzi wa nyumba 40 za makazi eneo la Medeli-Dodoma; jengo la ghorofa tano la biashara eneo la Balewa – Shinyanga, majengo sita ya biashara yenye thamani ya Shilingi bilioni 14.7 yaliyojengwa kwa ubia kwa kushirikiana na sekta binafsi yalikamilika katika kipindi hiki. Shirika pia limekamilisha utekelezaji wa mradi wa ukandarasi wa ujenzi wa bweni la wasichana katika Chuo Kikuu cha Mzumbe wenye thamani ya Shilingi milioni 976, na nyumba za makazi Dar es Salaam (eneo la *Regent Estate*).

Aidha, Shirika limetumia Shilingi bilioni 5.3 kugharimia miradi iliyio katika hatua mbalimbali za ujenzi. Miradi hii inahusu ujenzi wa nyumba 34 zinazoendelea kujengwa kwa ajili ya kuuzwa katika eneo la Mbweni JKT- Dar es Salaam; majengo sita ya ghorofa yenye nyumba 48 za makazi eneo la Kibla Arusha; Awamu ya Pili ya ujenzi wa ghorofa mbili zenye nyumba 40 eneo la Medeli – Dodoma; na ujenzi wa nyumba nne za makazi eneo la LDA – Arusha. Shirika pia linaendelea na ujenzi wa majengo 43 ya biashara yenye thamani ya Shilingi bilioni 96.6 yanayojengwa kwa ubia. Mingi ya miradi hii inatarajiwu kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/11.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Shirika lilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 35.9 kutoptaka na kodi za pango la nyumba linazozimiliki. Hadi kufikia Juni, 2010, Shirika likikuwa limekusanya Shilingi bilioni

33.6. Makusanyo haya ni ongezeko la asilimia 24 yakilinganishwa na kiasi cha Shilingi bilioni 27.05 kilichokusanywa mwaka jana kipindi kama hiki. Ongezeko hili linatokana na marekebisho ya viwango vya kodi kwenye nyumba za makazi yaliyoanza kutekelezwa Julai 2009 pamoja na uwezo zaidi wa kukusanya kodi na malimbikizo unaotokana na marekebisho ya Sheria Na. 2 ya 1990 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/11, Shirika linatarajia kukusanya Shilingi bilioni 36 kutokana na kodi za pango. Shirika litatumia sehemu ya mapato hayo kulipia riba ya mikopo ya mabenki itakayochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, matengenezo ya nyumba, kuongeza hazina ya viwanja na shughuli nyinginezo za maendeleo. Katika jitihada za kuongeza mapato na kumudu majukumu yake barabara, Shirika litaendelea kutumia fursa ya marekebisho ya sheria Na. 2 ya 1990 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 na Sheria Na. 11 ya 2005 kuwahamasisha wapangaji kulipa kodi kwa wakati. Natoa wito kwa wapangaji kulipa kodi zao kwa wakati ili kuepuka kadhia ya kuondolewa kwenye nyumba na kunadi mali zao ili kufidia madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/10 Shirika liliendelea kuyafanya matengenezo majengo yake yapatayo 2,392. Aidha, Shirika liliendelea kutenga asilimia 25 ya mapato yake yatokanayo na kodi za pango kila mwaka kwa ajili ya matengenezo. Matengenezo haya hufanywa kulingana na mpango maalumu unaolenga kuzifanya matengenezo makubwa nyumba zake zote katika kipindi cha miaka mitano (5) yaani, 2006/07 mpaka 2010/2011. Katika kipindi husika, jumla ya majengo 867 na nyumba 2,543 zimefanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 7.4. Kwa mwaka 2010/2011 shirika litaendelea kutenga asilimia 25 kwa ajili ya kuzifanya matengenezo makubwa nyumba linazozimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, itatakumbwa kuwa mwaka 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya mikopo ya nyumba (*mortgage financing act*) na sheria ya umiliki wa sehemu ya jengo (*the unit titles act*). Sheria hizi zililenga kutoa fursa kwa waendelezaji wa nyumba kupata mikopo ya kujengea nyumba na pia kuzilikisha kiurahisi kwa wanunu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia fursa hiyo Shirika limeelekezwa kujikita zaidi katika kufanya biashara ya kujenga nyumba na kuziwa (*real estate developer*) kuitia mikopo ya benki badala ya kuwa mpangishaji na mkusanyaji wa kodi za pango tu (*Landlord*). Katika kutumia fursa hii, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Shirika limejipanga kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa na utoaji wa ajira kuitia sekta ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na mpango mkakati wa shirika wa miaka mitano ( 2010/2011 – 2014/2015), Shirika litaanza na ujenzi wa nyumba 1,000 katika mwaka 2010/2011 kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa nyumba na hasa katika jiji la Dar es Salaam. Aidha, litaanza ujenzi wa majengo ya vitega uchumi na nyumba za makazi katika mikoa mbalimbali nchini. Miradi hii ni pamoja na majengo ya biashara katika maeneo ya Upanga, Magomeni na Lumumba (Dar es Salaam); Majengo ya biashara na makazi maeneo ya Sumbawanga – (Rukwa); Babati – (Manyara); Mvomero –

(Morogoro); Karume/Azimio – (Lindi), Barabara ya Boma – (Moshi), Shangani-(Mtwara), Kingo – (Morogoro) na Barabara ya Nyerere – (Mwanza); Medeli (Dodoma) na pia Mikoa ya Shinyanga, Singida na Tabora.

Aidha, Shirika linatarajia kujikita kwenye ujenzi wa nyumba kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini kwa kushirikiana na wadau wengine. Miradi hii yote inakadirisha kugharimu kiasi cha Shilingi bilioni 100. Katika utekelezaji wa miradi hii, Shirika linatarajia kukopa kutoka kwenye vyombo mbalimbali nya fedha. Kwa mujibu wa mpango huu wa miaka mitano (kuanzia mwaka wa fedha 2011/12) Shirika litakuwa linajenga wastani wa nyumba 3,000 kila mwaka na mikoa yote itahusishwa katika ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuhakiki wapangaji wa shirika lilianza kutekelezwa nchi nzima kuanzia mwezi machi, 2010. Lengo ni kubaini wapangaji haramu na wale wanaotumia nyumba za Shirika kwa manufaa binafsi. Katika kipindi hiki kifupi jumla ya wapangaji 379 wamebainika kupangisha nyumba kwa watu wengine pasipo idhini ya Shirika. Aidha, wapangaji 28 wamepangisha nyumba kwa watu wengine baada ya kupewa vibali na Shirika. Kwa mwaka wa fedha, 2010/11 shirika litaendelea na mchakato wa kufuta upangaji wa wapangishaji hao haramu yaani *sub renting* na kuhalalisha upangaji kwa watumiaji wa sasa. Aidha, hatua kali za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi ya watumishi wa Shirika watakaobainika kushiriki katika njama hizi za kujinufaisha binafsi kupitia upangishaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti iliyopita, niliarifu kuhusu azma ya *NHC* kuuza baadhi ya nyumba zake ambazo gharama za kuziendesha ni kubwa kuliko mapato. Zoezi hili linahitaji maandalizi makubwa, maandalizi hayo yanahu kuhusika kuwatambua wapangaji wa nyumba hizo na uwezo wao wa kulisipu ununuzi, kutafuta benki zitakazowakopesha fedha za kununua hizo (*flats*) na pia kuwaelimisha wahusika taratibu za umilikishwaji nyumba hizo chini ya sheria ya umilikishaji wa sehemu ya jengo. Maandalizi haya yakikamilika ndipo zoezi la uuzaaji wa nyumba hizi utaanza kutekelezwa. Napenda kurudia tena kwamba *NHC* watauza sehemu tu ya nyumba zao zinazowapa hasara kuziendesha na siyo nyumba zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliedelea kutoa huduma za utawala na usimamizi wa rasilimali kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi. Maeneo yaliyozingatiwa ni uimarishaji utawala bora, maadili mema ya utendaji kazi, kujali wateja, kuweka mazingira bora ya kazi na kutoa huduma kwa wakati. Vilevile, mapambano dhidi ya janga la UKIMWI yaliimarishwa kwa kuhamasisha watumishi kujikinga na kupima afya zao kwa hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa rasilimali watu. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara yangu iliajiri watumishi wapya 89, kuwapandisha vyeo watumishi 135, kuwathibitisha kazini watumishi 131 na kuwapatia mafunzo watumishi 115. Lengo likiwa ni kuimarisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi za Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 79 na kuwapatia mafunzo watumishi 120.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Wizara kubainisha mahitaji ya watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri, ilifanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inayosimamia Halmashauri ili Halmashauri zione umuhimu wa kuajiri watumishi wanaohitajika na kuondoa upungufu mkubwa uliopo. Watumishi wapya watakaoajiriwa mwaka 2010/11 katika Halmashauri wataimarisha na kuleta ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi. Lengo ni kuajiri wataalam wa Sekta ya ardhi moja kwa moja kutoka vyuoni na kuwapangia vituo kwenye Halmashauri zenye upungufu wa wataalam hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazingira Bora ya Kazi ili kuboresha mazingira ya utoaji huduma, Wizara yangu ilikamilisha ukarabati wa jengo la Wizara ghorofa ya pili na sehemu ya maegesho ya magari ya viongozi. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itajenga kituo cha huduma kwa wateja (*Customer Service Centre*), pamoja na kukarabati sehemu ya mbele ya jengo (Ardhi House). Vilevile, Wizara itajenga jengo kwa ajili ya ofisi ya ardhi ya kanda ya Ziwa (Mwanza) na itaanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la Upimaji na Ramani (Ramani House).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa rasilimali. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara iliendelea kusimamia rasilimali zake kwa kutumia mifumo ya elektroniki iliyojengwa ambayo ina ingiza na kutunza kumbukumbu mbalimbali zinazohusu rasilimali watu (*Human Resource Management*) magari (*Vehicles Management*), kompyuta na kumbukumbu za wateja wanaofika Wizarani kupata huduma (*Visitors Management*). Mifumo hii ya usimamizi wa rasilimali inasaidia katika kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati ya matumizi ya rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapambano dhidi ya janga la UKIMWI. Katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuwahudumia kiafya watumishi wake wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (VVU). Mkakati wa kuwaleta watoa ushauri nasaha na kupima UKIMWI kwa hiari ulitekelezwa ambapo watumishi wengi wamehamasika kutambua hali ya afya zao. Katika kipindi hicho, watumishi 350 walijitokeza kupatiwa ushauri nasaha na kupimwa afya. Huduma ya dawa na lishe iliendelea kutolewa kwa watumishi walijitokeza kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI kila mwezi. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendeleza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuendelea kuwapatia huduma watumishi walioathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, habari na mawasiliano. Upatikanaji wa habari sahihi na kwa wakati kuhusu Wizara na Majukumu yake ni muhimu sana katika kudumisha Utawala Bora na Uwajibikaji. Katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kuboresha mawasiliano kwa umma kwa njia ya radio na televisheni pamoja na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Wiki ya Utumishi wa Umma na Nane Nane. Lengo ni kuendelea kuwaelimisha wananchi na Wadau juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaendelea kuboresha mawasiliano kwa kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ardhi, Wizara yangu iliendelea kuvisimamia Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya Upimaji Ardhi na Urasimu Ramani katika ngazi ya Diploma, Umiliki Ardhi na Uthamini pamoja na Uchapaji Ramani katika ngazi ya cheti. Katika mwaka 2009/2010, idadi ya wahitimu ilikuwa 109 kati yao 52 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora na 57 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaendelea na upanuzi wa Chuo cha Ardhi Tabora kwa kujenga mabweni, madarasa na maktaba ili kuongeza idadi ya wanafunzi katika Chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi ni pamoja na:-

- (a) Ardhi iliyopimwa na kumilikishwa inakadiriwa kuwa ni asilimia moja tu, hali hiyo imesababisha ardhi kutotumika ipasavyo na kusababisha migogoro ya ardhi kwa watumiaji mbalimbali;
- (b) Ufahamu mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa Hatimiliki, na leseni za makazi katika kuzitumia kama dhamana katika vyombo vya fedha ili kujiletea maendeleo;
- (c) Wizara kutokuwa na mfumo thabiti wa utunzaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi;
- (d) Sekta ya ardhi katika Halmashauri za miji na wilaya kuendelea kutotengewa fedha za kutekeleza majukumu yao;
- (e) Upungufu mkubwa sana wa wataalam wa sekta ya ardhi katika halmashauri za miji na wilaya;
- (f) Wilaya na vijiji kutokuwa na mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi;
- (g) Riba kubwa kwa wananchi wanaokopa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba inayotozwa na mabenki ambayo ni kati ya asilimia 17 na 25 kwa mwaka;
- (h) Viwango vya fidia kwa ardhi na mazao vinalalamikiwa na wadau wengi; na
- (i) Upungufu mkubwa wa nyumba mijini na wingi wa nyumba duni vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utatuzi wa matatizo au changamoto zilizojitokeza. Wizara yangu inaendelea kukabiliana na changamoto zilizojitokeza kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

- (a) Kuendelea kuweka mfumo wa alama za upimaji wa ardhi (*Geodetic Reference Frame*) ambao utawezesha kuharakisha upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani kwa gharama nafuu;
- (b) Kujenga kituo cha kupokelea picha za anga (*Direct Satellite Receiving Station*) nchini ili kurahisha upatikanaji wa picha za anga ambazo matumizi yake ni pamoa na kurahisisha upimaji wa ardhi;
- (c) Kuongeza kasi ya kupima ardhi na mashamba kwa ajili wa wawekezaji (*land bank*), kupima mashamba ya wanavijiji na urasimishaji wa maeneo yaliyojengwa bila kupimwa; na kuanzisha ofisi za ardhi za kanda ili kusogeza huduma karibu na wananchi;
- (d) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi; na Benki Kuu ya Tanzania imewezesha kuundwa kwa kampuni inayojulikana kama Tanzania, *Mortgage Refinancing Company (TMRC)*. Kampuni hii binafsi inamilikiwa na mabenki ambayo yamenunua hisa kwenye kampuni hiyo na hivyo kuongeza mtaji wa kukopesha mabenki ili nayo yaweze kutoa mikopo ya nyumba kwa muda mrefu (miaka 20-25 au zaidi) na kwa riba nafuu;
- (e) Kuyawezesha mabaraza ya ardhi na nyumba ya Wilaya kwa kuyapatia vitendea kazi, kufungua mabaraza mapya na kuongeza idadi ya vikao vya kusikiliza mashauri kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi;
- (f) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umilikishaji wa ardhi kisheria;
- (g) Wizara kwa kushirikiana na HAZINA na TAMISEMI zitasimamia fedha zinazorejeshwa kwenye Halmashauri (20% ya makusanyo yao) na kuhakikisha kwamba zinatumika kuendeleza sekta ya ardhi kama mwongozo wa fedha hizo unavyoolekeza na pia kuangalia uwezekano wa kuongeza asilimia hiyo;
- (h) Kutekeleza mradi wa *Land Information System* uliopendekezwa na Mtaalam Mwelekezi (*Swedesurvey/International Land Systems*);
- (i) Kuzijengea uwezo halmashauri za miji na wilaya ziweze kuandaa mipango ya uendelezaji miji na kuitekeleza;
- (j) Kuongeza kasi ya kusambaza matokeo ya tafiti na kutoa mafunzo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi;
- (k) Rasimu ya sheria ya uthamini inaandaliwa na viwango vya fidia vinaendelea kuishwa ili viendane na bei ya soko; na
- (l) Kuandaa Mpango/Programu maalum ya uhamasishaji na uvezeshaji wa ujenzi wa nyumba bora vijijini ili kuondokana na nyumba duni za nyasi na udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, kwa niaba ya Wizara yangu napenda kuwashukuru wadau wote walioshirikiana nasi mwaka 2009/10 katika kutekeleza majukumu yetu. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GTZ), Denmark, Uingereza, Sweden na Uhlanzi kupitia Mradi wa “*Business Environment Strengthening for Tanzania*” (BEST) na Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) na UN – Habitat.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushukuru sekta binafsi kwa kuunga mkono juhudhi mbalimbali zinazochukuliwa na Wizara yangu katika kuboresha maisha ya Watanzania. Shukurani za pekee ni kwa Waheshimiwa Wabunge kwa michango na hoja zao mbalimbali zilizohusu Wizara yangu. Naomba mwendelee kuwa wadau muhimu wa sekta ya ardhi ndani na nje ya Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Bw. Patrick Rutabanzibwa, kwa ushirikiano mkubwa alionipa kwa kipindi kifupi tangu ahamishiwe katika Wizara hii. Pia, nawashukuru Wakuu wa Idara, viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalam wote wa wizara kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu. Naomba waendelee na moyo wa kuchapa kazi hususan katika kipindi chote hasa katika kipindi hiki cha kurahisisha ufanyaji biashara nchini (*Cost of Doing Business*) kwa kuwa sekta ya ardhi ni mwezeshaji mkuu wa sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mwelekeo wa Serikali wa kuelekeza nguvu zake katika kuimarisha kilimo, Wizara yangu ina jukumu kubwa la kuhakkisha kuwa ardhi inapatikana kwa ajili ya mashamba makubwa na viwanda vyaa mazao yatokanayo na kilimo. Aidha, matumizi mengine makubwa ya ardhi yakiwemo ya uendelezaji wa nyumba (*Real Estate Development*), mahoteli, viwanda na kadhalika yanatengewa ardhi ya kutosha. Haya yote yatakelezwa iwapo HAZINA ya ardhi itaanzishwa na kuimarishwa. Vilevile, baada ya kukamilika kwa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine ina jukumu la kuhakkisha kuwa maeneo yenye migongano na migogoro sugu ya matumizi ya ardhi yanapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hili, Wizara yangu itaendelea kuhakiki, kupanga matumizi ya ardhi, kupima, kusajili na kutoa hati katika maeneo hayo ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki na hivyo kuondoa migogoro kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Natoa rai kwa Mamlaka na Taasisi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakkisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote kwa lengo la kuwaondolea wananchi umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2010/2011, naomba kutoa hoja

kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

**(i) Mapato:-**

- Mapato ya Serikali (sh.) 20,641,200,000

**(ii) Matumizi ya Kawaida:-**

- Matumizi ya Mishahara (sh.) 6,423,295,000

- Matumizi Mengineyo (OC) (sh.) 25,159,688,000

**Jumla Shilingi** **31,582,983,000**

**(iii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo:-**

- Matumizi ya Maendeleo (sh.) 22,265,078,000

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya matumizi ya mishahara, matumizi mengineyo na matumizi ya maendeleo kwa jumla tunaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 53.848.061.000.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena wewe, Naibu Spika, napenda kumshukuru Spika, Wenyeviti Wabunge kwa kuliendesha Bunge letu hili kwa umahiri mkubwa na pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.ardhi.go.tz](http://www.ardhi.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

### *(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JOB. Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanakamati wenzangu napenda kumpongeza Mheshimiwa Kapt. mstaafu John Z. Chiligati, kwa kazi nzuri anayoiendeleza katika kuingoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoa na Ndugu Patrick Rutabanzibwa kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Mwenyezi Mungu awatangulie na kuwalinda katika utekelezaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina idara saba(7) na vitengo tisa (9), Idara hizo ni Maendeleo ya Huduma ya Ardhi, Upimaji wa Ramani, Maendeleo ya Nyumba, Sera na Mipango, Utawala na Utumishi, Mifumo ya Habari na Mawasiliano na Idara ya Upangaji wa Miji na Vijiji.

Aidha Wizara inazo Taasisi na Mashirika yanayofanya shughuli zake chini ya uangalizi wa jumla wa Wizara ambayo ni:-

- (a) Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) ;
- (b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi;
- (c) Wakala wa Taifa wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*);
- (d) Chuo cha Ardhi Tabora; na
- (e) Chuo cha Ardhi Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 31/05/2010, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikutana na watendaji wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri katika Ofisi Ndogo ya Bunge Jijini Dar es Salaam. Katika kikao hicho, Kamati ilipitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Aidha, majadiliano yalifanyika kwa kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Dira ya Wizara;
  - (b) Dhima ya Wizara;
  - (c) Uongozi na Muundo wa Wizara;
  - (d) Majukumu ya Idara na Vitengo mbalimbali vya Wizara;
  - (e) Taarifa ya Taasisi zilizo chini ya Wizara;
- (f) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge katika mwaka wa fedha 2009/2010; na

(g) Kazi zilizopangwa kufanyika na Wizara kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2010/2011, yamezingatia maelekezo mbalimbali ya Serikali, bei katika soko na vipaumbele ambavyo Wizara imojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 12,013,543,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo; hadi kufikia Mei 2010, Wizara imepokea jumla ya shilingi 7,773,704,631 sawa na asilimia 65 tu ya fedha za miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya shilingi 10,669,957,642 ambazo ni maduhuli ya Serikali zimekusanya kutoka vyanzo mbalimbali nya mapato. Kiasi kilichokusanya ni sawa na asilimia 69 ya lengo la mwaka lililokuwa kiasi cha shilingi 15,550,006,000. Kati ya makusanyo hayo, shilingi 9,923,257,642 ambazo ni sawa na asilimia 93 ya makusanyo zinatokana na kodi ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya makusanyo ya mwaka huu hayatofautiani sana na yale yaliyokusanya mwaka jana ingawa makusanyo ya mwaka huu yako chini ya lengo kwa asilimia 31 kutokana na Halmashauri nyingi za Miji na Wilaya kutokutoa kipaumbele katika kusimamia makusanyo ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati yangu ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali kuhusiana na sekta ya ardhi, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imefanya kazi maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeweza kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine zinazohusika imeafiki kuanzia mwaka ujao wa fedha (2010/2011), watumishi wote wa ardhi waajiriwe moja kwa moja kutoka vyuoni na kupangiwa kazi katika Halmashauri mbalimbali ili kuwa na wataalam wenye sifa na watakaotekeliza sera na sheria za ardhi;

(ii) Jumla ya nyumba 1,844 zenyet wapangaji 12,391 zilizokuwa chini ya Msajili wa Majumba zilitambuliwa na kuorodheshwa na kuwasilishwa mbele ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Aidha, orodha hiyo inaonesha wapangaji wa nyumba hizo hulipa kodi ya shilingi bilioni 30.6 kwa mwaka;

(iii) Usimikaji wa alama 350 za msingi za upimaji kati ya lengo la kusimika alama 300 ulikuwa umefanyika;

(iv) Pia Wizara inaendelea kushirikiana na *TANAPA* pamoja na wananchi walio na makazi jirani na maeneo ya Hifadhi kutafsiri mipaka yenyе migogoro kwa nia ya kutatua tatizo la mipaka hiyo;

(v) Wizara inaendelea kuwahamasisha wananchi kujuu Sera, Sheria na Kanuni za ardhi katika kuendeleza miji. Aidha, eneo lolote likishatangazwa kuwa eneo la mradi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri husika hufanya tathmini ya mali na maendeleo ya wananchi na kisha kulipa fidia kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za Mwaka 1999 na Kanuni zake za mwaka 2001;

(vi) Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi na Programu zake umekamilika;

(vii) Mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 108 imekamilika kati ya lengo la kutayarisha mipango ya vijiji 100;

(viii) Elimu kwa umma kuhusu Sheria na Kanuni za ardhi imeendelea kutolewa na Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya pamoja na taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali kwa kupitia vyombo vya habari na mikutano ya hadhara katika kuwasaidia wananchi kupata uelewa wa haki zao za ardhi;

(ix) Wakala wa Vifaa vya Ujenzi wa Nyumba Bora na za gharama nafuu umefanikiwa kuhamasisha Halmashauri za Wilaya za Namtumbo na Mvomero kuanzisha vikundi vya vijana *Grassroot Building Brigades (GBBs)* katika kuwasaidia vijana kupata elimu ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu na kuitumia katika maeneo hayo. Aidha, wakala umeendelea kutoa elimu hiyo kupitia maonyesho ya sabasaba na nanenane;

(x) Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya kuendeleza maeneo yaliyo pembezoni mwa miji mikubwa ili kupunguza msongamano wa watu na magari katikati ya miji. Miradi inayotekelawa ni pamoja na ujenzi wa Dodoma *New City*, kituo cha huduma cha Luguruni, Kigamboni *New City* na maandalizi ya kujenga kituo cha huduma cha Kongowe kilichopo barabara ya Kilwa yameanza;

(xi) Mabaraza ya Ardhi katika ngazi ya Kata yamefunguliwa kwa ushirikiano wa Wizara na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inafanya tathmini kujuu ni Mabaraza mangapi yamefunguliwa katika kila Kata kwa kila Wilaya na namna Mabaraza hayo yanavyofanya kazi;

(xii) Wizara imekamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji 1,500 vilivyokuwa vimesalia kupimwa hapa nchini;

(xiii) Wizara imeonyesha juhudini katika kuboresha vyuo vya ardhi nchini kwa madhumuni ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Mfano, mzuri ni wa Chuo cha Tabora ambapo Serikali imetenga kiasi cha shilingi 1,300,000,000 kujenga majengo mapya kwenye chuo hicho na ramani ya majengo hayo imekamilika na Kamati na iliona ramani hizo;

(xiv) Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) limefanikiwa kutekeleza miradi ya vitega uchumi kwa kujenga nyumba 40 za makazi Medeli, Dodoma, kukamilisha ujenzi wa ghorofa tano za biashara Balewa, Shinyanga na ujenzi wa nyumba mbili za makazi *Regent Estate*- Dar es Salaam; na

(xv) Wizara imeendelea kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI kwa watumishi wake ili kuepuka maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto, pamoja na jitihada zilizofanywa na Wizara katika utekelezaji wa Bajeti ya 2009/2010, Wizara iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Sekta ya ardhi katika Halmashauri za Miji na Wilaya kuendelea kutotengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo;

(ii) Upungufu mkubwa wa wataalam wa sekta ya ardhi katika Halmashauri za Miji na Wilaya;

(iii) Ukosefu wa takwimu za miliki za viwanja hivyo kukwamisha upatikanaji wa mapato ya kutosha;

(iv) Uhaba wa viwanja vilivyopimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

(v) Vijiji na Wilaya kutokuwa na mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi;

(vi) Ardhi ya nchi iliyopimwa na kumilikishwa inakadiriwa kuwa ni asilimia moja tu, hali hii imeongeza migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali; na

(vii) Ufahamu mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa Hatimiliki na leseni za makazi katika kuzitumia kama dhamana katika vyombo vya fedha ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeridhika na namna Wizara inavyojitahidi kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza Bajeti ya Wizara na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Jitihada hizo ni pamoja na:-

(i) Kujenga kituo kidogo cha kupokelea picha za anga nchini ili kurahisisha upatikanaji wa picha za anga na kuharakisha upimaji wa mashamba ya wananchi;

(ii) Kuanzia mwaka ujao wa fedha Wizara kwa kushirikiana na Hazina itahakikisha fedha inayorejeshwa kwenye Halmashauri inatumika kuendeleza sekta ya ardhi;

(iii) Wizara pia imeanza kuweka mfumo wa alama za upimaji ambao utawezesha kuharakisha upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani kwa gharama nafuu;

(iv) Kuhamasisha Halmashauri za Miji na Wilaya kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa mipango ya uendelezaji miji; na

(v) Elimu juu ya manufaa ya umilikishwaji ardhi kisheria imeendelea kutolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inasimamia sekta muhimu mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2010/2011, sana ambazo zinahusu hali halisi ya kila siku ya maisha ya binadamu. Ni vema sekta hizi zikaangaliwa kwa umakini kutokana na ukweli kwamba binadamu anategemea sana ardhi katika kupata riziki yake pamoja na malazi. Hivyo basi, Kamati ina ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi holela bado ni changamoto kubwa inayoikabili nchi yetu. Hali hii inatokana na ukweli kwamba maeneo ya viwanja yaliyopimwa ni machache sana hivyo kutoa mwanya kwa maeneo mengi kujengwa kiholela. Kamati inashauri Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya upimaji wa viwanja na pia ihakikishe Halmashauri za Miji na Wilaya zinatumia ipasavyo fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya ardhi na kutoa kipaumbele katika masuala ya upimaji ardhi sambamba na yale ya afya na elimu;

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inashauri Serikali kwamba imefikia wakati wa kupiga marufuku ujenzi wowote mpya katika maeneo ya mijini na badala yake Serikali itenye maeneo pembezoni mwa Miji kama vile kwa Dar es Salaam Kibaha, Kisarawe na mengineyo. Hii itasaidia kupunguza foleni mijini na kusaidia kukua kwa miji ya pembezoni;

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya pango la ardhi kwa mwaka 2009/2010, yamekuwa chini ya lengo kwa asilimia 31 kutokana na Halmashauri za Miji na Wilaya kutotoa kipaumbele katika kusimamia makusanyo ya pango la ardhi. Kamati inashauri Serikali izisimamie Halmashauri hizi ipasavyo kuhakikisha zinakusanya mapato hayo;

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iharakishe mchakato wa ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba ili wananchi wapate mwongozo bora wa ujenzi wa nyumba;

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuharakisha suala la uwekaji wa mipaka kwenye maeneo ya maji (Bahari na Ziwa) ili kuimarisha ulinzi na usalama hasa katika maeneo ya mipaka na nchi zetu jirani;

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua juhudhi za Serikali kwamba Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) lijikite zaidi katika ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha badala ya kuwa mpangishaji tu, na kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa limejiwekea mpango mkakati wa miaka mitano (2010/11- 2014/15) wa kujenga nyumba mpya 15,000 nchini; Kamati inashauri kuwa ujenzi wa nyumba hizi ufanyike katika Wilaya zote nchini ili kuwanufaisha wananchi wa maeneo mbalimbali;

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa hulazimika kugharamia ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika miradi yake na kusababisha nyumba zinazojengwa na Shirika kuwa ghali, Kamati inashauri taasisi zinazohusika kama vile Halmashauri za Miji na Mamlaka za Maji na Umeme ziwekeze ipasavyo katika miundombinu husika ili kila mwananchi aweze kumudu gharama za nyumba za Shirika;

(h) Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inashauri Shirika la Nyumba la Taifa kuanzisha ujenzi wa majengo makubwa hasa katika maeneo yenyeye migodi na kuyatumia kama vitega uthumi na hivyo kuongeza pato la Shirika na pia kukuza uthumi wa nchi;

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za ukusanyaji kodi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa hukwamishwa na Wizara na taasisi za Serikali kutolipa kodi ya pango kwa wakati. Kamati inashauri Wizara na taasisi hiyo zilipe kodi kama inavyotakiwa kwani zinasababisha Shirika kukosa mapato ya kutosheleza kuhudumia miliki yake na kujenga nyumba mpya kwa ajili ya kuuza na kupangisha;

(j) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha utaratibu wa kutoa Hatimiliki katika kila Mkoa na sio kwenye Kanda tu. kwa kufanya hivyo Serikali itarahisisha upatikanaji wa hatimiliki kwa wananchi hasa wale walioko Wilayani. Aidha, muda wa upatikanaji wa hatimiliki ufikiriwe kwani wananchi wanalazimika kusubiri muda mrefu kabla ya kupata hakimiliki zao;

(k) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inategemea kuanzisha kituo cha kupokelea picha za anga (*Satellite Receiving Station*) kurahisisha upatikanaji wa picha hiyo na pia kuharakisha upimaji wa mashamba ya wananchi. Kamati inashauri maandalizi ya kuwatafuta wataalam wa kukiendesha kituo hicho yafanyike mapema kwani kinaweza kikatumika kama soko la picha za anga kwa nchi zinazotuzunguka na hivyo kuongeza pato la nchi;

(l) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali itenye fedha kwa ajili ya Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHRBA*) kuuwezesha Wakala kuanzisha Kanda maalum kwenye maeneo mbalimbali

nchini kuwarahisishia wananchi kupata matokeo ya utafiti wa mbinu mbalimbali za kuinua hali ya makazi yao kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu;

(m) Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wananchi wamekuwa wakimiliki maeneo muhimu kama vile ya ufukweni bila kuyaendeleza kwa nia ya kuyauza kwa wawekezaji kwa bei ya juu. Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua kwa mujibu wa Sheria, dhidi ya watu ambao hawayaendelezi maeneo yao na ikibidi Serikali iyachukue hayo maeneo;

(n) Mheshimiwa Naibu Spika, bado Kamati inasisitiza uadilifu kwa wafanyakazi wa Wizara hasa katika suala la ugawaji wa viwanja na usimamizi wa ardhi. Hii itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka kila siku; na

(o) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iendelee kusimamia na kuwahimiza watumishi wake kujilinda na ugonjwa wa UKIMWI ili kuepuka maambukizi mapya na upungufu wa nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya fedha kwa mwaka 2010/2011. Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2010/2011, ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yameandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa utayarishaji wa bajeti kitaifa na maeneo ya kipaumbele yanayolenga kutekeleza sera na mikakati ya Wizara.

Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inaafiki Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 48, jumla ya shilingi 58,276,262,000 kati ya hizo, shilingi 26,693,279,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, shilingi 25,159,688,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 6,423,295,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha fedha zinazombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua bajeti hii nao ni:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti; Mheshimiwa Hassan R. Khatibu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mjumbe; Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mjumbe; Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mjumbe; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mjumbe; Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mjumbe; Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mjumbe; Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mjumbe; Mheshimiwa Magdalena Sakaya Mjumbe; Mheshimiwa Ally Said Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Khamis Seif Mjumbe; Mheshimiwa Lucas Selelii Mjumbe; Mheshimiwa Jacob Shibili, Mjumbe; Mheshimiwa Guido Sigonda, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed Rajabu Soud, Mjumbe; Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mjumbe; Mheshimiwa Aziza Ali; Mjumbe; Mheshimiwa Lucy Mayenga; Mjumbe na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer; Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Z. Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Katibu Mkuu wake Ndugu Patrick Rutabanzibwa; Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya kazi pamoja. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati kuiongoza Kamati hii, kwa miaka mitano michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa katika kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashilillah na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya na Yona Kirumbi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kuwashukuru sana wananchi wa Kongwa kwa kuniamini kwa kushirikiana nami na kwa maendeleo makubwa ambayo tumefanya katika miaka mitano. Nimshukuru sana mke wangu Dr. Fatuma kwa kunivumilia kwa kutokuwepo kwangu nyumbani kwa muda mwangi nikatumikia Jimbo la Kongwa na Taifa letu. Lakini mwisho nataka kuwathibitishia wananchi wa Kongwa kwamba nina afya njema, nina uzoefu mkubwa zaidi na kwa hiyo nadhamiria kuwatumikia zaidi kwa miaka mitano kwa kasi zaidi, nawaomba mnunge mkono hasa wana CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y MHE. ALI SAID SALIM - MSEM AJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii naisoma kwa niaba ya Mheshimiwa Ali Said Salim ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Wizara hii. Japokuwa mwenyewe yupo lakini hali yake sio nzuri, kwa hiyo nitaisoma kwa niaba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 99 (7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kwa ushirikiano mzuri wanaonipa ndani na nje ya Bunge. Pia nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Job Ndugai Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira kwa kazi yake kubwa ya kuongoza Kamati kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano. Aidha, ni kwa Waziri Kapteni John Chiligati na timu nzima ya watendaji wote katika Wizara. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla hatujaeleza changamoto zinazohusu ardhi ya Tanzania na matumizi yake, ni vema tukajikumbusha takwimu zinazoelezea ardhi tuliyonayo. Tanzania ina eneo la ardhi lipatalo 886,200 kilomita za mraba. Kufuatana na taarifa ya hali ya mazingira ya mwaka 2008, inaonyesha asilimia 75% haitumiki au ni ngumu kuitumia kutokana na hali yake ya uasili (mito, maziwa, milima, miamba na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi haitoshi kutokana na mgawanyo tuliuonyesha hapo juu na matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo ni asilimia 10.6% tu ya ardhi yote, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

(a) Utafiti ufanyike ili kubaini jinsi ya kutumia hekta 34 milioni zaidi ya hekta 10.1 milioni zinazotumika kwa sasa, kwani utafiti unaonyesha ukikusanya ardhi yote inayoweza kutumika kwa kilimo ni zaidi ya hekta 44 milioni; na

(b) Kwa kuwa ardhi inayoongelewa katika sheria namba 5 na ile inayoongelewa katika sheria namba 4, kwa uhalisia ni ile ile na hakuna utenganisho uliowazi. Hali hili ni chanzo kikuu cha migogoro. Aidha, ardhi hugawiwa na mamlaka mengi. Kwa mfano; *TIC* inaweza kummilikishwa mgeni ardhi ya uwekezaji bila kuzingatia kama ardhi hiyo ni ya wanakijiji na kwa hiyo Serikali inaweza kutwaa ardhi kwa shughuli za uchumi na kuwauzia wawekezaji bila ya kujali maeneo hayo kuwa yanatumiwa na wanakijiji. Mifano mingine ni upanuzi wa Hifadhi (*Expansion of National parks, Ruaha, Loliondo hunting blocks*), upanuzi wa bandari Kurasini.

Hivyo basi ni lazima tuifanyie marejeo Sera ya Ardhi na tuangalie upya Sheria zote mbili za Ardhi kwa nia ya kuziunganisha na kuwa Sheria moja ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa zinaonyesha kuwa, athari ya uwekezaji katika ardhi kwa wazalishaji wadogo, migogoro mingi kijijini ambayo inaishia kwa watu kuuwana, kiini chake ni ardhi ambayo inakuwa adimu kwa mhitaji na watumiaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na madai kuwa uwekezaji umekuza uchumi mkuu wa kiwango cha kati ya 5.2% mpaka 7% lengo likiwa kufikia 10%, lakini ukuaji huu umelalamikiwa kutoleta matokeo katika hali halisi ya maisha ya wananchi

katika ngazi za chini, badala ya kumpunguzia umaskini, uwekezaji umeongeza umaskini kwa kumpora hata kile kidogo alichokuwa nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo imeshuhudiwa mara nyingi wawekezaji wasio Watanzania wakimiliki ardhi, waliwaondoa wananchi wa asili katika maeneo yao na kuharibu kabisa mifumo yao ya maisha. Mara nyingi imetokea kwa sababu ya kukiuka makusudi sheria na taratibu zilizopo, udhaifu wa mifumo ya utekelezaji wa sheria na dharau kwa vyombo vya ngazi za chini za utawala na wananchi wao kwa vile maamuzi hufanywa ngazi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limetendeka kwa kuhusisha viongozi wa kisiasa zaidi, mifano mingi katika maeneo mengi hapa Tanzania unyang'anyi huo unapata Baraka za wanasiasa, hii ni *bad news* kwa Waheshimiwa waliofanya au wanaotuhumiwa kushirikiana na watendaji kupora ardhi ya wananchi bila kufuata utaratibu wa Sheria namba 5 ya Ardhi ya Vijiji. Kambi ya Upinzani inasema wanasiasa hao wajiandae kuwajibika kwa wapiga kura wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna athari kubwa ya uwekezaji kwenye ardhi ya wazalishaji wadogo. Uharibifu wa vyanzo vya maji kwenye ukulima, ufugaji, uchimbaji na uvuvi wa asili vimevurugwa na uwekezaji kwa namna mbalimbali. Mfano huko Bulyankulu mwaka 1996 zaidi ya ajira 500,000 zilipotokea mgodi ulipofunguliwa. Hao walikuwa wachimbaji wadogo na watoa huduma kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea uhaba wa chakula kwa vile ardhi inayofaa kwa kuzalisha chakula inatumika kuzalisha malighafi zisizoliwa na kufanya wazalishaji wa chakula kukimbilia kutafuta vibarua katika maeneo mapya ya uwekezaji; Mfano, migodini na maeneo ya wanyamapori kwa ajili ya utalii. Hadi mwaka 2007 zaidi ya hekta 641,000 wamegawiwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwekezaji huo pia wananchi wameondolewa katika ardhi yao bila fidia au kwa fidia ndogo. Mfano, kaya 86 ziliondelewa kupisha mgodi wa Geita katika Kijiji cha Mtakuja, watu zaidi ya 250 hawana pa kuishi kwa takriban miaka mitano.

Uanzishwaji wa mgodi wa *Resolute (Tanzania) Limited*, wakulima, wafugaji na wachimbaji wadogo na familia zao wapatao 400 wa Vijiji vya Mkwajuni, Isanga, Insunga Ngwanda na Mwaluzwilo, eneo la Lusu, Wilaya ya Nzega walitimuliwa, hadi leo hii hawajawahi kufidiwa mali zao walizokuwa nazo na wanaendelea kutokuwa na makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi wa Kijiji cha Namawala Kilombero wako hatarini kuondolewa kijijini kumpisha mwekezaji aliyepewa 62% ya ardhi yao yenye ukubwa wa 9272.5 na kuathiri zaidi ya wakazi 10,000 na watoto wa shule 200. Haya yote yanafanyika na Serikali inayojiita sikivu inayaona. Hayo ndiyo maisha bora waliyoahidiwa mwaka 2005? Je, ni haki kwa familia hizo kuendelea kutoa ridhaa kwa Chama cha Mapinduzi kuendesha Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani kuondoa athari hizo ni: Kwanza wawekezaji wasiruhusiwe kwenda kujitafutia ardhi kwenye vijiji bali kazi hiyo

ifanywe na Kituo cha Uwekezaji kwa njia shirkishi kwa kuitia wananchi. Pia pale wananchi waelimishwe na kujua faida ya uwekezaji katika ardhi yao na wao wawe ni wanahisa na ardhi yao iwe ni sehemu ya mtaji badala ya wenye ardhi kuwa vibarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara chache hutokea wakalipwa fidia stahili lakini sehemu nyingi ardhi imekuwa ikitololewa bure na wananchi kwa ahadi kuwa watapata fursa za ajira kwenye mashamba au viwanda au migodi ikianza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni wananchi wa maeneo ya migodi ya madini kama Kahama, Buzwagi, Nzega, Tarime na sehemu nyingine za uwekezaji wa nishati uoto kama Rufiji, Kisarawe, Kilwa, wakati wa uanzishaji wa mashamba kwa ajili ya nishati uoto. Tafiti zinaonyesha kuwa zaidi ya hekta laki sita (641,000) zimegawiwa kwa wawekezaji hadi sasa kwa ajili ya kilimo cha nishati uoto nchini, nyingi zikiwa Wilaya za pwani kama vile Bagamoyo (zaidi ya 200,000), Kilwa (zaidi ya 200,000), Rufiji (zaidi ya 50,000), Kisarawe (zaidi ya 10,000) na nyingine nyingi kwa Wilaya nyinginez.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wilayani Kondoa, Kata ya Kisese, Kijiji cha Atta wanakijiji wamekuwa wakilima kilimo cha kujikimu kwa miaka takriban 20 kwenye eneo hilo, lakini kwa hatua ambayo wameshindwa kuelewa wanaambiwa eneo hilo limeuzwa kwa mwekezaji. Katika kadha hiyo mwekezaji huyo anatumia Askari Polisi kuwakamata wanakijiji na hivi sasa vijana kumi waliokutwa wakilima kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe wamekamatwa pamoja na majembe yao yako Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Chubi, Kata ya Mbumbuta huko huko Kondoa walitimuliwa katika eneo lao bila fidia na wengine wamewekwa ndani wanaitwa wavamizi. Kambi ya Upinzani inauliza, hivi ni kweli mtu mwenye miaka 70 amezaliwa na kukulia kijijini hapo anaweza kuwa mvamizi? Na ni kwa nini Watanzania wanakuwa tanga tanga katika maeneo yao ya asili? Tunaitaka Serikali iweke mipango endelevu kwa kuwapa umuhimu wa kwanza wahusika wa maeneo yanayotakiwa kuuzwa, aidha, ihakikishe wanaojiita wawekezaji katika ardhi wafuate utaratibu uliowekwa katika Sheria ya Viji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa matatizo haya yote yanayohusiana na migogoro inayotokea katika ardhi, iwe baina ya wakulima na wafugaji au wawekezaji na wanavijiji ni kutokana na kutokufahamika au wahusika ambao ni watendaji wa Serikali kwa kutumiwa na wanasiwa kwa kutokuelea vizuri sheria za ardhi au makusudi kutokufuata sheria hizo kwa sababu zao binafsi. Suala hili linawenza kupatiwa ufumbuzi kwanza kwa wanavijiji kuelewa vizuri utaratibu wa umilikishwaji ardhi kwa wawekezaji na ni nini wajibu wao, katika mchakato huo wa wageni kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi ilianzishwa tangu mwaka 2001 kwa Sheria ya Bunge Na. 30 ya mwaka

1997. Lengo kubwa ni kutafiti kuhusu ujenzi wa nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya bei nafuu. Hili ni jambo jema kabisa na inaonyesha kuwa wanashirikiana na Halmashauri na Miji katika utendaji wa kazi zake. Aidha, sasa wakala huyu anazihamasisha Halmashauri na Miji kuunda *Grassroots Building Brigades* kwa lengo la kuhakikisha teknolojia hiyo inafika hadi ngazi za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona, kuwa teknolojia hiyo ingeweza kufika inakotakiwa kwa haraka sana kama ingewekwa kwenye mitaala ya Vyuo vya Ufundu Stadi (*VETA*). Tunashauri hilo kwani kwa sasa mafundi wengi ambao wanatumiwa katika shughuli za ujenzi mijini na vijijini ni wale waliomaliza katika vyuo hivyo. Hili linatokana na hali halisi kuwa wananchi wanaweza kumudu bei zao za kutolea huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuwa ni ukweli kuwa miji mingi imepangwa vibaya mno kiasi kwamba inasababisha hata Serikali kutoa huduma za msingi kwa wananchi. Je, suala hili katika kadhia nzima ya ujenzi wa nyumba bora na za bei nafuu limezingatiwa vipi? Serikali inakiri kuwa kuna udhaifu mkubwa wa watendaji kutokutekeleza sheria zilizopo na pindi muda ukishapita katika utekelezaji inaonekana ni uonevu kwa wananchi. Hili nalo linatakiwa kufanyiwa kazi ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Miji ya Pembezoni ili kupunguza msongamano wa watu na magari. Kambi ya Upinzani imekuwa ikitisemi mara kwa mara kuwa wananchi wamekuwa wako hatua mia (100) mbele ya Serikali na hivyo kusababisha Serikali mara kwa mara kulipa fidia kutokana na kutokuwa makini katika mipango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Serikali inaelewa kuwa baada ya miaka 30 ijayo kuanzia sasa idadi ya watu itakuwa ni kiasi gani na hivyo ni jukumu la Serikali kupanga mipango yake ya makazi ya watu na huduma za kijamii kwa watu watakaokuwepo kwa kipindi hicho. Hivyo Mji kama wa Dar es Salaam na Pwani zinatakiwa sasa hivi ziwe na ramani za miji ya pembezoni tayari ambazo wananchi wanatakiwa wajenge kulingana na ramani hizo. Vinginevyo itakuwa kama yaliyotokea kwenye mji mpya wa Luguruni ambapo watendaji kwa kushirikiana na wanasiwa wamejichotea fedha za walipa kodi katika zoezi la kulipa fidia. Tunarudia tena tuwe na mipango ya maendeleo ya muda mrefu na sio mipango ya kulipua tu kutokana na mahitaji ya muda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi. Tanzania kwa sasa imekuwa na Tume nyingi mno ambazo kwa njia moja ama nyingine zinafanya kazi ya kurudufu kazi za tume nyingine, Tume hii imekuwepo lakini migogoro ya matumizi ya ardhi imekuwepo na inazidi kuwepo. Aidha, mapato yatokanayo na ardhi hayakidhi

japokuwa Tanzania tuna ardhi kubwa sana. Tulitarajia kuwa ardhi itoe mchango mkubwa sana katika bajeti ya Taifa na hivyo kupunguza utegemezi wa miaka yote kwenye bajeti ya nchi, hilo bado halijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwa kuwa Tume ya Mipango imekwishaanzishwa, hivyo tume zote zinazohusiana na jinsi gani Tanzania ya miaka ijayo itakavyokuwa katika sekta zote zingevunjwa ili kuipa nguvu kiutendaji Tume moja ya Taifa ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kwa njia hii kutakuwa hakuna kurushiana mpira kiutendaji. Haiwezekani kuwa na Tume ya mipango ya ardhi peke yake na huku kuna Tume ya Mipango ya Taifa, ambayo kwa mantiki halisi na ardhi ni sehemu yake. Kwa njia hii tunaweza kupunguza ukubwa wa Serikali kwa kuunganisha taasisi ambazo zinafanya kazi zinazohusiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba (*NHC*). Kama tulivyokwishaona kwenye semina iliyofanyika juzi na vyombo vya habari, kuhusu mpango mkakati wa kubadili kabisa mwelekeo wa Shirika la Nyumba la Taifa na kuliletea heshima kubwa Shirika hili mionganoni mwa jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi matarajio ya Watanzania, menejimenti ya shirika inaangalia upya muundo wa Shirika la Nyumba la Taifa ili kuona kama muundo uliopo unakidhi haya matarajio ya Watanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari chini ya mpango mkakati wake Shirika limeendesha zoezi la kuwatambua wapangaji wanowapangisha watu wengine katika nyumba zake kwa kulangua (*sub letting*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni kawaida kwa wapangaji kuendesha biashara ndani ya biashara, maana kuwa wao ni wapangaji lakini wanakuwa wao ndio *National Housing* kwa kupangisha na kuchukua kodi. Hili lilikuwa limeota mizizi na kulifanya shirika liendelee kuonekana miaka yote ni tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudzi za uongozi mpya suala hilo litafikia tamati na Serikali itapata stahili yake. Kwa hivyo, ni vema tukampongeza kwa hatua hiyo, kwa kuwa unyonyaji huo ulikuwa hauinufaishi *NHC* wala Taifa bali watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika biashara hiyo ya kupangishana nyumba hizo wapangaji halali walikuwa wakililipa Shirika kodi ndogo huku wao wakipata mamilioni ya fedha. Kwa mfano, kuna nyumba mpangaji mmoja alikuwa akililipa Shirika shilingi

200,000/= kwa mwezi na yeze kupangisha mtu mwagine kwa shilingi milioni 2.6 kwa mwezi na hapa kodi hiyo ililipwa kwa mwaka ambayo ni sawa na shilingi milioni 30.2. Wengine walikuwa wakililipa Shirika shilingi 150,000/= kwa mwezi na kupangisha watu wengine kwa laki nane hadi milioni 1.5. Mlolongo hapa ni mrefu na hii ni mifano michache tu, Serikali imekuwa ikilalamika kila mara na kuwa na bajeti tegemezi kila mwaka, kumbe fedha halali za Serikali zinaingia mifukoni kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali na Waheshimiwa Wabunge wote kuliangalia suala hili, hivyo basi, biashara hii katika nyumba za umma haipaswi kuendelea kwani ni unyonyaji na dhuluma kwa Watanzania wengine na isitoshe imekuwa ikiipotezea Serikali mapato kwa kuwa ni mfumo wa siri unaokwepa kodi halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tutoke hapa tulipo tunahitaji Watanzania wa kuthubutu na hayo ni maamuzi magumu ambayo lazima waliokuwa wananaufaika wataanza kupiga kelele. Kadhalika, wameshafanya maamuzi magumu kwa kufuta mikataba 55 ya miradi ya ubia, kwa watu walioingia mikataba na Shirika, lakini miaka mitano au zaidi ikapita na hawakuweza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke wakati barabara ya Ubungo inajengwa, Mheshimiwa Magufuli akiwa Waziri wa Ujenzi alifanya maamuzi magumu na alipata lawama nyingi lakini sasa kila mtu anafurahi barabara hiyo ilivyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba tuwaunge mkono kwa dhati kabisa kwa kuchukua maamuzi ya kuleta faida kwa Watanzania walio wengi. Kwa ujumla kuifuta mikataba hiyo ni kurudisha mali hii kwa Watanzania wenye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mawasilisho mazuri yenye lengo la kuunga mkono hatua ambayo Serikali imechukua. Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji wengi lakini kwa utaratibu wetu nadhani kila mtu atafikiwa. Sasa tuanze na wale ambao hawajapata nafasi kabisa ya kuchangia katika kipindi hiki cha bajeti. Yuko Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, atafuatiwa na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami na baadaye Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, atafuatia. Hawa ni wale ambao hawajachangia kabisa, halafu watafuata waliochangia mara moja ambao ni Mheshimiwa Ephraim Madeje, atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert Mtangi na wengine nitawataja baadaye.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema na ulinzi wake, jinsi alivyoniokoa na alivyoniponya katika ajali ambayo ilitokea tarehe 6 Mwezi wa tano, 2010. Lakini, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Spika na wewe mwenye

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi yako kwa ujumla, niishukuru Serikali, *IGP*, niwashukuru wataalam katika Wilaya yangu ya Bukombe kwa jinsi walivyoshughulika na Jeshi la Polisi, nimshukuru Mke wangu kwa jinsi alivyonihudumia, pia Dr. Sharif pale *MOI* kwa jinsi alivyonihudumia. Mungu awabariki na wanasiasa faida na maombi yangu kwenu ni kwamba, Mungu awasaidie mshinde katika uchaguzi ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika Kituo chetu cha Polisi wamenisaidia sana, nimeona kupitia maombi yao ya kupata umeme kituoni, tumekubali kupitia Kamati yetu kupitia Mfuko wa Jimbo tutawawekea *Solar* ili waweze kufanya kazi vizuri katika Kituo chao cha Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba waliyoiweka mbele yetu leo. Ninayo machache nitakayotaka kuzungumza katika hotuba hii. Suala la kwanza naona wameligusia katika ukurasa wa 63, suala la fidia. Nimeona nitumie nafasi hii kuongelea suala la fidia. Ni kweli fidia zinazotolewa kwa watu katika maeneo yao ni ndogo sana, kama walivyoeleza kwamba, wadau wengi wamelalamikia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo tatizo katika Wilaya yangu. Wako wananchi ambao wameondolewa katika maeneo yao kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya, lakini katika maeneo yao fidia waliyopewa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mfano wa maeneo machache katika eneo la Ushirombo pale Mjini eneo la Butambala, unakuta mwananchi amefidiwa na amepewa hundi ya shilingi 15,000. Mwananchi huyo alikuwa anaishi katika eneo lile, na hawa watu wamehangai sana, eneo la Katente. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kufidia watu hawa. Sheria ya Ardhi Na. 5 na Na. 9 za mwaka 1999 na Na. 8 ya mwaka 2007 zitumike ipasavyo kwa sababu wananchi hawa wanahangaika. Fidia hiyo wamepewa kutoka mwaka 2007, wamezunguka katika Wizara lakini bado hawajapata msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wapo wananchi katika eneo la Maganzo, hapo hapo Mjini Ushirombo. Baba Askofu ametusaidia amejenga Kituo cha Afya kizuri sana, wamepata ufadhili. Mfadhili akasema ye ye uwezo wake ni kujenga kituo, hivyo Serikali imsaidie na ye ye kuchangia kwa kulipa fidia wananchi. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna ya kumsaidia pengine zile fedha zinazokopeshwa kwenye Halmashauri kutoka Wizarani, mtusaidie mikopo hii kwa ajili ya kuendeleza maeneo katika Wilaya yetu, kwa sababu vinginevyo wananchi hawa tutawaondoa katika maeneo yao lakini wataendelea kubaki maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali isimamie hili vizuri. Lakini pia kwa ajili ya wale waliofidiwa pesa kidogo sana, wengine wamepewa hundi ya mia mbili kumi na kitu. Kwa hiyo, tuombe labda Mheshimiwa Waziri, anapohitimisha atoe kauli awaambie hawa wananchi wanafanyaje. Kwenye maeneo waliyoondolewa zimegawiwa

Taasisi mbalimbali. Zile Taasisi hazijalipa fidia yoyote na tunapata shida sana na kwa hiyo, tunaomba watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni Kilimo Kwanza. Suala la Kilimo Kwanza, linakuwa ni gumu sana kufanikiwa katika Wilaya yetu ya Bukombe kutokana na wananchi kutokuwa na Hatimiliki za maeneo yao, kwani wanashindwa kupata mikopo kutoka katika maeneo mbalimbali. Naipongeza Serikali, mwaka 2007 walipima vijiji katika Wilaya ya Bukombe lakini hadi leo hawajatoa Hatimiliki katika Vijiji vile jambo ambalo linafanya hata Hatimiliki kwenye maeneo ya mtu mmoja mmoja iwe vigumu sana kupatikana, kwani hadi sasa hakuna aliyepata hata mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapohamasisha Kilimo Kwanza na wananchi hawana zana za kutoa dhamana ili waweze kupata mikopo, inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie mbona, tumeppima mipaka ya vijiji muda mrefu sana, toka mwaka 2007 mpaka leo, nini kinachelewesha hapa katikati? Naomba Serikali ifuatilie, itoe Hatimiliki katika vijiji vyetu ndani ya Wilaya ya Bukombe ili wananchi waweze kupewa Hatimiliki za kimila na hapo ndipo watakapoweza kukopesheka na kupata hata mikopo kwa ajili ya kuendeleza Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iliangular hili na ikiwezekana Mheshimiwa Waziri atwambie ni kwa nini imechukua muda mrefu sana bila ya Wilaya ya Bukombe kupewa Hatimiliki, hata kijiji kimoja, hakuna mwananchi hata mmoja, wananchi zaidi ya laki tano na kitu na ambapo Serikali imechagua eneo la Bukombe kuwa Ghala la Chakula, tunafanyaje kilimo chetu, tunapataje mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ilisimamie hili na iendelee kutusaidia ili wananchi hawa waweze kukopesheka. Tunapata tabu mno, sasa hivi maeneo mengi katika Wilaya yetu ya Bukombe yanafaa sana kwa kilimo, lakini kilimo hakitusaidii kwa sababu wanalima kwa jembe la mkono. Hivyo, naiomba Serikali ilifikirie hili katika bajeti yake hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema leo sizungumzi mengi sana, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa jinsi walivyotusaidia katika Wilaya yetu ya Bukombe. Wametuongeza Kata, wameongeza Jimbo, wameongeza Wilaya, na wametupa Mkoa. Kwa kweli, hii ni heshima kubwa sana, naamini wananchi wa Bukombe kuitia heshima kubwa ambayo imetolewa na Serikali ya Awamu ya Nne, wataendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Bukombe kwa jinsi wanavyoniamini na jinsi watakavyoendelea kunipa ushirikiano. Kimsingi tumekuwa na Majimbo mawili, naamini wanajua mchango tuliofanya. Hivyo, nawaomba waendelee kutuunga mkono. Wapo watu wengi ambaao walipita wakasema huyu sasa hivi hata akili zake zimechanganyikiwa. Nasema hapana, mimi ni mzima na naomba, tuwe pamoja na nitakuja kugombea katika Jimbo la Bukombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nimtakie Mheshimiwa Waziri kazi njema kwa utekelezaji wake na Mungu ambariki sana. (*Makofi*)

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nikiwa mtu wa pili kuchangia katika Wizara hii. Mwanzo kabisa, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mawili, matatu ya kusema katika eneo hili, nianze na sehemu ya kwanza ambayo ni upimaji. Naishauri Wizara ijitahidi kuhakikisha kwamba inapima vijiji vyote katika nchi hii maana ukipima vijiji na kuwapa hati wanavijiji, hapo ndipo watakuwa na uhakika na ardhi yao. Lakini pili, kupima vijiji kunasaidia kuondoa migogoro ya kugombana kati ya kijiji na kijiji ama kugombania maeneo kati ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, katika eneo hilo la pili vijiji vinapopimwa iwe sambamba na kupima maeneo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni wazi bado kuna mgogoro katika baadhi ya mipaka ambapo baadhi ya nchi, nina ushahidi na nchi moja siwezi nikaitaja ya jirani ambayo walikuwa na tabia ya kusogeza yale mawe ya vipimo (*beacons*) ndani ya nchi yetu. Niliona kwa macho, jambo ambalo sio zuri. Lakini pia tukiwa kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali, Ofisi yako ilikubali kupitia Katibu Mkuu kwamba ni kweli jambo hilo limekuwa likitokea hapa na pale. Kwa hiyo, nashauri kuwa makini sana katika suala zima la upimaji wa ardhi katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitendawili ambacho hatujui kitateguka lini kati ya mpaka wa Malawi na Tanzania hasa kwa upande wa Ziwa Nyasa. Ukienda Malawi unakuta lile Ziwa lote kwenye kingo ya mipaka ya Tanzania linajulikana kwamba ni la Malawi na linaitwa Ziwa Malawi, lakini ukiija Tanzania tunaliita Ziwa Nyasa na katika mipaka yake kwetu inaonekana tunagawana katikati, kitu ambacho kwao hakipo. Lakini kwa upande wa Msumbiji wao wamekata katikati kwa maana Msumbiji na Malawi wanapakana katika Ziwa hilo la Nyasa lakini kwa huko linajulikana Malawi. Mimi nadhani hapa inatakiwa ufumbuzi wa haraka ufanyike lakini tupewe maelezo ya kina, tatizo ni nini? Kila mwaka maongezi, tatizo ni nini hasa, tujue.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya Mikoa na Wilaya na yenyele bado haijajulikana vizuri. Hili jambo litachukua mpaka miaka mingapi, haijulikani. Mimi mwenyewe katika Wilaya yangu ya Nkansi kwa upande wa Kaskazini bado haijulikani mpaka halisi ni Lyamba la Mfipa au ni eneo la kupita Lyamba la Mfipa eneo la

Kanyamkaa. Wakati mimi nakua kwa mfano ukifika eneo la Kanyemkaa karibu na pale inapoanza Mbuga ya Katavi pale ndipo mpaka ulikuwepo. Palikuwa na kibao kinachoonyesha sasa unaingia eneo la Sumbawanga kwa maana ya Ufipa. Baadaye ikaonyesha kwamba ni eneo la Kizi, lakini baada ya kugombanagombana ikaonekana Lyamba la Mfipa na pale kibao kilipo leo ni mwanzo wa Lyamba la Mfipa pale unapotokea barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda. Sasa na eneo hilo tulitazame vizuri, je, vipimo vinasemaje hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria zinazohusiana na vijiji au ardhi, nashauri sheria zote zitafsiriwe kwa Kiswahili. Ninashukuru baadhi ya sheria hata zile za Mabaraza ya Ardhi zimetafsiriwa kwa Kiswahili lakini, je, sheria zote zinazohusiana na ardhi maana zinamgusa mwananchi kwa ukaribu zaidi mmezitafsiri kwa Kiswahili ili wananchi waweze kuelewa? Nadhani haijafanyika hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika Mabaraza ya Vijiji, Kata na kuendelea, Sheria hizi kwa Wanakamati wenyewe wa Vijiji, wale Wajumbe saba wenye mnyumbuliko wa tatu kwa nne au Wajumbe tisa wenye mnyumbuliko wa nne kwa tano bado wanavijiji pia hawajafahamu vizuri sheria hiyo na matokeo yake baadhi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanaingilia kusikiliza na kuhukumu kinyume cha sheria kesi ambazo Mabaraza ya Ardhi yalipaswa kuzisikiliza na kuzitolea maamuzi. Wanafanya hivyo kwa makusudi na mbaya zaidi wanakula hata rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yupo Hakimu mmoja katika Mahakama ya Mwanzo ya Namanyere ambapo alihukumu kinyume cha utaratibu, wanakijiji wa Kamati ya Ardhi ya Kijiji cha Lunyala pale karibu na Namanyere wote walitozwa faini ya shilingi 60,000/= kila mmoja au kifungo cha miezi nadhani mitatu au minne. Wananchi wale walilipa hiyo faini nami niliweza kulishughulikia mpaka Mahakama Kuu, lakini uamuzi bado unasuasua, Hakimu yule bado yupo na bado anazidi kuwanyanyasa wananchi na Mahakama yenyewe inawasaidia hao Mahakimu. Kama suala nimekwishalifikisha Mahakama Kuu ili waweze kulifanyia ufumbuzi, Mahakama Kuu iliyopo pale Sumbawanga hawatoi jibu lakini kumbe tunapata habari kwamba wao wanashirikiana na Hakimu huyo katika kudhulumu haki za wananchi, je, hiyo ni sawa? Chombo ambacho tunasema kinatoa haki kwa wananchi, wamekaa kimya? Sasa kwa kuitia Wizara yako, ninaomba uwasiliane na wahusika hao ili kumbaini huyo Hakimu ambaye amefanya unyama huo na sheria dhidi yake zichukulike na msizidi kuwanyanyasa wananchi kwa sababu wengi hawazijui hizi sheria, si vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miji yetu ipimwe na ninashukuru kwa uamuzi mzuri wa kupima eneo lile la Kigamboni na kuonyesha jinsi ambavyo mji ule utakuwa ni wa kisasa. Hili pia liwe ni funzo kwa maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niishukuru Wizara hii jinsi ambavyo imeweza kutupatia fedha za *Revolving Fund* ili tuweze kuupima mji wa Namanyere na mji huo uwe mzuri sana na katika mkoa wa Rukwa sidhani kama kuna mji ambao umepimwa

vizuri kama mji ule wa Namanyere. Ni mji ambao ni mzuri sana. Lakini Mheshimiwa Waziri, naomba Wizara yako mnisaidie kutupatia fedha nyingine maana uwezo wa kulipa tunao kuliko Halmashauri nyingine na hiyo inathibitika wazi katika mafaili yako. Tupewe fedha nyingi ili tuweze kupima maeneo mengine yale ya Isunta, Mji mwema, pamoja na maeneo mengine katika eneo ambalo barabara ya lami itapita, naomba hilo tusaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba Sheria za Ardhi ziende sambamba na zile Sheria za Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ili pasiwepo na malumbano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ninaomba kuunga mkono tena hoja hii kwa mara ya pili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Ephraim Madeje atafuata halafu Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Magalle Shibuda na Mheshimiwa Michael Laizer wajiandae.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii. Napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kutuandalia hotuba nzuri ya bajeti ambayo inaleta matumaini. Nawapongeza pia kwa mafanikio makubwa waliyoyapata katika Wizara yao pamoja na watendaji wao katika kipindi cha miaka mitano. Kwa kweli mmefanya mambo makubwa na mazuri. Nawapongeza hasa kwa kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vile vilivyokuwa vimebakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya hapa na pale ambayo yanapashwa kurekebishwa. Kwanza, ujenzi holela, ni tatizo kubwa kwenye miji mingi. Wote tunajua kwamba mji ukishajengwa kiholela, inakuwa ni vigumu kuupanga. Hata ukitaka kuweka miundombinu ya barabara, maji inakuwa ni tatizo. Ikitokea janga la moto hata magari ya Zimamoto inakuwa si rahisi. Lakini la kushangaza wakati watu wanaanza kujenga, Serikali inakuwa inawaona, inasubiri mpaka wanajenga nyumba zinaisha basi unakuta ndio wanaanza kubomoa. Naishauri Serikali kwamba ipime maeneo yote kuepusha usumbufu wa kuwabomolea watu nyumba zao na vile vile kuepusha Serikali kuwajibika kulipa fidia kubwa. Vile vile nilikuwa nashauri kwenye vile viwanja vitakavyokuwa vimepimwa vitolewe kwa bei ndogo. Sasa hivi viwanja vinatolewa kwa thamani ya shilingi 400,000/=, 800,000/=, 1,000,000/= je, ni Mtanzania gani wa kawaida ana uwezo wa kuchukua hivyo viwanja? Msipoangalia viwanja vyote vilivyopimwa vitaishia kwa watu wenye uwezo tu. Nilikuwa napendekeza Serikali iangalie itafanya nini kuhakikisha kwamba na watu wa kawaida wanavipata vile viwanja na viwanja hivyo vitolewe kwa gharama ndogo. Watanzania wengi wangependa kuishi katika nyumba nzuri za kisasa, lakini kwa sababu ya uwezo basi unakuta Watanzania wengi wanaishi katika nyumba ambazo sio nzuri na wala sio za kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ushirika wa nyumba, unaweza ukawa ndio mkombozi kwa tatizo hili. Unaweza ukawasaidia wale wananchi wenyewe uwezo mdogo ambao hawana fedha nyingi kwa wakati mmoja wa kuweza kujenga nyumba. Naipongeza Serikali kwani kwa kupitia hotuba hii tumeambiwa tuendelee kuwashawishi wananchi, kuhamasisha waweze kuanzisha ushirika wa kujenga nyumba, wajenge nyumba nzuri waweze kuishi katika nyumba za kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kagera, tayari tumeshaanzisha ushirika wa kujengeana nyumba katika Wilaya ya Muleba, Bukoba, Missenyi na Karagwe. Wanawake wamejiunga, wanaendelea kudunduliza akiba zao polepole, kinachohitajika sasa hivi ni tupate wapi fedha ikiwa kama msaada au mkopo ili kuweza kujengea nyumba zile za kwanza na hii iendelee kuwa kama *Revolving Fund*. Nyumba hizo zinazojengwa zitakuwa ni nzuri, za kisasa, nyumba hizi zinatakiwa kujengwa katika maeneo yaliyopimwa, Serikali itatakiwa kuweka miundombinu, maji barabara hao akina mama wanachama, mwanachama anakabidhiwa nyumba ikiwa imekamilika ndio mkopo wake na ye ye mwenyewe anaendelea kulipa pole pole huo mkopo na atarejesha katika miaka 15 hadi 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika kama huu upo nchini Uganda, nchini Kenya na unafanya kazi vizuri. Ushirika kama huu huko Marekani nimekwenda New York nimeona kwamba yale maghorofa mengi tunayoyaona yamejengwa kwa kupitia ushirika wa kujengeana nyumba na vilevile yanaendeshwa kwa ushirika huo. Katika bajeti hii, mmetutuma kwamba tuendelee kuhamasisha wananchi waweze kuunda ushirika kama huo, lakini kama niliyotangulia kusema wanawake wa Kagera wameshathubutu, wameanza, kuna wanachama zaidi ya 251 na wamesajili wameshakuwa na akiba zaidi ya shilingi milioni 34. Nawapongeza Wakurugenzi wote ambao wameshawapatia viwanja kwa mfano Mkurugenzi wa Halmashauri ya Missenyi. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, je, ni Benki zipi sasa Serikali imeziandaa au ni Benki zipi ambazo Serikali imeingia nao makubaliano ili tuweze kupata mikopo au misaada kutoka kwenye asasi hizo na tuziingize kwenye *Women Cooperatives* au *House Cooperatives* waweze kujenga nyumba nzuri na tuweze kupata makazi bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati namalizia mchango wangu, napenda kuwapongeza viongozi wetu akinamama waliotumia muda wao mwingi kuandaa mikakati, kushawishi hadi idadi ya wanawake ikaendelea kuongezeka, wakaendelea kuchaguliwa kuwa viongozi na wakaendelea kuwemo kwenye vyombo vyamuzi. Pongezi hizi ziwaendee Mama Anna Abdallah, Mama Anne Makinda, Mama Getrude Mongella, mimi binafsi wamekuwa msaada mkubwa kwangu kwani mara zote wamekuwa washauri wangu na wamekuwa wakiniongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, kwa kuwa nachangia kwa maneno ikiwa mara ya kwanza, nawapongeza wanawake wa CCM wa Mkoa wa Kagera walioniweka madarakani miaka mitano iliyopita. Nimeshirikiana nao, tumefanya mambo mengi mazuri na makubwa, ni tegemeo langu kuwa sikuwaangusha. Ninawapenda na nyie mnanipenda. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kukipongeza Chama cha Mapinduzi ambacho kimeridhia kwamba sasa wanawake katika uongozi tufikie 50 kwa 50. Kwa sababu hiyo basi nawapongeza wanawake wote wa Mkoa wa Kagera waliokwishatangaza nia ya kugombea Udiwani na Ubunge. Nyie ni majasiri, msiogope, mnaweza. Wale wanaowasema vibaya, wakawakatisha tamaa au kuwachafua msiwajali, hawana mwelekeo, nia yao ni kupunguza kasi yenu tu. Msikate tamaa, endelea mbele kwa mbele, nina uhakika kwamba mtashinda. Ndugu zangu wakazi wa Mkoa wa Kagera na mimi nawatangazia kuwa ninakuja kugombea. Naomba mnipokee na mniunge mkono. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja na namtakia mafanikio Mheshimiwa Waziri tunategemea kuwa naye katika Bunge lijalo.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja. Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyoitoa na pia kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi kilichopita na kwa mipango yao mizuri ambayo wameiwakilisha hapa kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya maamuzi ya kuhamia Dodoma takribani zaidi ya miaka 30 iliyopita. Uamuza huo, sisi watu wa Manispaa ya Dodoma, tuliupokea kwa mikono miwili na kwa kweli tunaendelea kuukubali na bado tunaendelea kuutarajia na kuona siku ambapo ndoto hii itatimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili azma hii ya Serikali itimizwe, Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (*CDA*) iliundwa. Iliundwa kwa nia njema kabisa na ni chombo ambacho kimefanya mengi ambayo ni mazuri. Sasa leo naomba nizungumzie matatizo yanayohusu fidia kwa wale ambao wanatwaliwa ardhi yao katika Manispaa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati *CDA* ilipoundwa, ilipewa hatimiliki ya eneo lote la Manispaa. Kwa bahati mbaya kabisa, kwa kipindi kirefu hadi sasa hivi kumekuwa na migogoro mingi sana kuhusu ardhi. Sisemi kwamba inatokana na huo uamuza wa Serikali lakini ni kwamba hilo tatizo lipo. Hivi sasa kuna kesi nyingi sana, kesi za vikundi vyta wakazi na kesi nyingine za watu binafsi dhidi ya Serikali. Hawa watu wametafuta Mawakili katika kujaribu kupigania haki zao. Kama nikiwataja kwa uchache kuna wananchi wa Chinyoa wameweka Wakili ili wasibomolewe makazi yao kwa sababu wameshakuwepo pale zaidi ya miaka 15. Vilevile kuna wenzao wa Njedengwa, kuna watu binafsi na baadhi ya wananchi walipewa fidia ambayo wanalamikia kwamba ilikuwa haitoshelezi kufuatana na Sheria, hao ni wananchi wa Ng'ong'ona ambao walipisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Lakini pia wafanyabiashara ambao wamekuwa wakitoa huduma muhimu kwenye maeneo ya katikati ya mji huu ambao nao pia wanatishiwa kubomolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nililet hili suala kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika kwa sababu mara kwa mara nimekuwa nikilizungumzia hapa Bungeni lakini kwa bahati mbaya hili suala huwa linaelekezwa kwa Ofisi ya Waziri

Mkuu kwa sababu ndiyo wenyewe dhamana ya *CDA* na katika kufanya hivyo mara nydingi huwa linaishia *CDA*, yale mambo ambayo huwa nazungumza hapa yanaishia *CDA* na *CDA* ndiyo wanajibu. Sasa mimi hivi leo ninamwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya ardhi, atamke waziwazi na pia ikiwezekana atoe maelekezo kwa *CDA* kwamba kwenye masuala ya fidia Sheria zipo na zipo wazi na kwa kweli ni muhimu zitekelezwe. Mimi ombi langu ni hilo wala si zaidi ya hapo ili hao wananchi wa Dodoma ambao kwa kweli tumepiga kelele kwa muda mrefu sana kuhusu masuala ya ardhi waweze kupata angalau faraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze zaidi ninachotaka sio kwamba *CDA* isipange Mji huu, tunajivunia kwamba kati ya miji ambayo imepangika vizuri sisi tuna asilimia kubwa lakini kitu ambacho tunataka ni kwamba pale ambapo Sheria ya Ardhi inamlinda mwananchi huyu, ni aibu kwa hawa wananchi kuanza kuhanganya kutafuta Mawakili wakati Serikali, Katiba na Sheria ipo ambayo inamlinda huyu mwananchi. Kwa hiyo, tunaomba sana kwa kweli hili suala liangaliwe. Najua labda kuna matatizo ya Itifaki au madaraka kwa sababu Waziri wa Ardhi labda yuko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu lakini hilo mimi nadhani tungeliweka pembedi tuangalie haki za wananchi na jinsi ya kuzikidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli sina mengi zaidi, naomba tena kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini, kwa imani ambayo wamekuwa nayo kwangu mimi. Katika hili, naomba nizungumzie kwa masikitiko sana tukio moja ambalo lilitokea tarehe 28 mwezi wa Juni. Tarehe hiyo magazeti mawili yalinishushia kashfa ambayo ilikuwa ni nzito sana kwamba nilikuwa nimetoa rushwa wakati nilipogawa sare za Chama cha Mapinduzi kwa Makada wa CCM. Ni kweli niligawa hizo sare lakini ilikuwa ni ahadi ya muda mrefu sana zaidi ya mwaka mmoja na nusu na niligawa baada ya kupata ridhaa kamili kabisa ya Ofisi ya Chama, Wilaya na katika kugawa hizo sare ilikuwa Katibu awepo wakati nafanya hicho kitendo lakini kwa bahati mbaya alipata dharura akawa ameenda Dar es salaam, alikuwa anauguliwa. Kwa hiyo, napenda wananchi wa Dodoma Mjini waelewe hilo na wasiwasikilize wale wote ambao wanataka lieleweke vinginevyo. Najua hii kashfa ilikuzwa na wale ambao hawanipendi. Lakini mimi nasema watashindwa na watalegea moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kwamba naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kusema machache katika siku hii ya leo. Lakini nianze pia kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya TAMISEMI na Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kuisaidia Wilaya ya Muheza kupata Kata kumi kwa sababu watendaji wa Wilaya ya Muheza walipoalikwa kuja TAMISEMI barua ilichelewa kuwafikia, kwa hiyo, wakati wa kufanya tathmini hawakuja na kwa hali hiyo Muheza tulitolewa nje. Lakini kwa sababu ya msaada huo nilioutaja kwa viongozi hao tumefanikiwa kupata Kata mpya, nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie watu wa Muheza kwamba wapo wanaotaka kuwadhalilisha watoto wa Muheza, kila siku wanawaonesha katika vyombo vya habari kwamba wanatembea bila viatu. Wanania mbaya hawa, huwezi ukawa na dhamira ya kutaka kuwa Mbunge au kutaka kura halafu unawadhalilisha wazazi wa watoto wale ambao unataka kwenda kuwaomba kura, nasema washindwe.

**MBUNGE FULANI:** Na kulegea. (*Kicheko*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme vilevile kwamba wananchi wangu wa Muheza wasiwe na wasiwasi, tatizo la maji, ni kweli lipo lakini waliochangia kwa kiasi kikubwa kuleta tatizo hilo ni baadhi ya wananchi wenyewe wa Muheza waliokuwa wanafanya kazi katika Wizara yenye ya Maji na Umwagiliaji, wakatoa hatimiliki ya maji ya Mto Zigi ambao chanzo chake ni Wilaya ya Muheza kule Amani, hatimiliki hii wakapewa watu wa Tanga Mjini bila kujali Muheza wanahitaji maji. Nataka kuwahakikishia wananchi wa Muheza, tumekwisharejesha hatimiliki ile na mpango wa Benki ya Dunia unaendelea vizuri kabisa, maji yatapatikana bila wasiwasi. Katika awamu ile, mpango wa kudumu wa muda mrefu tutapata maji kutoka Mto Zigi na hatimiliki tumeshairejesha. Ili kuwathibitishia, sasa maji kutoka Pongwe yamefika katika Kata za Mlingano na yameshafika Chuoni. Kwa hiyo, tunafanya kazi kubwa na tutafanikiwa kuondoa tatizo la maji kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie habari ya ardhi na bila shaka nianze tena kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi ngumu na nzito sana na hana Naibu lakini anajituma kweli kweli. Katika matatizo ya Ardhi, Wilaya ya Muheza amekuja. Waheshimiwa wote mnafahamu Wilaya ya Muheza imezungukwa na mashamba zaidi ya 18 ya Mkonge. Ukianzia Hale hapa unakwenda mpaka Pongwe kushoto kwako na kulia kwako ni Mashamba ya Mkonge matupu ambayo yako kwa idadi kubwa wala hayaendelezwi. Sasa ukifikiria mashamba hayo yalichukuliwa miaka 80 na 90 iliyopita wananchi wakahamishiwa katika sehemu za milimani na sasa wananchi wamezaliana kwa wingi kweli kweli, wataishi wapi kama sehemu yote ya ardhi asilimia 60 ya Wilaya ya Muheza ni ya Mashamba ya Mkonge, sisi tutaishi wapi? Tulihamishwa katika maeneo ya mtandao na Mabonde, tukakimbilia milimani, leo katika mpango mzima wa kuhifadhi mazingira, wananchi wanaambiwa sasa wananchi watoke milimani ili kuhifadhi misitu. Wananchi 1,028 wa Derema, Amani wameshalipwa fidia kutoka Benki ya Dunia na wanatakiwa warudi sasa mabondeni. Wataishi wapi kama mashamba 19 yote yapo hayaendelezwi na wao hawana ardhi watakwenda kukaa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri alifika akaona hali halisi. Katika Shamba lile la Kibaranga, amekwenda kule Azimio Ranchi, amekwenda Kilapura kote na amefika Bembwera kote, ameona hali halisi. Ni matumaini yangu kwa kweli Mheshimiwa Waziri baada ya Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuomba mashamba ambayo hayaendelezwi hati zile za zamani zifutwe ili ipatikane nafasi ya kutoa ardhi kwa wananchi wenye matatizo, hilo litakamilishwa. Najua umeshachukua hatua kubwa baada ya Baraza hilo kukamilisha hatua zake na ninaimani kabisa baadhi ya mafaili ya kuomba hatimiliki zifutwe sasa yako

katika meza ya Mheshimiwa Rais ambaye yeye ndiye mwenye mamlaka ya mwisho ya kufuta hatimiliki kwa yale maeneo yasiyoendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu mgogoro wa shamba moja japokuwa yote yana migogoro lakini hili moja ni shamba ambalo lina mgogoro zaidi Shamba la Kumbulu. Shamba hili, wananchi wameshaandika barua wamempelekea Mheshimiwa Waziri, wamepeleka kwa Waziri Mkuu, wamepeleka mpaka kwa Rais ya kutishiana maisha, wako tayari kufa. Hilo ndilo walilosema. Mimi nimeona kumbukumbu za barua ambazo umemwandikia Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwamba waende Kumbulu waondoe tatizo hilo na sina hakika kama Mkuu wa Mkoa wa Tanga na Mkuu wa Wilaya ya Muheza wamefikia wapi. Lakini nilichotafuta mimi na nikakiwasilisha ni kwamba shamba lile la Kumbulu liliuzwa kwa mwekezaji mmoja lakini mwekezaji huyu kwa bei hiyo ndogo sana aliopewa ni miaka 12 imepita hajakamilisha ulipaji wa fedha za shamba alilouziwa. Bado kuna zaidi ya shilingi milioni 12 anadaiwa kwa miaka 12 hajalipa. Sasa sisi Watanzania hivi kweli ndiyo aina ya wawekezaji tunaowatafuta? Tunamuuzia kwa bei ya shilingi milioni 40 halafu anachukua miaka 12 hatulipi fedha zetu halafu bado tunasimama tunasema tunao mkataba halali na mwekezaji huyu. Aibu tupu hii, hata kama mimi sijakwenda shule siwezi kuamini kama hapa kuna mkataba halali kwa miaka 12 bila kutulipa fedha zetu. Kwa nini Watanzania tusichukue nafasi hiyo ya yeye kushindwa kulipa fedha kwa miaka 12 kama eneo la mchakato wa kuondoa matatizo. Tunaweza kumwachia eneo la ardhi lakini hawa wananchi ambao wamekwishaingia pale tuwape nafasi ya kumiliki ardhi. Hilo nalo linatushinda?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala lingine la Shamba la Kwafungo. Hili kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri hakuwa amepata nafasi lakini alikuwa na dhamira ya kwenda kule Kwafungo. Hivi karibuni wananchi wamelima katika shamba hili la *Kwafungo Estate*, wakapanda mahindi, amri ikatolewa na Maafisa Maliasili, mahindi yao yakakatwa. Lakini Maafisa Maliasili wanadai kwamba wananchi wameingia katika eneo la misitu wakati mawe yanaonesha kabisa wako ndani ya eneo la Shamba la Mkonge la Kwafungo. Sasa hata Maafisa Ardhi hapa wanapaswa kusaidia na kumsaidia Mkuu wa Wilaya, kama yeye ndiye aliyetoa amri na hilo likafanyika alipaswa kuangalia kwanza kama ni kweli hawa wamevamia katika eneo la misitu au wako ndani ya Shamba la Kwafungo. Wananchi wale mimi nimewaambia ukweli kama kweli wako ndani ya eneo la misitu hata mimi kama Mbunge wao nafasi yangu ya kuwatetea ni ndogo sana lakini wanapokuwa wako katika eneo ambalo hawakustahili kutolewa, mimi kama Mbunge nitaendelea kusimama hata kama nitakuwa si Mbunge lakini nitakuwa nimeshaweka rekodi na wataalam wataendelea kuwafuatialia wananchi wale wawezekutukeneza haki yao wanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba muda ni mfupi, niliyokuwa nimedhamiria kuyasema ni hayo kwa leo, nakushukuru sana na nategemea Serikali italiangalia suala la mashamba katika Wilaya ya Muheza, tuweze kurudi katika maeneo yetu hata baada ya kuambiwa tutoke milimani tulikohamia, maeneo yote yamechukuliwa na mashamba ya mkonge, tunahitaji mahala pa kulima, hatutaweza kutekeleza Kilimo Kwanza kabla hatujapata ardhi. Tumenunua *power tiller* 50 na yamekwishasambazwa,

tunahitaji mahala pa kulima. Hatutaweza kutekeleza Kilimo Kwanza kabla hatujapata ardhi. Naomba Serikali ilitazame hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofī*)

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu niweze kuja ndani ya Bunge leo na kuweza kuchangia mchango wangu na nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pole kwa wasafiri wote wa Reli ya Kati ambapo vyombo vya habari vimetangaza kwamba treni imekuwa ikisimama zaidi ya mara 30 baada ya injini kufeli. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukue hatua za haraka ili kunusuru hali hiyo. Kama sasa hivi inafeli na haiwezi kwenda inaweza ikafeli *brake* ikapitiliza moja kwa moja halafu ikawa hatari zaidi kama yaliyotokea mwaka 2002 pale Igando - Msagali. Kwa hiyo, tunaomba sana, wananchi wale, wanalipa kodi wanahitaji usafiri wa kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia moja kwa moja kuhusiana na *issue* ya viwanja ambavyo walijigawiwa Madiwani pamoja na Watendaji wa Halmashauri ya Kigoma Vijijiini. Ni eneo la Kigoma Kaskazini, eneo la Mwandiga, eneo hilo ni Njiapanda ya kwenda Kasulu kuna mpango wa kujenga *Stand* kubwa pale na mpango huo utafadhiliwa na NSSF. Lakini mpaka sasa wameshindwa kufanya kazi hiyo kwa sababu vile viwanja bado wamevhodhi na Mheshimiwa Rais katika Kijiji cha Nyarubanda alitoa tamko kwamba watu wote waliochukua viwanja bila kufuata sheria wavirudishe. Sasa naomba kujua ufuatiliaji. Mheshimiwa Waziri unasemaji kuhusu hilo, umeshalipata na kama hujalipata, tunaomba ulifuatilie ili vile viwanja viweze kurejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wote tunavyofahamu kwamba ardhi ni mali, ardhi ni utajiri na mahitaji ya ardhi ni makubwa na yanaeleweka kabisa kwamba tunahitaji ardhi kwa ajili ya mashamba madogo na makubwa ya mazao ya kibiashara, kwa ajili ya miji na vijiji vilevile ardhi kwa wafugaji kwa ajili ya malisho yao na kwa ajili ya shughuli za viwanda, utalii na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa hayo ya ardhi, tumeona nchi yetu sasa imeingia katika matatizo makubwa, migogoro ya ardhi imekuwa mingi sana na ukiangalia kwa mwaka 2008/2009 kulikuwa kuna taarifa kutoka Wizara ya Ardhi ambayo ilionesha matatizo ambayo yapo na mashauri mbalimbali ya ardhi ambayo yalipelekwa katika Wizara hiyo. Wizara ilikuwa ikishughulikia matatizo ya ardhi au migogoro, 9,228 kipindi hicho lakini vilevile inaonekana kila mwaka matatizo ya ardhi au migogoro ya ardhi ambayo inafikishwa katika Wizara hiyo ni takribani 5,000 na

vilevile utagundua kwamba kuna mashauri mengine ambayo yameenea nchi nzima yanaendelea kufanyiwa kazi kama takribani 11,279. Bado kuna mengine ambayo hayajafikishwa katika mkondo maalum ili kufikishwa Serikalini ambapo ni koo na koo, ndani ya familia kunakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaona kabisa kwamba ardhi imekuwa ni tatizo kubwa kulingana na umuhimu wake. Tumekuwa tukishuhudia migogoro mingi ya wakulima kugombea mipaka, wakulima kwa wakulima wenyewe wakigombea mashamba, wakulima pamoja na wafugaji na hii tukiangalia mifano ambayo ilijitokeza kule Kilosa, Kiteto, Kilindi na maeneo mengine watu wamekuwa wakipigana na wengine wakipoteza maisha. Kwa mfano, Kilindi inasemekana watu karibu watano walifariki katika vita ile na nyumba 500 zilichomwa moto. Kwa hiyo, tunaona kabisa ardhi jinsi inavyoweza kusababisha matatizo katika nchi yetu. Ukiangalia pale Kilosa kuna watu wanane inasemakana walifariki na watu kama 800 walihama vijiji kwenda maeneo mengine ambapo napo walileta matatizo kwa sababu ardhi ile haikuwa ya kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba haya yanaweza yakatatuliwa kama Serikali yenye we itaamua kutumia vizuri takwimu zake na tafiti ambazo zilikuwa zikifanyika. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, walifanya tathmini ya kuangalia eneo gani ambalo linafaa kwa ajili ya malisho, ikaonekana kama kuna hekta milioni 88.62 ambazo zingefaa kwa malisho na wakaangalia kama wakitoa hekta milioni 60 tu ambapo inaweza ikahudumia mifugo kama milioni 20 na ukiangalia takwimu za Serikali zinaonesha kwamba mifugo iliyopo ni takribani milioni 19, kwa hiyo, kama wataamua kutumia vizuri takwimu hizo, wanaweza wakaepusha kabisa migogoro ambayo inatokea kwa wafugaji kukosa ardhi na kwenda katika ardhi ya wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukiangalia tafiti zingine zinaonesha kwamba hekta milioni 44 zinafaa kwa ajili ya kilimo. Lakini tukiangalia ambazo zinatumika sasa hivi ni hekta milioni 10.6 kwa hiyo hekta milioni 34 bado zipo. Ukiangalia kwa kaya kwa sasa hivi mwananchi anatumia hekta mbili kwa uwiano na ni tofauti Mkoa kwa Mkoa. Kwa hiyo, kama Serikali itaamua kutumia zile hekta 34 milioni zilizobakia maana yake tatizo la wakulima kukosa ardhi na kugombea ardhi litakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, bado kuna migogoro mingi kati ya wawekezaji na wananchi. Ukiangalia Barricks, tumekuwa tukisikia mara nyingi kuwa pale *North Mara*, watu wakipigwa risasi na wawekezaji kwa kuvamia eneo la migodi. Tukiangalia pia katika sekta nyingine ya utalii, kumekuwa pia na matatizo hayahaya ya wawekezaji kupambana na wananchi kwa mfano kule Loliondo na Gurumeti, Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia upande mwengine, Serikali na wananchi imekuwa na migogoro pale ambapo kunatakiwa kuendelezwa eneo fulani la makazi. Kwa mfano, ukiangalia upanuzi wa Kiwanja cha Ndege pale Kipawa, Dar es Saalam, limekuwa ni tatizo kubwa, wananchi wamekuwa wakilalamikia fidia zao kuwa ni kidogo. Tunaangalia pale Luguruni, Chanika, Kibamba matatizo ni hayohayo. Sasa inavyooneka

ni kwamba Serikali mara nyingi inakuwa haifuutilii. Mimi nitaka kutupa lawama kwanza kwa wale watendaji ambao ni Maafisa Mipango au au wanao-*plan* miji, unakuta maeneo mengine mtu anabomolewa nyumba yake, ameshaijenga na alipata kibali kabisa kutoka Halmashauri husika lakini baada ya muda unaambiwa kuwa hapa inatakiwa ipite barabara, hapa linatakiwa lipite bomba sasa mlikuwa wapi mwanzoni kutoa kibali wakati mtu tayari amemaliza kujenga na kibali kimetoka katika ofisi hiyo hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba kumekuwa na matumizi ya nguvu wakati wa kuwatoa wananchi. Wananchi unakuta wamekataa kutoka katika eneo hilo ili waweze kupata kwanza fidia zao lakini unakuta fidia haitolewi, muda unapita mpaka mradi pia unataka kutekelezwa, nguvu inatumika, wanakwenda FFU, wanabomoa nyumba, wananchi wanakuwa kama vile wakimbizi katika nchi yao, kwa hiyo, sasa utaratibu huo urekebishwe. Hiyo ilionekana pia kule Ihefu. Nadhani hakuna asiyefahamu hali halisi ilivyo mpaka ikaundwa Tume. Vilevile fidia imekuwa ikilipwa kidogo sana, hailingani na hali halisi ya nyumba aliyokuwa nayo mtu. Unakuta mtu mwingine anapewa fidia labda nyumba ilikuwa nzuri, inaeleweka anapewa milioni mbili, atanunua wapi kiwanja cha milioni mbili na kujenga nyumba ya kueleweka?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeona kuna tatizo la kesi kuchukua muda mrefu sana vijijini na hata mijini. Ninaomba Serikali iangalie jinsi gani inaweza kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, leo ameonyesha kwamba kutakuwa na ongezeko la posho kwa Wazee wa Mabaraza ya Ardhi kutoka shilingi 20,000 mpaka shilingi 30,000, hii inaweza kusaidia kidogo kuongeza utendaji au morari ya wazee hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matatizo haya ya ardhi, ninashauri Sheria zetu yaani Sheria ya Ardhi, Na.4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na.5 ya mwaka 1999 na ile Sheria Na.2 ya mwaka 2002 inayohusu kusuluhisha migogoro ya ardhi, ziangaliwe upya, kama kuna matatizo zirekebishwe na tayari tumeyaona na tumeyabainisha na kama hazina tatizo basi tatizo litakuwa katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea hilo tatizo la ardhi, naomba niongelee kidogo kuhusu matatizo ambayo wananchi tunayapata katika dhima au dhumuni zima la ujenzi. Tanzania ni nchi ambayo Mtanzania anatumia pesa yake mwenyewe mfukoni kujenga nyumba yake bila kupata mkopo mahali popote ndiyo maana unakuta watendaji wengi wamekuwa wakitumia njia mbalimbali mbadala hata ya kupokea rushwa ili mradi tu aweze kukamilisha jengo lake. Tunaomba hii Sheria ya Mikopo ya Nyumba ielezewe vizuri watu wapate kuielewa na vilevile riba ambayo inatolewa kwa ajili ya mikopo ya nyumba iangaliwe ili watu wengi waweze kukopa na kufanikiwa kujenga nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri atueleze, katika *report* ya CAG ya mwaka 2009/2010, imeonyesha kwamba kuna kama shilingi bilioni moja, milioni 154 hazikukusanywa kutoka katika mauzo ya viwanja vya Kurasini. Kwa hiyo, naomba kujua kwa nini pesa hizi nyingi hazikukusanywa. Mimi ni Mjumbe wa PAC, kwa hiyo, lazima kidogo nisemee *issue* ya CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimegundua pia tukiangalia katika Bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii kwa mwaka 2010/2011, ni ndogo, ni shilingi bilioni 22, milioni 265. Ukiangalia bajeti hii, shilingi bilioni 17 tunategemea kutoka nje sasa zisipotolewa hizi pesa maana yake miradi mingi itakwama, upimaji viwanja utakwama na mambo mengine ambayo yanatakiwa yafanyike yatashindikana kwa sababu pesa za ndani zitakuwa shilingi bilioni nne tu. Kwa hiyo, nataka Serikali iangalie ni jinsi gani inaweza kuachana na mawazo ya kutegemea nje na tuwe tukitumia pesa zetu za ndani kwa maana ya kwamba tufikirie njia nyingine zaidi za kuongeza mapato kuliko hizi ambazo tunategemea zaidi Sigara, Bia na vinywaji vingine baridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa sababu jana tu nimetoka Bariadi na ningeomba nianze kusemea mambo ya Bariadi. Kwanza kabisa, ninapenda kuwapongeza wakulima wote wa pamba kwa kuwa wamepata shilingi 600 lakini bado ninafikiri shilingi 600 haijatosha ingefikia angalau 800. Ninaomba kabisa wakulima wasichanganye pamba na maji na vitu vingine kwa sababu hivi vitatufanya tusiwe na bei nzuri mwaka unaokuja. Mwisho, ninaiomba Serikali iwakamate watu wote wanaochezea mizani kwa sababu hawa ni wezi. Hayo nimemaliza kwa sasa lakini baadaye nitamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka kumpongeza sana Waziri kwa kuwa amefanya kazi vizuri sana kwa muda wa miaka mitano. Kweli kuna ufanisi mkubwa sana katika Wizara yake ambao unaanza kuonekana kwa sasa pamoja na changamoto ambazo amezizungumzia katika *para* 95, mimi ninapenda kuzungumzia katika changamoto zingine hizi mbili ambazo nafikiri kuwa ni muhimu tukaziangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mambo ya vijijini, ni vizuri tumeanza kuwapimia watu vijijini lakini ile nia inayoelezwa sana ni kwamba ili wakakope, kwa hiyo, mimi natoa rai kwanza kwamba tafadhali usipime ili ukakope kama hauna mradi usiweke rehani ardhi yako au nyumba yako. Naomba hii elimu iwepo, watu watapoteza makazi, watu watapoteza mahali pa kulima, hilo ilikuwa ni rai ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai ya pili, tunazungumzia sana juu ya urekebishaji wa matumizi ya ardhi vijijini. Vijiji vilishapangwa mwaka 1974 kila mmoja ana ardhi yake, kila mmoja ana mahali pake, haya mambo ya kusema tu kila wakati kuwa mrekebishe

matumizi ya ardhi katika kila kijiji, yatatuletea taabu. Baadhi ya watu wetu wanafikiri kuwa ardhi ni ya kijiji, ardhi wanaweza wakaigawa, wakaifanya wanavyotaka. Naomba elimu itolewe kwamba hakuna tena ardhi ya kugawa hapa, kila mmoja ana mahali pake amepewa ile hati ili tuhakikishe kuwa hakuna migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa hati Mheshimiwa Waziri ulishanieleza hapa, ukaniambia kuwa hiyo ya milele siyo ya miaka 33, ulishasema. Sasa kama ni hivyo isisitizwe hiyo na pia wananchi waelezwe kuwa hakuna kodi kwa sababu wengine wanaanza kusema wakipata hiyo hati wataanza kulipia kodi halafu baada ya hapo wasipolipia watanyang'anywa hiyo ardhi yao, naomba hilo uliwekee mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatimiliki, Waziri amesema kuwa Sheria inampa haki kutoa hati siku 180, mimi ninafikiri kwa hali ya sasa na juzi hapa tumepitisha Sheria ya watu wanaoweza wakaenda kwenye mabenki ili waweze kujenga nyumba, siku 180 ni nyingi mno kutoa hati. Watu hawawezi wakachukua *offer* kama tu njia ya kukupa mkopo, haiwezekani. Kwa hiyo, ninashauri hili jambo liangaliwe upya. Kwa kuwa umeshagawanya sasa kanda mbalimbali, Mwanza kuna Kanda na sehemu zingine, hebu watu wako kidogo wakorogekoroge kidogo ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, siyo hivyo tu, siku hizi kama tulivyosema kwenye sera yetu ya *UDP* ni kwamba ardhi ni mali na ardhi Wazungu wanasesma *in-exchange*, ina *value*, watu siku hizi wanauza ardhi kwa sababu mbalimbali lakini ukiuziwa ardhi mlolongo mpaka uje upate, Wazungu wanasesma *completion* kwamba umemamaliza ku-transfer, ni kazi ngumu sana. Uende *TRA*, utoke *TRA* urudi tena Ardhi halafu tembea tena *TRA* halafu sijui nenda tena Wilayani halafu sijui kwa nani, inabidi kuangalia ili hizi *transfer* zifanyike kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *master plan*, sisi kwetu Bariadi tumefurahi sana kuwa tumepata Mkoa mpya unaitwa Simiyu, safi sana. Mimi Wilaya yangu ambayo ndiyo Jimbo langu, tumepata Wilaya inaitwa Ikilima na tutakuwa na Makao Makuu Bariadi na tutakuwa na Makao Makuu ya Wilaya Lugangabilili, sasa usituachie tuanze kujenga holela. Mkuu wa Mkao yuko pale halafu chini yake kuna kitu gani sijui, tunaomba *master plan* mara moja, tuambie wapi tunataka na ni Lugangabilili ya namna gani, ni mji ambao baada ya miaka 50, sisi wengine hatuko hapa lakini watakuja kutushukuru kwamba kulikuwa na Waziri Chiligati ambaye alishughulikia hili jambo na Mzee Cheyo pia akiwa Mbunge wao. Tunakuombea urudi hapa na Mheshimiwa *President* akupe hiyo hiyo Wizara ili tuhakikishe kuwa Lugangabilili inakuwa ni mji safi na pia tuna Bariadi Mkao ambao umeandaliwa sawasawa, kwa hiyo, *master plan* hizi, sisemi kwa utani, wanachotaka watu waliobanana, tungewahamisha tukawapeleka katika *satelite town* zingine kuliko kusema eti nimekupa leseni. Hizo leseni kama baadhi ya

nyumba ziko pale, sitaki kuwaudhi watu, lakini unajua wewe mwenyewe Dar es Salaam, kweli ukimpa mtu leseni si unampa geresha tu, nani atakayempa mkopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuangalie afya, maana ya *town planning* ni kwamba watu waweze kuishi kwa usalama. Wewe mwenyewe umetuambia zaidi ya 50% ya Watanzania watakuwa wanaishi mjini kama wataishi mjini waishi kwa usalama, kwa ustadi kwenye mji ambao unapendeza. Katika baadhi ya miji tuliyonayo sasa hivi kuna sehemu ambazo hata huwezi ukapitisha jeneza, hili jambo liangaliwe lakini kikubwa ni Bariadi pamoja na Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia juu ya uchaguzi, nimepita hata kule kwangu *Vuvuzelas* kibao. Mimi ninachosema tu huu ndiyo wakati wa kushindana, tushindane vizuri tu, najua kule kuna mpinzani mmoja lakini bado hajanifikia mimi lakini yuko katika maoni ya Chama cha Mapinduzi, ye ye ameendelea kwa vitu viwili, kutafuta wachawi na kuwapa semina halafu na kugawagawa vifedha kidogo kidogo na watu wa TAKUKURU hawamuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna mwingine ambaye ye ye kaolewa, ye ye katoka nje, ye ye anahubiri jambo ambalo nataka kulisema kwa uzito kuwa Chama cha Mapinduzi hakihubiri watu wamwage damu ili kupata Jimbo, ye ye anahubiri hata kwa damu lazima apate Jimbo la Bariadi Mashariki. Mimi ninamuambia kule alikotoka akamwage damu yake ye ye mwenyewe sisi kule Bariadi hatuna damu ya kumwaga kwa ajili ya Ubunge, sisi tunataka kushindana kwa njia ya amani, tunataka kushindana kwa njia ya hoja, tunataka kutaniana tunapofanya mambo yetu, huu ndiyo uchaguzi, mnatoka pale mnashikana mikopo, wewe mpenzi wangu, wewe ndugu yangu, watu wa Bariadi ni ndugu zangu. Kwa hiyo, CCM haizungumzi juu ya damu ninyi watu wa CCM mmemtoa wapi, ni CCM gani hiyo ambayo inayohubiri mambo ya damu? Hebu mwambieni aondoke katika Bariadi yetu ili tuweze kufanya uchaguzi ambao uko sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimeenda kule nimegawa fedha kwa ajili ya Jimbo ambazo tumepewa na Bunge hili, nimezipeleka kwenye miundombinu watapata vibarabara vidogo vidogo, watu watapata shule, watu watapata maji, hiyo ndiyo sera na Mbunge makini anafuatilia maendeleo siyo mambo ya kumwaga damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakwambia CCM ni kijani siyo damu. Namwita Mheshimiwa Michael Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niseme machache kuhusu bajeti ya Waziri wa Ardhi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, kwa kweli nilikuwa ninajiuliza kwa

nini Rais hajampa Naibu Waziri lakini baadaye nikaona kwamba kazi aliyoifanya amemuona kuwa anaweza kuifanya kazi hii hata bila ya Naibu Waziri, nakupongeza sana. Ninampongeza na Katibu wake pamoja na timu yake nzima kwani mafanikio haya ambayo wananchi wa Tanzania wanayaona ni kutokana na kazi yako na timu ya Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hakuna kitu kinachofanana na ardhi, ardhi ndiyo uhai, ndiyo makazi, ndiyo biashara, ndiyo mali, kwa hiyo hakuna kitu kingine kinachoshinda ardhi. Kama ardhi ni nzuri na inafaa basi haki itendeke, kila Mtanzania aliyeko Tanzania awe na haki ya ardhi. Kwa hiyo, naomba leo Serikali isikilize kilio cha wafugaji ambao wamekuwa wakikimbia kila mahali na kufukuzwa kila mahali kwa ajili ardhi ambayo wanaporwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia historia za hifadhi zote, wafugaji walikuwa wakiishi humo lakini wakatolewa. Maeneo ya uwindaji, mfugaji hana haki, muwindaji ndiyo ana haki, mfugaji anaondolewa. Maeneo ya madini, yakiwemo madini, wafugaji wanaondolewa. Wakulima wanaondoa wafugaji, naomba wafugaji wapimiwe maeneo, wasiwe wanakimbiakimbia na kusemekana kwamba wametoka wapi, kama kuna mtu ambaye hajui kwamba mfugaji ametoka wapi ajue kuwa wafugaji ni Watanzania, kwa hiyo, wanapaswa wawe na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgogoro mkubwa sana uliopo Loliondo na ndugu zangu wanatajataja sana Loliondo. Ningependa kusema kwamba Wilaya ya Ngorongoro, 59% ni Hifadhi, 41% ndiyo siyo hifadhi. Hifadhi ya Serengeti inapakanana na Loliondo na hao watu walioko Loliondo ndiyo wamehamishwa kutoka Serengeti. Hili eneo la Loliondo ambalo limekuwa na mgogoro kwa muda mrefu, nakuomba Mheshimiwa Waziri, wewe ni Waziri wa Ardhi, halafu wewe ni Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi ambapo Chama cha Mapinduzi ndiyo Chama Tawala, kwa hiyo, kotekote wewe unafaa, lishughulikie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wengine wamepeleka kadi nyingi sana huko kwa ajili tu ya hiyo ardhi ya Loliondo kuwa Wamasai mnanyanyaswa na Tanzania nzima inajua kwamba Wamasai wote ni CCM na wanataka kutubadilisha kwa njia hiyo ya malalamiko na kusema kwamba Wamasi wote ni wakimbizi, wanateswa, wanafukuzwa, hiyo lugha ndiyo inatumika kutubadilisha tuichukie CCM lakini ninaomba Serikali ilitazame eneo hilo. Mnafahamu Ngorongoro wao hawajawahi hata siku moja kumpata Mpinzani, awe ni CHADEMA, CUF, NCCR baada ya kura za maoni wanasema tumeshampata Mbunge.

**MBUNGE FULANI:** Tunakuja huko.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Njooni lakini hampati. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba eneo lile ambalo linawakasirisha wafugaji, hawa Wamasai wanaokaa huko, ni malisho yao. Jamani Serengeti inatosha. Acheni hilo eneo, hawakumnyima muwindaji awinde huko, lakini kumuondoa asifuge katika eneo lake ndiyo chuki iliyotokea wananchi wameanza kuichukia CCM na kuihama CCM. Naomba eneo hilo ambalo tulikuwa tunabishana hapa na Ndugu yangu Mheshimiwa Ndesamburo bahati mbaya ameondoka kwamba attachukua Loliondo kwa njia hiyo na mimi nikamwambia hawachukui na hizo kadi tukitoka kwenye hili Bunge niende kuhamasisha hao watu wa Loliondo zote walizochukua wazirudishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Loliondo, Vijiji vya Esoitsabu, Lulosokwa, Oleipiri, Arashi, Piyeya, naomba eneo hilo libaki kuwa malisho ya mifugo. Waziri utoe kauli hapa hapa kwa sababu vijiji hivyo vimepimwa, wana hati, sijui sasa wanawezaje kwenda kumega eneo ambalo lina hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Waziri katika Bajeti iliyopita ilitaja baadhi ya Wilaya kama kumi hivi ambazo watajengewa nyumba za bei nafuu, Longido ikiwemo. Lakini nashangaa kwenye bajeti ya mwaka huu ameisahau tena, haipo na haikutajwa sehemu yoyote. Naomba na sisi Longido tujengewe hizo nyumba isiwe mnajenga tu katika miji, muende hata katika Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la upimaji wa maeneo, hatimiliki za kimila. Hatimiliki za kimila kwa kweli zinahitajika sana hasa katika maeneo ya wafugaji. Tunasikia kila bajeti hatimiliki za kimila zipo. Kuna maeneo ambayo yanastahili kabisa katika maeneo ya wafugaji, kuna watu ambao wanahitaji wapimiwe maeneo yao pamoja na kwamba katika Jimbo langu vijiji vyote vimepimwa, lakini hizo hatimiliki za kimila zinahitajika pamoja na hati za mashamba. Ulipokuja katika Jimbo nilikueleza kwamba tuna wakulima wengi wanahitaji hati ya mashamba na ninaomba Watalaan waende huko ili waweze kutupimia mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini ningewomba Waziri wakati wa majumuisho asisahau kusema neno kuhusu Loliondo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nina Mambo matatu ama manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, kwenye taarifa ya Waziri na Taarifa ya Uchumi wa Nchi, inaonesha kwamba sekta ya ujenzi, *Real Estate*, ni moja ya sekta

ambazo zinakua sana lakini sekta hii haina *regulator*. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba watu wanajipangia bei wanavyojua wao wenye, bei za watu kupanga nyumba, taratibu za kulipa na *currency* inayotumika kulipa. Miaka miwili iliyopita, nilishauri katika Wizara hii kwamba tuangalie uwezekano wa kuanzisha *Real Estate Regulator* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sekta hii ambayo inakua sana na ambayo inasababisha matatizo mengi sana kwa wananchi kwa maana ya malalamiko ya kodi na kadhalika, iwe na *regulator* wake ili kuweza kudhibiti na kutoa leseni kwa watu ambao wanafanya shughuli za nyumba na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, ninaomba nilirejee tena ombi hilo ili Serikali iweze kuangalia ni jinsi gani inaweza ikafanya ili ku-*regulate* sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni *National Housing*, kwenye Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma, tulipokutana nao mwaka jana katika hesabu zao za mwaka juzi tulikuta kwamba wame-*under value assets* zao na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akawa amekataa hata kuangalia hesabu za *National Housing* kwa sababu hazikuwa zina-*reflect* hali halisi ya Shirika na baadaye kwenye Kamati tukawarudisha kwamba waende wakaifanyie kazi, wakafanye *evaluation*. Baada ya kufanya *evaluation*, thamani ya mali za *National Housing* ikapanda kutoka bilioni mia mbili mpaka bilioni mia sita. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba hii ni moja ya Shirika kubwa sana ambalo tunalo hapa nchini na *actually* ni moja ya mashirika makubwa sana Kusini mwa Jangwa la Sahara. *National Housing* sasa hivi wana Mkurugenzi mpya ambaye ametoka sekta binafsi kwa vyovypote vile atakuja na mawazo mapya ya kwenda kusaidia Shirika liweze kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tulikuwa tumeshauri kwenye Kamati kwamba Shirika liangalie uwezekano wa ku-*migrate* kutoka katika Shirika ambalo limeundwa kwa mujibu wa sheria liende kwenye Sheria ya Makampuni, Sura ya 112, kama kampuni ili baadaye waweze kuorodhesha hisa zao kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na *transparency* lakini pia kuliwezesha Shirika kukopa kutoka kwa umma badala ya kutoka kwenye mabenki kwa ajili ya kuendeleza shughuli hizo za ujenzi wa nyumba. Naomba hilo pia nilisisitiza katika mchango wangu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni malalamiko ambayo nililetewa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma. Kuna wapangaji wa *National Housing* ambao wanaendesa shule muda mrefu sana, shule ya Kifaransa ambao walikuwa wameomba kuwe na kitu kama *PPP* kati ya *National Housing* na wao kwa sababu wanapokuwa *treated* kama watu binafsi ambao wamepanga kwenye nyumba, maana yake ni kwamba gharama za malipo zinakuwa kubwa, wanazihamishia kwenye *fees* ambazo watoto wanazilipa. Kwa hiyo naomba Waziri na watu wa *National Housing* kwa sababu wapo hapa wajaribu kuangalia, kuna *mode* mbalimbali ambazo wanawenza kuzifanya hasa kwenye shughuli kama hospitali, shule ambazo zinatumia nyumba za *National housing*. Mnawenza mkaangalia ni jinsi gani ambavyo mnawenza mkafanya *cost*

*sharing* au vitu kama hivyo ili kuhakikisha kwamba gharama haziendi kwa wale watu ambao wanazipata zile huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya amelizungumzia, suala la ardhi ya kijiji cha Mwandiga na Waziri nilishamweleza suala hili muda mrefu sana, aliniahidi kwamba anakuja Kigoma na alikuwa kila akienda *airport* ndege inaahirishwa, angeweza kwenda hata kwa gari lakini hakwenda, sasa sijui ameogopa labda wale watu waliochukua vile viwanja walihakikisha kwamba ndege inaahirishwa tu asiweze kufika lakini tatizo hili ni kubwa sana. Mashamba ya watu wa Kijiji cha Mwandiga yamechukuliwa bila kufuata utaratibu na watu wamechukua vile viwanja matokeo yake ni kwamba hatuwezi kufanya shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Mhonga ameeleza, Shirika la Hifadhi ya Jamii, *NSSF*, kufuatana na maendeleo ya miundombinu ambayo imejengwa pale Kigoma, walikuwa na *project* ya kujenga stendi ya mabasi ya kimataifa kwa sababu kutokana na barabara ambazo zimejengwa hivi sasa ambapo unaweza kutoka kwa basi kutoka Uvira - Kongo mpaka Kigoma, sasa ili kutokuujaza Mji kwa mabasi na malori na kadhalika, tulikuwa tunataka malori na mabasi yaishie pale Njiapanda ya Mwandiga na pia watu wanaofanya biashara za teksi na kadhalika waweze kupata biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mradi ule unashindwa kuendelea kwa sababu kuna watu ambao wamehodhi viwanja na Rais ameshaagiza alipokuwa anahutubia pale Nyarubanda kwamba watu wote ambao walichukua vile viwanja bila kufuata taratibu, Serikali ya Kijiji ilikuwa haihusiki, vile viwanja virejeshwe. Tayari nimeshaongea na Waziri na sasa sijui kama muda unaruhusu, ni vizuri kama angeweza kwenda kule na akaweza kuona, ili achukue hatua za haraka tusije tukakosa hiyo *project*, kwa sababu ni *project* ya kampuni ambayo inatarajia kuja kupata faida baadaye. Kwa hiyo, naomba Waziri aweze kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna suala la mpaka kati ya Manispaa ya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, katika eneo hilo hilo la Kijiji cha Mwandiga na katika Kijiji cha Kalangabo ambavyo ndivyo vinapakana na Manispaa. Watu wa Manispaa wamehamisha jiwe na mpaka kutoka katika mpaka wa asili ambao ni mto na kupanda juu na kuchukua eneo kubwa sana la ardhi na kuchukua mashamba ya watu na kama unavyofahamu kitu kikishakuwa ndani ya Manispaa, siyo Kijiji tena kinachohusika na kupanga ile ardhi ya pale, ni Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, naomba na hili pia Waziri aweze kuliangalia ili kuhakisha kwamba ardhi ya wanakijiji cha Kalangabo na mashamba yao hayachukuliwi. Vilevile ardhi ya watu wa kijiji cha Mwandiga na mashamba yao wahakikishe hayachukuliwi ili kuhakikisha kwamba tunalinda haki za watu hawa ambao wamekuwa wakilima katika maeneo hayo miaka yote hiyo sasa ghafla tu jiwe linahamishwa tu na watu wenye nguvu, hali inakuwa siyo nzuri kwa wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, napenda kuishukuru Wizara, mwaka 2005 katika Halmashauri yetu na hili Mheshimiwa Cheyo hatalifurahia sana kwa sababu yeche ni *Liberal*, hapendi mambo ya kupima vijiji, lakini kwa sisi ambao tuna mlengo wa kushoto kidogo, upimaji wa vijiji, ni jambo la msingi sana. Mwaka 2005 katika Jimbo langu kulikuwa kuna vijiji vitano ambavyo vimepimwa, tukawa tumeiomba Serikali na sasa hivi nashukuru kwamba Vijiji vyote vya Jimbo la Kigoma Kaskazini vimepimwa. Kwa hiyo, tunapenda kuwashukuru sana Wizara kwa kazi hiyo ambayo mmeifanya ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna vijiji kumi na moja vya Jimbo la Kaskazini, katika ukurasa wa 83 wa Hotuba ya Waziri katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, Kijiji cha Kagunga, Nkele, Mgaraganza, Mwamgongo, Kigalye, Kagongo, Bugamba, Bubango, Mpanga, Zafe na Kiziba hivi ni vijiji ambavyo vinazunguka Hifadhi ya Gombe, vijiji vyote hivi pia vimefanya mipango ya matumizi bora ya ardhi. Napenda niwashukuru sana Wizara kwa msaada huu na hasa ukizingatia kwamba Wizara yenyewe inaongozwa na Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi, hakubagua kwa sababu Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA anatoka Kigoma Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru binafsi Mheshimiwa Chiligati kwa kazi hii ya kusaidia na kuhakikisha kwamba mipaka ya vijiji vyetu inakuwa salama. Naomba tu uhakikishe kwamba zile hati baada ya kupima zinafika kwenye vijiji ili wanavijiji sasa waweze kuangalia ni jinsi gani ambavyo wataweza kugawana maeneo yao kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana sana kwa kunipatia nafasi hii. Naamini unaelewa maana ya sana sana, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu ni moja, hivi vyama ni mtindo tu wa kufanya kazi. Kwa hiyo, hatuwezi kubagua maendeleo ya wananchi kwa sababu ya itikadi. (*Makofi*)

Lakini nafahamu miaka ile ya 1980, kuna nchi moja, sitaitaja jina, tulikuwa wote katika semina kule Uingereza, Kiongozi wa Upinzani tuliyekuwa naye huko alisema kwamba kwao kama wewe upo Chama cha Upinzani hakuna duka, hakuna barabara, hakuna maji na hakuna kitu chochote, kwa hiyo, wananchi wanakugeuka, wanajiuliza ni kazi gani kuwa na Chama cha namna hiyo? Sisi Tanzania tunajenga umoja wetu usiwe na ubaguzi wa namna yoyote ile kwa sababu yoyote ile. Kwa hiyo, Waheshimiwa muwe na amani kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze jambo moja, leo ni tarehe 6 Julai, kesho ni tarehe 7 Julai, ni *public holiday*. Mkiangalia, wale wenye ratiba zetu za kazi za Bunge, tarehe nane ndiyo siku tunayoingia tena siku ya Alhamisi, siku ya Alhamisi ni kipindi maalum kwa maswali kwa Waziri Mkuu. Siku hiyo ya Alhamisi hapatakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 38(5), kama Waziri Mkuu ana matatizo maalum siku hiyo kipindi kinakuwa hakipo, kwa hiyo, tarehe 8/7 kipindi hicho hakitakuwepo.

Lakini pia kwa mujibu wa Kanuni ya 30(6), tunaambiwa kwamba Spika pia anaweza kupanga utaratibu mwingine wa kuendesha Bunge vizuri. Kwa hiyo, tunataka kutumia zile dakika 30 za maswali kwa Waziri Mkuu kwa maswali ya kawaida. Tutafanya dakika thelathini baada ya dakika thelathini kutakuwa na Wizara mbili, kwa hiyo tunataka kutumia nusu saa ile nyingine ya saa moja ya maswali ili kusudi tuweze kusoma hotuba ya Wizara nyingine ambayo itakuwa Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo halafu tutasoma pia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, tukiwa na saa moja tutashindwa kukamilisha vizuri hizi Wizara.

Napenda pia Waandishi wa Habari waelewe maana kuna mmoja ametuandika vizuri sana *page nzima*, kwamba hajawahi kuona Bunge dhaifu kama hili, watu wanajipongeza, wanatangaza nia, Naibu Spika anasema mjibu kwa ufupi, muda ni mfupi, Wizara mbili wakati mmoja. Jamani hebu angalieni, hili siyo tatizo la Bunge, ni tatizo la sheria zinazoingilia uchaguzi. Safari hii tumetunga Sheria za Gharama za Uchaguzi, nayo ina *impact* katika ratiba za kuendesha Bunge. Kwa hiyo, ndiyo maana tume-squeeze siyo kwa sababu tunapenda kukimbia, hapana! Yapo matatizo.

Sheria ya Gharama za Uchaguzi imerudisha ratiba nyuma. Hujatekeleza mambo fulani fulani kabla ya tarehe hizo unakuwa *disqualified* moja kwa moja. Vivyo hivyo, Tume ya Uchaguzi nayo ina tarehe zake za kampeni maalum, zinajulikana, usipozitimiza wakati huo tena kampeni haiendi na mzunguko wake ndiyo maana Bunge la safari hii, ni kweli limekuwa fupi sana. Kwa hiyo, tunaomba mtuelewe, msiandike tu kuwaweka wananchi waelewe kwamba tumeamua kukimbia si kweli. Kwa hiyo, ndiyo maana utakuta tunakuwa na Wizara mbili siku moja, tusipofanya hivyo, hatufiki mwisho.

Jambo lingine mjue tumebadilisha utaratibu, zamani Bunge la Bajeti, hatupitishi *Finance Bill* mpaka tumalize Wizara zote, kwa hiyo, hakuna Wizara ambayo itakuwa na uwezo wa kutumia fedha zile mpaka tumalize ile miezi yetu miwili na nusu. Toka mwaka jana, Waziri akishamaliza kusoma hotuba yake ya Bajeti na sisi kujadili, tunapitisha pia *Finance Bill*. Kwa hiyo, hii nyingine ni utekelezaji tu, tunaotaka kuwa-question Mawaziri kwamba utekelezaji wenu katika miaka iliyopita haukuwa sahihi na yote tunayowakosoa hapa ni kwa ajili ya *better efficiency* ya utekelezaji baadaye. Kwa hiyo, ndiyo maana tunakwenda hivyo na wala hatujavunja sheria na Mabunge mengi yanafanya hivyo, hii ya kwetu haikuwa sawasawa kidogo. Kwa sababu tunajadili hapa miezi miwili ndiyo tunapitisha *Finance Bill*, by the time Serikali inaanza kukusanya pesa inaingia wakati wa

masika hakuna kazi inayoweza kufanyika. Kumbe kwa mtindo huu sasa tukishapitisha *Finance Bill* Serikali inaweza kuendelea kukusanya mapato yake kama kawaida na kuweza ku-allocate funds kwa maendeleo. Kwa hiyo, ni mabadiliko ambayo yana maelezo siyo kwamba tunafanya tu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hilo, nawaombeni tena twende tukawasikilize wenzetu Walemvu wa Usikivu. Ni heshima kwao pia watajisikia ni sehemu ya jamii yetu, ni kitu cha utu, naomba mkahudhurie ile semina kidogo halafu muondoke.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, nilibakiwa na wachangiaji wawili. Mheshimiwa Magalle Shibuda.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi pamoja na nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Chiligati kwa juhudi zake mbalimbali ambazo anafanya kwa kuhakikisha kwamba sera ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakuwa katika mwegemeo wa kutambua uasilia wa maslahi ya Watanzania. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara hii ndugu yetu Patrick Rutabanzibwa pamoja na watumishi wote kwa juhudi zao ambazo wanajitahidi kuhakikisha wanakabiliana na matatizo yote.

Napenda kuwaasa ndugu zangu na watani zangu wa Manyoni Mashariki kwamba wahakikishe ndugu yetu Chiligati wanamrejesha. Nawaomba wagogo watani zangu mtambue ya kwamba huyu Mheshimiwa Chiligati, mtoto wenu, ana thamani, anathaminika, anasadikika. Sasa kama mkimwacha huyu, majuto ni mjukuu.

Vile vile, napenda nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wa Njombe Kusini watambue ya kwamba Mheshimiwa Anne Makinda ni taswira ya kwamba mmelea mtoto mwenye sifa, mwenye wasifu wa kusadikika na kupendeka. Kwa hiyo, naomba mumepende mumpe kura zenu zote ili tuendelee kuwa naye na aendelee kutoa mchango wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, vile vile napenda kutumia fursa hii kuwaasa ndugu zangu wa Maswa kwa sababu kila muwamba ngomba, ngozi huvutia upande wake. Natambua Maswa sasa hivi tuna majimbo mawili na natambua kwamba

hivi sasa kuna kilio na kuna uhondo wa maneno mengi ambayo yanapitishwa na mafataki wa kisiasa. Kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu wa Maswa zingatieni kwamba huu ndiyo msimu wa mazalia ya mbu ambayo yanaweza yakasababisha maradhi mkajikuta kwamba ni wapweke hampati maendeleo. (*Makofi*)

Lakini napenda kuwakumbusha, niliwaasa kwamba hiki ndiyo kipindi cha msimu wa wajinga ndio waliwao, waleni sana kwa sababu wakati mlipokuwa mnadaiwa michango ya shule hawakuleta fedha, mnapodaiwa michango ya kujenga Vituo vya Afya hawaonekani, lakini leo wanataka kuja kuwababaisha. Ndugu zangu, watu wa Maswa nawaomba mhakikishe ya kwamba hambabaishwi na uongo wa mafataki.

Vile vile napenda nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi, nawaasa watu wangu wa Maswa. Nawaomba muamue kwa busara na hekima kwamba Maswa haitadidimimia ikiwa upande mmoja utakosa uwakilishi wa Shibuda. Nasema haya kwa sababu tuna historia ya *SHIRECU* tulikuwanayo ililiwa na Mumiani. Sasa jiulizeni hawa wanaokuja hawana historia ya kudhulumu watu? Hawana historia ya wizi? Hawana historia ya ubinafsi? Kwa hiyo, naomba yote haya myasimamie ili tuhakikishe kwamba Maswa haitatetereka. (*Makofi*)

Ndugu zangu wa Maswa ili Maswa iweze kuendelea, umoja wa fikra na maamuzi magumu yenye kuamua kwamba, kula tutawala, lakini hatuwapi, kura ndio itakayosalimisha Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchungu wa mwana aujuaye ni mzalendo wa Tanzania. Sasa naomba njielekeze kwenye hoja ya masuala ya ardhi. Ardhi inahitaji ipewe tafsiri makini sana kwa sababu ukiangalia vita ya kwanza, ya pili migogoro duniani inasababishwa na matatizo ya ardhi. Ukiangalia vita ya ukombozi wa Bara la Afrika, ukiangalia mifarakano hata ndani ya nchi yetu wakulima na wafugaji ni ardhi, tatizo ni ardhi.

Kwa hiyo, ninaomba sana na namwomba Mheshimiwa Waziri na watalaam wote mzingatie ya kwamba rasilimali ardhi ndiyo utulivu wa Taifa letu. Umoja na mshikamano wa nchi yetu uko kwenye ardhi. Tukitetereka tukaanza kuwa na sheria gandamizi kwa wazalendo tukatetea wawekezaji muelewe kwamba mnaanza kuweka joto ambalo ni hatari kama *volcano* kama lililotokea Zimbabwe, *FRELIMO* wakapigana Mozambique, *SWAPO* wakapigana Namibia. Kwa hiyo, napenda niwakumbushe kwamba historia ina utata sana, zamani tulikuwa tunasema wanyonyaji, lakini historia imebadilika siku hizi mang'amuzi ya historia yanasema kwamba siku hizi tunaita wawekezaji.

Lakini katika mapambano ya vita, palizuka maneno unyonyaji na haya yaliendelea. Lakini napenda kusema ya kwamba hakuna mtu anayetegemea kwamba mgeni atakuja ajenge nchi ijitegemee. Ni lazima tutambue kwamba sadaka ya ustawi na maendeleo, sadaka kwa uhuru wetu, sadaka kwa amani na utulivu ni sheria ambazo zitahakikisha ya kwamba hawa ambao kwa lugha ya kisasa wanaitwa wabia, hao hao muelewe ya kwamba waswahili wanasesma mtu haachi asili yake. Hakuna ambaye atakuja

aseme kwamba nakuja kujenga Tanzania anakuja kufanya biashara ya ardhi ili aweze kuikamua. (*Makofii*)

Kumbukeni tuna mikataba ya mikosi, bandari, reli yote hii haijatusaidia. Achilie mikataba mibovu ni nini Watanzania tumekuwa na uwoga na wasiwasi wa kwamba kila mkataba unaozungumzwa au kila hoja inayokuja kuhusu mwekezaji tunakuwa na hofu ya kunyonywa. Kwa hiyo, ninawaomba na napenda vile vile niwakumbushe ya kwamba fikra zilizozaa uwoga wa Watanzania zimesababishwa na Watanzania wataalam ambao wametuweka kwenye hali ya migogoro ya kunyonywa. Sasa mnaposema kwamba Watanzania wabadilike fikra, ninaomba baadhi ya watalaam ambao siyo wazalendo waanze kubadilika fikra tujengee hoja ambazo zitawaondoa Watanzania kuwa na wasiwasi na Wabunge tutakuwa hatuna wasiwasi kama hatutakuwa matajiri wa mikosi tena kama inavyoendelea hivi sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaonyesha ya kwamba kila tunapotaka kuwa na mkataba wazalendo tunakuwa wapiga debe wa kauli na maneno matamu. Mtapata ajira, pato la Taifa litaongezeka, jiulizeni pato la Taifa likiongezeka: Je, pato la kaya linaongezeka? Soweto Afrika ya Kusini walidai Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Pato la Taifa la *South Africa* lilikuwa kubwa sana, Zimbabwe lilikuwa kubwa, lakini wazalendo: Je, hivi mnajua kiu ya TANU, kilio cha TANU, kilio cha mapinduzi matukufu ya Zanzibar, watalaam ambao mmezaliwa baada ya mapinduzi na baada ya mapambano ya kupata uhuru hebu someni itikadi ya Tanzania na historia mjenge na muimarishe uzalendo wenu ili muwe na fikra endelevu kwa maslahi ya Tanzania. Muwe na fikra za mapinduzi ya kulinda uzalendo. Ninawaomba sana haya tuyaweke katika tafakari zenu kwamba mnalifanyia nini Taifa na mnaacha wosia gani kwa Watanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, napenda vile vile mueewe ya kwamba Katiba ya Tanzania inazungumzia ujamaa na kujitegemea. Kwa hiyo, nawaomba sana mueewe kwamba hakuna agano jipya la kujenga uchumi endelevu bila kutambua agano la kale ambalo lilizaliwa na TANU na *Afro Shirazi* na hivyo tukawa na kauli mbiumbalimbali kwa maslahi ya Taifa letu. Lindeni uhuru wetu siyo muanze mje kutupa masalio ya mbu ambao watahatarisha usalama na umoja wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kutoa angalizo kuhusu uchoyo wa watalaam ambao ni waandaaji wa mikataba au sheria za fidia. Hivi wawekezaji wanakuja na mabilioni, unaona aibu gani Mtanzania akalipwa fidia inayofanana na maoni ya mahitaji ya maisha bora? Nawaomba mtafakari ili hapo mnapofanya haya mambo yenu ya kutoa muweze kutusaidia. Thaminisheni uzalendo wenu kwa maamuzi na sheria mnazotuvekeea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maswa pana madai ya ardhi. Siku hizi mnasema ardhi ni mali. Maswa tunadai sio chini ya shilingi milioni 100 fidia kwa huduma mbalimbali zilizotolewa. Tuishi kwa maneno ambayo tunayasema kwa kuwa yawe na vitendo vyatutafisiri maana ya hayo tunayoyasema. Ninaomba sana fidia kwa watu wa Maswa waliota viwanja vyao. Tumeambia ardhi ni mali, kwa hiyo, naomba tafadhali sana hilo.

Vile vile wafugaji wapewe ardhi na wapendelewe, tusitoe tu kwenye viwanda na wawekezaji wanaokuja kuja kuweka mashamba naomba tuondoe ugomvi wa ardhi kati ya wazalendo na mzalendo kwa kuwapendelea wageni.

Baada ya kusema hayo napenda kuzungumzia suala la kodi ya shirika la nyumba. Zamani tulikuwa na makundi ya Uhindini, Uzunguni na Uswahilini. Sasa naomba Shirika la Nyumba mlififikirie kulipa ruzuku kwa sababu ya mfumko wa bei kwa vifaa vya ujenzi, la sivyo, tusipotoa ruzuku pakaanza kuzuka matabaka, gharama ya kuzuia hasira za matabaka itafanana na ANC walivyodai uhuru mpaka watoto wadogo wakapigwa risasi wana kiu ya haki. Wapeni ruzuku ili mhakikishe mna-control kupanda kwa bei. La sivyo, tutajikuta kwamba tuna Uzunguni, Uhindini na Uswahilini.

Hapatakalika! Sasa hivi jamii ya *South Africa* wana matatizo sana ya amani. Watanzania kwa kweli tunahitaji amani na utulivu. Lakini kila shirika liwe nyenzo ya kujenga amani na utulivu kwa maslahi ya kesho. *TANU na Afro Shirazi* walitoa kilio chao na sasa ninawaomba pia watendaji wa leo wawezee kuwa na amani na utulivu ambao unajengwa katika misingi ya nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba Shirika la Nyumba watembelee Maswa waje kutujengea nyumba bora kwa sababu tunaanzisha Makao Makuu ya Mkoa mpya. Ahsanteni. (*Makofi*)

#### **NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kunifagilia. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipata nafasi hii. Lakini kabla ya kuchangia naomba nitumie nafasi hii tena kumshukuru Rais kwa kuunda Mkoa wa Njombe na Wilaya ya Wanging'ombe, tunaahidi tutajitahidi kutekeleza wajibu wetu ili lengo la Serikali la kuunda Mkoa huu na Wilaya hii liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na ya kina. Pili, ningependa vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Patrick Rutabanzigwa kwa kusimamia Wizara hii. Namfahamu ni mtu makini, mzoefu na mwenye uwezo mkubwa wa kuongoza Wizara yote ile. Nakutakia mafanikio mema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile kutumia nafasi hii tena kuwashukuru wapigakura wangu wote na wananchi wote wa Wilaya ya Njombe, hasa Njombe Kaskazini kwa imani ambayo wameonyesha wakati wote na kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi. Imani huzaa imani. Nakushukuru ni kuomba tena.

Baada ya salama hizo ningependa kutoa ushauri ufuatao kwa Wizara hii. Moja, kama alivyosema mwenzangu aliyenitangulia, ardhi haiongezeki lakini watu wanaongezeka. Kwa hiyo, Watanzania tutumie vizuri ardhi tuliyonayo kwa sababu tukiharibu hatutaipata tena. Kwa mfano, upanuzi wa miji na vijiji unaelekea kumeza ardhi ya kilimo na kuongeza umaskini. Kitendo cha kufuga mifugo kwa kuwatembenza

nchi nzima kinaharibu ardhi nzuri na mabonde mazuri ya kilimo kama vile ya Lwiche, Rukwa, Kilombero, Pangani, Rufiji mabonde ambayo yangekuwa ni ghala la chakula kwa nchi hii na hazina kubwa ya chakula kwa nchi hii yanamalizwa na kwato za ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukajificha, lakini ni kweli kwamba rasilimali hii ikipotea tutakuja kujuta wenyewe tusichezee shilingi chooni, tutunze ardhi ndiyo silaha yetu ambayo tumbekiwa nayo kama Watanzania. Siasa zinatupa shida, lakini tukubali kwamba *we can hide but we can't escape. It is a reality*, ardhi ndio silaha kuu tulinayo, ni lazima tuitunze kama lazima tuishi. Mabonde haya ndiyo ghala la chakula na tungeweza kuwa *net exporter* wa chakula kama tungetii hii. Kumbuka adui mkubwa wa mazingira ya binadamu ni binadamu mwenyewe, kwa lengo la kutaka kujiendezeza anajikuta anajimaliza mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi nzuri nashauri itumike kwa kilimo na uzalishaji mali. Ardhi mbaya itumike kwa majengo. Ningependa vile vile kushauri kwamba sheria ya vijiji ya mwaka 1975 itazamwe upya kwa sababu karibu miaka 30 imepita na wakati ule ule tulikuwa tunagawa vijiji kwa idadi ya watu. Sasa hapa naipongeza Wizara, imepima vijiji vyote 11,000.

Lakini nauliza kama unapima vijiji, kimoja kiko katikati, vingine viko pемbeni, vingine viko nyuma, hiki cha katikati ukishakiwekea mipaka hakiwezi kupanua shughuli za kilimo kwenda ng'ambo ya eneo la mpaka. Nilidhani tunetumia nafasi vile vile kutazama uwezekano wa kuunganisha baadhi ili vionekane *economically viable*. Vionekane ni viwanda mama ama la sivyo tutaunda vijiji ambavyo vitakuwa ni vitovu vya utawala na kuongeza gharama za utawala wakati uwezo wa kuzalisha mali utazidi kushuka kwa sababu unamezwa na majengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kwamba tunapopanua vijiji na miji tunaongeza umaskini. Ni lazima tuongeze huo umaskini. Lakini bila sera, bila kuamua kwamba ardhi hii ndio ghala letu, ndiyo *source* yetu ya uzalishaji mali na kusema majengo yawe upande gani na ikiwezekana yawe ya ghorofa kwa sera ya Serikali kusimamia ardhi, ardhi hii itakwisha na nchi yote itajaa majengo.

Miji yote itaunganika kati ya Dar es Salaam mpaka Morogoro, Morogoro mpaka Dodoma, Dodoma mpaka Tabora itakuwa imejaa miji kama ilivyo Kilimanjaro leo. Kilimanjaro leo imejaa majengo, samahani kwa nia nzuri tu, na makaburi. Sasa makaburi tunajenga kwa saruji. Kama tungakuwa tunajenga kwa udongo wa kawaida wangeweza kusema baadaye wangeweza kuondoa mifupa na kuweka pengine ukalima mashamba. Sasa hii saruji ambayo tumeeneza nchi nzima kwa kujenga makaburi nayo ni *disadvantage* kwa maana tunakokwenda ardhi inazidi kwisha na kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naongea lugha ambayo huenda haipendezi lakini ukweli lazima usemwe tuisubiri watu wafe ndipo tuanze kusema. Ardhi ni lulu na haiongezeki na hakuna njia. Ukienda China, Beijing na mahali pengine robo tatu ya mboga za mjini zinalishwa kwa kilimo kinachoitwa *urban family*.

Kwa sisi miji yote imejaa majengo tu, kwani msimbazi pangefaa kwa kilimo, lakini yamejaa majengo. Unapanga eneo la viwanda, hatujengi, kwani eneo zuri, hata pale Njombe lisiwe kwa ajili ya kilimo cha mboga kulisha mji? Hayo mawazo hayapendezi kwa sababu maeneo mazuri yanapendeza kupima viwanja. Viwanja mnaelewa maana yake. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba ili twende na wakati, sheria hii ya mwaka 1975 itazamwe upya na tafsiri ya kijiji itazamwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe unajua kuna vijiji kama Kibaigwa, zaidi ya 40. Kuna Uwemba, Mtwango, Illembula vyote vile ni vijiji Miji, vinazidi kuongezeka tu. Sasa kama hatuingilii na tunaacha vinakuwa hivi hivi, *centre* iko huku tunaacha mpaka tuje tubatize kwamba ni mji mdogo wakati umejengwa shaghalabagala na gharama za kuurekebisha ni ngumu tutapata matatizo.

Nilikuwa nashauri tungeangalia sasa hivi na kuwa sera mpya ikiwezekana kutazamwa upya. Unapima vijiji hivi na kuweka mipaka yake halafu vya pembeni vyenye ardhi navyo umevipima huyu wa katikati kwa sababu tu viliwekwa awe kwa sababu ya *population* ni cha utawala ukishazingira kiwe ni kijiji kitawezaje kuunganika na vingine ili viwe *economically viable*? Kwa nini tusitumie nafasi hii kuunganisha vijiji hivi hata dhana ya kijiji tuka-*define* upya, kijiji maana yake familia 500 au vipi.

Mahali pengine hata miji mnaunganisha kwa lengo la utawala wa kiuchumi, tukawa tunakwenda mbele. Vinginevyo tutakuwa tumepitwa na wakati na baadhi ya mambo haya tukikiuka misingi, misingi itatukiuka. Kijiji kinatakiwa kuwa ni kiwanda mama kwa sababu nacho kikigeuka tena ni mji utazalisha wapi chakula?

Pili, nawapongeza kwa kuchora ramani za matumizi ya ardhi. Lakini tatizo kubwa hata mijini ni usimamizi wa kutumia hizi ramani zinabaki tu ramani zimechorwa kwa gharama kubwa lakini wasimamizi hawapo. Kwa hiyo, mambo yanakwenda shaghalabagala kama kawaida na mahali inaonekana hapakupimwa na ndio maana nchi hii hakuna mji wowote ambao umepimwa vizuri isipokuwa labda hiyo Kigamboni ambayo sasa wanafikiria. Nakumbuka labda kama Mwadui na Mgololo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukajificha, lakini palipo na hazina yako ndipo palipo na roho yako. Roho yangu mimi iko kwenye ardhi. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii na viongozi wa taasisi zake kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri, pongezi na kuomba na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pungezi kwa mkakati wa kuboresha eneo la kigamboni kuwa mji mpya wa kisasa. Mkakati huu ni mzuri na unapaswa kuungwa mkono kwa dhati na wananchi wote na hasa wale wanaoishi huko Kigamboni kwa muda mrefu hadi sasa. Mabadiliko hayo ni kiungo cha kisasa kwa utalii na kuongeza pato la Taifa. Hata hivyo, elimu itolewe hasa kwa wakazi ili wasipoteze fursa nzuri zilizopo kwa kutoelewa mfumo halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pungezi kwa Wizara kwa kufupisha muda wa kuwezesha hati miliki za ardhi kupatikana. Hata hivyo, bado upo urasimu ndani ya Halmashauri na hata Halmashauri nyingine kama Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kukosa Afisa ardhi mwenye viwango vyta utendaji katika ngazi ya Afisa Ardhi Wilaya. Udhafu wa aina hii unachangia Wizara ya ardhi kubebeshwa lawama zisizostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupata Afisa Ardhi.

Natoa pungezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kufanya maamuzi mazuri katika mgogoro wa kiwanja Na. 205 kati ya mwananchi aliyejenga nyumba katika eneo hilo (Ndugu Hazilina) na kutakiwa kuivunja. Kama nilivyoainisha hapo juu, kukosekana kwa Afisa Ardhi Wilaya kutaweza kuchangia ucheleweshaji wa utekelezaji wa ushauri wa Mheshimiwa Waziri na kutoa mwanya wa mgogoro huu kuibuka baada ya Bunge kuvunjwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuvunjwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri utaratibu halali wa kupima eneo hilo ili kuwezesha zaidi ya nyumba 10 zilizopo katika eneo lenye mgogoro kupatiwa haki badala ya hoja ya mtu mmoja kiwanja Na. 205 kutawala. Haki iendelee kutendeka kwa wote. Wale wanaotumia nafasi zao za uongozi kushawishi na kupotosha ukweli juu ya mazingira halisi ya mgogoro wa kiwanja hicho wasipewe nafasi ya upendeleo na upotoshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji ardhi katika maeneo ya Serikali za Kijiji. Kijiji cha Misozwe/Manyoni, Kata ya Misozwe katika Wilaya ya Muheza kimeombwa eneo la ekari 100 na wawekezaji ili wajenge kitivo kikubwa cha kuhifadhi watoto yatima na waathirika wa Ukimwi na waathirika wa madawa ya kulevya. Wawekezaji wamekubali kuwasaidia wananchi hao katika mambo yafuatayo:-

- Kuwapa wananchi wa Kijiji cha Misozwe (Manyoni hisa 5%) ya thamani ya mradi huo.
- Kuwasaidia wananchi hao kujenga mabweni katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Misozwe kwa wasichana na wavulana.
- Kusaidia kuvuta umeme katika shule hiyo ya Sekondari ya Kata ya Misozwe.

- Kusaidia kujenga mfumo wa barabara na maji kwa ajili ya shule hiyo ya sekondari, mabweni ya wanafunzi, nyumba za walimu na maabara mbili zilizopo hapo shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri unaotakiwa, wawekezaji wametoa maombi rasmi kwenye Serikali ya Kijiji.

- (a) Halmashauri ya Maendeleo ya Kata (*WDS*) imekaa na kukubali maombi yao na kuandika muhtasari.
- (b) Mkutano Mkuu wa kijiji umekaa na kukubali maombi ya wawekezaji hao kutoka Italia wanaoita *Roseta Famiglia*. (*NGO*) hiyo Roseta Famiglia iliandikishwa mwaka 2005 kama *NGO* na ina hati zote. *NGO* hiyo ilinunua nyumba ya ghorofa moja Tanga mjini eneo la Raskazoni na imekuwa inawalea na kuwasomesha watoto zaisi ya 30 kwa muda wote huo.
- (c) Dhamira yao ni kuongeza huduma hiyo kwa kupata eneo. Kituo wanachokusudia kujenga kitakuwa kikubwa kuliko vyote barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, hatua hizo hazitoshelezi kuwawezesha Roseta Famiglia kupewa eneo la ubia na Kijiji cha Misozwe? Naomba ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba Wizara iboreshe mabaraza ya Kata yanayohusu ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonekana, wajumbe wengi hawaelewi kazi zao na wajibu wao katika kuendesha kazi za mabaraza hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza wajumbe wanaoteuliwa basi kabla ya kuanza kazi hiyo waandaliwe semina ili iwe dira ya utendaji wao wa kazi kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ninaomba Wizara iendelee kushirikiana na Halmashauri na Manispaa au Jiji katika upimaji wa ardhi hasa vijijini. Ni vyema watu wakajua mipaka ya maeneo hayo katika kuishi kwao ili kusiweko na mgogoro wa wananchi katika maeneo hayo. Kinachotakiwa wananchi waishi kwa amani na utulivu hasa panapokuwa wananchi hawagombani neema na faraja huwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha nikingoja majibu mema.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:- Kwanza pongezi za dhati kwa Wizara kuanzia Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Makamishna na kadhalika. Kwa utendaji mzuri na wa

kifanisi wanayoifanya, kweli mafanikio ni makubwa sana ukilinganisha wakati tumeingia Bungeni 2005 na sasa, "Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni".

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara, naomba wakaze buti, mambo yazidi kuwa safi, Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Wizara hii imetupa semina na katuonyesha mambo na mipango mizuri, napongeza hilo, lakini wasiwasi wangu ni juu ya siasa (wanasiasa) mara nyingi siasa zikizidi kwenye utekelezaji mambo huharibika hivyo ombi langu ni kwamba tusiingize sana siasa kwa wataalamu wetu, wapewe nafasi wafanye kazi zao kwa kufuatana na taratibu za kazi zilivyo kama tutafanya hivyo mambo yatakwenda kama yalivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mikakati mizuri iliyopangwa na Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), kwanza nimtie moyo Mkurugenzi mpya kwamba ari zaidi aliyoanza nayo aongeze kasi zaidi na tuko pamoja kumsaidia kama Wabunge ili afanikishe azma yake. Pamoja na hayo, naomba (*NHC*) watukumbuke Mkoa wa Singida kwani Mkoa ambaa ndio unafunguka sasa na wawekezaji wengi wamekuja Singida barabara zote ziendazo Mwanza – Arusha – Mbeya – Tabora – Manyoni – Dodoma – Dar es Salaam na kadhalika, zote zitafunguka.

Pia tuna madini mbalimbali, mradi wa umeme wa upepo, zao la biashara la alizeti, vitunguu vitamu kuliko vyote, kuku na kadhalika. Hivyo, uchumi wa Singida utakua na tutahitaji uwepo wa nyumba za kutosha hivyo tunaomba mje mjenge pia Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine naomba sana muwakumbuke Askari Polisi na Magereza hasa wa mikoani ukianzia Singida na walimu na kadhalika. Ni mradi mzuri sana kama mtajenga nyumba za waalimu vijijini kwani watakuwa ni walipaji wazuri tu kupitia ajira yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii: Nini hatima ya *Singida Motel Hotel* na *Peoples Club*? Vyote viko Singida mjini. Ni mali ya nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri na Katibu wake na Wakurugenzi wote wa wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni muhimu kuliko kitu chochote. Ardhi ni makazi, ni mali, ni uchumi, maendeleo yote hupatikana huko kwenye ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi toka kwa wafugaji kwa ajili ya kuporwa ardhi kwa ajili ya hifadhi ya eneo la uwindaji na maeneo ya wakulima. Naomba Wizara yako iangalie sana ni namna gani ya kutatua kilio cha wafugaji, kwanza kuwapimia eneo lao la malisho. Kuna usemi kwamba watu wengine wakihamia eneo la wafugaji wanasema wana haki ya kuhamia kwa sababu Katiba inasema, Mtanzania ana

haki ya kwenda popote. Lakini mfugaji hana haki kama hiyo ya kuishi popote, kwenye eneo la vijiji vya Loliondo kuna mgogoro mkubwa sana kwa ajili ya kutenga maeneo na kuchukua tena eneo la malisho ambayo ni tegemeo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kuhusu ujenzi wa nyumba yenze gharama nafuu kwenye bajeti ya mwaka jana 2009/2010 kwenye maeneo ambayo Wizara yako imepanga kujenga nyumba hizo ni pamoja na Wilaya ya Longido. Kwa masikitiko makubwa, kwenye bajeti hii sikuona kabisa jina la Longido popote kwenye hotuba yao. Vipi? Kuna nini? Wilaya ya Longido ni Wilaya mpya, naomba kama ulivyosema kwenye bajeti yako mwaka jana utukumbuke kutujengea nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maendeleo mengi ambayo watu wa longido wanaona kwenye wilaya nyingine lakini wao hawapati. Naomba wataalamu wote wa Wizara yako wakumbuke ombi la wananchi wa Longido, kwani baada ya kuona kwamba wamepewa ahadi mwaka jana niliwatangazia kwamba watajengewa nyumba hizo. Ili ahadi hiyo itimie, Wilaya hii iwekwe kwenye mpango wa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba. Pia napenda kumpongeza Waziri na Katibu Mkuu pamoja na timu yote ilioshiriki kuchambua hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara hii iwe makini sana kwa sababu kuna ujenzi holela ndani ya miji yetu. Hili ni tatizo kwa sababu hakuna mpango mzuri wa miundombinu kama vile barabara, miundimbinu ya maji umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujenzi holela linaleta taabu baadaye, kwani ukitaka kubadilisha mji kuleta miundombinu wananchi wanapata hasara kwa kuvunjiwa majumba yao na Serikali kupata hasara kwa kulipa fidisa na ugomvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *contractor* wa ujenzi ni lazima wasimamie kwa makini juu ujenzi wa nyumba za ghorofa ili wajenge nyumba zenyenye ubora ili zisiletie maafa, kwa sababu tatizo hilo lipo nchini mwote sio Dar es salaam pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali iwe na umakini wa kusimamia migogoro ya ardhi inayotkea mara kwa mara ili kupunguza mapigano na mauaji pamoja matatizo mbalimbali. Sheria hii ya ardhi iangaliwe na kuboreshwa zaidi na ifanye kazi zake kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile migogoro ya wafugaji na wakulima pia nayo ishughulikiwe. Tunajua kuwa Serikali imefanya kazi kubwa kwa kuwapatia maeneo wafugaji, lakini hata hivyo migogoro haiishi, ni lazima Wizara wakae kwa tahadhari pia katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, nawatakia kila kheri katika utendaji wao wa kazi.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri, ngumu, yenye malalamiko na mazingiraa magumu. Nawapongeza kwa kuwa malalamiko ya ardhi, viwanja na mashamba yamepungua kiasi. Ninaamini nguvu zaidi ikiwekwa, karibu yote yatamalizika.

Nawapongeza pia kwa hotuba nzuri. Ombi langu ni moja tu, maeneo matamu yaliyomo katika hotuba hii yatafsiriwe kwa vitendo katika kipindi cha bajeti hii. Mwisho wa kipindi hiki, tathmini ikifanyika iweze kuwa na thamani kweli ya fedha itakayokuwa imetolewa, siyo itakayokuwa imetumika! Ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu unaonekana kana kwamba yapo maeneo makubwa yasiyotumika, lakini ukweli ni kuwa pamoja na kuwa eneo hilo ni kubwa, maeneo ya kilimo, mifugo na makazi siyo makubwa kiasi hicho. Ombi langu ni kwamba, ni vyema Serikali kufanya mambo kadhaa ili kukwepa migogoro mikubwa ambayo inaelekea kulikabili Taifa letu siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubainisha na kutoa hati miliki za maeneo ya makazi (mjini) mashamba na ufugaji zoezi hili lifanyike mapema. Ni vyema ikazitaka Halmashauri zote nchini kukamilisha zoezi hilo mapema na maelekezo haya yaende na tarehe ya kukamilisha mazoezi hayo, iwe bayana na adhabu iwekwe kwa Watendaji Halmashauri za Wilaya ya watakaokiuka.

Maana yangu ni kuwa iwapo vijiji vyote vitapimwa na kumilikishwa kwa Serikali za Vijiji, wananchi mmoja mmoja wanaweza kupima maeneo yao polepole, kulingana na uwezo na kuhamasika. Hatari iliyopo, hili lisipofanyika maeneo haya huchukuliwa, na wanaoyakalia kupoteza haki yao ya kumiliki maeneo. Ili kuwalindia haki zao, ninaona ni vyema maeneo makubwa yapimwe na Serikali kwa gharama zao na marejesho yatafuata baadaye polepole kama kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Taasisi za Serikali kama shule, zahanati, viwanja vya michezo na kadhalika, navyo ni vyema vikabainishwa, vikapimwa na kila kimoja kikakabidhiwa hatimiliki. Ombi hili ninalitoa kwa kuwa maeneo hayo ni ya umma. Yakiwa ya umma hata uangalizi wake nao unakuwa wa umma, “*No Mans land*”.

Katika hali hiyo, umma usipokuwa na ufahamu wa thamani ya ardhi, matokeo yake ndiyo tunayoyashuhudia kila leo, matatizo ya kuvamiwa maeneo hayo bila mwenye maeneo hayo (umma) hata kupiga kelele, kuyaunda maeneo hayo. Ni vyema taratibu za kuyapatia hati miliki maeneo hayo mapema yaweza kuwa suluhu ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado lipo tatizo la fidia kutolingana na thamani halisi ya soko la kinachofidiwa. Tabia ya Serikali ni kukusanya mapato mengi kwa kutumia

kidogo, lakini ni vyema ikayatenda hayo kwa kutenda haki. Njia nzuri ya kutenda haki ni kuzipatia mara kwa mara sheria zinazotumika ili mara kwa mara zirekebishwe ili fidia hiso ziwe na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombi maalum kwamba Wizara hii kupitia ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) Halmashauri ya Wilaya ya Ksimba ivipime Vijiji vya Bupamwa (Mwamashimba) na Nyamilama ambayo ni Makao Makuu ya Tarafa za Mwamashimba na Nyamilama. Vijiji hivi vinakua haraka kuwa miji midogo, haijachangamkia “tenda hiyo”. Ikibidi watakiwe kufanya hivyo. Vijiji hivi kama vitakuwa kama miji midogo kwenda mikubwa bila kupimwa itakuwa aibu, fedheha na jambo la kutisha. Naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia hoja hii kwa kumpungeza Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji kwa hotuba nzuri ilioandaliwa kwa umahiri mkubwa. Mchango wangu, naanza kwa kuzungumzia juu ya majengo yanayojengwa hivi sasa, yazingatie miundombinu kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Kwa kweli wapo ambao hawazingatii hayo. Inasababisha Watanzania hao washindwe kukidhi mahitaji yao kwenye majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, hawazingatii maegesho ya magari. Inakuwa tatizo kubwa kwa wenye vyombo vya usafiri. Tatizo lingine ambalo ni kero kubwa ni ujenzi holela. Kwa kweli hali hii ni hatari kubwa kwa wananchi, kuna matatizo ya wagonjwa kuunguliwa nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kuunga mkono hoja.

**MHE.CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kwa hotuba ilioandaliwa kwa utaalamu na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nalipongeza Shirika la Taifa la Nyumba (*NHC*) kwa hatua madhubuti zinazochukuliwa kuimarisha uendeshaji wa shughuli za shirika. Lengo la kujenga majengo mengi ya kuuza na ya kupangisha linastahili pongezi. Kinachohitajika sasa ni kuanzishwa kwa Benki ya Nyumba (*Housing Bank*) ambayo itawapa wananchi mikopo ambayo itawawezesha kununua nyumba kutoka kwenye shirika, vinginevyo mpango mzuri wa kujenga nyumba za kuuza hautafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi pekee duniani ambayo wananchi wanajenga bila mikopo, yaani wanajenga kwa fedha tasilimu. Utaratibu huu unashawishi ujisadi na wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili linahusu upimaji wa miji na vijiji ili kuondokana na ujenzi halali. Nimeshauri mara nyingi kwamba:-

- (a) Ujenzi wowote ambao unafanywa kwenye maeneo ambayo hayajapimwa usimamishwe na watu wasijenge kwenye maeneo ambayo hayajapimwa kuanzia sasa.
- (b) Juhudi kubwa zifanywe kupima viwanja kwa wingi kuzunguka maeneo yaliyojengwa kiholela kuyazima yasiendelee kupanuka.
- (c) Maeneo ya zamani au yenyе nyumba ndogo kama za magomeni, Dar es Salaam, yapangwe upya na yaendelezwe kwa kujengwa maghorofa yenyе ghorofa tano au zaidi. Kufanya hivyo kutawezesha maeneo hayo kuchukua watu wengi zaidi na wakati huo huo kuwa na maeneo ya huduma za jamii.
- (d) Zile nyumba ndogo ndogo za *NHC* zilizouziwa wananchi zikombolewe (*should be bought back*) ili yaendelezwe kwa kujengwa maghorofa, lilikuwa kosa kubwa sana kuuzwa kwa nyumba hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, upimaji wa kijiji ufanywe kwa lengo la kuvifanya vijiji vitovu vya maendeleo na uchumi wa wananchi na sio tu mkusanyiko wa watu. Kwa hiyo, lengo ni kuandaa mpango wa maendeleo wa vijiji na upimaji wa mipaka, ni sehemu tu ya mpango mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU SAIDI ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuzungumzia suala la mwekezaji aitwaye au ajulikanaye kwa jina la Ruben, ambaye amewekeza Serengeti, ameiomba ardhi ya vijiji vya Wilaya ya Lindi na Wilaya ya Kilwa. Sipingi uwekezaji kama wanakijji wenyewe wangekubali, bali napinga jinsi mchakato unavyokwenda kwani unakwenda kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa ndiye aliyelibeba suala hili, kikao cha *full council* Lindi, Mkuu wa Mkoa alikuwepo ili kusisitiza kupita kwa mwekezaji huyo, na mwekezaji mwenyewe (Mzungu alikuwepo) ndani ya kikao hicho akisubiri maamuzi.

Katika Wilaya ya Kilwa Mkuu wa Mkoa alikuwepo siku ya tarehe 1 ili kuhimiza upitishwaji wa mwekezaji huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya *full council* ya dharura mwekezaji huyo (Mzungu) alikuja ndani ya eneo lakini akakuta kikao kimesimama kufuatilia muhtasari ambao walidai wameusahau. Kwa ujumla, Madiwani walidai waende kufuatilia vijiji ambavyo walidai kwamba vilikubali kutoa ardhi yao, lakini hawakukubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya vijiji hivyo ina Shule za Msingi na Sekondari, visima, zahanati na Vituo vya Afya, kuna Gereza Kuu la Kilimo la Kingurungundwa na maeneo mbalimbali ya mashamba ya wanavijiji hivyo. Mwekezaji amedai atawatafutia eneo la kuishi na atawajengeia vyumba kitu ambacho mimi naona ni uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji huyu kama aliweza kuwafukuza Wabunge wasiingie katika eneo lake: Je, wananchi wa Kilwa wanyonge wa kawaida watakuwa na sauti gani juu ya manyanyaso ambayo yangeweza kutokea baadaye?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba lifuatiliwe suala hili kwani linahusu maisha ya wananchi wengi, kwani vijiji 22 ni wakazi wengi. Jambo hili lisipelekwe haraka haraka liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini sera ya mikopo ya kujengea nyumba itaanza kutumika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa upimaji ardhi maeneo ya vijijini hasa kumilikisha ardhi kimila utaanza lini hasa Wilayani Chunya?

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za kutenganisha ardhi kwa ajili ya malisho na wakulima hasa Wilayani Chunya zitakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kigezo cha wingi wa watu ndicho kinathaminiwa kuliko ukubwa wa eneo hasa wakati wa kupandisha mamlaka ya utawala?

**MHE. FATUMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii ningependa kwanza nizungumzie kuhusu nyumba. Kwanza ielevwee kwamba kwa binadamu yejote bila kuwa na nyumba yake ambayo ni mali yake anakuwa hana utulivu katika kichwa chake. Nyumba za kupanga watu wengi wanakuwa katika manyanyaso makubwa kutoka kwa wamiliki wa nyumba.

Wizara ya Ardhi kupitia mashirika yake kwa nini hawajengi nyumba za kuwauzia wananchi hasa wasio na uwezo wa kujenga nyumba zao wenye? Wananchi kama hao watalipa kidogo kidogo na vyumba vingine watawapangisha wengine na kodi hiyo pia itachangia malipo ya deni la nyumba hiyo kwa Wizara ya Ardhi. Kwa kufanya hivyo, wananchi wataipenda Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoke nje kwa mfano Kenya, Uganda na hata Marekani wakachukue taaluma ya kushirikiana, kujengeana nyumba ili Watanzania nao waweze kusitirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee juu ya ardhi. Wakati Serikali inahitaji ardhi ya wananchi ama kupima viwanja au ardhi hiyo kuwagawia wawekezaji, basi ni kwanini wamiliki wa ardhi hiyo hulipwa pesa kidogo sana, pesa ambazo hawawezi hata kuanzisha maskani mapya, yaani kujenga au na kuanzisha mashamba mapya? Kwanini pia wanapohamishwa wasiwe wameshajengewa nyumba sehemu nyingine ili wasipate taabu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ambayo ina dhahabu au almasi kwanini Wizara isifanye mpango wa kumfanya huyo mwekezaji akaingia ubia na yule aliye na sehemu hiyo ambayo mgeni anakuja kuwekeza? Hili linamfanya mwananchi kuingia katika umasikini wa milele na kumwingiza Mtanzania katika umasikini wa milele. Lini Serikali itawaonea huruma Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni mwanasheria, naomba Serikali iwaonee huruma Mahakimu walioko katika Mahakama za Ardhi, wao hawana majengo yaliyo na hadhi ya Mahakama. Hakimu hayuko katika usalama pale anapokaa kuhukumu. Ni vile Watanzania wenyewe ni watu wa amani, lakini msishangae siku moja ikatokea hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilitamkwa kuwa wazee wa mabaraza ya ardhi wameongezewa posho za vikao kutoka chini kwenda Sh. 30,000/=. Je, Waziri posho hii ni sawa? Mzee wa Baraza anakaa juu ya kiti sawa na masaa anayokaa Mheshimiwa Hakimu na pia anayokaa Karani wa Mahakama.

Mzee wa Baraza anatoka masafa marefu kama Hakimu au Karani, kwanini Mzee wa Baraza asilipwe nauli kutoka kule anakokaa hadi Mahakamani kisha hiyo Sh. 30,000/= ikawa ndiyo *sitting allowance*?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Pamoja na pungezi hizo, ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Nyumba la Wilaya ya Karagwe, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya yalianzishwa kuwa na Ofisi zao Wilayani ili kurahisisha na kutoa huduma kwa wananchi wa Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Ardhi la Wilaya ya Karagwe liko Wilaya ya Bukoba Mjini na hivyo wananchi wa Karagwe huwajibika kusafiri umbali mrefu sana kutafuta haki yao. Ninaomba Serikali ipeleke Baraza la Ardhi la Wilaya Wilayani Karagwe ili kusogeza huduma ya Sheria karibu na wananchi. Vile vile Mabaraza mengi ya Ardhi hayana usafiri wa uhakika. Nashauri Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya yapatiwe usafiri ili waweze kutenda kazi zao kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kwa muda mrefu wameshindwa kupima viwanja vipyta kutokana na kukosa Afisa Ardhi Mteule. Tunaomba tupatiwe Afisa Ardhi Mteule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NHC*, Naipongeza Serikali kwa kuteua kijana mahiri sana tena kutoka sekta binafsi kuongoza

Shirika hili muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Naomba apewe ushirikiano wote kui-reform *NHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru *NHC* kwa kuwekeza Mkoani Kigoma na hasa katika Manispaa ya Kigoma Ujiji kwa kujenga majengo ya maofisi. *NHC* sasa iangalie jinsi watakavyokwenda mbele na kujenga majengo ya kibiashara katika miji midogo inayokua sana kama Mwandiga (*frame za maduka along Mwandiga – Manyoni Road*) na Kalinzi (*Balozi Salim Ahmed Salim Community Centre*). Hii itasaidia kupanua shughuli za *NHC* kupata mapato zaidi na kupanua shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri *NHC* iundwe upya kupitia *Cap.212* ili hapo baadaye Shirika liuze hisa *DSE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *real estate*, sekta hii inakua kwa kasi sana (*construction sector grows at the rate of 7%*). Hata hivyo, kama nilivyokwishesema miaka ya nyuma katika Wizara hii, sekta ndogo ya nyumba (*real estate*) haina *regulator*. Matokeo yake ni kuwa bei za nyumba nchini zinapanda sana kiholela, wapangaji wanatozwa kodi bila utaratibu maalumu na hivyo kuleta unyonyaji mkubwa sana.

Serikali ianzishe Mamlaka ya kuratibu *real estate* (*Real Estate Regulatory Authority*) ili kudhibiti bei za nyumba, kodi za nyumba na ushindani katika soko la ujenzi wa nyumba. Haiwezekani kuwa na sekta nzima ambayo haina *regulator*. Leseni za watu kupangisha nyumba zinatolewa na nani? Ni nani ambaye anahusika na malalamiko ya kodi (*rent*), ni nani anayedhibiti upandaji holela wa kodi, nani anayedhibiti ubora wa huduma za nyumba ili kuhakikisha kuwa raia wanapata huduma bora? *Tanzania Real Estate Regulatory Authority (TRERA)* ni chombo muhimu sana kulinda haki za wateja na wauzaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Mukigo pia, kijiji cha Nyarubande kuna tatizo kubwa sana la ardhi ambapo wananchi wamenyang'anywa ardhi zao na Baraza la Ardhi. Ninamwomba Waziri aende Kigoma kumaliza matatizo haya kwani ardhi kwa wananchi wa Kigoma ndio silaha pekee ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Ilala-Sharif Shamba (kiwanja chenye mgogoro), Mheshimiwa Waziri Chiligati anajua tatizo la kiwanja chenye mgogoro kati ya mwananchi na Kanisa la Anglicana (na Kituo cha Mafuta cha *Lake Oil*). Nina maslahi katika mgogoro huu kwani mhusika mkuu ni dada yangu kutoka Kigoma. Mahakama Kuu ilimaliza kesi na kumpa ushindi mwananchi. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeonesha nia ya kukata rufaa. Hata hivyo, Kanisa la Anglicana limekodisha eneo hili kwa mwendelezaji binafsi na kuanza kujenga bila kufuata utaratibu wala sheria za kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nililileta mbele ya Waziri na akaahidi kulifuatilia na akafuatilia. Hata hivyo, inaonesha kuwa haki haitendeki kwa mwananchi mwenye malalamiko. Hisia zinajengeka kuwa, kwa kuwa Mheshimiwa John Chiligati ni muumini wa Kanisa hilo, basi analinda maslahi ya Kanisa hasa ukizingatia kuwa mlalamikaji ni Muislam. Mimi sijui Mheshimiwa Chiligati anasali Kanisa gani na wala

siamini kuwa Komredi anaweza kufanya maamuzi kutokana na dini yake. Hata hivyo, hisia hizi sio nzuri kwa kiongozi iwapo haki haionekani kutendeka. Ninaomba suala hili limalizwe kwa kutoa haki kwa mwenye haki. Mnyonge asionewe katika nchi yake. Ninamwomba Waziri aendelee kulimaliza suala hili kwa mazungumzo ya pande zote. Nchi yetu imejijengea sifa kwa kutetea unyonge. Hivyo, mnyonge apewe haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya Kijiji cha Mwandiga. Kijiji cha Mwandiga kinapakana na Manispaa ya Kigoma Ujiji. Ukaribu huu umeleta migogoro mikubwa ya ardhi na hata wananchi kunyang'anya ardhi yao kwa kisingizio cha sheria kuwa Mwandiga ni Mji Mdogo/*Trade Centre*. Inashangaza kuwa Mwandiga inaonekana ni Mji Mdogo kwenye kunyang'anya tu wananchi ardhi yao ya mashamba badala ya kuipa Mamlaka ya Mji Mdogo. Bila kufuata taratibu za kugawa ardhi kwa Mujibu wa Sheria ya Ardhi, wananchi wa Kijiji cha Mwandiga, wamenyang'anya mashamba yao. Hata mpaka kati ya Kijiji cha Mwandigo na Kata ya Gungu katika Manispaa ya Kigoma umesogezwa na kuchukua ardhi kubwa sana ya Mwandiga (badala ya mpaka wa asili ambao ni Mto).

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais, Mheshimiwa Dr. J.M. Kikwete, alipokuwa Kigoma, katika Kijiji cha Nyambande alitangaza kuwa ardhi yote iliyochukuliwa bila kufuata taratibu ni ardhi batili na hivyo, watu wote waliopewa ardhi katika eneo la Njiapanda ya Mwandiga wanapaswa kunyang'anya ardhi hiyo na kuruhusu Serikali ya Kijiji cha Mwandiga kupanga mipango mizuri ya ardhi ikiwemo kujenga Kituo cha Mabasi cha Kimataifa kwa msaada wa Shirika la NSSF (*Mwandiga International Motel*). Naiomba Serikali kuititia Bunge lako Tukufu iseme ni lini itatekeleza agizo hili la Rais ili kulinda ardhi ya wananchi wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya mpaka kati ya Manispaa ya Kigoma – Ujiji na Kijiji cha Kalalangobo (Kata ya Kagongo) ambapo Manispaa imehamisha jiwe la mpaka na kuingiza mashamba ya wananchi eneo la Manispaa. Ninaomba Wizara isaidie kumaliza tatizo hili kwani watu wa Manispaa wamekuwa wababe sana.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nyingi sana kwa Wizara kwa mabadiliko makubwa yanayofanyika katika sekta hii muhimu, nashauri Wizara iangalie upya mikataba kati *NHC* na wawekezaji binafsi yaani ubia katika kuendeleza makazi katika Miji yetu, hasa Dar es Salaam. Kwa sasa *NHC* imekuwa ikiingia ubia katika kujenga majengo kwa ajili ya biashara na makazi yaani *NHC* ina viwanja ama majengo ambayo imepanga kuyaboresha ama kuyajenga. Ni vipi *NHC* iingie ubia na mwekezaji binafsi ambaye huchangia fedha za ujenzi kisha anamilikishwa jengo husika kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile viwanja vingi vya *NHC* viko katika “prime areas”, *NHC* haihitaji kutafuta wawekezaji binafsi kwani yenyewe inaweza kupata pesa kutoka katika mabenki kwa ajili ya miradi hiyo. Kinachoshangaza ni pale mwekezaji huyo anapopewa hatimiliki kwa ajili ya kupata mikopo hiyo. *This does not make any business sense. It also leaves a lot of questions rather than address them.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate ufanuzi katika hili.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika hoja hii kwa maandishi. Ushirikiano kati ya Taasisi ya EPZ na SEZ na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Makazi, je, kuna ushirikiano gani kati ya Wizara na Taasisi hizo mbili ambazo zinahitaji ardhi ya kutosha kwa ajili ya kufanikisha shughuli za kuendeleza uwekezaji? Kuna taarifa kwamba taasisi hizi zinapata taabu sana za kupata ardhi kama vile walivyofanikiwa kupata eneo la kutosha kule Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ardhi ya Watanzania katika hali ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Ni ukweli usiopingika kati ya nchi hizi tano za Jumuiya, Tanzania ndio yenye utajiri wa ardhi. Wizara inajipanga vipi katika kuhakikisha kuwa Sheria za Ardhi tulizonazo zinafanyiwa mapitio ili kuhakikisha hakuna mwanya au upungufu katika sheria zetu utakaoweza kutoa mwanya kwa wasio Watanzania kuweza kumiliki ardhi yetu ambayo inabidi tuidhibiti kwa njia yoyote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa, napongeza jitihada za kuliimarisha Shirika kwa maslahi ya Watanzania. Ushauri wangu ni kwamba mikakati ambayo Shirika imepanga ni vizuri utekelezaji wake ukawa wa haraka kuokoa upotevu wa fedha na kukomesha wanaotumia Wizara kujinufaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia kuhusu hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali muhimu sana hapa duniani. Nchi yetu ya Tanzania tunajivunia sana ardhi yetu jambo ambalo ni adimu sana katika nchi nyingine. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwa Serikali kwanza kutoa elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na thamani ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango iliyopo ya kushughulikia migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji kwa upande mmoja au wawekezaji na wanavijiji kwa upande wa pili, je, Serikali inayo mikakati gani ya muda mfupi na mrefu ya kushughulikia migogoro niliyotaja hapo juu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana kwamba mingi katika migogoro ya ardhi inayopatikana au kutokea hapa nchini, inasababishwa na viongozi na hasa watendaji huko vijijini na inatokana na kutoijua vizuri Sheria ya Ardhi. Je, Serikali inayo mipango gani ya makusudi ya kuwaelimisha watendaji hao ili waweze kukabiliana na changamoto hiyo na kuepukana na migogoro ambayo mara nyingi inahatarisha maisha ya wanavijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumba za Serikali (*NHC*) zinazopangishwa na hasa Mjini Dar es salaam kuna matatizo katika kupangishwa kwake na inaelekea hakuna kumbukumbu sahihi juu ya nyumba hizi. Inasemekana mtu aliyepangishwa anawenza kuhama na yeche kumpangisha mtu mwengine kwa bei ya juu zaidi bila Serikali kupata

taarifa, sijui Serikali inasemaje kuhusu suala hili? Kama hali niliyoeleza hapo juu ni kweli basi kuna uwezekanao wa hata nyumba kuuzwa na Serikali ikawa haina taarifa ya kuuzwa kwa nyumba hiyo. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina kuhusu tetesi hizi.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima wa afya na kuweza kushika kalamu na kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Spika, Wenyeviti na watendaji wote wa Bunge hili, kwa umakini wenu wa kuliendesha Bunge kwa viwango vikubwa, Mwenyezi Mungu azidi kuwapeni nguvu, amina. Pia nampongeza sana Waziri na watendaji wake wote kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, nampongeza Waziri Kivuli (Msemaji wa Kambi ya Upinzani), kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, katika utambulisho wa leo kwa wageni, watendaji wengi wa Wizara nimesikia wanakaimu. Namwomba Waziri, watendaji hawa wathibitishwe kwani kufanya kazi kwa kukaimu, ufanisi wake unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango mizuri ya Wizara bado jitihada kubwa zaidi inatakiwa ili mipango hiyo ipate kufanikiwa. Juzi tumeoneshwa mipango mizuri ya Mji Mpya wa Kigamboni, tuhakikishe kuwa ramani hiyo inafanikiwa isibakie kwenye makaratasi na *cassette* za *video* tu. Mara nyingi Serikali inapanga mipango mizuri lakini utekelezaji ndiyo inakuwa kasheshe kwani mipango bila ya uhakika wa kupata fedha, ndio unaosababisha matatizo au mambo mengi kukwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumesikia habari si nzuri ndani ya vyombo vyta habari kuwa viongozi mbalimbali wameuza sehemu za wazi za kuchezea watoto. Tunaiomba Serikali iwachukulie hatua kali wale wote waliohusika ili iwe fundisho kwa wengine wanaotumia dhamana zao vibaya kwa kuifanyia ubadhirifu Serikali ambayo wananchi ndio waliowaweka kwa kodi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara na Waziri kwa kuthubutu kulibadilisha Shirika la Nyumba na kubadilisha uongozi na jitihada za watendaji wapya tunazona hasa kuokoa kodi za Serikali ambazo wajanja wachache wasioitakia mema nchi hii wanajinufaisha, hongera sana Waziri Chiligati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, hivi karibuni tumepitisha Sheria ya Mifugo ambayo inataka tugawe ardhi kwa wakulima mbali na wafugaji mbali. Serikali ifanye jitihada za makusudi ili mambo haya yafanyike haraka sana isije ikasababisha vurugu. Kwani kufanya hivyo, itaepusha matatizo yanayotokea kila siku kwani kugawa ardhi kama sheria inavyotaka ni vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa hoja yake kwa umahiri mkubwa. Aidha, naipongeza Wizara kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM 2005 – 2010. Ninaimani kuwa Wizara itaendelea kusimamia masuala yote yaliyojitekeza kama changamoto ambazo zimeorodheshwa na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia mafanikio katika uchaguzi wa mwaka 2010, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii ili kumpongeza Waziri na watendaji wake wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba kwa kweli katika Mawilaya lina watendaji ambao ni wabadhirifu sana, wanakusanya fedha kiasi ambacho hazilisaidii Shirika bali wanajaza matumbo yao tu. Mfano Jiji la Tanga, mpangaji anapangishwa nyumba ikiwa mbovu kabisa na anaamua kuikarabati kwa fedha zake mwenyewe. Shirika linafikia kusema kuwa mhusika hakuitengeneza nyumba hiyo bali ni Shirika, kumbe lililofanywa na Shirika ni aidha kubadilisha mabati chakavu au kuweka rangi. Nina wasiwasi na Shirika wakati mwengine kutoa mahesabu ambayo sio ya ukweli ya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Jiji la Tanga, Plot No.61AB-KBII, hapa mpangaji alikarabati mwenyewe sehemu kubwa ya nyumba hiyo karibu 85%, mwisho mpangaji huyo pia wakati anapewa mkataba wa upangaji nyumba hiyo yote ilikuwa anamiliki yeye. Cha kushangaza baada ya ukarabati wa jengo lote na akawa amechelewa kulipia fedha ya jengo la awali aliloanza kutengeneza alinyang'anywa sehemu ile na akahamishwa sehemu nyingine ambayo aliikarabati ambayo hapo awali ilikuwa ni sehemu ya jiko na choo.

Alicoambiwa ni kuwa lile ni eneo tofauti na lile la kwanza wakati eneo la kwanza kwa nyumba ile vilikuwa ni vyumba viwili vya kulala na eneo la ukumbi wa kupumzikia. Inawezekana nyumba hiyo hiyo moja iliyokuwa na namba moja ya kitalu kubadilishwa na kuwa ni *block* mbili tofauti? Naliomba Shirika litembelee Jiji la Tanga kuna dhambi kubwa zinazofanywa na watendaji ambao wanajichotea fedha za umma kwa manufaa yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania itajengwa na wenye moyo.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hatari kubwa inayoikabili nchi yetu ni migogoro ya ardhi. Hivyo basi, inahitajika jitahada za makusudi za kuhakikisha sheria zilizopo zinasimamiwa na migogoro inatatuliwa katika muda muafaka. Kutokutoa maamuzi kwa wakati kunaongeza chuki kati ya wananchi na Serikali yao. Naomba dosari hizo na changamoto zilizopo zishughulikiwe kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza pale ambapo tayari vijiji vimepimwa na mipango ya matumizi ya ardhi imeridhiwa, inakuaje maamuzi ya wananchi kwa ardhi yao yanapingwa na ngazi nyingine za Serikali. Kwa mfano, yapo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo au ufugaji. Inatokea Serikali kuwaondoa wafugaji katika ardhi ambayo tayari katika mipango ya kijiji wamesharidhia. Kimsingi wananchi wanaondolewa Mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi yao. Ni vyema basi Serikali itamke bayana kwamba sasa matumizi ya ardhi yatapangwa na Serikali na si vinginevyo ili kuondoa mgogoro, vinginevyo maamuzi yanafanywa na kijiji yaheshimiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo mgogoro wa zaidi ya miaka 10 wa ardhi kule Kakese – Mpanda, kwa shamba linalojulikana kama Shamba la Benki hadi sasa hakuna maamuzi yaliyotolewa na Serikali. Kwa niaba ya wananchi, tunahitaji maelezo ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi, naomba kupewa maelezo kwa nini hakuna Baraza la Usuluhihi la Ardhi katika ngazi ya Wilaya, inaanza kwenye Kata na Mkoa. Niombe Wizara kuangalia umuhimu wa ngazi hii ya Wilaya na kuridhia kuanzisha Mabaraza hayo ili haki pia gharama ziweze kupungua hasa ukiangalia umbali wa Kata/Wilaya na Makao Makuu ya Mkoa, kasi ya sasa hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hati za kumiliki ardhi mijini, inasikitisha sana, kuna usumbufu mkubwa wanaopata wananchi kupata hati hizo kwa matumizi mengine ambayo yanahitaji kuwepo kwa hati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Miji kwa mfano Dar es Salaam migogoro mingi ya ardhi imetokana na watumishi kuwepo kwa muda mrefu na kufanya kazi kwa mazoea au mali zao. Si Dar es Salaam pekee ni takribani Miji yote nchini kwa sababu Serikali imeacha utamaduni wa kuhamisha wafanyakazi. Ni vema mkaangalia faida na hasara ya watumishi kukaa kituo kimoja kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalazimika nami niseme kuhusu mpaka wa Wilaya ya Mpanda na Nkasi. Kwa niaba ya wananchi wa Mpanda, hatukubali kuendelea kupokonywa ardhi yetu. Mpaka halali ni Chizi tangu enzi za Mkoloni na si Kanyamkaa kama inavyodaiwa na Mheshimiwa Nyami, Mbunge wa Nkasi katika mchango wake. Hivyo basi, ni lazima sasa Wizara iingilie kati mpaka huu ambaeo Mheshimiwa Mbunge anataka kuonyesha kama ni mgogoro hata hapa ulipo leo, Wilaya ya Mpanda imepokonywa ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Shirika la Nyumba, kama nilivyoeleza katika semina, ni Shirika la Taifa hivyo mipango yake iwe inaangalia nchi hii kwa upana wake ili wananchi wote wanufaikie kwa kuwepo kwa Shirika hili. Vinginevyo hata maana ya kuwepo kwake hakutakuwa na maana kama litabakia kuwa ni la sehemu moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenyе ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono, naomba kuchangia maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya, kwa kuwa Mabaraza hayo, ni muhimu sana katika kutatua migogoro ya ardhi na kwa kuwa yameanzishwa Mabaraza ya Ardhi katika Wilaya 39 tu, je, kwa nini Mabaraza haya yasianzishwe kila Wilaya ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa mipaka ya vijiji, je, Serikali ina mpango gani wa kupima vijiji vyote vya Wilaya ya Mpwapwa na kuwakabidhi hatimiliki ili hati hizo ziwasaidie wananchi kupata mikopo kutoka katika benki? Fedha ambazo zitasaidia kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti ujenzi holela katika miji, ujenzi ambao hauzingati *master plan* ya miji?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza kitaaluma Maafisa Ardhi na kuongeza udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ardhi ili kupata Maafisa Ardhi wengi hadi kwenye Kata? Pia kuna mpango gani wa kuwapatia vitendea kazi vya kisasa, usafiri, (magari, pikipiki) na kuboresha maslahi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), wana mpango gani wa kujenga nyumba za gharama nafuu za kupangisha na kuuza kwa gharama nafuu kwa wananchi hapa nchini ukiwemo Mkoa wa Dodoma na ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa?

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi vijijini, bado unasuasua. Jimbo la Igalula ni la vijijini, uhamasishaji wa upimaji ulifanyika sana, wataalamu wakaanza kuvinjari kwenye Jimbo lakini utekelezaji wa kupima vijiji katika Jimbo hilo haupo. Je, Wizara na watendaji mnasahau tulikotoka? Hivi ahadi ya kupima vijiji na utekelezaji unaeleweka juu ya uchangiaji, je, wataalamu vipi wanalikimbia Jimbo hili kwa kuwa mnaona watu hawapo wala vijiji havipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna Tarafa mpya moja na Kata tano mpya sambamba na Vijiji, je, wananchi wasipojua kiutawala wako wapi, utawala bora utapatikanaje bila kujua mipaka yao kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha kusubiri jibu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasema nini kuhusu suala la wananchi wa Kaliua wapatao 23 walivyoondolewa kwenye ardhi yao na kubomolewa nyumba zao tangu mwaka 2003 kwa madai kwamba wanapisha upanuzi wa barabara kutoka Urambo – Kaliua – Kigoma. Baada ya nyumba

hizo kubomolewa, viongozi wa Serikali walijenga nyumba zao za biashara, hakuna barabara iliyojengwa na hadi leo hawajalipwa chochote, huu ni mwaka wa tano suala hili nalifikisha Serikali lakini halijafanyiwa kazi. Uonevu kama huu wa watu maskini utaendelea mpaka lini? Wananchi hawa wanataabika kwa miaka yote wakidai haki yao bila mafanikio wala msaada wa Serikali. Serikali ileze leo ni lini wananchi hawa watalipwa haki yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Hifadhi ya Misitu wa Geita (*Geita Forest Reserve*) lililopimwa mwaka 1952 na kupewa GH mwaka 1953. Viongozi wa Serikali ngazi za Mkoa na Wilaya wamevamia eneo hilo la misitu na kupima viwanja 1,396. Wataalamu wa Halmashauri ya Geita wameuza viwanja 551 kati ya viliviyopimwa mwaka jana 2009. Wananchi wenyе nia njema walimuita Naibu Waziri wa Maliasili kwenda kushuhudia kinachoendelea. Baada ya kufika alipiga marufuku viwanja vilivyouzwa kujengwa nyumba kwani ni hifadhi ya misitu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4/7/2010, Mkuu wa Wilaya ametangazia wananchi waliouziwa viwanja 551 wajenge haraka nyumba kabla uchaguzi haujafika. Hili ni eneo la hifadhi, wanasiasa wanaingilia na kutoa maagizo yao ili kujijenga kisiasa kuelekea uchaguzi ujao. Serikali inasemaje/inatoa kauli gani juu ya eneo hili la msitu wa Serikali wa Geita ambao unauzwa na viongozi waliopewa dhamana?

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri John Chiligati, pamoja na wasaidizi wake wote, kwa kuandaa hotuba ya bajeti hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Chiligati na wasaidizi wake kwa kufuatilia vizuri kero zinazowafikia katika Wizara ya Ardhi kwa umakini na kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa, namuomba Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hoja hii atoe ufanuzi ni lini Wapimaji wa Ardhi wa Wizara walipima na kutafsiri mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na Mji wa Mikumi pamoja na Vijiji vya Lumango, Ruhembe, Kihelezo, Kidegobasi hadi Kitete na waliwashirikisha viongozi gani wa Serikali za Vijiji au Wilaya? Nauliza maswali haya kwa sababu nimeshtushwa na maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika kifungu cha 50 kinachotamka kuwa Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na TAMISEMI wamekwishatatu migogoro baina ya Hifadhi ya Taifa Mikumi na vijiji vinavyopakana navyo. Kwa masikitiko makubwa, natamka kuwa maelezo hayo sio sahihi kwa sababu sijataarifiwa juu ya zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufuta kabisa migogoro baina ya Hifadhi ya Taifa Mikumi na Vijiji vinyopakana navyo, naiomba sana Wizara/Serikali ihakikishe inawashirikisha kikamilifu viongozi wa Serikali za Vijiji katika hatua zote na taratibu za upimaji kwa kuanza na “briefing” ya awali, mpango wote utakavyofanyika na pia hasa tafsiri ya Waraka au GN ya mwaka 1975 iliyotiwa saini na Mheshimiwa Marehemu Baba

wa Taifa, kwa maana hii mipaka ya Vijiji vya Kata za Ulanga na Kihangali vinavyopakana na hifadhi vitafsiriwe pia kulingana na *GN* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba tamko la Mheshimiwa Waziri kubainisha mahali ambapo mpaka wa Wilaya ya Mvomero na Kilosa unakatiza wapi katika barabara ya lami ya kutoka Morogoro kwenda Mikumi jirani na kijiji cha Doma? Ni kwenye Mto jirani na Doma au eneo kilichopo kibao katika hifadhi kilichoandikwa “Karibu na kwa heri Wilaya ya Mvomero”?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa jinsi walivyoanda hotuba hii ya bajeti. Naunga mkono hoja hii. hotuba imeandaliwa kwa kuweka wazi nini Wizara imefanya na matarajio yake kwa kipindi kijacho. Ni kutokana na hayo matarajio, imenilazimu niombe ufanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alisimamisha uongozi wa ardhi, Kinondoni kwa tuhuma mbalimbali na kusababisha adha kwa walioomba viwanja na wanaotarajia kupata huduma. Je, Waziri anachukua hatua gani ili shughuli zisisimame wakati uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya matatizo ya namna hiyo ni mengi si kwa Dar es Salaam peke yake, bali kwa sehemu kubwa ya maeneo ya miji yetu. Je, kwa nini Mheshimiwa Waziri asiagize Wakuu wa Mikoa wengine wasiwaonee aibu Maafisa wa Ardhi wanaovuruga utendaji wa kazi zao, ili mradi tu wafuate sheria. Nalisema hilo kwa sababu wakati nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya niliwhi kumfukuza Afisa Ardhi wa Mkoa na nikaambiwa, kisheria nilifanya makosa ingawaje baadaye aliondolewa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aweke msukumo wa kupima maeneo kwa ajili ya wawekezaji wakubwa ili ugomvi wa kupambana na wanavijiji upungue kwa hivi sasa. Wapo pia wawekezaji feki ambao wanashirikiana na baadhi ya viongozi wa vijiji kugawa ardhi bila kufuata taratibu. Nashauri suala hili lipewe umuhimu ama sivyo, nia nzuri ya Serikali kuwakaribisha wawekezaji katika azma ya kilimo kwanza inaweza isifanikiwe. Sera ya upimaji na ramani nadhani itazingatia suala hili, ili kupunguza hofu za wananchi na wale wanaotaka kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha kanda kwa ajili ya usajili wa Hati na mambo mengine. Hili limesaidia sana kupunguza gharama, muda na hata rushwa katika kupata hati hizo. Kazi iliyopo sasa ni kuzisaidia ofisi hizo ili ziwe na zana, samani, vyombo vya usafiri na kwa kushirikiana na ofisi za Wakuu wa Mikoa husika watoe nafasi nzuri za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuomba mambo yafuatayo yazingatiwe na Wizara:-

Kwanza, uanzishwaji wa Benki ya Nyumba upewe umuhimu wa pekee, maana kutegemea Benki ya Azania, *CBA*, *ICB*, *SBL* na *UBA* kwa mikopo ya nyumba kwa riba kubwa, itakuwa vigumu kwa wale wanaojenga nyumba za kuishi na siyo binafsi za biashara, kuweza kulipia mikopo hiyo.

Pili, naiomba *NHC* iangalie upya sera yao ya upangaji ili wale wanaopangisha nyumba hizo kwa watu wengine badala ya wao walioingia mkataba, wachukuliwe hatua. Pia nawaomba wanipatie nyumba ya kupanga kwa familia yangu kubwa.

Tatu, ujenzi wa nyumba kwa maeneo yenyе uhaba mkubwa wa nyumba kama Sumbawanga upewe kipaumbele kwa hali ya juu ili azma ya Rais Kikwete kutaka maeneo yote ambayo yako pembezoni yapewe umuhimu wa pekee kwa hali na mali. Nategemea uongozi mahili wa sasa wa *N.H.C.* upewe kila msaada ili utekeleze matarajio hayo bila kuingiliwa na uongozi wa mara kwa mara wa Wizara ila tu mahali ambapo ukiukwaji wa sera utadhihirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani yetu ya uchaguzi, kazi mojawapo ambayo tutaulizwa na wapiga kura, ni kutokana na hatua ndogo inayofanywa katika kupima mashamba kwa madhumuni ya kurasiimisha mali za wananchi ili waweze kukopa fedha kwa maendeleo yao. Hivi kweli tunayo maelezo ya kutosha kuhusu tatizo hili? Kwa nini Wizara isitumie wataalam toka Vyuo vyetu vya Ardhi vifanye kazi hiyo, kwa miaka mitano iliyopita, tungekuwa angalau na idadi kubwa kuliko hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara imalize kwa haraka viwango vya fidia kwa mazao mbalimbali. Hili ni lalamiko kubwa kila mahali tunapokwenda. Je, kwa nini Mheshimiwa Waziri asitoe mashamba yaliyoachwa wazi kwa kuwagawia wataalam wetu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine ili wakatoe utaaliam kwenye maeneo yanayozunguka vijiji kadhaa, kwa nia hiyo hiyo kuwafanya wataalam hao wawe ni sehemu ya kilimo kwanza kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kukuombea kheri, fanaka, baraka kwenye uchaguzi mkuu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Pamoja na hayo naomba kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu ardhi, viwanja na rushwa. Suala la ardhi na viwanja ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Maana juu ya ardhi ndipo binadamu huishi na kufanya shughuli zao zote. Hivyo, ardhi ni zawadi muhimu sana kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa maana hiyo kila mtu anayo haki ya kuitumia kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Hata hivyo Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu Tanzania suala la ugawaji wa ardhi na hususan viwanja vya kujenga nyumba za makazi au za biashara limetawaliwa na rushwa sana. Leo hii iwe Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na kote nchini, si rahisi sana kupata kiwanja cha kujenga bila kutoa rushwa. Rushwa imekuwa kama ugonjwa! Aidha, viongozi wengi wanaofanya kazi katika Idara ya Ardhi nchini kote wana tabia ya kuhodhi viwanja vingi na baadaye kuviuza kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hili lilitokea Dar es Salaam hivi karibuni, ndiyo hali halisi inayotokea nchini kote! Maafisa Ardhi kuhodhi na kuuza maeneo ya wazi Jijini Dar es Salaam ni kitendo cha aibu ambacho hakiwezi kuvumiliwa hata kidogo. Mimi binafsi nampongeza sana Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuchukua hatua kali dhidi ya wale wote waliohusika. Aidha, naomba Wizara hii impe ushirikiano mkubwa Mheshimiwa Lukuvi ili kuhakikisha kwamba tabia hiyo mbaya sana ya kula rushwa inakomeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba ili kukomesha vitendo vya rushwa katika Idara ya Ardhi nchini kote, viongozi na maeneo ya wazi na viwanja vinavyogawiwa, ufanywe mara kwa mara. Aidha, viwanja vigawiwe kwa watu *Physically*, nasema hivyo maana wakati mwingine viwanja hivyo hugawiwa kwa watu vivuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashauri Maafisa Ardhi wasikae eneo moja kwa kipindi kirefu kwani kwa kufanya hivyo maafisa hao hujenga mazoea na kufanya rushwa kama jambo la kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu matumizi ya hati miliki za kimila. Kwanza naipongeza Wizara kwa kuanzisha hati miliki za kimila. Hati hizo hasa kwa wanachi wa Wilaya ya Mbozi kama Wilaya ya mfano, zimekuwa za manufaa makubwa sana. Hata hivyo, bado hati hizo hazitambuli na taasisi za fedha hasa benki. Kwa sehemu kubwa hati hizo zinabaki kuwa na manufaa zaidi kwa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni jitihada gani sasa zinazofanywa na Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuhakikisha kwamba hati hizi zinatambuliwa na benki ili wananchi wafaidike na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigamboni ya Kisasa, tarehe 4/07/2010, Wizara iliendesha semina kwa Wabunge wote. Semina hiyo ilikuwa na lengo la kuwafahamisha Wabunge mpango wa kuujenga Mji wa Kigamboni kisasa zaidi. Binafsi napenda kukiri kwamba mpango wa Kigamboni mpya ni mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango huo mzuri kwa Mji wa Kigamboni bado nina wasiwasi katika maeneo yafuatayo namwombwa Mheshimiwa Waziri ajibu:-

(1) Je, haiwezekani kupunguza kipindi cha kuujenga mji huo cha kutoka 2011 – 2030? Kwa maoni yangu kipindi hicho ni kirefu mno.

(2) Sanjari au sambamba na mpango huo wa Kigamboni je, kuna mipango gani kwa Miji mingine kama vile Manzese, Tandale, Temeke ambayo pia inapangwa vibaya sana?

(3) Je, Wizara inafanya kazi sambamba na Wizara ya Miundombinu ili kuhakikisha kwamba ujenzi wa miji mipyä unakwenda pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji, umeme na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa Shirika la Nyumba la Taifa, (*NHC*). Hivi karibuni shirika limepata mtendaji wake mkuu Ndugu Nehemiah Mchechu. Ndugu Mchechu ameonekana kuja na nguvu mipyä, mipango mizuri ya kulinusuru shirika. Nampongeza sana. Naomba:-

- (a) Serikali impe ushirikiano katika kazi yake hii mipyä na nzuri.
- (b) Serikali isimwingilie tusimamie kwa utaratibu wa *eyes on hands off*.
- (c) Kodi za nyumba zipandishwe zipo chini sana.
- (d) Nyumba ziwe kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wengine wa Wizara hii kwa kutuletea hotuba nzuri licha ya ufinyu wa bajeti uliopo, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, Mipango Miji, ni vizuri utaratibu wa mipango miji yetu ukazingatiwa na kuheshimiwa sheria zilizopo ili kutuepusha na miji isiyokuwa na mpangilio.

Pili ni Sheria ya Majengo. Ili tuwe na majengo yenyé viwango vinavyostahili ni vizuri Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na ili kuharakisha kuleta sheria hii muhimu sana, kwani muda si mrefu twaweza kuwa na kilio kikubwa sana hapa nchini, tunamwomba Mwenyezi Mungu atuepushe.

Tatu, ni kuhusu viwango vipyä. Ni vizuri kabla ya kugawa viwanja vipyä miundombinu husika iwepo kwanza, mfano, barabara, umeme, maji na kadhalika.

Nne, Hati za viwanja au nyumba. Ninaipongeza Wizara kwa utaratibu mipyä unaharakisha upatikanaji wa hati na kuwatoa urasimu wa ramani.

Tano, *NHC*, ni vizuri tukaliwezeshwa Shirika letu la Taifa la Nyumba ili litekeleze majukumu yake ipasavyo, kiundaji na kiutendaji.

Sita, mikopo ya ujenzi. Serikali iharahakishe utaratibu utakaowezesha mikopo ya kujenga nyumba ya muda mrefu wa riba nafuu uwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakieni kila la kheri na naunga hoja mkono.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo rasilimali ya msingi kwa kila mtu. Rasilimali hii isipogawiwa vizuri na kutunza vizuri athari yake ni kubwa ikiwa ni pamoja na kuhatarisha umoja, mshikamano, utulivu na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Kero ya Ardhi kila Wilaya. Tume hiyo kwa kila Wilaya ilipokea malalamiko mengi na kuelekeza utatuzi wake. Lakini hadi sasa wale Maofisa Ardhi ambao walifanya makosa hawajachukuliwa hatua zinazofaa na kama hatua zimechukuliwa hakuna taarifa yoyote kwa wadau. Ni wazi kuwa Maafisa Ardhi wamebekwera kinga kubwa. Ni vema kurejea sheria inayotoa kinga kwa watumishi wanaosababisha migogoro mikubwa ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Babati ni kati ya maeneo yaliyokumbwa na matatizo makubwa ya ugawaji wa ardhi, upimaji na fidia na bila shaka matatizo haya yapo kila mahali. Hii inaonesha kasoro kubwa katika maeneo haya matatu; upimaji, ugawaji na ulipaji na fidia. Haiwezekani nchi nzima inalalamika, Rais anaunda Tume. Bado malalamiko ni mengi. Tuone umuhimu wa kupitia tena Sheria zetu za Ardhi na tuangalie hasa matatizo yako wapi? Nadhani tatizo lipo kwenye mfumo mzima na jinsi watendaji wanaofanya kazi na kusimamiwa na jinsi baadhi yao walivyojilimbikizia mali. Wananchi wanao, wanalamika na mwisho hukata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa ngazi mbalimbali hasa ya Wilaya hawana utashi wa kutatua matatizo ya wananchi kwa sababu wengine ni sehemu ya migogoro ya ardhi. Ni muhimu kugundua utaratibu uliopo ili viongozi wasipate nafasi ya kujinufaisha kwa kupewa maeneo na hivyo kusahau migogoro ya ardhi. Pale inapobainika viongozi wamenufaika kwa kuwa na nyumba na mali ni muhimu kuwa na sheria inayotaka mali hizo zitaifishwe. Wananchi wamechoshwa na vitendo vyta viongozi kutumiwa na Maafisa Ardhi hasa Wilayani kujinufaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi ya Shamba la Katani (*Babati Sisal Estate*). Shamba hili lilifutwa na Mheshimiwa Rais mwaka 1999, lina ekari 4,349 na linamilikiwa na Tanga *Gen. Industries Limited*, kwa hati Na. 9946 ya 1970.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hati kufutwa na shamba kuthaminishwa kuwa Shilingi milioni 48.897,224 ambazo wananchi wa Jimbo la sasa Babati Mjini wamelipa na fedha zote hadi leo zipo Wizara ya Ardhi kama fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmiliki alikwenda Mahakamani kwa kukataa fidia. Kesi inaendelea na hadi leo, wananchi wamesota kusubiri haki itolewe. Sasa wananchi wanadai fedha zao na wana nia ya kuishtaki Serikali kwa sababu "haki inayocoleleweshwa kwa miaka mingi (10) ni sawa na haki iliyonyimwa". Binafsi

nimeeleza sana jambo hili kwa Kata na mikutano yote ya hadhara lakini wananchi wameshindwa kuelewa sababu za kesi hii kuchelewa kwa kiasi hiki wakati na fedha zao milioni 48.8 zipo Wizarani. Hii ni hali tete na hasa tunapofikia mwisho wa awamu ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina ili wananchi wa Babati Mjini wapate kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia kila la heri wewe na watendaji wako. Naunga mkono hoja yako ili pamoja na hayo, tuendelee kuaminika.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Capt. Chilligati pamoja na Katibu Mkuu, wataalam wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe ushauri au ombi. Kwa kuwa kumekuwa na viwanja vingi hapa nchini ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu na kusababisha kuwa na mapori mijini na kutokuwa na maendeleo au uboreshwaji wa makazi. Je, Serikali kwa nini isifute hati hizo na kugawa upya kwa watakaoweza, kuviendeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kumekuwepo na malalamiko kwamba watumishi wa ardhi hutumia majina ya watu mbalimbali kuhodhi viwanja wakati kumbe ni vyao. Ningombaa Wizara ifuatilie kwa kina malalamiko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanja vya wazi (*Open Space*). Nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa hatua alizochukua katika kitengo cha ardhi, kwa wale waliobadilisha matumizi yake. Ningombaa na kushauri Serikali itoe kauli kwa wote walipewa usajili wa viwanja hivyo wajisalimishe kwenye ofisi husika, pia wale watakaobainika wachukuliwe hatua za kinidhamu ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia suala la upimaji wa viwanja. Niipongeza Wizara kwa kutenga fungu la mkopo kwa kupima viwanja kwa Idara ya Ardhi ili wapime viwanja vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa gharama ya upimaji ni kubwa na watu wengi kushindwa kulipa gharama hizo na kuchelewesha mzunguko huo, hivyo basi tungeomba Wizara angalau kupunguza kidogo gharama hasa kwa wale wa vijijini kwani uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu itolewe kwa wananchi juu ya umuhimu wa kupatiwa hati na umuhimu wa kupima, kwani watu wengi hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusambaza sheria ya ardhi, kama vipeperushi ili kila mwananchi ajue haki zake za kumiliki ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu Hati. Niipongeze sana Wizara kwa kurahisisha upatikanaji wa hati, katika Halmashauri zetu hapa nchini. Pamoja na kurahisisha upatikanaji wa hati hizo kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi kwa ajili ya kugonganisha viwanja na kuleta manung'unico au malalamiko ambayo kuingiza hasara kubwa kwa kulipa fidia mbalimbali zisizo za lazima (*double allocation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara kwa kukarabati Chuo cha Ardhi, Tabora na kusitisha uhamishwaji wa Chuo hicho kwenda Morogoro. Hivyo basi niombe Serikali iendelee kutenga fedha kwa kuboresha chuo hicho ili kiwe cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapewe vitendea kazi nya kisasa. Wapewe usafiri na gari la chuo, wakufunzi wakopeshwe pikipiki ili kurahisisha huduma zao hapo chuoni kutokana na umbali uliopo na kujenga nyumba za wakufunzi za kutosha katika eneo hilo la chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba niwapongeze wale wote wanaomsaidia Waziri ili afanikishe shughuli muhimu za maendeleo ya makazi, nikimsisitiza Waziri mwenyewe aendeleze kazi hiyo kwa moyo mmoja ili wananchi wasiendelee kulalamika kwamba wanaporwa ardhi yao waliorithi au waliyoipata kwa jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni kitu muhimu sana kwa maisha ya mwanadamu, tukizingatia sio kwa makazi tu lakini ndio inayotupa chakula na tukaweza kuishi, naiomba Serikali yetu iache maneno matupu kila siku tuitumie ardhi ili tuweze kuendelea kiuchumi na kutoka kwenye umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kubadilisha uongozi wa Shirika la Nyumba, kwani kwa kweli tuliongea sana kuhusu Shirika liliwyopoteza mwelekeo wake, ilikuwa ni shirika linalosubiri kodi lakini matengenezo ili wapangaji wakae maeneo mazuri ilikuwa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa Shirika ambao wameanza hivi sasa tafadhali sana ondoeni dosari ambazo zinawaaandama. Sasa naomba nitoe mchango wangu wa ushauri kama ifuatavyo:-

(1) Usajili wa wapangaji ambao ulifanyika miaka miwili iliyopita urudiwe upya, kwani wapangaji ambao sio halali wamo ndani ya hizo nyumba.

(2) Nyumba ambazo bado mnazihitaji mzifanyie matengenezo hasa mabomba yanayotoa maji machafu na *sewages* zote zimeziba, mabomba yanavuja na kumwaga maji.

(3) Wafanyakazi waliomo kwenye ofisi za Wilaya au Kikanda muwabdalishie kwani wamekaa muda mrefu wanaboronga.

(4) Jitahidini kujenga nyumba nyingi ndogo ili watu wa kipato cha chini waweze kukodi au kununua, kuishi kwenye nyumba nzuri ni maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi inaendelea kwenye kujenga nyumba nzuri ili Watanzania waishi kwa raha, basi kama hivyo ndivyo tunapoingia kwenye maeneo ya watu kwa ajili ya maendeleo yao tuwaweke kwanza tuwaeleweshe kwa ukaribu, uelewano uwepo sheria za ardhi zitumike, mimea ifidiwe kisheria na mali iliyopo ndani ya eneo husika tusifanye dhuluma kwa kuwaonea wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumwondoaa mtu kwenye eneo lake alikozaliwa na kuishi kwa muda wote wa maisha yake ukamkabidhi fedha kidogo ukamwambia aondoke kuna mwekezaji au Serikali ina dhamira ya maendeleo fulani, fedha ni fedha hujamwonesha mahali pa kujenga, hana usimamizi wa mtu wa kumwongoza, fedha anaila, je, Serikali inategemea huyu mwananchi ataishije?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali au Wizara iangalie eneo la mbadala kwanza, walio wazee waangaliwe kipekee ili baada ya pale wasihangaike, tuwe na huruma na wananchi wetu hususan wale wazee ambao hawana mtu wa kuwaongoza, sio kuwafidia fedha kidogo na kuwapeleka kwenye maeneo ambayo yana mzozo na kuwaacha hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwaomba tena wote ambaao wanataka maendeleo ya kutumia ardhi, tuitumie ardhi kwa manufaa ya nchi yetu, sio manufaa. Binafsi ni hatari kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, kwa kuwa gharama za kufungua kesi katika Mabaraza ya Ardhi hasa Kata na Wilaya ni kati ya Shilingi 10,000/= na 20,000/= kutegemeana na maamuzi ya Baraza husika na kwa kuwa pale Baraza linapolazimika kwenda *site* gharama hulipwa na mlalamikaji na mlamikiwa nusu kwa nusu.

(a) Je, Serikali haioni kuwa hali hii huwanyima wananchi maskini ambao mara nyingi ndio wanaonyang'anywa ardhi yao hasa wajane au walioachana au kutengana ambaao kimsingi hawana chochote?

(b) Kwa kuwa gharama hizo ni kubwa kuliko hata gharama za Mahakama ya kawaida ambapo gharama ya kufungua *file* ni Shilingi 1,500 – 2,500 tu, je, Serikali haioni

kuwa yenewe kwa kutokutoa mwongozo mahususi na kutenga fedha za kuendeshea Mabaraza haya ndio inayosababisha wanyonge kunyanyaswa na matajiri?

(c) Ni lini Serikali itatoa maelekezo bayana kuhusu Makatibu wa Mabaraza ya Kata kulipwa mshahara, fedha zinazolewaka ili wafanye kazi zao kwa moyo na ufanisi? Je, kutokuwa na *scheme* inayolewaka si ndio msingi wa rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, je, kipindi cha Wenyeviti wa Mabaraza ya Wilaya ni muda gani? Pia je, iwapo kuna vipindi maalum, kuna utaratibu gani wa kufanya tathmini ya mwenendo na tabia zao kabla ya kuongezewa muda? Pamoja na hayo je:-

Kwanza, kwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Karatu analalamikiwa sana kwa unyanyasaji hasa wa akinamama maskini na kuendesha Baraza kibabe je, ili Wizara isiondoke na kauli ya Mbunge tu iko tayari kuchunguza mwenendo mzima wa Mwenyekiti huyo kabla ya muda wake kuongezwa?

Pili, kwa kuwa wananchi hawaelewi panapotokea malalamiko dhidi ya Wenyeviti wa Mabaraza haya Serikali inatoa tamko gani ili wananchi wasiendelee kupoteza haki zao kwa kukosa mtiririko unaoelewaka kama ilivyo kwa Mahakama ambapo ngazi za rufaa zinajulikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa kusimamia masuala ya ardhi kwa uadilifu mkubwa. Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wamenipa ushirikiano mkubwa na wananchi wa Muleba Kusini. Naomba ushirikiano huu uendelee ili kulinda haki za wanyonge katika kufaidika na ardhi ambayo haitoshi na hivyo kuhitaji usimamizi ulio makini. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao ushauri ufuatao kwa Serikali:-

Kwa kuwa sera na Sheria ya Ardhi Namba 4 na 5 za mwaka 1999 zimeleweka bayana hitaji la kugawa ardhi kwa kuzingatia mahitaji na usawa ili kuepusha walafi wachache kuhodhi ardhi ya nchi yetu, nashauri ukaguzi mahsus (*special audit*) ufanyike nchi nzima kusaini watu waliopewa ardhi kubwa sana na wameihodhi bila kuviendelea ili igawiwe kwa wananchi wasio na ardhi na nyingine ibaki kwenye milki ya Serikali kwa matumizi ya baadaye. Kugawa ardhi kiholela au kwa sababu za rushwa kutasababisha machafuko siku za usoni na hivyo kuhatarisha usalama wa Taifa letu. Watoto wetu na wajukuu wao wanayo haki ya ardhi kama sisi. Sio busara kutegemea Serikali kutoa fidia kubwa katika kutwaa tenda ardhi kwa ajili ya wananchi wetu wakati ardhi hiyo ilitolewa sawa na bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtoa hoja aeleze tahadhari inayochukuliwa na Wizara kukabiliana na tatizo hilo, ambalo tayari maeneo mengi ya nchi yetu yamekumbwa na migogoro ya ardhi kutokana na ulafi wa watu wanaojiita “wawekezaji”. Nasubiri maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa hotuba nzuri na ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi haiongezeki lakini watu wanaongezeka hivyo Watanzania tutumie vizuri ardhi yake. Kwa mfano, badala ya kutumia mabonde ya Luiche, Rukwa, Usangu, Pawaga, Kilombero, Rufiji, Wami, Ruvu, Pangani, Ruvuma tutumie kwa kuendeleza kilimo. Haya ni maghala yetu ya chakula. Tanzania ikitumia vizuri mabonde haya itakuwa tajiri kwa kuuza chakula nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu kugawa miji kunaongeza umaskini kwa sababu majengo yanameza ardhi ya kilimo na kuwafukuza wakulima toka maeneo yao. Naomba kutoa ushauri, utaratibu ufanywe ili Serikali (*NHC*) ijenge nyumba za maghorofa badala ya nyumba fupi (*bungalow*) ambazo zinameza maeneo makubwa (sheria).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali au Wizara ifikirie kurekebisha Sheria ya Vijiji ya 1975 ili badala ya kuongeza vijiji kuwe na mpango wa kuanganisha baadhi ya vijiji ambavyo vimeungana na kusababisha vijiji-miji na vijiji minyororo mfano: Vijiji-toka mji wa Njombe hadi mpakani na Makete vimeungana vijiji vitatu. Tazama mfano Ukurasa wa 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kufikiria kurudisha Kamishina wa Maendeleo Vijijini ili kuratibu maendeleo vijijini. Leo kuna vijiji-miji vingi vinavyohitaji kupangwa vizuri lakini vinakua bila ushauri wa kitaalam. Tusipoziba ufa tutajenga ukuta. Kwa mfano, leo Wilaya ya Njombe ina vijiji-miji zaidi ya 42 vyenye ukubwa kama mji mdogo wa Kibaigwa lakini vinaendeshwa kama vijiji vya kawaida. Mifano, Mtwango, Ilembula, Uwemba, Makoga, Kipengere, Mdandu, Matembwe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iharakishe kuwamilikisha wanyonge ardhi yao ili wasipokonywe na watu wachache wenye uwezo. Ardhi ndiyo rasilimali pekee iliyobaki kwa maskini wa Tanzania. Wakipoteza ardhi ndiyo nwisho wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasi kubwa ya kukua kwa miji na vijiji nashauri kila kijiji kiwe na mwanakijiji ambaye atapewe elimu ya kawaida ya kusimamia ardhi na ujenzi wa nyumba kwa mpangilio ili kupunguza matatizo ya kubatiza vijiji vikubwa kuwa miji- midogo wakati havina sifa ya miji-midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwe na mkakati wa kupunguza uhaba wa viwanja vya ujenzi wa majengo katika Miji na Miji Midogo, Manispaa, Majiji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa vijiji minyororo ni Njombe, Ramadhani, Wikichi, Mgodechi, Ulembwe, Igagala, Uselule, Ng'anda, Makoga, Mdusi, Igosi, Mafinga, Kipengere, Moronga (14 villages) Makete District au Makambako, Lyamkena, Kiumba, Ikelu, Ilunda, Mtwango, Ilunduma, Lusisi, Mhadzi, Igima, Mlevela, Nyumbanitu, Itulike na Ramadhani, Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kaka yangu Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba ya Bajeti hii nzuri yenye mikakati mahsusini ya sekta zote zilizomo ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niendelee kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Kepteni John Chiligati kwa kazi nzuri aliyofanya kwenye jimbo lake, kazi ambayo ilinitia moyo siku zote nami kuunga mkono. Hivyo ninamuombea Mwenyezi Mungu wapiga kura wake wamuunge mkono kwa kumpa kura za kishindo, arudi tena Bungeni kusimamia Bajeti yake aliyoianaa vyema. Nasema nikiwa na imani kuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naye atapigwa kura za kishindo na ninaamini uwezo wa Mheshimiwa Kepteni John Chiligati na Waziri anautambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa hatimiliki ya ardhi ya kudumu, napenda kuikumbusha Serikali kuwa utaratibu uliopo sasa wa kupata hatimiliki kwenye Ofisi za Kanda au Wizarani ni tatizo kwa wananchi wengi mfano wananchi wa Mkoa wa Singida kufuata Ofisi ya Kanda Dodoma au Dar es Salaam. Ugumu huu unatokana na gharama kuwa kubwa sana kwa sababu ya nauli, malazi na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, naiomba Serikali kupeleka huduma hii karibu na wananchi yaani Wilayani au Mkoani ili kuwapunguzia mzigo wananchi. Hii itasaidia wananchi wengi kupata hatimiliki za nyumba, mashamba na ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maafisa ardhi kukaa kituo kimoja kwa muda mrefu, naomba Serikali kuangalia maafisa ardhi katika halmashauri zote nchini wale ambao wamekaa muda mrefu kuhamishwa kwani wengi wao wanakuwa na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea hata pengine kupokea rushwa ndipo mwananchi apewe huduma. Usumbufu huu bado upo wa kupata viwanja hata wilaya za mkoa wetu wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kila mkoa kuunda kamati ndogo ambayo itapita kila halmashauri kuongea na wananchi ili kuondoa kero zinazoendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maafisa ardhi waliokaa muda mrefu na kuonekana kuwa kero sasa kuhamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya nyumba za *NHC*, bado kuna tabia ya wakazi wa nyumba *NHC* kumilikishana nyumba hizo kinyemela bila Serikali kujua. Kwa kuwa wapangaji wote wanajulikana vyema basi kuwepo ukaguzi wa mara kwa mara ili kukomesha tabia hii mbaya ambayo wapo wapangaji wachache bado hawana maadili ya upangaji hasa Dar es Salaam na mikoani pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria ya ardhi, nashukuru sana Serikali kwa kutunga sheria ya kumiliki ardhi yenye kuwajali wananchi wote hususani wanawake. Itakuwa ni vizuri sana endapo elimu ya sheria hii itafikishwa vijijini kwa wananchi ambao ndio walengwa. Hivyo naomba Serikali kutafisiri sheria hii kwa lugha ya kiswahili ili watu wote waweze kusoma na kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upimaji wa ardhi vijijini, kwa kuwa hati ya kumiliki nyumba au ardhi imekuwa ikitumika kumdhaminii mwananchi aliyewekwa mahabusu, sasa ni vyema kasi ya kupima viwanja iwe kubwa ili kila raia awe na hatimiliki ya nyumba yake au ardhi yake ili wasipate usumbufu wa kumdhaminii mtu aliyewekwa mahabusu au mkopo benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusikia hatua iliyofikiwa na Serikali katika kupima ardhi. Kuhusu mabaraza ya ardhi, naipongeza sana Serikali kuanzisha mabaraza ya ardhi kwa ngazi ya mkoa na sasa ngazi ya wilaya. Pia naishukuru Serikali kupandisha posho za wazee wa mabaraza haya kutoka shilingi ya Kitanzania 30,000 badala ya shilingi 20,000 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwanza, naiomba Serikali kuongeza kazi ya kujenga ofisi za mabaraza ya wilaya na mikoa, pili, kuhakikisha wazee wa mabaraza haya wanayo maadili mema pia wenye kutosheka ili kuepuka rushwa katika mabaraza haya na kukabiliiana na tabia ya kupendelea baadhi ya watu bali haki itendeke na tatu, kutafuta njia ya kuondoa msongamano wa kesi hizi za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachoraji wa ramani za nyumba, kwa kuwa hati ya kumiliki nyumba inatakiwa kuambatanishwa na ramani ya nyumba na kwa kuwa gharama ya kuchorewa ramani ya nyumba ni kubwa hasa kwa watu binafsi, naiomba Serikali kusaidia wananchi kuchora ramani za nyumba zao bure ama kwa gharama nafuu hii itasaidia sana kila mkazi kuwa na ramani ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kujenga nyumba na kuwakopesha wafanyakazi. Naishukuru sana Serikali kwa kuendelea kujenga majengo ya *NHC* kwa lengo la kusaidia wafanyakazi kupata nyumba za kupanga. Naiomba Serikali iendelee kujenga nyumba hizi kwa lengo la kuwakopesha wafanyakazi au wananchi kwa ujumla

ili kuwasaidia wafanyakazi wengi kupata nyumba za kudumu kwa kudhaminiwa na mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Waziri na Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kuwasilisha hotuba hii vizuri na ninaunga mkono Bajeti hii kwa moyo mkunjufu na Mungu awatie nguvu, afya, mshikamano na utumishi uliotukuka katika kutekeleza majukumu yao kupitia Bajeti.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kuhusu Wizara hii. Mimi kwanza nina malalamiko kuhusu ofisi za mikoani au wilayani, ni matatizo makubwa. Kuna ubadhilifu wa viwanja au ardhi zao wanagawa viwanja ambavyo viro kwenye mito, kwenye vyanzo vya maji na vina matatizo mfano Bukoba kuna mvua za mara kwa mara kw ahiyo kunakuwa na matatizo mafuriko na mito ya kupeleka maji ziwani imebanwa, maji yanakosa pahala pa kuteremkia. Je, hao wanaogawa viwanja hivyo au ardhi kwa nini wasichukuliwe hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, kulaghai watu huo sio ufisadi? Je, Wizara inawachukulia hatua gani na malalamiko yangu ni kila siku pamoja na mimi ni muathirika wa mafuriko nimepakana na mto mkubwa unaotiririka mpaka ziwani lakini wameruhusu watu wakajenga humo kwa kupanda miti ukabana. Kwa hiyo, makosa ni ofisi ya ardhi ndio wamewagawia viwanja hivyo na kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji viwanja, watu wengi wanalamika, wangkuwa wamepimiwa na ugaiwaji wa viwanja bila mpangilio usingekuwepo, upimaji unasemwa tu, bila vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za *NHC* zilizoko Bukoba Mjini ziliwa sehemu mbili, Kashai na Miembeni, za Kashai zimenunuliwa kwa wale wakazi waliokuwemo je, hizi za kata Miembeni tatizo eti ziko manispaa, hizo ni kama kitega uchumi cha wachache, sasa Waziri naomba tamko kuziuza au kuzikarabati kama hazikarabati wanaoishi humo wazinunue kwani zimechakaa, hazina sehemu ya kumwaga maji machafu, naomba majibu kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa *plan* ya kujenga Kigamboni kuwa mji wa kisasa kama sina maneno bila vitendo kama tunavyoona kwenye vitabu, ramani bila vitendo inakuwa porojo, wasiwasi wangu mimi ni mmoja amba tumeathirika na fidia pamoja na manyanyaso yatakayowapata wananchi kama yanavyowapata wananchi wa Kipawa na Mbagala ambako tunaanzisha miradi kabla hatujajiandaa pa kuwapeleka wananchi wetu mapema wakawa na makazi ndio tunavunja kuliko kuwaweka kwenye maeneo ni aibu kubwa. Mtanzania wa sasa anafamilia, naomba majibu kwa faida ya wananchi wote Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu kuhusu majengo pamoja na upangishaji nyumba za *NHC* kupangishwa na wazungu na wahindi kama tunavyoona Tanzania nzima *NHC* wanapanga wahindi tu ndio wanaopata nyumba hizo Bukoba Mjini, Dar es Salaam, Mwanza huwezi wewe Mwafrika kupewa nyumba hizo, wahindi heri

waweke mifugo kuliko kupakana na Mwafirika. Siambiwi, nimeshaona mwenyewe. Nini tamko lako Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rushwa, Wizara hii imeja ukitaka ardhi, nyumba kupanga usipotoa rushwa hupati nyumba na ndio maana unakuta migogoro inakuwa mingi sana na mingine inasababishwa na ofisi, mtu mmoja anapewa kiwanja akianza kujenga wanaibuka kama watano, je, Wizarani mnalijua? Nafikiri linajulikana mnawalinda. Kama Wizara wasipokuwa wakali migogoro haitaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafika mahali wanagawa viwanja nya wazi kama kiwanja cha wazi hasa sehemu *NHC* vinagawiwa, ni kwa nini nyumba hizo zisiuzwe zikapunguza migogoro, nyumba zimebanana na zinaonekana ni uchafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, kuna ujenzi holela katika miji yetu. Hii ni kutokana na miji hiyo kuhama kwa wananchi wengi katika miji hiyo na kazi ndogo sana ya upimaji wa viwanja. Katika hali hiyo ujenzi usiokuwa na mpango utaendelea sana katika miji yetu. Je, Serikali ina mpango gani kabambe wa kupima viwanja ili kuepukana na ujenzi usio wa ramani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali asilia lakini huongezeka zaidi thamani ardhi hiyo pale ambapo imepimwa ardhi hiyo. Ukubwa wote wa ardhi tuliyonayo hapa Tanzania hautakuwa na thamani kama ardhi hiyo itakuwa hajapimwa. Kupimwa kwa ardhi kutaondoa ardhi hizo kupewa wageni kwa uwekezaji bila ya kushirikishwa wananchi wenyewe kwa hivyo upimaji wa ardhi na kumilikishwa vijiji ni muhimu mno, maendeleo hayo yanayowahusu Watanzania hayatawezekana bila ardhi kupimwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi kwa upimaji wa ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sasa mpaka baina ya nchi yetu na Malawi una mgogoro. Kila mwaka ahadi inayotolewa kuwa suala hilo linashughulikiwa lakini ufumbuzi wake haupatikanai. Ileweke kuwa kulipiga dana dana suala la mpaka hapo baadaye itakuja sababisha mgogoro mkubwa. Watanzania hawatakubali kuambiwa kuwa Ziwa Nyasa hawana haki nalo na inaweza ikatokezea utawala huko Malawi ukasema sisi hatuna haki ya kulitumia Ziwa la Nyasa. Ni vyema Serikali kwa haraka sana wakalitafutia ufunguzi suala hilo. Ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni muhimu sana kwa maisha ya Mtanzania na ndiyo inayomfanya mwananchi kujiona ni Mtanzania. Kwa miaka mingi ardhi yetu imekuwa haina thamani kubwa lakini katika siku za karibuni ardhi imekuwa na thamani kubwa kwani imekuwa kama dhamana ya kuombea mikopo na hata kuweka rehani. Kwa muda sasa kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi na hata kufikia watu kuuana. Pamoja na ardhi ya nchi yetu kuwa kubwa sana zaidi ya ile ya Kenya, Uganda na Rwanda kwa pamoja bado hakuna mipango kabambe na mizuri ya kugawa ardhi hii. Hali inayopelekea baadhi ya watu kuhodhi maeneo makubwa bila hata kuyaendeleza huku wengi wakikosa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi kumekuwa na urasimu mkubwa katika kufuutilia kupata hati za ardhi (*title deed*). Wakati zoezi hili kwa nchi nyingine huchukua miezi mitatu, kwa Tanzania imekuwa ndoto. Baadhi ya watendaji kwa makusudi wamekuwa wakikwamisha utoaji wa hati hizo ili wananchi watoe rushwa. Tunaomba Wizara iboreshe huduma hii ili wananchi wengi wapate hati hizo na waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi ndiyo rasilimali muhimu kwa maendeleo ya wananchi ni wazi kuwa ardhi hii isipogawanywa vizuri kutakuwa na athari kubwa zaidi ya hizi tunazoziona.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya wazi vimekuwa vikitumiwa na vigogo bila kujali kwamba viwanja hivyo ni kwa matumizi maalum kama michezo na huduma za jamii. Kuna ushahidi wa wazi kuwa baadhi vigogo na wafanyakishara wakubwa kwa kushirikiana na wafanyakazi wa ardhi wanagawa viwanja hivyo. Pale Magomeni Makuti Chama cha Mapinduzi wamejenga ofisi yao ikavunjwa na wananchi na sasa wameweka *countainer* kama ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa eneo hilo wamelalamika na kuandika barua nyingi lakini bado halijaondolewa. Mimi binafsi nimefutilia bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wawekezaji, kumekuwa na migogoro mingi pale wawekezaji wanapopewa eneo. Fidia inakuwa ndogo sana na mara nyingi fedha (fidia) hiyo haitolewi kwa wakati. Hali hii imepelekea wananchi kulalamika na hata kuleta mahusiano mabaya sana kati ya wawekezaji na wananchi. Hali hii imejitokeza kule Kilombero.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na wataalam wake wote kwa juhudini zao za kuboresha Wizara hii na kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kurasini walikubali kuhamishwa kwenye eneo lao ili kupisha upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam. Tathimini imefanyika mwaka 2008/2009 baadhi ya wananchi wamelipwa tayari na sasa wanabomo nyumba zao na kuondoka. Wale ambao hawajalipwa hadi sasa hawaelewi kinachoendelea, wako katika wakati mgumu kwa kushindwa kuendesha shughuli za maisha yao. Wapangaji waliokuwa wamepanga nyumba zao baada ya kuwekewa X wamehama tayari/wameondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliokwishalipwa wanabomo nyumba zao na kuziba mifereji ya maji hivyo kuleta mafuriko ya kutisha kwenye nyumba ambazo wananchi hawajalipwa. Nyumba zao zimepata nyufa kutokana na mafuriko ya mwaka huu wakati wa mvua za masika na wameshindwa hata kufanya marekebisho/matengenezo yoyote kwa sababu wanatakiwa waondoke, wanashubiri kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilieleze Bunge kuwa wananchi hawa watalipwa lini fidia yao ili waondoke na wakaendeleze maisha yao na familia zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii waainishe na kupima maeneo ya hifadhi za wanyamapori na misitu ya Serikali ili kuondoa tatizo la maeneo hayo tengefu kuvamiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Mipaka ya kueleweka iwekwe maeneo yote ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa ardhi kwenye halmashauri ni wachache sana hawakidhi mahitaji. Pia vifaa vya kupimia ardhi hii vichache/hakuna kabisa. Hali hii ya upungufu wa wataalam na vifaa inafanya halmashauri zetu kushindwa kufanya matumizi bora ya ardhi na hivyo kuleta migogoro ya ardhi kwa watumiaji mbalimbali pia kuwapa ujenzi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba zilizorudishwa Serikalini kwa kufuatiwa mikataba ya *sub-leasing* ziwanufaishe Watanzania wa kawaida siyo kuchukuliwa tena na wafanyabiashara wakubwa na washindi kama ilivyozoleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na mikataba ya nyumba za *NHC* kwa wapangaji kwa muda fulani, pengine miaka kumi warudishe nyumba Serikalini ili wengine wapangishwe hizi nyumba za *NHC* ni kwa ajili ya Watanzania wote siyo watu wa kundi fulani kuwepo na mikataba kutatoa fursa kwa mpangaji kujandaa kujenga nyumba yake ili aruhusu wanaoanza maisha kupata pa kuhamia. Pia itatoa kasumba ya wapangaji wa *NHC* kuona kwamba nyumba ni za kwao na hivyo kupeana wao kwa wao na watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba wahindi ndio wanakalia zaidi ya robo tatu ya nyumba za *NHC*, wanafanya biashara, wanakwenda kujenga kwao huku wakijiona kwamba wao ndio pekee wanatakiwa kukaa *NHC* maeneo mbalimbali huku Watanzania wazawa wakihangaika kupata makazi.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na jopo zima la wataalam wa Wizara hii kwa ubunifu katika kuboresha maendeleo ya makazi kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili kupitia semina tuliyofanyiwa Waheshimiwa Wabunge tumeridhika sana na mpango mzima wa mji mpya wa Kigamboni, naomba sana kupitia hotuba hii naomba kumpongeza *Director General* mpya kwa ushawishi wake katika kulisukuma hili wazo la ndoto hii ili baadae ndoto hii iweze kukamilika. Naomba binafsi kumuomba *Director General* huyu apewe kipaumbele cha kutunzwa na hata apewe ulinzi wa kutosha wa nyumbani, kwa uzito wa hili suala hasa kupitia mchakato huu wa ushindani ndani ya jumuia katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii isiwe inafanya mambo yake nusu nusu kama vile wanafanya mipango yao kwa kubahatisha kwani picha iliyopo Chalinze kwa ghorofa zile mbili ni kama tayari zimeshatekelezwa na hazizungumzwi tena vipi zitaendelezwa, hii haipendezi hata kidogo, hivyo tuelezwne nini kinachoendelea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, MKURABITA ni mpango mzuri sana katika masuala ya kuondoa umaskini nchini lakini Wizara hii ndiyo iliyopaswa kuwa ni kiini cha kuwapimia watu ardhi zao ili wapatiwe hati na hatimaye kuzipeleka benki na kupata mikopo yao kwa maendeleo ya maisha yao na vizazi vyao. Kasi iongezwe kutokana na *value* ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika semina tulizofanyiwa hivi karibuni tulielezwa kwamba mji mpya wa Kigamboni utahusishwa ujenzi wa ofisi za mabalozi binafsi, nashauri hili lipo ndani ya sera ya chama chetu cha CCM kuhamia Dodoma hivyo naomba hili liachwe kwani tutajikana sisi wenywewe.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, kwani hoja hii ni ya msingi sana kwa maisha ya watu walio wengi. Kwanza natoa pongozi kwa Waziri Mheshimiwa Chiligati, kwa umakini wake pamoja na kusikiliza shida za watu kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa upimaji shirikishi ni mzuri sana na pia unawapa nafasi wale ambao walijenga kabla ya eneo kupimwa, lakini tuzo la kulipia upimaji huo ni kubwa hasa kwa wananchi wa kawaida, ambao hali zao kimaisha si nzuri sana. Maelekezo ya kupoza gharama hizo, watu wanapenda kupimiwa lakini gharama iko juu. Pia ni vizuri halmashauri ziweze kupima maeneo ambayo bado hayajajengwa. Ili kupanga miji vizuri na upimaji huo uzingatие uachaji wa barabara pana ambazo zitakidhi haja, ramani iwe ya miaka hamsini au mia mbele na sio miaka mitano au kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameongelea fidia, ni nani ambae anatakiwa kuhakiki kama wananchi waliopisha ujenzi wa barabara au viwanda, anatakiwa kuhakiki malipo ya ardhi au nyumba ambazo zinabomolewa, kwani baadhi ya watu hawalipwi na baadhi ya watu wanapunjwa sana. Ingekuwa vizuri Wizara hii ikashiriki vizuri kuliko kuiachia Wizara ya Miundombinu kwa barabara, wananchi wamekuwa wakihangaika sana. Mbaya zaidi wathamini wa majengo wanapokwenda kuthamini, huwatalisha watu saini na bila kuandika na kuwaonesha walengwa watalipwa shilingi ngapi. Ni vizuri mkakubaliana malipo, ndio ukamtilisha saini, mbaya zaidi karatasi ambazo zimeandikwa lugha ya kiingereza ndio zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Watanzania wengi hawajui kusoma na kuandika kiswahili, sembuse kiingereza. Hii ni hila ya kutaka kuwatoa njiani wananchi wao. Kuna wananchi kadhaa ambao walibomolewa nyumba zao miaka zaidi ya mitano, eneo la Pasiansi Mjini Mwanza kupisha barabara na mpaka leo hawajalipwa pesa zao. Kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ndio ingesimamia tatizo hili na kujua watu hawa wanahitaji makazi. Pia wakazi wa Mwandiga mkoani Kigoma ambao niliwaleta mbele yako pia wangenufaika, kwani huko malipo hayo yanakopitia urasimu ni mwingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea nyumba na maendeleo ya makazi, ni vizuri nyumba hizo zikawa bora na za kuridhisha, lakini vifaa vya ujenzi viko juu sana, kama bati, mbao, saruji na kadhalika, huu ndio ujenzi tuliouzowea sisi Watanzania. Lakini ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, ni wangapi wanaozijua? Na ni Watanzania wangapi wanawenza kuja kuangalia mabanda ya Nanenane na Sabasaba? Ni Watanzania wangapi wanao upeo wa kuja kuangalia hilo? Pamoja na ujenzi wa kisasa wa nyumba, pia ni vizuri vifaa vya ujenzi vikapungua bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vizuri wakati Wizara inapima viwanja, iwe sambamba na uchanaji wa barabara, kwani kila halmashauri ina greda za kuchana barabara na vizuri kuuza viwanja ambavyo tayari kuna barabara ili miundombinu mingine iweze kufika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kheri Waziri kwa kazi zake za kuiongoza Wizara hii ngumu ya ardhi. Ahsante.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi sana kwa kazi nzuri inayofanywa na Mawaziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika mmetuletea hotuba nzuri na semina yenu juu ya *NHC*, na ya mji mpya wa Kigamboni, imetuzidishia ari zaidi na imani kubwa katika mioyo yetu kuwa sasa Wizara hii inapiga hatua thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zangu kuna ucheleweshaji mkubwa kupata hati ya kumiliki ardhi. Ombi *computerize the department* ili kuondoa matatizo ya kibinadamu, heshima ya Wizara mbele ya macho ya wananchi itapanda juu zaidi pindi Wizara ikiiondoa uchekeleweshaji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubabaishaji mkubwa katika matumizi ya *open space*, maafisa ardhi wanagawa *open space* katika miji yetu kwa ajili ya kujipatia manufaa binafsi. Ombi langu ni kuwa maafisa wa ardhi wapate *study tours* ya kutembelea Ulaya, *USA* au hata Nairobi tu wakaone *city squares* zilivyopangwa na kuheshimiwa. Naomba sana hawa maafisa wapate elimu ya *decent city land planning*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji wa vijiji, sisi Rufiji vijiji vyetu karibu vyote havijapimwa kabisa na pale walipopima kumezalishwa malalamiko, migogoro mikubwa na ugomvi kati ya kijiji na kijiji kwa kugomea mipaka. Upimaji huo Rufiji haukufanywa kwa ufanisi hata kidogo. Kwa mfano kuna ugomvi wa mipaka kati ya Kijiji cha Nyamwage na Kijiji cha Ikwiriri, Kijiji cha Mgomba na Kijiji cha Mbunju na Kijiji cha Mbunju – Mvuleni na Kijiji cha Ruwe. Ombi langu kwa Wizara iharakishe upimaji wa vijiji kule Rufiji ili kupunguza migogoro ya mipaka ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukodishwaji wa ardhi ya kilimo cha kibiashara na *TIC*, kuna utapeli mkubwa juu ya matumizi ya ardhi wanayopewa wawekezaji. Ombi langu ni kuwa Warufiji wawe washiriki katika ardhi yao, wasifanywe manamba,

washirikishwe kama wabia. Pili, kuwe na muda maalumu kwamba kama mwekezaji hajaendeleza ardhi aliyokodishwa kwa zaidi ya miaka mitatu, basi mwekezaji huyo anyang'anywe mara moja ili irudishwe kwa wanakijiji. Kuna mfano pale kijiji cha Nyamwage, Wilaya Rufiji kuna Waturuki walikodishwa ardhi kubwa, lakini mpaka sasa hawajaitumia ardhi hiyo. Mheshimiwa Waziri tunaomba wawekezaji wa sampuli hii wanyang'anywe ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHC* nyumba zake zimekaliwa na raia wa asili moja. Sasa Director *General* mpya alete haki kwa Tanzania wazalendo nao wapate fursa ya kukalia nyumba za *NHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali na hapana budi ni lazima ardhi ionekane katika mtazamo huo kwamba ni rasilimali ambayo kila uchao ardhi inaongezeka thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi hii, ardhi ni mali ya Taifa na msimamizi mkuu wa rasilimali hii ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni dhahiri kwamba raia yejote anayehitaji kutumia ardhi ni lazima apate kibali maalum kutoka katika taasisi yenye mamlaka ya kisheria kufanya hivyo. Kwa bahati mbaya katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni kumejitokeza migongano na mitafaruku mikubwa baina ya jamii mbalimbali wakiwemo wakulima na wafugaji, baina ya kijiji na kijiji au baina ya taasisi ya umma na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii inaashiria kwamba hali haiko shwari katika mgawanyo na matumizi ya ardhi tuliyanayo. Ni jambo lisilopingika kwamba pamoja na juhudu kubwa ya Wizara hii kupima ardhi ya Taifa kwa matumizi mbalimbali bado kasi ya upimaji na ugawaji wa ardhi haiendani na mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ni lazima Serikali iongeze kasi ya upimaji na ugawaji wa ardhi katika mikoa yote ya Tanzania ili ugawaji wa ardhi uendane na mahitaji halisi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo linawasumbua wananchi na hasa wale wanaohitaji maeneo kwa ajili ya ujenzi wa makazi. Miradi mbalimbali imebuniwa ya kupima viwanja kwa ajili ya ujenzi wa makazi. Lakini la kusikitisha ni kwamba takriban maeneo yote yanayopimwa viwanja hivyo hayakujengwa miundombinu muhimu kwa ajili ya matumizi ya jamii. Miundombinu hiyo ni pamoja na maji, umeme, simu, barabara ambayo kukosekana kwake kunaathiri sana na kuwafanya wamiliki wa maeneo hayo kushindwa kuyaendeleza maeneo hayo kwa wakati na vile vile kuwaongeza gharama za ziada zisizo za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuchukua juhudu za makusudi kuhakikisha kwamba yale maeneo yanayopimwa kwa kugawiwa wananchi kuyaendeleza basi ile miundombinu yote ambayo ni muhimu ni lazima yaimarishe kabla maeneo hayo hayajagawiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anaifahamu historia ya Shirika la Nyumba (*NHC*) na namna ambavyo imekuwa inapoteza mapato kutokana na ubadhirifu unaofanywa na mionganoni mwa watendaji wa shirika ambao si waaminifu, kadhalika na dhuluma inayofanywa na baadhi ya wapangaji ambao wamepanga nyumba za *NHC* kwa bei nafuu lakini na wao huzipangisha nyumba hizo kwa watu wengine kwa bei kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo *Tanzania Building Authority (TBA)* ambayo nayo inajenga na kumiliki majengo kwa niaba ya Serikali inahitaji kujigeuza kimtazamo ili nalo lijiendeshe kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa leo tunaishauri *NHC* kusimamia ipasavyo kodi za nyumba ilizopangisha, kujenga upya na kuwauzia wananchi ni lazima na *TBA* nayo ijikite zaidi katika kujenga na kuuza majengo na sio kubaki nayo jambo ambalo linaongeza gharama za uendeshaji kwa shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishauri *TBA* kwamba zile nyumba za Serikali zilizopo eneo la Kisasa Dodoma ziuzwe hususan kwa wananchi ambao wamepangishwa humo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuliokuwa tumewapa nafasi ya kuchangia wote wamemalizika. Sasa mtoa hoja huyu kwa sababu hoja nyingi ni za msingi kabisa na kwa sababu hana Naibu Waziri, nimeamua kumpa dakika arobaini zote achukue mwenyewe na za Naibu wake kumi na za kwake mwenyewe kusudi aweze kujibu hoja vizuri zaidi. Mheshimiwa mtoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja yangu niliyoitoa leo asubuhi. Kwa mara nyingine, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa ushirikiano, upendo na heshima kubwa walijonipa kwa kuwa mwakilishi wao humu Bungeni kwa vipindi viwili mfululizo.

Katika muda wote huu nimejitahidi kuwatumikia kwa bidii, unyenyekevu na uaminifu mkubwa. Kwa pamoja tumetekeleza ilani ya uchaguzi vizuri sana na napenda kuwashakikishia wananchi wenzangu wa Manyoni Mashariki kwamba bado nina nguvu, ari na utashi wa kuendelea kuwatumikia kwa miaka mitano mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii au kwa kusema humu Bungeni ama kwa maandishi. Yote yaliyosemwa tutayazingatia na ushauri mzuri tutauzingatia.

Kama ilivyo ada, napenda kuwatambua wale wote waliochangia katika hoja hii ya leo. Waheshimiwa waliochangia kwa kusema humu Bungeni ni Mheshimiwa Job Ndugai - Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Shoka Khamis

Juma - kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Ephraim Madege, Mheshimiwa Muhonga Ruhwanya, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Magale Shibuda, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Herbert Mntangi. (*Makofi*)

Waliochangia kwa maandishi, hawa nao sio haba, wapo karibu 41. Ni Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Anna Abdulhabib Komu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mosi Mussa, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Fatuma Fereji, Mheshimiwa Khdiya Al-Qassmy, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Dr. Gwido Singonda, Mheshimiwa Fatma Maghimbi na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni nyingi sana, pengine muda hautatosha kuzijibu zote lakini kabla sijaanza kuzijibu hoja moja moja, naomba nitoe ufanuzi wa jumla katika masuala yafutayo. Kwanza kuhusu majukumu ya Wizara ya Ardhi, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa jumla waelewe kwamba majukumu ya Wizara ya Ardhi ni kutunga sera na sheria zinazotawala masuala ya Ardhi, Nyumba na Makazi. Hili ndilo jukumu la msingi la Wizara. Sasa utekelezaji wa mambo yote haya kimsingi unafanywa na Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji na Halmashauri za Majiji chini ya Wizara yao, Wizara ya TAMISEMI.

Halmashauri ndio zinazoajiri wataalamu wote katika Sekta ya Ardhi chini ya TAMISEMI. Halmashauri ndio zinazotakiwa kupima viwanja Mijini, sisi tunatoa viwango tu na sheria lakini wanaotakiwa wapime Mijini ni Halmashauri. Halmashauri ndio zinatakiwa zipime mashamba ya wananchi na kutoa hati miliki za kimila. Halmashauri ndio zinatakiwa zipime na zigawe ardhi, sisi Wizara tunakamilisha tu mchakato ambao unaanzwa na Halmashauri kwa kutoa hati miliki na sasa hivi tunazitoa kupitia kwenye Kanda huko huko jirani na Halmashauri ziliko.

Kwa hiyo, kama upimaji viwanja mijini unakwenda pole pole na kama upimaji wa mashamba unakwenda pole pole, basi tuijulize huko huko kwenye Halmashauri ndio wenye jukumu, sisi Wizara ni wasimamizi tu na watoaji wa miongozo, watendaji halisi,

ni wenzetu wa Halmashauri. Aidha, Wizara inawajibika kuzisaidia Halmashauri kwa kuwapa miongozo na ushauri wa kitaalamu ili kazi hizo wazifanye kwa mujibu wa taaluma zao na kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba Halmashauri zetu lazima zibadili mtazamo kuhusu Sekta ya Ardhi ili zitoe kipaumbele kama wanavyotoa kipaumbele katika Sekta za Elimu, Afya, Maji na kadhalika watoe kipaumbele katika Sekta ya Ardhi kwanza kwa kuajiri wataalamu wa Sekta ya Ardhi na kuondoa upungufu wa wataalamu katika Halmashauri. Halmashuari nyingi sasa hivi hazina wapima ardhi, *land surveyors* hawapo, tunaposema sasa wapime viwanja haraka, watapimaje wataalamu hawana?

Kila siku nasema wanapokuwa hawana wataalamu wa elimu utasikia wanalamika, wakikosa wataalamu wa udakitari, manesi wanalamika, wakikosa mabwana shamba wanalamika wanapokosa wapima ardhi (*land surveyors*) hawalamiki, wala hawaajiri, hili ni kosa, tutapimaje ardhi na kuwamilikisha wananchi bila wataalamu hawa?

Ni lazima Halmashauri zione kwamba hawa nao ni muhimu kabisa. Tutapangaje Miji bila *town planners*? Halmashauri nyingi hazina Maafisa Mipango Miji, hawapo! Kwa hiyo, naomba sana Halmashauri wabadilishe huu mtazamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri jinsi wanavyonunua vitendea kazi vya Idara nyingine, vile vile wanunue vitendea kazi kwa Idara ya Ardhi, kupima ardhi lazima uwe na vifaa. Vifaa havipo katika Halmashauri nyingi, watapimaje ardhi kwa wananchi? Vile vile kupima ardhi unahitaji rasilimali fedha, Halmashauri zinatenga hela za maji, hela za barabara, hela za afya, hawatengi hela za kupima ardhi, hili ni kosa.

Vile vile Halmashauri unapoomba kasma kwenye Serikali kuu wataomba kasma za elimu, wataomba kasma za maji, za barabara, za afya, hawaombi kasma za ardhi, hili ni kosa. Kwa hiyo, kwa kifupi nataka kusema kwamba ili kweli sekta ya ardhi ilete mabadiliko ya haraka, ni lazima kwenye Halmashauri kuwe na mabadiliko ya fikra ili hii Sekta ya Ardhi ipewe kipaumbele kinachostahili ili yote haya ambayo Waheshimiwa Wabunge mnataka yafanyike basi yaweze kufanyika kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yakifanyika, mabadiliko makubwa sana yatatokea, kwani ardhi yote itapimwa, itapangiwa matumizi bora na itamilikishwa kwa Watanzania. Mamilioni ya Watanzania wana ardhi lakini bado ni masikini, Watanzania wana ardhi, ni ma-*landlord* lakini ma-*landlord* ambao ni masikini kwa sababu hawakopesheki, lakini tukishapima ardhi yao, tukawamilikisha sasa watakuwa wanakopesheka. Maendeleo ya nchi au ya mtu binafsi hayawezi kuja kwa hela zako za mfukoni mwako, mikopo ndicho kichocheo cha maendeleo, yawe ya nchi ama ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia limezungumzwa na watu wengi sana. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, mtu mwenye nyumba au ardhi anapotakiwa apishe mradi fulani kwa manufaa ya umma au kwa uvezeshaji binafsi

kisheria lazima alipwe fidia, ndivyo sheria inavyosema. Anastahili kulipwa fidia. Kama mwananchi anapisha mradi wa barabara ama mradi wowote, halafu halipwi chochote huko ni kuvunja sheria. Ni haki yao, lazima walipwe fidia. Hivyo, matukio yaliyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna baadhi ya maeneo fulani fulani hapa nchini wananchi wameondolewa katika maeneo yao bila ya kulipwa fidia, hiyo sio sawa.

Wana haki yao na Wizara yangu itaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba ile haki yao ya kulipwa fidia wanaipata wote pale walipo, pamoja na wale wa Kurasini ambaao Mheshimiwa Mbunge wa Temeke amewasemea, wana haki ya kulipwa fidia, na sisi tutasimamia kwamba sheria itekelezwe. Sisi tunatunga sheria na tunasimamia itekelezwe; pale inapovunjwa ni wajibu wetu kusema kwamba hapa sheria imevunjwa, fuata sheria.

Aidha, sheria inaelekeza kwamba fidia italipwa kwa mujibu wa bei ya soko kwa wakati huo. Mthamini Mkuu wa Serikali anatakiwa mara kwa mara afanye utafiti wa bei ya soko ili kuhuisha viwango vya fidia. Kazi hii alianza kuifanya mwaka 2009/2010 kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya bajeti, na sasa hivi wanaendelea kufanya katika Mikoa mbalimbali ili tuhuishe na tuboreshe viwango vya fidia na tupunguze au tuondoe malalamiko ya wananchi kuhusu kulipwa fidia ndogo. Fidia lazima izingatie bei za wakati huo, bei ya soko na sio wananchi wapunjwe, hiyo sio sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ardhi ya wawekezaji kutoka nje, sheria yetu za ardhi hairuhusu raia wa nje kumilikishwa ardhi isipokuwa tu huyo raia wa nje awe mwekezaji na awe amethibitishwa na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) kwa kupewa hati au *certificate* kama mwekezaji. Hivyo ndio sheria inavyosema. Hata akishatambuliwa bado kwa utaratibu wa sasa huyu mwekezaji atakwenda kwa sheria ya sasa akapate idhini ya Kijiji kuititia Mkutano Mkuu wa Kijiji, yaani *Village Assembly*. Wale ndio wenye kauli kwamba ardhi yao mwekezaji apewe ama asipewe, na hata kama wakikubali, bado huo uamuzi wao na mihtasari ya vikao vyao vya Kijiji vinakwenda kwenye Halmashauri ili Kamati ya Ugawaji wa Ardhi wakiwemo na Madiwani watazame kama hili jambo limekaa sawa sawa.

Madiwani wakimaliza, hili jambo linakuja kwa Waziri wa Ardhi, naye sharti aridhike kwamba wananchi hao katika Kijiji hicho kweli wanayo ardhi ya ziada ya kumpa huyo mwekezaji. Kama hawajafanya mpango wa matumizi bora ya ardhi, Waziri ataagiza Kijiji kifanyiwe mpango wa matumizi bora ya ardhi, kwa sababu ule mpango utaonesha kama Kijiji kina ardhi ya ziada ya kutoka kwa mwekezaji ama hakina? Haya yote tukisharidhika, ndipo Rais anapelekewa kutoa idhini ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umewekwa ili kulinda ardhi ya wanavijiji. Kwa hiyo, wanaofikiri kwamba ardhi inaporwa tu holela holea sio kweli, tunao utaratibu mgumu kweli. Pamoja na kwamba tunalinda ardhi ya wanavijiji, lakin wawekezaji wanalamika, wanasema Tanzania kwa mlolongo huu nilioutaja inawachukua miaka miwili mpaka miaka mitatu mpaka aje apate hiyo ardhi, kumbe akienda nchi nyingine inamchukua wiki mbili au wiki tatu amepata.

Ndio maana kwenye hotuba yangu nimesema kwamba ili kutatua tatizo hili sasa tutatenga maeneo maalum kwa ajili ya wawekezaji, yaani *land bank*, ili mwekezaji akija asiende kwenye Vijiji, akute Serikali imeshatenga maeneo ya wawekezaji, *land bank*. Huu ndio ufumbuzi ambao utawaondolea kazi wanavijiji kufikiria je, wana ardhi ya kutoa au hawana? Itampunguzia vile vile mwekezaji muda, mlolongo wa kupata ardhi ya kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeagiza kwamba Halmashauri za Wilaya kwa sababu hii *land bank* tunaipata kwa njia mbili. Njia ya kwanza na ya haraka tumeagiza Halmashauri za Wilaya watuletee orodha ya mashamba ambayo yametelekezwa, kuna mashamba yametelekezwa kwa miaka mingi, yamekuwa ni mashamba pori, hayalimwi, waliopewa hawalimi, kodi hawalipi, ardhi imekaa bure.

Tumewaambia wayaorodheshe, waanzishe mchakato wa kuyafuta kwa kuwapa *notice*, baadaye wayalete Wizarani na sisi tutampelekea Mheshimiwa Rais ili tuyafute. Tukishafuta, wa kwanza kufikiriwa ni wananchi wanaoishi katika maeneo ya jirani ambao hawana ardhi ndio watakuwa wa kwanza kufikiriwa, halafu pili, ardhi kama bado ipo ndipo sasa tutaitenga kwa ajili ya wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tutaanzisha zoezi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, zoezi la kupanga matumizi ya ardhi katika Wilaya na katika Vijiji. Zoezi hili litaonesha ni maeneo gani ambayo yana ardhi ambayo sasa hivi haitumiki, na hata katika miaka ishirini ijayo haitatumika, hayo maeneo ndio tutayatenga yawe kwa ajili ya wawekezaji na kwamba tutatenga maeneo haya ya *land bank*.

Nataka kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hatutachukua eneo la Kijiji, hatutachukua mashamba ya wanavijiji ili tuyatenge kuwa ya wawekezaji, wala hatutaathiri mahitaji ya Kijiji fulani kwa miaka kumi au ishirini ijayo. Haya yote tunayazingatia ili zoezi hili lisiathiri ardhi ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wetu na sheria yetu ya ardhi, hawa wageni tunawakodisha ardhi kwa muda fulani inaitwa *lease*. Sisi hatuna sheria ya kumpa mtu ardhi iwe yake milele ukiacha ya Vijijini. Ile ardhi ya vijiji, ile hati miliki ya kimila ndio haina muda. Hii ya wawekezaji haina muda. Ama miaka thelathini ama sitini, muda ukiisha inarudi Serikalini ni kama tu wewe umempangisha mtu nyumba yako kwa miaka kadhaa akishaondoka nyumba inakuja kwako. Ardhi hii ni hivyo hivyo, akishaondoka huyu mgeni kwa sababu tulimkodisha, ardhi inarudi mikononi mwa Watanzania.

Baada ya kusema haya, nijaribu kupitiapitia hoja za Waheshimiwa nyingi sana. Ngoja nijitahidi nitakapoishia ni hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati ya Ardhi kwa kweli walitushauri tu kwa mfano kuhusu makusanyo ya pango la ardhi, walitushauri kwamba tuongeze makusanyo na sisi tunesema tutazingatia.

Sasa hivi tunajaribu kushirikiana na Halmashauri, hivi viwanja vyote ambavyo vimemilikisha kuviweka katika kompyuta ili tuwe tunavifuatilia kwa kompyuta nani amelipa, nani hajalipa kwa sababu sasa hivi watu wengi kwa kutumia tu majalada watu wengi hawalipi na sio rahisi kuwagundua. Lakini tukishaweka katika kompyuta, sasa tutagundua haraka ili waweze kulipa.

Kamati na baadhi ya Wabunge wametushauri, kwamba utaratibu wa kumilikisha wananchi ardhi badala ya kuishia kwenye Kanda, ufile mpaka kwenye Mikoa, kwa kweli hilo ndio lengo letu, mara ya kwanza kazi yote ilikuwa inafanyika Wizarani, tumepeleka kwenye Kanda, lengo letu tupeleke mpaka kwenye Mikoa na hatimaye tufike mpaka hata kwenye Halmashauri, lakini inatakiwa sasa tupate wataalamu wa kutosha kwenye Halmashauri huko na tupate rasilimali fedha za kutosha, tukishakamilisha hayo, sisi tupo tayari kuteremsha haya madaraka yaende mpaka kwenye Halmashauri.

Vile vile, Kamati imetushauri kuhusu ujenzi holela kutokana na uhaba wa viwanja, kama nilivyosema awali mwenye jukumu la kupima viwanja ni Halmashauri za Miji na Wilaya. Sasa hivi wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa wataalamu kupima, hawa zana za kupimia, hawana hata fedha za kugharamia hili zoezi. Haya mawili, matatu yakifanyika nina hakika tutaanza kuona kasi ya kupima viwanja Mijini, kwa hiyo, ujenzi holela utapungua, kwa sababu kila mtu atajenga mahali ambapo pamepimwa.

Kuweka mipaka kwenye maeneo ya majini ni ushauri mzuri, tunajiandaa kufanya hiyo kazi, wataalamu tunao sasa hivi ni vifaa tu ili tuweze tukapima na tukachora ramani ndani ya bahari na kwenye maziwa.

Wataalamu wa kuendesha kituo cha kupokea picha za *satellite* waandaliwe mapema, tumeshaanza kuandaa, mwezi Septemba tunapeleka wataalamu wetu saba ambayo ni awamu ya kwanza kwenda kujifunza Ufaransa jinsi ya kuendesha kituo hiki kwa sababu kituo hiki ni cha kwanza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio nchini tu, nchi ambazo zina vituo hivi Afrika, kusini mwa Sahara, ni Afrika Kusini tu. Kwa hiyo, sisi tutakuwa ni wa pili, lakini tunawapeleka wataalamu wetu wakajifunze, halafu wakirudi tutapeleka na kundi lingine kwa sababu mwaka huu wa fedha tunataka tuanze hiki kituo cha kupokea picha za *satellite*.

Kambi ya Upinzani walikuwa na mambo mengi, moja lilikuwa ni kwamba wananchi wa Kijiji cha Ata, Kata ya Kisese na Kijiji cha Chubi, Kata ya Bumbuta wameondolewa kwenye maeneo yao na hilo eneo limetolewa kwa mwekezaji.

Tumewasiliana na Kondoa mchana huu, wametueleza kwamba hili eneo haliko katika Kijiji cha Ata ni Kijiji cha Chubi, wamemkodisha mwekezaji kwa taratibu za kisheria kabisa, kampuni inaitwa *Quality Food Product* kwa ajili ya kilimo cha alizeti na kwamba kila kitu kilifuata mkondo wa sheria na hakuna wanavijiji ambao walikuwa katika eneo hilo wakaondolewa ili apewe mwekezaji.

Hiyo ndio taarifa tumepewa kutoka Kondoa mchana huu, na ametutumia *fax* mpaka na ripoti ya Tume ambayo ilikwenda kuchunguza jambo hili na ripoti hiyo ilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na sisi mchana huu wametutumia *fax* ya nakale yake. Kwa hiyo, hakuna kitu kama hicho ambacho kilisemwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na tatizo la miji mingi kwamba miji imepangwa vibaya mno kiasi cha kusababisha Serikali kutotoa huduma za msingi. Ni kweli ujenzi holela ni tatizo na nimeshasema sababu zake ni uwezo wa Halmashauri ya Miji kupima viwanja sasa hivi ni mdogo. Kwa hiyo, kama wakizingatia ushauri watenge fedha za kupima viwanja, wawe na watalaam hali hii itabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani vilevile kulikuwa na suala la udhibiti wa ukuaji wa miji na majiji, jibu ni lile lile kwamba kasi ya kupima ikiwa kubwa tutapunguza ujenzi holela katika miji na kinachotakiwa tu ni rasilimali, vifaa, watu na fedha. Kulikuwa kuna hoja nyingine kwamba Tume imekuwepo, lakini migogoro ya ardhi bado ipo. Kwa hiyo, Tume inafanya kazi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba kazi ya Tume yenye ni kutoa miongozo na kutoa ushauri wa kitaalam na kufundisha zile timu za Wilaya zifanye hiyo kazi. Kazi zinafanya na timu ya matumizi bora ya ardhi ya Wilaya, Tume inafundisha tu. Tatizo wakishafundishwa na Tume ikafanya nao kazi kwa vijiji vitatu, vinne, vitano wakishaambiwa sasa endeleeni peke yenu wanaishia pale pale kwa sababu zile nilizozitaja kwamba hawatengi fedha za kufanya kazi hii, wakibadilika na mambo yatabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Omar Kwaangw' kuhusu kuchelewa kulitumia eneo lililokuwa la *Babati Sisal Estate* kutoptaka na mgogoro uliopo. Huu mgogoro bado upo, tumeulizia wamesema mgogoro uko Mahakamani, kwa hiyo, kama uko Mahakamani nadhani si sahihi sisi kuutolea maelezo hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Godfrey Zambi ameuliza je, Sheria ya Ardhi imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili? Sheria za Ardhi ziko nyingi ambazo zimeshatafsiriwa kwa Kiswahili ni ile Sheria ya Vijiji Na. 5 imeshatafsiriwa kwa Kiswahili. Sheria ya Utatuza wa Migogoro ya Ardhi kwa maana ya ile inayounda Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata na Wilaya Na. 2 imeshatafsiriwa. Vile vile Sheria ya Kupanga Matumizi Bora Ardhi Na. 6 vilevile imeshatafsiriwa kwa Kiswahili. Hivi sasa

Sheria ile ya mikopo ya nyumba nayo iko BAKITA inatafsiriwa kwa Kiswahili na ile Sheria ya kupangisha sehemu ya jengo nayo inatafsiriwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zingine zilizobaki bado tuko katika mchakato na zenyewe kuzitasiri kwa Kiswahili. Lengo letu Sheria zinazohusiana na mambo ya ardhi zote ziwe za Kiswahili ili wananchi waweze kuzielewa vizuri na wazitumie ili wasije wakadhulumiwa ardhi yao. Mheshimiwa Godfrey Zambi vile vile na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Omari Kwaang' walizungumzia habari za ugawaji wa viwanja umetawaliwa na rushwa na kwamba maofisa wanahodhi viwanja na baadaye wanaviuza kwa bei ya ulangazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uadilifu ni la muhimu sana katika hii sekta ya ardhi. Ni sekta ambayo inagusa maisha ya kila mtu. Kwa hiyo, na sisi pale Wizarani tunajitahidi sana kusimamia ili wale wote ambao wataonekana wanakiuka taratibu hizi watachukuliwa hatua. Katika kipindi hiki wafanyakazi wanne wamefukuzwa kazi kwa kukosa uadilifu katika Wizara yangu na wafanyakazi sita wamesimamishwa kazi na wako Mahakamani kujibu tuhuma hizi za kukosa uadilifu katika utendaji wao kazi pale Wizarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vipyaa viwekewe miundombinu. Hili limeelezwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita na wengi tu wamelieleza. Ni kweli, ulimwenguni kote huwa mnapokwenda kujenga nyumba, miundombinu imeshatangulia, kama ni barabara zimeshatangulia, kama ni maji yameshatangulia, umeme umeshatangulia. Sisi kwetu hapa ni kinyume chake, *National Housing* anajenga nyumba halafu sasa yeeye mwenyewe anaanza kujenga barabara, yeeye mwenyewe anaanza kuweka umeme. Yeye mwenyewe anaweka maji.

Kwa hiyo, gharama ya ile nyumba inakuwa kubwa, kwa sababu wewe unalipia na umeme, aliyegharamia *National Housing*. Kwa hiyo, hili tunalifanyia kazi kwa kushirikiana na wenzetu wengine wa umeme, wa maji, wa barabara ili na sisi Watanzania tubadilike. Tufanye kama wenzetu wanavyofanya katika nchi zingine kwamba ujenzi wa nyumba unaendana na ujenzi wa miundombinu. Kwa hiyo, hili Waheshimiwa Wabunge tunalifanyia kazi ndani ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti alizungumzia kuhakikisha kuwa shughuli na huduma zinaendelea katika Ofisi za Dar es Salaam, katika Ofisi za Manispaa baada ya kufungwa. Nimecheki, nimeambiwa kwamba zile huduma muhimu zinatolewa. Mheshimiwa Kimiti, siyo kwamba zile Ofisi za Kinondoni, Ilala na Temeke zimefungwa mia kwa mia. Lakini zile huduma muhimu bado zinatolewa kwa wananchi. Lakini jambo lenyewe bado linachunguzwa katika ile Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za usajili wa hati ngazi ya Mkoa na Wilaya, nimeshajibu. Mheshimiwa Susan Lyimo, fidia ndogo na kuchelewa kutolewa kwa wakati. Hili nalo nimeshajibu kwamba fidia lazima iwe kwa bei ya soko na kwaba Mthamini Mkuu wa Serikali lazima mara kwa mara aweze kuhuisha kwa sababu bei

zinabadilika mara kwa mara. Kwa hiyo, bei zikibadilika na yeye lazima abadilishe viwango vya posho ili wakati wowote posho ilipwe katika kiwango cha bei ya soko. Ikichelewa kulipwa kwa zaidi ya miezi sita mpaka mwaka, basi yule anayetakiwa kulipwa atalipa na riba ya asilimia sita.

Kwa hiyo, kila anapochelewa kulipa kuna riba ya asilimia sita ndivyo Sheria inavyosema na wote wanaohusika na ulipaji fidia walijue hilo kwamba jinsi wanavyochelewa kulipa hayo malipo huyo anayetakiwa alipwe atalipwa na riba ya asilimia sita kila mwaka ambayo ile riba inachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo alikuwa anasema fidia ndogo tayari hilo tumeshajibu. Kwa kushirikiana kati ya Wizara yetu na *EPZ* (maeneo maalum ya kiuchumi na maeneo ya mauzo ya nje) ni ushauri mzuri, tutashirikiana. Udhibiti wa wageni wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya ardhi, hilo ni angalizo zuri na sasa hivi tunaangalia sheria zetu kama kuna mwanya. Wageni wanawenza wakatumia mwanya fulani wapate ardhi. Tunafanya mapitio ya Sheria ya Ardhi ili tuzibe ile mianya ili tuweze kuilinda ardhi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu alikuwa na mambo mengi sana. Lile la Ushirika wa Nyumba tunampongeza sana Mheshimiwa Mushashu kwamba kule Kagera wameanzisha ushirika wa kujenga nyumba. Ni jambo jema na tutamtuma Mkuu wa Idara ya Nyumba pale Wizarani aende Kagera akutane na vile vyama vya ushirika ili tujenge ushirikiano jinsi ya kuvisaidia vile vyama hasa kuviunganisha na zile benki ambazo zimeanza kutoa mikopo ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Madeje amesema kwamba *CDA* kuna migogoro mingi. *CDA* wanachukua maeneo, hawalipi fidia ama fidia ndogo. Alisema Wizara itoe tamko.

Mheshimiwa Madeje ni kwamba fidia ni haki ya mwananchi ambaye anapisha mradi. Kwa hiyo, kuna watu ambao wanapisha mradi hapa wa *CDA*, hawajalipwa fidia, hili ni kosa, lazima walipwe fidia. Fidia lazima ilipwe kwa mujibu wa soko (bei ya soko). Kwa hiyo, suala la fidia ndogo vile vile limetawaliwa na sheria. Bei ya soko, kama *CDA* hawatumii bei ya soko basi tunawaambia watumie bei ya soko. Fidia haitakiwi icheleweshwe. Yule anayechelewesha fidia ajue kwamba atakapoanza kulipa fidia lazima atalipa na riba ya asilimia sita juu ya kile ambacho alitakiwa alipe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Emmanuel Luhahula kule Bukombe alisema fidia ndogo. Nimeshatoa majibu kwamba watu wanachelewa kupata vyeti vya vijiji, ile inaitwa *Village Land Certificate*, tutajitahidi mwaka huu wa fedha vijiji vyote vile ambavyo vimeshapimwa na mipaka yake inajulikana, tutajitahidi mwaka huu vyote tuwape zile hati za ardhi ya kijiji, zinaitwa *Village Land Certificate*. Kwa sababu kama vimepimwa hakuna mgogoro, hakuna haja ya kuwacheleweshea kupata. Ila sasa kupimwa ili wapate hatimiliki, ni lazima vijiji vifanyiwe kwanza matumizi bora ya ardhi na Halmashauri ndiyo yenye jukumu hilo.

Sisi tunaweza tukaja kutoa tu utaalama na kuwashauri, Mheshimiwa Mbunge lakini Halmashauri yako ndiyo yenye kazi hiyo. Wakianya matumizi bora ya ardhi sasa wataanza kutambua mipaka ya mashamba ya mkulima mmoja mmoja na kutoa hatimiliki ya kimila vile vile hiyo kazi inafanya na Halmashauri. Sisi Wizara tutawasaidia kwa kuwashauri na kuwapa utaalamu wa kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Kabwe Zitto wameeleza tatizo kwamba kuna watu kule watendaji na Madiwani kule Mwandiga wamejigawia viwanja na kwamba Mheshimiwa Rais alikuwa kule juzi amesema virudishwe. Tumesikia jambo hili, ilikuwa mimi mwenyewe niende, lakini nikapata mkasa wa ndege wiki nzima kila siku nakwenda *Airport*, ndege haipo. Baadaye nikashindwa kwenda. Lakini muda bado upo, sisi Mawaziri tunaendelea mpaka Mheshimiwa Rais atakapoapishwa ndiyo siku na Uwaziri unakwisha. Kwa hiyo, muda upo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo sheria zetu kwamba Mawaziri hawa wataendelea na shughuli zao za Uwaziri na *cabinet* itaendelea kukaa mpaka siku Rais anapoapishwa pale *stadium* akimaliza kuapa tu Mawaziri wote hamna Uwaziri, ana kazi sasa ya kuunda Baraza jipya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kabwe Zitto bado muda wa kwenda Kigoma ninao mpaka atakapoapishwa Rais mwingine. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba tumezipokea, tatalishughulikia jambo hili kwa sababu maagizo ya Mheshimiwa Rais kama ambavyo Mheshimiwa Kabwe Zitto alivyosema ni lazima tuyatekeleze na mimi naahidi bado safari yangu, nitatafuta nafasi ya kwenda huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita kwamba Serikali iharakishe utaratibu wa kuwakopesha mikopo ya kujenga nyumba ya muda mrefu na riba nafuu. Sasa hivi baada ya kupitia ile Sheria ya Mikopo kuna benki tano ambazo sasa hivi tayari zinatoa mikopo ya nyumba. Tumezitaja kwenye hotuba yetu lakini narudia tena ni *Azania Bank*, *Commercial Bank of Africa*, *International Commercial Bank*, *STANBIC Bank* na *United Bank of Africa*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa tayari wameshaanza kutoa mikopo ya nyumba hivi sasa. Mabenki mengine bado hayajaanza kutoa mikopo, lakini tatizo lao nimeshawahi kilitaja safari moja kwamba wao au mabenki mengi yanapata mikopo ya muda mfupi na riba kubwa. Sasa ye ye akishapata mikopo wa muda mfupi hawezikakupa wewe mteja wake mkopo wa muda mrefu, atafilisika. Ndiyo maana sasa imeshaundwa kampuni inaitwa *Watanzania Mortgage Re-Financing Company*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hii kazi yake itakuwa ni kukopesha mabenki hapa nchini mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu, ili mabenki nao yatukopeshe sisi wateja mikopo ya muda mrefu, miaka 10, 15, 20, mpaka 25 na riba nafuu. Kwa hiyo, kampuni hii nadhani itaanza mpaka mwezi wa Septemba itaanza kufanya kazi yake kwa hiyo, mabenki mengi yataanza kukopesha. (*Makofi*)

Kuna watu wameuliza pamoja na Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba je, tutaunda na Benki ya Serikali ya kutoa mikopo kama ilivyokuwa ile benki kama Benki ya Nyumba

(THB)? Jibu ni kwamba hapana, Serikali kwa sasa hatuna utaratibu wa kuunda benki ya Serikali ya kukopesha mikopo ya nyumba, badala yake benki hizi hizi zilizopo tutaziwekea mazingira ili zitoe mikopo ya muda mrefu kwa Watanzania na kwa riba nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna swal la Mheshimiwa Kabwe Zitto, ushauri kwamba tuanzishe mamlaka ya kuthibiti sekta ya nyumba. Ni ushauri mzuri na kwa kweli tumeshaanza, tumeshaanza kuandaa sheria ambayo itadhibiti utealam wa biashara ya nyumba. Ni sheria ambayo italinda haki za wanaouza nyumba, italinda haki za wapangaji, italinda haki watu wanaonunua nyumba. Kwa hiyo, sheria hiyo ya udhibiti wa masuala ya nyumba inaandaliwa itakuja. Kwa sasa hivi haipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ponsiano Nyami ameleezea kwamba vijiji vyote nchini vipimwe ili kuondoa migogoro ya ardhi, jibu ni kwamba tumeshapima vyote. Ila uchaguzi wa mwaka jana mwishoni kama mtakumbuka kuna vitongoji vipyta vilianzishwa na vijiji vipyta vilianzishwa kama 300 hivi, vipyta kabisa. Hivi navyo mwaka huu wa fedha tutavipima. Lengo letu vijiji vyote vijulikane mipaka yake ili kuondoa migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nyami kuhusu mipaka kati ya Wilaya ya Nkasi na Wilaya Mpanda na Wilaya ya Sumbawanga, ni suala tu la kuja kutafsiri *Government Notice* maana hizi Wilaya si mpya ni za zamani na lazima mipaka yake imefafanuliwa katika *Government Notice*. Tutakuja Mheshimiwa Nyami tuone tatizo liko wapi, kwa sababu halitakiwi liwepo.

Mheshimiwa John Cheyo alisema kwa nini mnapanga matumizi bora ya ardhi vijijini wakati kila mwananchi ana eneo lake? Mheshimiwa Cheyo ni lazima kabisa tupange, kijiji lazima tupange ili eneo la huduma za jamii, zahanati, shule wapi, lijulikane, eneo la makaburi lijulikane, eneo la malisho, mifugo lijulikane, eneo la makazi lijulikane ili atakayeondoka aende kujenga nyumba kwenye makaburi, tuseme wewe umevunja sheria akamatwe, anayechukua ng'ombe amekwenda kwenye eneo la kilimo, akamatwe kwamba umevunja sheria. Kwa hiyo, kupanga haya matumizi Mheshimiwa Cheyo ni lazima tupange ili tuondoe migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jackson Makwetta, amesema vijiji tuviunganishe hivi ili viweze kuwa na shughuli pana za kiuchumi. Sasa suala la kuunganisha vijiji, Mheshimiwa Mzee wangu, Mzee Makwetta ni huko huko kwenye Wilaya na kwenye Halmashauri na wanavijiji wenyewe, mkikubaliana Wizara yangu haina neno itakuja kurekebisha tu ile mipaka mtakayokuwa mmekubaliana ninyi huko.

Mheshimiwa Makwetta alizungumzia pia suala la wanavijiji wapewe elimu kuhusu sheria ya usimamizi ardhi. Ni ushauri mzuri na ndivyo tunavyofanya na ndiyo maana tunahangaika kuzitafsiri hizi sheria zote kwa Kiswahili ili waweze kuzielewa. Tunawafundisha mpaka jinsi ya kupanga matumizi bora katika kijiji chao. Huwa wanapanga wenyewe wanavijiji hawa hawa baada ya Tume kuwapa hii elimu.

Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, alizungumzia kasi ya upangaji, matumizi ya ardhi, haiendani na mahitaji ya watu. Ni kweli na nimeshasema tuna tatizo, kasi ndogo kwa sababu wataalam wachache, kwa sababu ya zana chache na fedha za kufanya hiyo kazi haziwekwi. Lakini nina hakika sasa Halmashauri tumeshaelewana, TAMISEMI tumeshaelewana. Haya mambo yatarekebishwa ili kazi iende kwa kasi kwa sababu Watanzania sasa wanataka ardhi yao ipimwe, wanataka wamilikishwe, hiki ndiyo kilio cha Watanzania. Kwa hiyo, lazima na sisi tubadilike ili tuweze kukidhi haya mahitaji ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, amezungumzia mkakati wa muda mfupi, wa muda mrefu wa kushughulikia migogoro ya ardhi na kuelimisha wananchi, watendani vijijini. Tunao mkakati hasa hasa kwa kutoa elimu kwa kushirikiana na Halmashauri. Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika naye alikuwa na suala hilo hilo na jibu ni hilo hilo.

Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, amezungumzia kutenganisha ardhi kwa ajili ya kilimo na malisho ya mifugo Wilayani Chunya. Halmashauri ya Chunya imekwishakuwa tayari kwa ajili ya kuweka matumizi ya ardhi ya Wilaya yenu. Tume inaweza kuja kushirikiana na ninyi katika kutoa ushauri na mwongozo ili kazi hiyo ifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Michael Laizer, alisema toa tamko kuhusu eneo la Loliondo. Wiki tatu zilizopita nilikwenda Loliondo, nimekaa na Wenyeviti wote wa vijiji, Madiwani wote, wataalam wote na nikatoa kauli ya Serikali pale kwamba lile eneo la Loliondo la *controlled area* ile hifadhi imeshika eneo lote la Tarafa ya Loliondo na Sare. Sasa lile *controlled area* tunairudisha nyuma ili vile vijiji 22 vibaki na ardhi yao na hilo jambo tumeshakubaliana nalo, ambacho hatukukubaliana pale ni lile eneo ambalo wanyama wanapita linaitwa Ushoroba ambapo wanyama wanapita kwenda Masai Mara, Kenya, halafu wanarudi. Mazalia yao, Wizara ya Maliasili na Utalii wanataka eneo hili, ni dogo tu, upana wake hautazidi kilomita tano, saba kwa sababu lina umuhimu wa mazalia ya wanyama, Wizara ya Maliasili na Utalii wanataka liwe chini ya Serikali Kuu. Wanavijiji wanataka liwe mikononi mwa vijiji chini ya utaratibu wa hifadhi ya wanyamapor (WMA). Hapo ndipo tatizo lililobaki Mheshimiwa Laizer na Ofisi Waziri Mkuu imeunda Tume kwenda kule kwenda kutazama jambo hili.

Kwa hiyo, nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tume ikishamaliza kuangalia jambo hili ambalo ni Ushoroba tu ndiyo iliyobaki, maeneo mengine yote wanavijiji watajipangia ile ardhi kwa kadri wanavyotaka wenyewe na hii itakuwa ni mara ya kwanza tangu tupate Uhuru wamefurahi sana. Wala hawatarudisha kadi za CCM kwa sababu Serikali ya CCM imesikia kilio chao, ardhi yao imewarudishia. Kwa hiyo, hawana haja ya kutanga tanga kutafuta vyama vingine. Endeleeni na chama chenu hicho hicho Mheshimiwa Michael Laizer kama mlivyokuwa tangu zamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mambo ni mengi sana na kengele ya kwanza imeshalia. Mheshimiwa George Lubeleje aliuliza Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kitaaluma Maafisa Ardhi na kuongeza udahili wa wanafunzi wanaojiunga katika vyuo vya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wataalamu wa sekta ya ardhi, tuna Chuo Kikuu cha Ardhi pale Dar es Salaam, tuna Chuo Cha Ardhi pale Morogoro, tuna Chuo Cha Ardhi pale Tabora. Hivi vyuo vya Tabora na Morogoro, vinatoa wataalamu katika ngazi ya *Diploma* na ngazi ya Cheti; Chuo Kikuu Cha Ardhi Dar es Salaam, kinatoa watalaamu katika ngazi ya *Degree*. Kwa hiyo, kwa kweli watalaamu wapo. Tatizo kama nilivyosema ni utashi mdogo wa watumiaji wa wataalamu hawa ambapo tatizo ni Halmashauri za Wilaya kuwaajiri watalaamu hawa kila mwaka.

Sasa tumezungumza na TAMISEMI na tunaendelea kuzungumza kwamba kwa sababu Halmashauri zinasuasua kuwaajiri, basi tufanye kama wanavyofanya madaktari na mabwana shamba ambao wakimaliza vyuoni, moja kwa moja wanapangiwa kwenye maeneo ya kazi kwenye Halmashauri. Pengine hili tukilifanya hivi, tutapunguza upungufu wa wataalamu hawa waliopo kwenye Halmashauri, kwa sababu watalaamu wapo lakini kuwaajiri ndio inakuwa tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kuongeza kasi ya kuunda Mabaraza ya Ardhi; wamezungumzia Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Arfi, ni kweli, sheria inasema tuwe na Baraza la Ardhi la Wilaya katika kila Wilaya. Tatizo ni kwamba pesa ambazo Wizara inapeleka ili kuanzisha mabaraza haya ni kidogo sana. Kwa hiyo, bado tunaongea na wenzetu Serikalini, wakituongeza uwezo wa Kifunguedha na sisi tutaongeza kasi ya kuunda haya Mabaraza. Sasa hivi tunayaunda katika zile Wilaya ambazo zina kesi nyingi na tunaunda katika zile Wilaya ambazo kutoka Baraza moja mpaka Wilayani ni umbali mkubwa sana. Hizo ndizo ambazo ninazipa kipaumbele kwa sasa hivi, lakini tatizo letu kwa kweli ni hilo la nyezo kidogo ambazo tunapata katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatma Magimbi alizungumizia majengo ya mabaraza ya ardhi na nyumba za wilaya hayana usalama uKifunguananisha na majengo ya Mahakama nyingine. Hilo nalo ni kweli lakini kila tukipata uwezo na sisi tutaongeza usalama kwa kuweka uzio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami alizungmuzia Mahakama za Mwanza kuendelea kusikiliza migogoro ya ardhi na nyumba. Hili si sawa; kesi za ardhi zinaanzia kwenye Baraza la Kijiji, halafu zinakwenda kwenye Baraza la Kata halafu zinakwenda kwenye Baraza la Wilaya, zikitoka hapo zinakwenda kwenye Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi na juzi juzi kwa sababu kitengo kile cha Mahakama Kuu ya Ardhi kimezidiwa, Jaji Mkuu ameruhusu Mahakama Kuu nyingine nazo zisikilize hizi kesi na huu ndio mlolongo wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, akasema lakini hawa watu hawa Wenyeviti, wanachaguliwa na nani? Wanakaa muda gani? Watu hawa wanachaguliwa na Wizara yangu na wanakaa kwa muda wa miaka mitatu. Akikosea, yupo Msajili wa haya Mabaraza pale Wizarani, leteni mashitaka; maana Mheshimiwa Dr. Slaa ana matatizo na yule mtu, nasikia ananyanyasa wateja, anawafokea wateja, ananyang'anya haki zao. Lete shauri hili kwa Msajili wa Mabaraza haya, yuko pale Wizarani kwetu, huyo bwana atachunguzwa na kama anafanya mambo hayo hatua

zitachukuliwa kwa sababu sisi tunataka watu watumikiwe kwa heshima na taadhima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi, ameeleza mengi kuhusu kule kwake Muheza. Tumemsikia Mheshimiwa Mntangi, tumeanza kuyashughulikia, baadhi ya mashamba tumeshayapeleka kwa Mheshimiwa Rais, ili afute zile hatimiliki na akishamaliza kuzifuta tutakuja kule tuangalie jinsi ya kuyashughulikia; hasa kwa wale ambao hawana ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine yote tutayajibu kwa maandishi ili kila mtu hoja yake iweze kupata majibu na natamka kwamba naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 48 – Wizara Ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* .....Sh. 4,395,011,900

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimemuomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko ni lini ahadi yake ya kupima mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na vijiji vinavyopakana navyo kwa sababu alitenga fedha katika Bajeti iliyopita na kuahidi zoezi hilo lingefanyika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe maelezo kwa Mheshimiwa Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo; ni kweli kwamba tunayo ahadi ya kupima vile vijiji vilivyo jirani na hifadhi ya Mikumi na leo mchana nimezungumza na wataalamu wangu wamenihakikishia kwamba wiki ijayo wataalamu watakuja katika Jimbo lako Mheshimiwa Mbunge na hiyo kazi itaanza. (*Makofi*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka ufanuzi tu kwamba kutokana na hii *transformation* ya *National Housing*, badala ya kuwa ni *landlord* ndio wanapokea kodi tu katika majumba ambayo wamerithi, sasa wanatakiwa pia kujenga nyumba kwa ajili ya kuwauzia Watanzania. Mimi nilitaka tu kujua kwamba *National Housing* pia itahusika kwa watu ambao wana viwanja vyao na wanahitaji kujengewa? Naomba kupata ufanuzi kwamba wanaweza kufanya kazi hiyo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi kwa swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sasa hivi tunalibadilisha shirika hili kutoka kuwa mpangishaji tu wa nyumba na kukusanya kodi, ili liwe ni shirika la kujenga nyumba kwa Watanzania na hasa hili ndio lilikuwa lengo tangu awali lilipoanzishwa mwaka 1962. Kujenga nyumba kwa Watanzania hasa Watanzania wa kipato cha katni na kipato cha chini, watakapojenga nyumba kwa kipato cha juu ili tu wapate faida kubwa na ili faida ile waje waitumie kujenga nyumba za Watanzania wa kipato cha chini. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kimsingi hili ni shirika litakalokuwa linajenga nyumba nyingi na sio kajumba kamoja kamoja, bali nyumba, *estates*. Hawa ni watu wanaojenga nyumba nyingi ili Watanzania wengi zaidi waweze kupata nyumba, hilo ndio jukumu lao la msingi. Lakini kwa sababu wenye vile vile wanafanya kazi ya ukandarasi kama mtu sijui yuko wapi huko na anataka akafanye mpango wake na *National Housing* kwa kutumia makandarasi wake wakamjengea, hilo hatuwezi kulikataa moja kwa moja, lakini jukumu la msingi ni kujenga nyumba nyingi, kwa kiingereza wanasema ni *estate* na ndio maana mwaka huu wanajenga nyumba 1,000 kwa ajili ya Watanzania wengi zaidi.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi naomba kuuliza swali moja ambalo niliuliza wakati wa kuchangia kwa maandishi. Kuna tatizo zima la kupatikana kwa ardhi kwa ajili ya kuendeleza programu za *EPZ* na *SEZ* kwa mamlaka ya *EPZ*; na nilimuomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni kwa jinsi gani Wizara yake itaweza kusaidia katika kuzipatia ardhi programu hizi kama vile ambavyo imepatikana ardhi ya hekta 8,000 kule Zinga Bagamoyo, na ikashindikana kupatikana maeneo ya kutosha kwa maeneo ya Kilimanjaro na Tanga? Naomba jibu katika hilo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa swali Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, kuhusu upatikanaji wa ardhi kwa yale maeneo maalum ya kiuchumi yaani *Special Economic Zones* na maeneo maalum ya kuzalisha bidhaa kwenda nje, (*Export Processing Zones*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hili linafanana na lile la wawekezaji tu wengine ambao mwekezaji anataka kuwekeza katika kilimo, ama katika viwanda. Nimesema sasa hivi kuanzia mwaka huu wa fedha, tutafanya jitihada za kutenga maeneo maalum kwa shughuli hizo maalum, ndio kile kitu kinaitwa *land bank*. *Land Bank* ni maeneo ambayo tutaanza kuyatafuta na kuyatenga kwa ajili ya shughuli maalum kama hizo. Tutaanza na yale mashamba yaliyotelekezwa na yapo mengi karibu kila mkoa. Kuna mashamba ambayo kwa miaka mingi hayalimwi, wenye wenyewe mashamba hawalipi kodi, yamekaa tu ni mapori; tutaanza na hayo kuyashika ili yawe ni *land bank*, lakini baadaye vile vile ipo ardhi katika Tanzania hii ambayo sasa hivi haitumiki na hata kwa miaka 20 au 30 ijayo, haitumika. Unaweza ukasafiri hata saa nzima uko kwenye mapori tu, hayo yote tunataka ardhi hiyo nayo isaidie kuzalisha mali kwa Watanzania. Kwa hiyo, hii ndio juhudii ambayo tunaifanya katika mwaka huu wa fedha kupitia *land*

*bank na hawa wenye maeneo maalum ya uwekezaji na haya ya mauzo ya nje tutaweka katika mpango ule wa kupata ardhi kuitia land bank. (Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi naomba ufanuzi tu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 81, Jedwali namba 7, Mkoa wa Dodoma una Wilaya sita, lakini hapa ninaona vijiji vilivyopimwa kwa Bajeti ya mwaka 2009/2010 ni 54 tu vya Wilaya ya Bahi na Chamwino. Sasa mimi ningependa tu nipate ufanuzi, je, Wilaya ya Mpwapwa vijiji vyote vimeshapimwa? Halafu na wilaya nyingine zilizobaki za mkoa wa Dodoma.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwamba kwa mwaka uliopita, tulipima vijiji vyote vilikuwa ni 1,500 ambavyo vilikuwa havijapimwa kwa nchi nzima. Kwa hivyo vya Dodoma vile 54 kwa wilaya alizozitaja za Bahi na Chamwino, ni vile ambavyo vilikuwa havijapimwa. Vinginevyo vijiji vingine vyote pamoja na vya Wilaya ya Mpwapwa, vimeshapimwa kwa maana ya kuweka ile mipaka ya vijiji.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa suala zima la hatimiliki za kimila lilivyofanywa na lilivyoendeshwa hasa kule Mbozi ambako ndio ilikuwa ni Wilaya ya mfano. Lakini nimekuwa nazungumza suala hili hapa Bungeni kwamba kwa wilaya ya Mbozi kwa sasa tuna wananchi karibu 14,972 ambaao tayari wana hatimiliki hizi za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati mbaya sana, hizi hatimiliki za kimila mpaka leo hazikubaliki na vyombo vya fedha, hususan Benki. Kwa hiyo, wananchi wamebaki wanategemea hizi hatimiliki za kimila kutoka Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na tunavyoolewa wote Mfuko wa Pembejeo wa Taifa bado unapewa pesa kidogo sana na hauwezi ukatoa mikopo kwa wananchi wote ambaao wana hatimiliki za kimila kwa nchi nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, Serikali imefikia wapi sasa kuzungumza na vyombo vya fedha hususan Benki, ili ziweze kukubali hati za kimila na wananchi hawa waweze kufaidika kwa kuwa nazo? Vinginevyo zinabaki kama mapambo tu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa swali la Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatimiliki za kimila ni hati ambazo zina nguvu sawa za kisheria kama hati zozote zile. Kwa mfano, hati tunazozipata huku mijini mbele ya sheria ni sawasawa na zile hati za vijijini. Tena hii ya mijini ina muda, miaka 33, miaka 66, miaka 99, zina muda. Zile za vijijini zile hazina miaka 30 wala 60, ni hati ambayo ni nzito zaidi. Ni jambo jipya ambalo itabidi tuendelee kuelimishana sisi wenye hati zile na vyombo mbalimbali vya fedha, lakini kwa sababu tulianza kule Mbozi, sasa hivi

wakulima wale aliowataja ambao wana hatimiliki, mikopo waliyonayo sasa hivi inayozunguka pale, ni shilingi bilioni 10, bila hati za kimila, walikuwa wana sifuri, walikuwa wana sifuri, walikuwa hawakopesheki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kwa matatizo lakini ndio tumeshaanza hivi na kwa kuwa, jambo lenyewe ni geni lakini jinsi litakavyozoleka na mabenki yatakuwa na imani na hizi hatimiliki, tunaendelea kuwaelimisha na baadhi wameshaanza kutoa. Nilipotembelea kijiji kimoja kwene Jimbo lake mwaka jana, nilikwenda na Meneja wa Benki ya *NMB* wa pale Mbozi, tukaenda mpaka kijijini. Kufika pale, kwene maswali wakasema lakini sisi tunakwenda na hizi hati zetu miliki, lakini Meneja hazikubali, sawasawa? Nikamwambia, Meneja jibu; maana nilikuwa nae wa upande wa Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ye ye akasema kwamba hizi tunazikubali na nimeshaanza kutoa mikopo, lakini baadhi yao kabla hajamaliza mkopo anataka mkopo mwingine tena. Sasa amalize kwanza mkopo huu. Akasema ukishakopeshwa ni lazima unalipa kwa vipindi fulani fulani, kama una shida nenda kamwambie mtu wa benki nina shida. Sasa kwenda kulipa halipi na akataka na orodha ya watu ambao wameshakopa pale kijijini lakini zile *installments* zao hawalipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikawaambia pale kijijini, bahati mbaya siku ile Mheshimiwa Zambi hakuwepo kwa sababu Bunge lilikuwa linaendelea hapa lakini salamu zake nilimtolea kule kwamba na sisi tuonyeshe uaminifu ili mabenki yatuamini. Lakini imeshaanza na shilingi bilioni 10 zimeshakopeshwa katika lile Jimbo la Mheshimiwa Zambi, kupitia hatimiliki za kimila. Hii ni hatua. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nadhani mtakapoanzisha mikopo ya muda mrefu kwa wakulima itakuwa ni zaidi, na sasa ukikopa kama *over draft* inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, tunaendelea; Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa kaka yangu Waziri ambaye ameitumikia nafasi yake ile kwa uaminifu na kwa ustadi, hakutuangusha wa mkoa wa Singida. Kwa hiyo, tunaamini wananchi wa Jimbo la Manyoni watakurudisha tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, niliuliza kwanza kabisa nikasema katika ule mpango wa ujenzi wa nyumba za *National Housing*, je, Mkao wa Singida upo? Nikauliza na ile *Singida Motel* ambayo sasa hivi imekuwa ikibadilishwa tu jina na hatujui hatima yake, imetengenezwa lakini bado ipo. Kwa hiyo, nikataka kujua na naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mbunge mwenzangu kutoka mkao wa Singida Mheshimiwa Dada yangu Martha Mlata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Housing* katika mpango wao wa miaka mitano wanakusudia kujenga nyumba 15,000 na watagusa mikoa yote pamoja na mkoa

wa Singida. Mkoa wa Katavi utakapoundwa bado. Sasa ameuliza vilevile kwa hiyo hili kwamba jina Singida limo, nasema Singida imo na mikoa yote itaguswa, hii *National Housing* mpya ambayo inataka kutoa huduma kwa Watanzania wote kwa mikoa yote. Wameomba tu sisi Wabunge tuwape msaada na sisi wanasiwa tusiwaingilie ingilie sana, wafanye kazi kwa utaalim wao na sisi tumewaaahidi hili kwamba macho yetu tutakuwa tunawatazama lakini mikono yetu hatutaweka ndani ya shirika ili wafanye sawasawa, watekeleze haya malengo kuwajengea nyumba Watanzania wa mikoa yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza *Singida Motel*, jengo hili la *hotel* ni jengo la *National Housing*, kwanza tuwashukuru *National Housing* sisi watu wa Singida, wamelikarabati sasa ni moja ya hoteli nzuri sana pale Singida inaitwa *Singida Motel*, *National Housing* wametumia shilingi milioni 60 kuikarabati ile hoteli, sasa hivi ni nzuri kabisa. Kwa hiyo, kinachosubiriwa sasa ni upate mwekezaji au mpangaji ambaye kweli ile hoteli ataiendesha vizuri, atoe huduma nzuri, atengeneze faida nzuri ili Watanzania wanaopita Singida pale waweze wakaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *National Housing* wako katika mchakato wa kumpata mpangaji mahiri ambaye hoteli ile ataitunza vizuri na atatoa huduma nzuri ili jina la Mkoa wa Singida wanaopita watalii waweze wakatoka na sifa nzuri kupitia ile hoteli. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 20 ameeleza utoaji na ubatilishaji wa miliki na ametaja kabisa kwamba kwa mujibu wa sera ya Taifa na Sheria ya Ardhi, mtu anaposhindwa kulipia kodi ananyang'anywa, sasa nimekuwa nikimlalamikia sana Mheshimiwa Waziri kila mwaka kwenye Bajeti yake, kuna mwananchi mmoja alipewa kiwanja mwaka 1984 pale *Sinza Plot, No. 594 B*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu bwana, mwananchi huyu amekuwa aKifunguuatilia sana mara ya kwanza alipewa mtu mmoja ambaye alishindwa kulipia masharti ambayo yameelezwu kwenye sera pamoja na sheria za ardhi. Lakini hadi leo mwananchi huyu mwenye kiwanja halali ambaye anatambulika mpaka kwenye mtaa na kithibitisho Mwenyekiti wa Mtaa ameshamthibitisha mwenye kumiliki kiwanja kile ni Alex Nyawazwa, sasa kila aKifunguuatilia anakuta kwamba ile barua imepelekwa kufutwa kwa Rais, naomba ufanuzi hivi kufuta kwa Rais inachukua muda gani, maana yake awamu ya tatu ilishapita, sasa awamu ya nne, ufutaji wa hati ile haijatokea, sasa itafutwa lini?

**MWENYEKITI:** Unaamanisha hiyo hati, ama kama ni *principle* tu kwamba ukipeleka mambo kwa Rais yanatumia muda gani, kwa sababu kama ni binafsi ningependa mkutane na Waziri maana yake kuna maswali mengi zaidi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala limekuwa nalichangia kila mwaka kumsaidia huyu mwananchi lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu atufafanulie tu sasa inachukua muda gani kufutwa hiyo hati kwa mwananchi yejote ambaye anatafuta hati yake hakupewa?

**MWENYEKITI:** Ulimwandikia kuhusu mtu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu upo na huyo bwana alishaandikiwa haonekani mpaka leo toka mwaka 1984.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa madhumuni ya kusahihisha rekodi katika *Hansard*, ile hoteli ya Singida ilikarabatiwa na *National Housing* kwa shilingi milioni 600 na sio shilingi milioni 60 kama nilivyosema. Naomba *Hansard* ichukue hii takwimu sahihi.

Sasa kuhusu suala la dada yangu Mheshimiwa Esther Nyawazwa nataka niseme tu kwamba nilichukue ili tukalifanyie kazi na wataalam wangu wote wanaskia kwa hiyo, nataka niwatume hapa hapa kwamba wakirudi Dar es Salaam waanze na hili, hili suala la *Plot. No. 594 E. Sinza*, watazame nini kinachoendelea, wanipe majibu yake nini kinachoendelea kabla Bunge halijakwisha na mimi Dada yangu Nyawazwa nimweleze tumefika hatua gani. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mheshimiwa Chiligati ni kaka yangu, Mheshimiwa Chiligati ana vyeo vingi kweli, Waziri mwenye dhamana kubwa ya Serikali tena hana Naibu, Mheshimiwa Chiligati ni Katibu Mwenezi na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Mheshimiwa Chiligati ni Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, Mheshimiwa Chiligati kwa nafasi zote hizi ametimiza wajibu wake vizuri sana na amefanya kazi bila kuchoka, jitihada hizi zimetambuliwa na wanawake wa mkoa wa Singida vilevile Mheshimiwa Chiligati ni mlezi wa wanawake wa UWT, mkoa wa Singida. (*Makofi*)

Katika mchango wangu wa maandishi nilitumwa na wanawake wa mkoa wa Singida hususan wanawake wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwamba wanampongeza sana kwa kazi nzuri alizofanya kwa nafasi zote hizi bila kuchoka na wanamhakikishia kwamba watampigania kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba anarudi hapa Bunge. (*Makofi*)

Sasa wanawake hawa wako kwenye *television* wanasubiri wanasikiliza je, mbona hajaongea kukubali hizo pongozi. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana mnasemwa, Mheshimiwa Waziri unataka upongeze utoe nia na wakakuchangie fomu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeweka akiba ya mwishoni kabisa kwa hiyo, ngoja niwashukuru sana akinamama wa mkoa wa Singida, mimi ndiye mlezi wa UWT mkoa wa Singida na kwamba bado na nguvu na nia na ari ya kuendelea na nategemea msaada wao mkubwa sana ili niweze kurudi na niendelee kuwa mlezi na shughuli za maendeleo za mkoa wa Singida. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu nipaye ufanuzi katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimezungumzia kuhusu mgogoro wa shamba lililokuwa liKifunguahamika kwamba shamba la benki kule Kakese.

Katika kipindi cha utumishi wangu wa kuwatumikia wananchi wa Mpanda, kwa miaka mitano nimeandika swal na nilipata fursa ya kumuuliza Waziri Mkuu swal la papo kwa papo na mpaka leo hakuna ufumbuzi juu ya hilo, nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi wa Mpanda muda ambao Serikali inachukua katika kutatua tatizo hilo la ardhi kule Kakese.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo yafuatayo kwa Mheshimiwa Said Amour Arfi. Hili la mgogoro wa ardhi Kakese nikiri kabisa kwamba halijafika mezani kwangu nikalishughulikia, lakini maadamu sasa Mheshimiwa Mbunge amelileta, tena amelileta katika Bunge lako Tukufu na wataalam wote wa Wizara yangu wako hapo nyuma wamemsikia, naomba atuachie tukalishughulikie na kama nilivyomjibu Mheshimiwa Esther Nyawazwa nategemea wataniletea majibu nikiwa hapa hapa Dodoma ili unapoondoka uondoke na majibu ya Wizara.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwa kuwa maeneo ya wazi yana umuhimu mkubwa sana na mara nyingi yanaachwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye lakini maeneo mengi ya wazi yamekuwa yakinumiwa vibaya, yakibadilishwa na watendaji ama wa Serikali za Mitaa ama wa Serikali Kuu na katika mchango wangu wa maandishi nimewandikia Mheshimiwa Waziri nadhani hakupata muda wa kuyajibu yangu yote, lakini nina mfano hai wa Mwenyekiti wa Mtaa wa pale Magomeni Makuti ambaye ametoa eneo la wazi kwa ajili ya ofisi ya CCM na wananchi wa maeneo yale wamelalamika sana na naomba ninukuu ambacho amekujibu Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa anasema kwamba niliwaruhusu waweke ofisi yao pale kwa sababu hiki ni Chama Tawala, najua baadaye watarirudisha tu, wanaweza hata kununua nyumba wakahamia si Chama Tawala bwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maneno kama haya yanatoka kwa mtendaji wa Serikali, hili ni tatizo, lakini tumeona kwamba mara nyingi wana CCM wanapofanya makosa wanapokiuka taratibu, Serikali inapata kigugumizi sasa nilikuwa naomba kuuliza kwa sababu Mheshimiwa Waziri pia ni Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi na kwa maana hiyo watendaji wa CCM yeze ni bosi wao lakini pia kwa hili yeze ni bosi kwa maana ya kwamba ni Waziri mwenye dhamana ya Wizara husika, kwa hiyo, nilikuwa naomba atoe tamko anamwambia nini mtendaji huyu na watendaji wengine wenye tabia kama hizo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi kwa suala Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Kwanza katika mipango miji kuna maeneo ambayo ni ya wazi ni kweli kwa kipindi kirefu tumekuwa na matatizo ya maeneo ya wazi ama kuvamiwa ama tu

halmashauri ya mji wanakaa wanabadilisha matumizi. Sasa mwaka jana nimetoa *circular* kwa halmashauri zote kwa sababu mimi ndiye Waziri ninayesimamia ile sheria ya mipango miji, kupiga marufuku halmashauri inakaa halafu inasema eneo fulani la wazi tubadilishe matumizi liwe kitu fulani, nikapiga marufuku kwamba wala msileté, kwa wanapotaka kubadilisha lazima wapate kibali kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji. Nikasema wala msileté ombi kama hilo kwa sababu halitakubaliwa ili tulinde maeneo machache yaliyobaki yasiendelee kuvamiwa kwa sababu mji hauwezi kukaa bila mapafu, maeneo ya wazi ndiyo mapafu ya mji kupunua, sasa tunajimaliza wenyewe. Kwa hiyo hili ni tamko ambalo nimeshalitoa kwa wote na hilo tatizo la Magomeni Makuti amesema nitoe tamko, tamko lile tufuate sheria za mipango miji. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nachangia na wakati Mheshimiwa Waziri anajibu kuhusu kupanga matumizi bora katika vijiji nilimweleza kwamba uangalifu mkubwa sana unahitajika kwa sababu kuna vijiji vingine huwezi ukapanga zaidi ya ilivyo. Kwa mfano huwezi ukaenda Moshi ukabomoa makaburi yote eti unapanga hapa watu wote wa Moshi sasa watakuwa wanazikana utaleta vita, huwezi pia ukaenda kubomoa makaburi kwa rafiki zangu wa Iringa kule utapata bunduki nyuma ya kichwa chako. Najua sasa hivi wengi tumekaa miaka 36 baada ya kupangwa mwaka 1974, leo tena kama ndiyo sera au ilani mpya ya Chama cha Mapinduzi unataka kutupanga tena basi uhakikishe kwamba tutakuwa kweli na vita na Chama cha Mapinduzi kwa sababu tumechoka kugeuzwa kama chapati, kwa hiyo, nilikuwa nataka tu kwamba ni vizuri tukawaelimishe wananchi ili tujuue tunataka kufanya nini lakini kusema tu, kila kijiji kiishi kama mjini hii kwa sasa hivi haiwezekani, leo hii wengi wetu tuKifungua tunaenda kuzikwa katika mashamba ya baba zetu na hatujafikia mahali ambapo sasa tutazikwa kwenye makaburi ya kijiji kizima. Kwa hiyo, kuna vitu ambavyo lazima viende pole pole, vijiji vipyta, sawa, vijiji vilivyopo nilikuwa nataka kuwaambia tu hebu mfanye mambo haya kwa uangalifu tuna-deal na watu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu naomba nimjibu Mheshimiwa John Cheyo kama ifuatavyo; pengine hatuiaelevana dhana ya kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji, nadhani tatizo liko pale, sasa nataka anisikilize kwa makini nini kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nataka Mheshimiwa John Cheyo ajue ni kwamba hawa wataalam kutoka kwenye Halmashauri ile Tume ya Mipango inayofundisha wataalam wa wilaya. Wanapokwenda kwenye kijiji ni wanakijiji wenyewe ndiyo wanaojipangia eneo lipi litumike kwa kazi gani hawa watalaam ni kuwawekea tu ile mipaka wao wenyewe ndiyo watasema eneo hili tunataka liwe shule, eneo liwe kwa shughuli wenyewe wanakijiji hawa wanachofanya hilo eneo unalosema kwa kazi fulani kuweka ile mipaka tu, unasema hili eneo la zahanati, eneo la makazi wenyewe wanakijiji wenyewe ndiyo wanaopanga hawapangiwi mtu mwingine anayekuja kwamba sasa eneo hili sisi tumekuja tunatoa amri liwe la hiki, hapana wenyewe hawa wanachofanya ni kuweka ile mipaka tu na baadaye ile mipaka sasa inatambuliwa kwa mujibu wa sheria ili mtu mwingine kama eneo wamesema eneo hili la malisho ya mifugo mtu mwingine yeye akapeleka jembe, ile *by-law* sheria ndogo ile imbane, Mheshimiwa John Cheyo, hicho ndicho tunachofanya tunafanya hivyo ili kuondoa migogoro kwa sababu kila eneo kama

halijaainishwa matumizi yake kila mtu aKifunguanya jambo pale atakuwa sahihi lakini ukishaainisha kwamba eneo hili wanakijiji wenyewe wanaainisha ni la matumizi haya basi mipaka inawekwa na sheria ndogo inatungwa kulinda matumizi yale ambayo wanakijiji wenyewe wametaka iwe hivyo. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi nilikuwa nimeeleza juu ya suala la gharama kubwa katika mabaraza ya ardhi, kwa kuwa dhana ya kuanzisha mabaraza haya ilikuwa inalenga zaidi kusaidia wananchi hasa wale wanyonge, maskini kabisa katika maeneo yetu mbalimbali hasa vijiji na kata lakini uzoefu sasa unaonyesha kwenye mabaraza, gharama ya kufungua faili ni kati ya shilingi 10,000 hadi shilingi 20,000 kwa maeneo ambayo nimeyafanya utafiti na pale ambapo baraza linapaswa kuhamia kwenye eneo la tukio kuangalia mgogoro kwenye shamba au kwenye ardhi gharama ile inakaribia shilingi laki moja au zaidi na wanatakiwa wachangie wote wawili wanaohusika. Uzoefu unaonyesha mara nyingi migogoro hii ni kati ya wenyewe uwezo na hasa mara nyingi wanaume dhidi ya akinamama na mara nyingi yatima au walioachika. (*Makofi*)

Sasa nilikuwa nauliza kama mahakama ya kawaida na hasa kwa maana hii hata mahakama ya Hakimu Mkazi na hata Mahakama Kuu faili linafunguliwa kwa kati ya shilingi 1,500 mpaka shilingi 2,500 ni sababu zipi zimetufanya mabaraza haya ambayo ndiyo yalilenga kusaidia wanyonge yamekuwa ghali zaidi, yamekuwa hayasadii, yamewafanya wale wanyonge haki zao zipotee na hasa mara nyingi kwa matajiri, nilitaka kujua ni nani anasimamia zoezi hili mara nyingi Waziri amejibu hapa kwamba ni kazi ya Halmashauri na TAMISEMI, ni kitu ambacho kimetupiwa huku na kule, kama kuna msajili kama ilivyo kwa mahakama ni kwa nini kusiwe na chombo kimoja kinaratibu mambo haya wananchi kweli wapate haki zao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kuhusu suala la Mheshimiwa Dr. Slaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Sheria ya Mabaraza ya Ardhi iliundwa ili kuharakisha na kurahisisha usikilizaji wa migogoro ya ardhi. Kurahisisha, kuharakisha na kupunguza msongamano wa kesi huko Mahakamani, hii ndiyo dhana yenyewe, kama kuna vitendo vinavyokwenda kinyume cha haya, ni makosa, tulitaka tujue hiyo ni Mahakama gani inayotoza shilingi 20,000 kuandikisha tu. Hii ndiyo inatakiwa iwe Mahakama rahisi kabisa kuliko Mahakama nyingine yoyote, ndiyo dhana yenyewe ya ile Sheria kwa hiyo, kwa kweli nitapenda Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, anipe taarifa zaidi, hilo ni Baraza lipi ambalo linatoza shilingi 10,000 hadi shilingi 20,000 kuandikisha kesi. Haiwezekani, ni kwenda kinyume cha matakwa ya hii Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la gharama za kwenda ku-*visit site* tumeanza kutoa magari na mafuta. Sasa hivi kila Baraza ambalo liko Makao Makuu ya Mkoa tumeshawapatia gari na mafuta ili kuwarahisishia, huyu Mwenyekiti wa Baraza na wale Wazee wa Baraza kuweza kwenda *site* kwenye kesi kutembelea hayo mashamba na

kuamua kesi. Kwa hiyo, suala la kuwabebesha gharama wale wenye kesi sasa hivi vilevile tumelifanyiakazi. (*Makofit*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh.2,645,679,000  
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*.....Sh. 689,207,400 Kifungu 1004 - *Management Information System*.... Sh. 434,666,700  
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 236,592,100  
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.....Sh. 251,150,800

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2001 - *Land Administration Division* .....Sh. 1,613,525,700  
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Division* .....Sh. 2,868,671,000 Kifungu 2003 - *Registration of Titles Unit*.....Sh. 550,971,600  
Kifungu 2004- *Valuation Unit* .....Sh. 435, 175, 900  
Kifungu 3001- *Physical Planning Division*.....Sh. 2,785,770,400  
Kifungu 3002- *Housing Division*.....Sh. 11,692,603,200

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit*.....Sh. 2,983,975,300

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Kifungu kidogo cha 260500 *Current Subsidies to Households and Unincorporate Business*. Nimejaribu kutafuta tafsiri ya hiki Kifungu nimeshindwa kukipata, naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 260500.

**MWENYEKITI:** Kinasema nini?

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinasema *Current Subsidies to Households and Unincorporate Business*. Sasa katika *District Land and Housing Tribunal* ninashindwa kuelewa hii *Unincorporate Business* pamoja na *Households* ni kitu gani?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kuhusu Kifungu hiki alichokieleza

Mheshimiwa Mbunge. Kifungu hiki hizi pesa shilingi 739,200,000 zinahusu malipo kwa Wazee wa Mabaraza (*assessors*) na zimeongezeka, zilikuwa shilingi 450,000,000 hadi kufikia shilingi 739,200,000 kwa sababu tumeongeza posho za hawa Wazee wa Mabaraza kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 30,000 kwa siku. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001- *Administration*

*and General* .....Sh.1,300,000,000

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh. 2,139,784,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2001 - *Land Administration Division*.....Sh. 15,821,799,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. Nilitaka tu niulize kwamba mwaka jana Mheshimiwa Rais alitembelea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, tunaenda kwa Kifungu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 4901 *Implementation of BEST programme...*

**MWENYEKITI:** Mmh!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tarehe 31 Oktoba, Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Mbozi pamoja na mambo mengine aliyofanya, ilikuwa ni kuzindua Kituo cha Kusajili Hatimiliki za Kimila yaani kama Masjala hivi na zoezi lile lilikuwa ni la kitaalam ambalo lilikuwa linafanywa kwa kutumia kompyuta. Rais alivutiwa sana na hatua ambayo ilikuwa imefikiwa na wananchi wakafurahi sana kwamba tumepata kituo kwa maana ya kurahisisha usajili wa hati zile.

Lakini baada ya Mheshimiwa kuondoka mpaka leo kile kituo hakijafanya kazi na hata zile kompyuta ambazo Mheshimiwa Rais alizitumia na zenyewe mpaka leo hazionekani. Wananchi wa Kijiji cha Halungu hawaelewi kinachoendelea, tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo kuna nini, na hiyo hatua itarejewa lini?

**MWENYEKITI:** Una hakika hiki Kifungu ndiyo chenyewe?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki kinahusu *BEST programme*, kwa uelewa wangu nafikiri ndiyo hapo, kwa sababu nadhani kinahusiana na elimu.

**MWENYEKITI:** *BEST* maana yake siyo *best*, hii ni *programme* inaitwa *BEST, is not best*. Unajua pale kwenye mshahara wa Waziri maneno hayo yalikuwa *yana-fit*, hapa sijui. Mheshimiwa Waziri hebu eleza hiki Kifungu kilichopo hapo ni cha nini.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni Kifungu ambacho kinalenga kufanya shughuli ambazo zitarahisisha uwekaji wa kumbukumbu za ardhi katika Ofisi ya Msajili wa Ardhi na Ofisi ya Kamishina wa Ardhi na ni mahali sahihi alipoelezea Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ile Masjala ya kutunza zile hatimiliki ni sehemu ya kumbukumbu ambazo zinatakiwa zitunzwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika hilo alilosema Ndugu yangu Zambi, sasa ye ye anangojea tu mpaka kwenye Kamati ya Matumizi, angeniambia mapema tu tungkuwa tumesharudisha hiyo kompyuta ambayo Rais alizindua halafu ikaondoka. Hata hivyo hiyo kompyuta itarudi. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2002 - <i>Surveys and Mapping Division</i> .....	Sh. 3,003,495,000
Kifungu 2003 - <i>Registration of Titles Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 3001 - <i>Physical Planning Division</i> .....	Sh. 0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Kifungu kwa Kifungu na kuyaptisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2010/2011 yamepitishwa na Bunge kihalali. Kwa hiyo, tunapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na nina amini ulipata muda wa kuwashukuru watu wa kule kwako pamoja na wanawake unaowalea na sisi wote tunakutakia kheri. (*Makofi*)

Kwa kweli Mheshimiwa Waziri unafanyakazi nyingi vizuri na tunawapongeza pia wasaidizi wako katika Wizara yako kwa kufanyakazi kwa uzalendo. Ni Wizara hii ambayo zamani ilikuwa na matatizo sana, lakini sasa tunaendelea na nadhani tukiongeza nguvu zaidi itakuwa ni faraja kwa Watanzania kutumia ardhi kwa ajili ya maendeleo yao. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri anapokuwa huko kwenye jimbo lake, msishushe kamba, bali muendelee kuongeza nguvu na *corruption* ilikuwa katika Wizara hii, wala ilikuwa siyo siri. Kwa hiyo, tunategemea kwamba mtaweza kuonyesha ulimwengu katika hili kwamba inawezekana Wizara ya Ardhi ikawa *corruption free zone*. Kwa hiyo, ninawatakia kila la kheri na kuapongeza tena.

Waheshimiwa Wabunge, hatuna matangazo mengine isipokuwa ni ile semina ya *Private, Public Partnership (PPP)* kesho saa nne asubuhi. Hiyo semina nadhani ni muhimu sana kwa Waheshimiwa Wabunge, mhudhurie kwa sababu ni jambo jipya sana, usije ukabanwa na wananchi kule wanakuuliza kumbe wewe hulifahamu. Sasa hiki ni kitu muhimu sana, na nadhani tukifanikiwa kitawenza kuendeleza zaidi maendeleo ya Tanzania kwa *speed* kubwa zaidi bila kutegemea pesa zetu wenye. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba niwashukuru sana kwa kazi njema mliyofanya kwa siku hizi zote na kesho ni sikukuu ya Sabasaba. Niwatakie sikukuu njema na mapumziko mema mpaka siku ya Alhamisi, tarehe 8, 2010 saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.55 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,  
Tarehe 8 Julai, 2010 saa tatu asubuhi)*

